## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU

# Kuhusu Taarifa ya Fedha za Serikali Kuu Kwa Mwaka Unaoishia Tarehe 30 Juni, 2015

## SERIKALI KUU

**Machi 2016**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

# RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU TAARIFA YA FEDHA ZA SERIKALI KUU KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2015

## SERIKALI KUU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi,
16 Barabara ya Samora Machel, S.L.P. 9080, 11101 Dar es Salaam.
Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Tarakishi:
255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, tovuti: www.nao.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na.FA.27/249/01/2014/2015 28 Machi 2016

Mh. Dkt. John Pombe Magufuli,
Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P. 9120,
Ikulu,
1 Barabara ya Baraka Obama,
11400 DAR ES SALAAM.

**Yah: Kuwasilisha Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu yaTaarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2015**

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (iliyorekebishwa 2005) na Kifungu cha 34 (1)(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008.

Ninayo heshima kubwa kuwasilisha ripoti kuu ya ukaguzi ya mwaka inayohusu taarifa za fedha za serikali kuu za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2015 kwa taarifa na hatua zako muhimu.

Katika ripoti hiyo, nimetoa mapendekezo yenye lengo la kujenga ambayo kama yatatekelezwa yanaweza kupunguza matukio ya ukiukwaji wa taratibu na kwa kiasi kikubwa kuboresha uwajibikaji wa watendaji wa Serikali katika masuala ya fedha.

Nawasilisha.

Prof. Mussa Juma Assad
MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

**Yaliyomo**

Yaliyomo....................................................................iv
Orodha ya Majedwali.......................................................ix
Vifupisho....................................................................xiv
Dibaji ......................................................................xviii
Shukrani.....................................................................xxi
Muhtasari ................................................................xxiii
Sura ya Kwanza ...........................................................1
1.0 Utangulizi..................................................................1
1.1 Mamlaka ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali...1
1.2 Madhumuni ya Ukaguzi....................................................2
1.3 Mbinu za Ukaguzi..............................................................3
1.4 Mawanda ya Ukaguzi.........................................................3
1.5 Viwango na taratibu za ukaguzi zilizotumika kutoa taarifa, .. Idadi ya Wakaguliwa na Muundo wa ofisi ya Taifa ya Ukaguzi....4
1.6 Majukumu ya kiSheria ya Taasisi zinazokaguliwa.......8
1.7 Matarajio ya matokeo ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.......................................10
Sura ya Pili......................................................................11
HATI ZA UKAGUZI.........................................................11
2.0 Utangulizi ....................................................................11
2.1 Maana ya hati ya ukaguzi ..........................................11
2.2 Aina za hati za ukaguzi/Maoni ya Ukaguzi.....................12
2.3 Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine.........................................................................13
2.4 Mchanganuo wa hati za ukaguzi kwa Serikali Kuu kwa miaka mitano mpaka 2014/15..............................15
2.5 Mchanganuo wa hati za Ukaguzi kulingana na aina ya wakaguliwa (2010/11 to 2014/15)............................16

Sura ya Tatu.....................................................................18
UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA YA NYUMA.................................................18

3.0 Utangulizi....................................................18

3.1 Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka iliyopita kwa kila Mkaguliwa....................................................18

3.2 Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka ya nyuma kuhusu ripoti ya mwaka ya Ukaguzi......20

3.3 Kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge (PAC)....................................................21

Sura ya Nne....................................................23

USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA )....................................................23

4.1 Mapitio ya Bajeti.................................................... 23

4.2 Mwenendo wa ujumla wa Ukusanyaji wa Mapato...............24

5.0 Utangulizi.................................................... 40

5.1 Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Majumuisho..............40

5.2 Usimamizi wa uwekezaji na maslahi ya Serikali............46

5.3 Ukaguzi Mamlaka ya Mapato Tanzania.........................53

5.4 Ukaguzi na Usimamizi wa Deni la Taifa.......................83

5.5 Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu.........97

6.0 Utangulizi....................................................104

6.1 Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani katika Taasisi.................104

6.2 Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi ...............................106

6.3 Mapungufu katika usimamizi wa vihatarishi ................108

6.4 Kupitia Mifumo ya TEHAMA ..................................109

6.5 Tathmini ya Kugundua na Kuzuia Udanganyifu...............111

Sura ya Saba....................................................114

USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA....................114

7.0 Utangulizi....................................................114

7.1 Mambo muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa usimamiaji wa rasilimali watu na mishahara............................114

WAKALA WA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE ZA SERIKALI...........132

8.0 Utangulizi....................................................132

8.1 Masuala Muhimu Yaliyojitokeza kwenye ukaguzi.............132

Sura ya Tisa .................................................... 179
USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA.................................179
9.0 Utangulizi....................................................179
9.1 Sheria na udhibiti katika Manunuzi ya Umma...............179
Sura ya Kumi.....................................................213
USIMAMIZI WA MATUMIZI............................................213
10.0 Utangulizi...................................................213
10.1 Mambo muhumu yaliyojitokeza kwenye Ukaguzi wa usimamuzu wa matumizi.....................................213
Sura ya Kumi na Moja.............................................232
USIMAMIZI WA MALI NA MADENI......................................232
11.0 Utangulizi...................................................232
11.1 Mambo muhimu yaliyojitekeza kwenye ukaguzi wa mali na madeni.......................................................232
11.1.11 Madeni tarajiwa.........................................187
Sura ya kumi na mbili............................................193
UKAGUZI MAALUMU NA MASUALA MENGINE.........................250
12.0 Utangulizi...................................................250
Sura ya Kumi na Tatu.............................................260
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO.......................................260
13.0 Utangulizi...................................................260
13.1 Kufuatilia Utekelezai wa Mapendekezo......................260
13.2 Usimamizi wa Fedha za Umma...............................261
13.3 Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara................262
13.4 Wakala wa Serikali, Taasisi nyingine na Mifuko Maalum...262
13.5 Ukaguzi wa Vyama vya Siasa................................263
13.6 Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba........................264
13.7 Mapungufu katika Usimamizi wa Matumizi..................265
13.8 Mapungufu katika Usimamizi wa Mali za Kudumu..........265
13.9 Matokeo ya Kaguzi Maalumu na mambo Mengine..........268

**Viambatisho**

Kiambatisho Na. 1.1: Orodha ya Wakaguliwa waliopata hati zinazoridhisha .............................. 270

Kiambatisho Na. 1.2(a): Orodha ya Wakaguliwa waliopata hati zenye Mashaka..............................281

Kiambatisho Na. 1.2(b): Orodha ya Wakaguliwa waliopata hati zenye mashaka 2014/2015.................282

Kiambatisho Na. 1.3 Taasisi zilizopata hati isiyoridhisha.......293

Kiambatisho No.3.1: Kiasi cha fedha kwa mambo ambayo hayajatekelezwa...........................295

Kiambatisho Na 3.2: Ufuatiliaji wa mapendekezo ya nyuma juu ya taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kila Mkaguliwa...................................297

Kiambatisho Na 3.3: Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa Wakala..300

Kiambatisho Na 3.4: Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa taasisi nyinginezo na Mifuko maalumu...........301

Kiambatisho Na 3.5: Ufuatiliaji na utekelezaji wa Ripoti ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa miaka ya nyuma............302

Kiambatisho Na 4: Fedha za Matumizi ya Kawaida: Makisio yaliyoidhinishwa, Halisi zilizotolewa na Matumizi Halisi.............................266

Kiambatisho Na. 4.2: Fedha za Maendeleo: Makisio yaliyoidhinishwa,Halisi zilizotolewa na Matumizi Halisi..............................331

Kiambatisho Na. 5.1: Tarehe za Taarifa za fedha za Taasisi zinatofautiana na Tarehe za Taarifa Jumuifu.....................................337

Kiambatisho Na. 5.2: Orodha ya Vitegauchumi vya Serikali vinavyojiendesha kwa hasara.............338
Kiambatisho Na. 5.3: Misamaha ya Kodi kwa mwaka wa fedha 2014/15.................................... 339
Kiambatisho 6.1: Orodha ya Taasisi zenye Mapungufu katika Mifumo ya Ndani.............................................340
Kiambatisho Na. 7.1: Upungufu wa wafanyakazi...................345
Kiambatisho Na. 8.1: Mali na Magari yalilyotelekezwa............347
Kiambatisho Na. 9.1: Mapungufu katika utekelezaji wa mikataba..348
Kiambatisho Na.9.2: Taasisi zilizokaguliwa na Mhakiki Mali.......350
Kiambatisho Na.10.1: Hati za malipo zenye nyaraka pungufu...358
Kiambatisho 10.2: Taasisi ambazo hazikuwa na stakabadhi ya kieleckroniki (EFD)..............................359
Kiambatisho10.3: Fedha kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa..360
Kiambatisho Na. 11.1: Kinachoonyesha taasisi ambazo hazijaanza kuainisha mali wanazomiliki kiukamilifu......361
Kiambatisho 11.2: Taasisi ambazo zina mali za kudumu ambazo zimefikia ukomo wa matumizi.................... 363
Kiambatisho 11.3: Nyumba za serikali ambazo ziko katika hali mbaya pamoja na viwanja visivyoendelezwa....365
Kiambatisho Na. 11.4: Taasisi ambazo zimelimbikiza madeni.....366

## Orodha ya Majedwali


Jedwali 2: Mamlaka ya Kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali..........................................2
Jedwali 3: Idadi ya Wakaguliwa 2014/15..............................6
Jedwali 4: Orodha ya Taasisi ambazo Ukaguzi wake haujahitimishwa...7
Jedwali 5: Aina za hati za ukaguzi....................................12
Jedwali 6: Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine................................................14
Jedwali 7: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka mitano mpaka 2014/15...................................................15
Jedwali 8: Mwenendo wa hati za Ukaguzi kwa kipindi cha........17
Jedwali 9: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa kila Mkaguliwa................................................19
Jedwali 10: Muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa miaka ya nyuma.......................................................20
Jedwali 11: Muhtasari wa utekelezaji wa maelekezo ya PAC ya miaka iliyopita...........................................22
Jedwali 12: Mwenendo wa makusanyo ya mapato kwa miaka mitatu......................................................27
Jedwali 13: Mwenendo wa uchambuzi wa bajeti kwa miaka mitatu.......................................................29
Jedwali 14: Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida dhidi ya Makisio.........................................30
Jedwali 15: Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida na matumizi halisi.........................................31
Jedwali 16: Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo dhidi Makisio ................................33
Jedwali 17: Uwiano wa fedha zilizotolewa na matumizi halisi kwa fedha za maendeleo....................................34
Jedwali 18: Mwenendo wa mapato yasiyo ya kodi kwa miaka mitatu (Kiasi katika Sh. Milioni).......................................36
Jedwali 19: Uchambuzi wa mkusanyiko yasiyo ya kodi kwa Wizara na Idara chini ya mpango wa kubakiza..................38

Jedwali 20: Jedwari 1: Orodha ya makampuni ambayo hisa zake zimepungua......................................................48
Jedwali 21: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita......................................................55
Jedwali 22: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2014/15.............56
Jedwali 23: Ufanisi kwa ujumla katika makusanyo ya mapato Tanzania......................................................58
Jedwali 24: Muhtasari wa kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Tanzania.........................64
Jedwali 25: Mwenendo wa Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka 2010-2015......................................................69
Jedwali 26: Bidhaa zilizokaa zaidi kwenye Forodha na maghala ya mali......................................................72
Jedwali 27: Magari yasiyoonekana kutoka nchini (Novemba 2014 – Januari 2015)............................................75
Jedwali 28: Tozo kutokana na ucheleweshaji wa dhamana zilizofutwa/kuisha- Orodha ya Makampuni..............76
Jedwali 29: Muhtasari wa riba ambazo hazijakusanywa na makampuni..............................................77
Jedwali 30: Kodi zilizofanyiwa tathmini na kutokukusanywa shilingi 29 7,296,619,239............................................80
Jedwali 31: Kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi halisi...........81
Jedwali 32: Taarifa ya fomu za mrejesho wa kodi ya ongezeko la thamani ambazo hazikuwasilishwa.....................83
Jedwali 33: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni kwa Miaka Mitano.....85
Jedwali 34: Deni la nje Juni 30 2011 hadi Juni 30 2015..........90
Jedwali 35: Mafaili ya wastaafu yaliyokaguliwa......................99
Jedwali 36: Jedwali Na.xx: Mafao ya Wastaafu yaliyozidishwa...100
Jedwali 37: Jedwali xx: Mafao ya Wastaafu yaliyopunjwa........100
Jedwali 38: Mafao ambayo hayakupelekwa kwa wakati...........101
Jedwali 39: Taasisi zenye mapungufu kwenye vitengo vya ukaguzi wa ndani..............................................105
Jedwali 40: Mapungufu katika utendaji wa Kamati za Ukaguzi..105
Jedwali 40: Mgawanyo wa Taasisi na mapungufu katika kamati za ukaguzi..............................................107

Jedwali 41: Mapungufu katika kudhibiti Vihatarishi.................110
Jedwali: Mapungufu katika TEHAMA..............................110
Jedwali 42: Mapungufu yaliyobainika katika urejeshwaji wa mikopo ya elimu ya juu..........................................115
Jedwali 43: Mishahara iliyolipwa kwa wafanyakazi ambao hawapo kwenye Utumishi wa Umma...............................117
Jedwali 44: Makato yaliyolipwa kwa niaba ya wafanyakazi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma.....................119
Jedwali 45: Taasisi zenye watumishi ambao hawajathibitishwa...121
Jedwali 46: Kutofanyika kwa tathmini ya uwazi ya utendaji kazi..123
Jedwali47: Wakuu wa Vitengo wanaokaimu katika nafasi mbalimbali................................................124
Jedwali 48: Taasisi zilizochelewesha kutuma makato kwenda mifuko ya Hifadhi ya Jamii..............................125
Jedwali 49: Posho ya kukaimu iliyolipwa bila kukatwa kodi ya mapato..................................................126
Jedwali 50: Taasisi ambazo watumishi wake wanapata mishahara chini ya kiwango kilichopitishwa kisheria...........................................128
Jedwali 51: Orodha ya ofisi za balozi zenye watumishi waliofanya kazi ubalozini zaidi ya muda ulioidhinishwa...........130
Jedwali 52: Makisio yaliyoidhinishwa na Makusanyo halisi.......134
Jedwali 53: Makisio yaliyoidhinishwa na Fedha zilizotolewa....136
Jedwali 54: Riba kwa kuchelewesha malipo.......................143
Jedwali 55: Magari yaliyotelekezwa.............................155
Jedwali 56: Wakala zenye Rejista ya mali za kudumu isiyokwenda na wakati na mali zisizo na alama za utambulisho..148
Jedwali 57: Madeni yasiyokusanywa...............................150
Jedwali 58: Wakala zenye kesi za Madai...........................151
Jedwali 59: Wakala zenye Madeni yasiyolipwa.....................153
Jedwali 60: Malipo yasiyoambatana na risiti za Kielektroniki...154
Jedwali 61: Wakala zisizotoza kodi ya zuio.......................155
Jedwali 62: Wakala zenye Masurufu Yasiyorejeshwa..............155
Jedwali 63: Wakala zenye malipo yasiyo na viambatisho.........156

Jedwali 64: Wakala zenye Mikopo kwa Watumishi ambayo haijarejeshwa............................................157
Jedwali 65: Wakala zenye makato yasiyowasilishwa mamlaka husika...................................................158
Jedwali 66: Mapato yasiyokusanywa kwenye Mauzo ya nyumba.159
Jedwali 67: Mapato yasiyopelekwa benki kwa usahihi............160
Jedwali 68: Uhaba wa watumishi na wanaokaimu.................161
Jedwali 69: Taasisi zenye madeni yasiyolipwa.......................169
Jedwali 70: Taasisi zenye madeni yasiyokusanywa................170
Jedwali 71: Taasisi ambazo hazikuzingatia taratibu za Manunuzi..171
Jedwali 72: Taasisi zenye Malipo yasiyo na viambatisho vya kutosha..............................................173
Jedwali 73: Taasisi zenye mapungufu katika usimamizi wa Mali..174
Jedwali 74: Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi...180
Jedwali 75: Taasisi zilizofanya Manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni................................................182
Jedwali 76: Manunuzi yaliyofanyika bila ushindini.................183
Jedwali 77: Mapokezi ya vifaa visivyofanyiwa Ukaguzi............185
Jedwali 78: Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi..............................................188
Jedwali 79: Orodha ya Taasisi za Serikali Kuu zilizofanya Manunuzi bila ya mikataba......................................189
Jedwali 80: Taasisi zilizofanya Manunuzi kwa fedha taslimu/ masurufu...............................................191
Jedwali 81: Manunuzi ya Vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasiodhinishwa.....................................192
Jedwali 82: Manunuzi ya Vifaa na huduma yasiyopokelewa......195
Jedwali 83: Mapungufu yaliyojitokeza katika Wizara na Idara za Serikali zilizokaguliwa.................................204
Jedwali 84: Matokeo ya Uchunguzi wa Zabuni Na. IE/08/2012-13/ HQ/G/199...............................................208
Jedwali 85: Mapungufu yaliyobainika katika taarifa ya Kurugenzi ya uhakiki mali za Serikali..............................211
Jedwali 86: Taasisi zenye malipo yasiyo na hati za malipo.......215

Jedwali 87: Orodha ya Taasisi zilizolipa katika vifungu vya bajeti visivyostahili............................................218
Jedwali 88: Taasisi zilizofanya malipo nje ya bajeti iliyoidhinishwa....................................220
Jedwali 89: Taasisi zenye masurufu ya muda mrefu...............222
Jedwali 90: Taasisi zilizolipa malipo zaidi ya stahiki...............224
Jedwali 91: Taasisi zilizohusika na matumizi yasiyo na manufaa kwa miaka miwili............................................226
Jedwali 92: Taasisi zilizofanya malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za mapokezi................................................229
Jedwali 93: Taasisi ambazo hazikuwakata watoa huduma kodi ya zuio....................................................230
Jedwali 94: Taasisi ambazo zinachanganya thamani ya Ardhi na Majengo.................................................235
Jedwali 95: Balozi ambazo zimeonekana kutotumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha...................238
Jedwali 96: Taasisi zenye vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye Leja ya Vifaa............................................239
Jedwali 97: Taasisi ambazo hazina nyaraka za umiliki wa Ardhi na Majengo.................................................240
Jedwali 98: Taasisi ambazo zina Mali za Kudumu zisizo alama na utambulisho..............................................241
Jedwali 99: Taasisi ambazo vifaa vyake vya zima moto vina mapungufu................................................242
Jedwali 100: Taasisi zenye kesi zinazoendelea........................244
Jedwali 101: Madeni ya Hospital za Rufaa..........................246
Jedwali 102: Taasisi zilizoshindwa kuonyesha madeni............248
Jedwali 103: Taasisi zenye madeni yasiyo na viambatisho........249

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| ACGEN | Mhasibu Mkuu wa Serikali |
| ADEM | Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu |
| AFRM | Mpango wa kujitathimni kwa Nchi za Afrika |
| AGITF | Mfuko wa Pembejeo za Kilimo |
| AO | Afisa Masuuli |
| APP | Mpango wa Manunuzi wa Mwaka |
| ASA | Wakala wa Mbegu za Kilimo |
| BOQ | Mchanganuo wa Gharama za Ujenzi |
| BoT | Benki Kuu ya Tanzania |
| CAG | Mdibiti na Mkaguzi Mkuu |
| CDF | Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi |
| CG | Serikali Kuu |
| CTA | Kibali cha Kazi cha Muda Mfupi |
| DART | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam |
| DDCA | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa |
| EFD | Mashine za Kielekroniki |
| ETD | Hati za Dharura za Kusafiria |
| FETA | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo |
| FRF | Jeshi la Zimamoto na Uokoaji |
| GCLA | Wakala wa Maabara za Serikali |
| GN | Tangazo la Serikali |
| GoT | Serikali ya Tanzania |
| GPSA | Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi |
| GST | Wakala wa Utafiti wa Miamba |
| HESLB | Bodi ya Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu |
| HQ | Makao Makuu |
| IFMS | Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha |
| IJA | Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA) |
| IPSAS | Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma |

| | |
|---|---|
| ISA | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi |
| KPU | Kitengo cha Uchapishaji Kijichi |
| LAPF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa Serikali za Mitaa |
| LGLB | Bodi ya Mikopoya Serikali za Mitaa |
| LGTI | Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa |
| LITA | Chuo cha Mafunzo ya Mifugo |
| LPO | Mikataba midogo ya Manunuzi |
| LST | Shule ya Sheria Tanzania |
| MCRF | Mfuko wa Maji |
| MDAs | Wizara, Idara na Wakala |
| MFAIC | Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa |
| MIS | Mfumo wa Usimamizi wa Teknolojia ya Habari |
| MKURABITA | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania |
| MOU | Hati ya Makubaliano |
| NAOT | Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania |
| NCT | Chuo cha Taifa cha Utalii |
| NEC | Tume ya Uchaguzi |
| NFFA | Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale |
| NFRA | Wakala wa Akiba ya Chakula Taifa |
| NHBRA | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania |
| NHIF | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya |
| NRF | Mfuko wa Taifa wa Maafa |
| NSCD | Idara ya Ujenzi ya Jeshi la Kujenga Taifa |
| NSSF | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii |
| OPRAS | Upimaji wa utendaji kazi wa wazi wa watumishi |
| OSHA | Wakala wa Usalama na Afya Kazini |
| PAA | Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya 2008 |
| PAYE | Kodi ya Mapato kwa Watumishi |
| PE | Taasisi inayofanya Manunuzi |
| PFA | Sheria ya Fedha za Umma |

| | |
|---|---|
| PFR | Kanuni ya Fedha za Umma |
| PMG | Mlipaji Mkuu wa Serikali |
| PMIS | Mifumo ya manunuzi ya Umma |
| PMO-RALG | Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| PMU | Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi |
| PO-PSM | Ofisi ya Raisi-Utumishi wa Umma |
| PPA | Sheria ya Manunuzi ya Umma |
| PPE | Mali, Mitambo na Vifaa |
| PPR | Kanuni za manunuzi ya Umma |
| PPRA | Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma |
| PSPF | Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma |
| REA | Wakala wa Umeme Vijjini |
| RITA | Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi |
| RS | Sekretarieti ya Mkoa |
| TAESA | Wakala wa Huduma za Ajira |
| TAGLA | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa |
| TANDREC | Kamati ya Maafa na Uokozi Tanzania |
| TANROADS | Wakala wa Barabara Tanzania |
| TASUBA | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni - Bagamoyo |
| TATC | Kituo cha Kuunda Mitambo na Magari Tanzania |
| TB | Bodi ya Wazabuni |
| TBA | Wakala wa Majengo Tanzania |
| TEMESA | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi |
| TFSA | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania |
| TGFA | Wakala wa Ndege za Serikali |
| TIA | Taasisi ya Uhasibu Tanzania |
| TMA | Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa |
| TMAA | Wakala wa ukaguzi wa Uchimbaji Madini Tanzania |
| TNMC | Baraza la Wkunga na Wauguzi Tanzania |
| TPDF | Jeshi la Wananchi Tanzania |
| TPSC | Chuo cha Utumishi wa Umma |

| | |
|---|---|
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TTSA | Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania |
| TVLA | Wakala wa Maabara za Mifugo |
| TZS | Shilingi ya Tanzania |
| UD | Idara ya Watumiaji |
| WDMI | Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji |
| WMA | Wakala wa Vipimo |

# Dibaji

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyorekebishwa 2005) pamoja na Kifungu Na. 34 (1) (c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na.11 ya mwaka 2008, nina heshima kubwa kuwasilisha ripoti yangu ya mwaka ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2014/15 ambayo inaonesha matokeo ya ukaguzi wa Serikali Kuu ikijumuisha Wizara/Idara/Wakala wa Serikali 150, Sekretarieti za Mikoa 25 na Balozi 34

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huwasilishwa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, baada ya kupokea ripoti hizo, Rais ataagiza wanaohusika waziwasilishe ripoti hizo mbele ya kikao cha kwanza cha Bunge ndani ya siku saba baada ya kuanza kwa kikao hicho.

Nina furaha kusema kwamba ofisi yangu (NAOT) imeendelea kutoa taarifa za ukaguzi na kuziwasilisha Bungeni kwa wakati kama Kanuni Na. 88 ya Kanuni ya Ukaguzi wa Umma, 2009. Natumaini ripoti hii itatoa mapendekezo muhimu na mwongozo juu ya mbinu bora za kuboresha utawala bora katika Sekta ya Umma.



Ripoti ya ukaguzi ya mwaka wa fedha 2014/15 inakua ni ripoti yangu ya pili kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali lakini pia, ni ripoti ya kwanza kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania , Mheshimiwa Dk John P. Magufuli.

Napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nikutakie kila la kheri katika kuyakabili majukumu yako mapya na changamoto za ofisi yako. Ni matazamio yangu kuwa tutafanya kazi pamoja vizuri katika kuwezesha serikali yako kufikia malengo yake.

Pia, nawapongeza wabunge wote ambao walichaguliwa katika uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2015. Nawahakikishia ushirikiano katika juhudi za kuwatumikia wananchi

Ofisi yangu imefanikiwa Kitaifa na Kimataifa katika kutimiza wajibu wa kisheria kwa sababu hiyo, imetokea kuaminiwa na wadau wengi.

Kimataifa, ofisi yangu imeendelea kufanya kazi yake ya ukaguzi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa kwa miaka minne ifikapo Juni, 2016. Katika hili napenda kutambua heshima iliyopewa ofisi yangu kuongoza kikao cha 69 cha Bodi ya Wakaguzi wa Umoja wa Mataifa (UNBoA) kwa siku mbili kutoka Julai 22-23, 2015 kilichofanyika katika Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa mjini New York, Marekani.

Hadi sasa ofisi yangu imeshawasilisha ripoti 22 kwa Baraza la Umoja wa Mataifa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2014 na ripoti 6 kwa vyombo vingine vya Umoja wa Mataifa. Ripoti hizi zilikua na ubora wa hali ya juu na zilikidhi viwango vinavyokubalika Kimataifa.

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania (NAOT) inatambuliwa katika kutoa mahitimisho ya ukaguzi na mapendekezo ambayo yamekuwa yakilenga kuhakikisha kuwa kunakuwapo uwazi na uwajibikaji katika mapato na matumizi ya Fedha za Umma ili kuisaidia Serikali kufanikisha malengo yake ya kijamii na kiuchumi kwa maendeleo ya nchi.

Napenda pia, kutambua kwamba,kumekuwapo na ongezeko la bajeti kutoka Shilingi bilioni10.3 mwaka 2005/06 hadi Shilinngi bilioni 57.4 mwaka 2014/15 ambalo limeisaidia ofisi yangu kuweza kujiendesha kwa uhuru zaidi katika suala la raslimali kama vitendea kazi, kuajiri watumishi wenye sifa, na ujenzi wa majengo ya ofisi katika mikoa sita kati ya mikoa 25. Ni matumaini yangu kwamba, ofisi yangu itaendelea kupokea bajeti ya maendeleo ili kusaidia kuongeza ufanisi wa kazi zetu.

Ofisi yangu inasaidia kuhakikisha kunakuwapo uongozi wa umma ulio bora na endelevu ikiwa ni pamoja na kulishauri Bunge kwenye masuala ya kifedha na sheria zake licha ya changamoto kadhaa zinazoikabili Ofisi yangu. Aidha, changamoto hizo ni pamoja na:

- Ofisi yangu inaendelea kujadiliana na Serikali kuhusu suala la kuboresha maslahi ya Wakaguzi.

- Uhaba wa wafanyakazi na vitendea kazi: Kwa kutilia maanani kuwa shughuli zetu zinaongezeka kila mwaka tunakabiliwa na uhaba wa rasilimali ikiwa ni pamoja na magari, mtandao wa kuunganisha ofisi zetu zote, kamera za ulinzi, vinasa sauti, vifaa vya uchapishaji na zana nyingine za ukaguzi.

- Kwa ujumla, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) inahitaji msaada endelevu wa bajeti ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi hasa ukizingatia majukumu yake ya ukaguzi yanapanuka nchini na kimataifa. Naamini kuwa, mgao wa fedha katika miaka inayokuja utakuwa wa kutosha ili kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kisheria.

Nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kwa kutumia weledi wao, taaluma zao na kujituma kwao ambako kumenisaidia kutekeleza majukumu yangu ya kisheria.

Prof. Mussa Juma Assad
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

## Shukrani

Napenda kutambua ushirikiano nilioupata kutoka kwa wafanyakazi na menejimenti za Wizara /Sekretarieti za Mikoa/Balozi ambazo watumishi kutoka Ofisi yangu walikagua nchi nzima na kimataifa. Pia napenda kutoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wote wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Tanzania kwa dhamira yao na kujitolea kwao wamenisaidia na kuniwezesha kutoa taarifa hii na kuwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa wakati kwa mujibu wa Sheria. Napenda pia, kuwashukuru Wakurugenzi, Watendaji Wakuu, wafanyakazi wote wa taasisi zilizokaguliwa na wadau wote ambao wamechangia kwa namna mbalimbali kuwezesha uandishi wa ripoti hii.

Napenda pia, kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Bunge - ya Hesabu za Serikali, kwa kujitoa kwao na ushiriki wao katika mazungumzo yaliyozaa matunda kwa maslahi ya umma. Kama taasisi iliyokasimiwa jukumu la kutoa uhakika na kuthibitisha jinsi fedha za umma zilivyotumika, tunalipa umakini mkubwa jukumu la kamati katika kusimamia uwajibikaji na kuwezesha uelewa wa pamoja wa mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali miongoni mwa wadau wote wa ndani na nje ya nchi.

Napenda pia kutambua kazi kubwa iliyofanywa na Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali chini ya Wizara ya Fedha kwa kuandaa na kuwasilisha taarifa juu ya uhakiki mali kwa baadhi Wizara/Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2014/15 ambayo nimeona niyajumuishe katika ripoti yangu .

Hali kadhalika, ninawiwa kuwashukuru wadau wengine wote ikiwa ni pamoja na Waziri wa Fedha, Mlipaji Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma chini ya Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wao na utoaji wa taarifa muhimu zinazohitajika kwa ajili ya maandalizi

ya ripoti hii. Napenda pia, kumshukuru Mpiga Chapa wa Serikali kwa kuharakisha uchapaji wa ripoti hii na kuniwezesha kuiwasilisha kwa wakati.

Aidha, napenda kutoa shukrani zangu nyingi za dhati kwa jukumu muhimu linalofanywa na Jumuiya ya Kimataifa hasa Serikali ya Sweden kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Sweden, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Sweden, Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Kusimamia na Kuboresha Sekta ya Fedha za Umma (PFMRP), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Ujerumani (GIZ), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), Serikali ya China na wote wanaotutakia mema ambao wamechangia kwa kiasi kikubwa kuleta mabadiliko chanya ya ofisi yangu. Michango yao katika kuendeleza rasilimali watu, mifumo ya Teknolojia ya Habari na ununuzi wa vitendea kazi vya ofisi yetu vimeleta manufaa makubwa kwa mafanikio yetu.

Mwisho napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kazi nzuri iliyofanywa na wafanyakazi pamoja na menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa ujumla kwa kujitoa kwao katika kukuza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma nchini.

## Muhtasari

**(i) Utangulizi**

Matokeo ya ukaguzi kwenye taarifa za fedha zinazoishia 30 Juni, 2015 za Wizara, Idara, Sekretarieti za Mikoa, Balozi, Wakala, Mifuko pamoja na taasisi zingine yameonyeshwa katika sehemu hii. Muhtasari huu unaainisha kwa kifupi hoja mahususi zilizojadiliwa kwa kina katika sura husika za ripoti hii zinazohitaji kufanyiwa kazi na Serikali, Bunge, na Menejimenti za taasisi za Serikali Kuu husika ili kuhakikisha kunakuwa na tija na ufanisi katika utendaji wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa ili kuwa na matumizi bora ya fedha ya mlipa kodi.

**(ii) Mawanda ya Ukaguzi**

Kwa ujumla, kuna Taasisi za Serikali kuu zipatazo 209 zinazotakiwa kukaguliwa. Hata hivyo, taasisi 199, zikijumuisha Wizara, Idara na Wakala 126, Sekretarieti za Mikoa 25, Mifuko 13, Taasisi zingine 24 na Ofisi za Mabonde tengefu 9 zilikaguliwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/15. Mamlaka ya Mapatao Tanzania (TRA) na Hesabu Jumuisho (Consolidated Account) zimejumuishwa kwenye taarifa hii. Kila taasisi iliyokaguliwa imepewa ripoti ya ukaguzi pamoja na barua kwa Menejimenti. Kwa upande mwingine, taasisi saba hazikujumuishwa katika ripoti hii; kwamba, taasisi mbili (2)1 hazijakaguliwa kabisa na sita (6)2 ukaguzi, ulikuwa unaendelea wakati ripoti hii inaandaliwa.

**(iii) Mwenendo wa jumla wa hati za Ukaguzi**

Kati ya Taasisi 199 zilizokaguliwa, 180 (asilimia 90) zilipata hati inayoridhisha ikilinganishwa na 166 (asilimia 94) ya mwaka uliotangulia. Taasisi 18 (asilimia 9) zilipata hati zenye shaka ikilinganishwa na 9 (asilimia 5) ya mwaka uliotangulia. Vilevile,

1. BRELA na Wakala wa Kuendeleza Mji w a Kigamboni
2. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Mfuko wa Barabara, Shirikisho la Mabunge ya Jumuiya ya Madola, SUMA, Taasisi ya Utafiti wa Mifugo, na Mfuko wa Maafa.

Taasisi moja (Mzinga Corporation) ilipata hati isiyoridhisha ikilinganishwa na taasisi moja (Consolidated Accounts) kwa mwaka uliotangulia. Misingi ya hati za ukaguzi yameelezewa katika sura ya pili katika ripoti hii na ripoti moja moja zilizotolewa kwa taasisi.

Kielelezo Na. 1 Linaonyesha matokeo na hati za ukaguzi kwa miaka mitano iliyopita

Kielelezo 1: Mwendo wa hati za Ukaguzi kwa Miaka Mitano




**(iv) Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita**
Ufuatiliaji wa mapendekezo ya ukaguzi katika ripoti za jumla na ripoti moja moja yalifanyika. Katika ripoti moja moja mapendekezo 2,644 yalitolewa, kati ya hayo; 1028 (asilimia 39) yalitekelezwa kikamilifu, 885 (asilimia 33) yapo kwenye hatua ya utekelezaji, 534 (asilimia 20) hayajatekelezwa na 126 (asilimia 5) yalipitwa na wakati na 71(asilimia 3) zilijirudia.

Katika mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti ya jumla ya mwaka 2013/14, kulikuwa na mapendekezo 46 ambayo hayakutekelezwa yanayohitaji serikali kuyafanyia kazi. Nimepokea majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali tarehe 20 Julai 2015; ambapo hoja nane (asilimia 18) zimetekelezwa, hoja 37 (asilimia 80) ziko kwenye hatua za utekelezaji na 1 (asilimia 2) haijatekelezwa. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya tatu.

**(v) Utekelezaji wa Maelekezo ya kamati ya bunge ya hesabu za Serikali Kuu**

Katika taarifa ya ukaguzi iliyopita kuna jumla ya maelekezo 9 yaliotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ambayo yalihitaji utekelezaji wa Serikali. Maelekezo sita yalitolewa katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2012 na 3 ni za mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni 2013. Kati ya maelekezo 9 yaliyotolewa, 1 (asilimia 11) limetekelezwa, 5 (asilimia 56) yapo katika hatua ya utekelezaji na 3 (asilimia 33) hayajatekelezwa.

Hakukuwa na maelekezo ya kamati kufuatia ripoti ya ukaguzi ya mwaka ulioishia tarehe 30/6/2014 kwa sababu Bunge lilifikia ukomo wake kikatiba uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 9/7/2015. Kwa sababu hiyo, kamati ya Bunge haikufanya vikao vyake vya kujadili mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi Mkuu kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kama kutakuwa na maelekezo ya kamati kuhusu ripoti ya mwaka 2013/14, yatajumuishwa kwenye ripoti inayofuata. Ufuatiliaji wa mapendekezo ya kamati ya bunge ya hesabu za Serikali kuu bado unaendelea. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya tatu.

**(vi) Mapungufu katika usimamizi wa Fedha za Umma**

Mwaka wa fedha 2014/15 kiasi cha Shilingi bilioni

6,445.11 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo Serikali Kuu pamoja na Serikali za mitaa kukiwa na ongezeko la asilimia 13.6 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi bilioni 5,674.03 katika mwaka wa fedha 2013/14. Hesabu zilizokaguliwa zilionyesha kuwa Serikali kuu iliidhinishiwa na Bunge makadirio ya Shilingi bilioni 4,389.02 lakini kiasi halisi kilichotolewa ni Shilingi bilioni 2,954.20 kikiwa ni pungufu ya Shilingi bilioni 1,434.19 sawa na asilimia 32.69. Wakati huo huo, kiasi cha Shilingi bilioni 38.02 sawa na asilimia 1.29 ya fedha iliyotolewa hazikutumika.

Shilingi bilioni 13,408.22 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kukiwa na ongezeko la asilimia 6.6 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi bilioni 12,574.94 kwa mwaka 2013/14. Hesabu zilizokaguliwa zilionyesha kuwa Serikali kuu iliidhinishiwa na Bunge makadirio ya Shilingi bilioni 11,646.20, lakini kiasi halisi kilichotolewa ni Shilingi bilioni 11,190.11, ikiwa ni pungufu ya Shilingi bilioni 456.08 sawa na asilimia 3.92 wakati; huo huo, kiasi cha Shilingi bilioni 33.68 sawa na asilimia 0.3 ya fedha iliyotolewa hazikutumika.

Kwa ujumla, katika kiasi chote kilichotolewa kwa mwaka huo, kiasi cha Shilingi bilioni 5,178.13 kwa matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 165.41 za shughuli za maendeleo zilitolewa kwenye robo ya nne ya mwaka wa fedha, yaani Aprili mpaka Juni 2015, sawa na asilimia 26.92 ya bajeti yote ya Serikali. Kiasi cha Shilingi bilioni 134.29 za Wizara ya Ujenzi (asilimia 99.89 ya fedha hizi zikiwa ni za Mfuko wa barabara) hazikupokelewa, hivyo kuathiri utekelezaji wa bajeti.

Kumekuwa na ucheleweshaji katika utoaji wa fedha kutoka Hazina pamoja na wafadhili kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii imesababisha

miradi mingi iliyoibuliwa kutotekelezwa kwa wakati na mingine kutotekelezwa kabisa. Kitendo cha kutotoa fedha za miradi kama zilivyoidhinishwa kumesababisha kuongezeka kwa gharama kutokana na riba katika ucheleweshaji wa malipo. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya nne.

**(vii) Msajili wa Hazina**

Wakati wa ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, nilibaini kupungua kwa uwekezaji wa serikali na vipaumbele vyake katika mashirika na taasisi nyingine, na wakati mwingine, kupungua kwa hisa zake na hata mwishowe kuwa hatarini kupoteza hisa hizo.

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa hisa za serikali zilishushwa thamani katika kampuni za TANICA, Kampuni ya Oxygen Tanzania na TDFL. Kushuka kwa hisa za Serikali kwenye kampuni ya TDFL kuliathiri hisa za Serikali katika benki ya ABC.

Wakati wa ukaguzi, nilipitia utendaji wa hisa zilizowekezwa na Serikali kwa washirika wa mradi wa pamoja (Joint ventures), mashirika ambayo Serikali ina hisa chache (associates) na matawi (subsidiaries) na kubaini Taasisi kumi na tisa (19) ambazo uwekezaji wake unatengeneza hasara ambapo Serikali haipati faida. Hasara ya muda mrefu na mapungufu katika Taasisi huondosha mtaji wa Serikali kwenye uwekezaji huo. Uwekezaji huo ndani ya Mashirika ya Umma ni kama vile Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), Shirika la Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASCO) na Twiga Bancorp umekabiliwa na uhaba mkubwa wa mtaji na kuwafanya washindwe kujiendesha bila ruzuku ya Serikali. Ijapokuwa kinacho sababisha hali ya sasa kinaweza kushughulikiwa, lakini umuhimu

wa kimkakati kwa nchi ni jambo lisilopingika. Hivyo, uwezeshwaji wa kifedha kutoka Serikalini unahitajika.

Pia, nilibaini kuwa Msajili wa Hazina alitoa taarifa ya madeni kiasi cha Shilingi bilioni 674.95 ambayo alikuwa akiyahudumia Kupitia mfuko mkuu wa Serikali; ingawa, hata hivyo, yalimuongezea msajili mzigo. Madeni hayo ni pamoja na dhamana zilizokwisha muda wake kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni 139.9, deni la Shilingi bilioni 473.4 kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) na madeni mengine ya Shilingi bilioni 61.7.

(viii) **Pensheni**

Wakati wa upitiaji wa malipo ya uzeeni na uwasilishaji wa makato ya kisheria, nimebaini waajiri, ikiwemo Hazina, wanachelewa kuwasilisha michango ya pensheni kwenye Mifuko husika ya hifadhi ya jamii. Ucheleweshaji umetofautiana kutoka miezi miwili mpaka 12 ambapo ni kinyume na sheria za pensheni. Kutokuwasilisha michango ya pensheni huchelewesha uandaaji wa malipo ya uzeeni ya wastaafu; pia huongeza gharama kwa Serikali kupitia tozo ya adhabu. Kwa mwaka huu pekee, Serikali imelipa tozo ya adhabu kiasi cha jumla ya Shilingi 52,826,519,506. Kwa maoni yangu, tozo hii ya adhabu iliyotozwa kwa Serikali na usumbufu usio wa lazima kwa wastaafu vingeweza kuepukika iwapo waajiri wangewasilisha michango kwa wakati.

(ix) **Mamlaka ya Mapato Tanzania**

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2015, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya kiasi cha Shilingi bilioni 10,744 kati ya makisio yaliyowekwa ya Shilingi bilioni 12,078. Hivyo, kuwa na upungufu wa ukusanyaji kwa kiasi cha Shilingi bilioni 1,334 ikiwa ni sawa na asilimia 11

ya makisio yaliyokusudiwa. Kwa wastani wa miaka mitano iliyopita, Mamlaka ya Mapato imekuwa ikikusanya pungufu ya makisio kwa asilimia nne isipokuwa kwa mwaka 2011/12. Yafuatayo ni mapungufu mbalimbali yanayohitaji jitihada za Serikali katika kuboresha ukusanyaji wa mapato na kufikia malengo iliyojiwekea:

(a) **Usimamizi wa misamaha ya kodi**

Taarifa ya makusanyo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka ulioishia 30 Juni 2015 ilionesha kiasi cha misamaha ya kodi iliyotolewa kuwa ni Shilingi bilioni 1,627 sawa na asimilia 2 ya pato la ndani la Taifa. Kiwango hicho bado kipo juu ikilinganishwa na lengo la Serikali la kupunguza misamaha hiyo kufikia asilimia 1 ya pato la ndani la Taifa.

(b) **Usimamizi wa pingamizi za makadirio ya kodi**

i. Kesi za muda mrefu katika bodi za rufaa ya kodi na Mahakama ya rufaa Tanzania za Shilingi bilioni 6,850. Hii imechangiwa na upungufu wa fedha katika bodi za rufaa na mahakama pamoja na udhaifu katika mfumo wa kushughulikia kesi hizi ikiwemo upungufu wa wataalamu wa kutosha katika bodi za rufaa ya kodi na mahakama.

ii. Taarifa za pingamizi za kodi zenye thamani ya Shilingi 580,718,607,384 hazikufanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi na Kamishna wa Mapato Tanzania mpaka tarehe 30 Juni 2015.

iii. Mamlaka ilishindwa kukusanya amana ya kiasi cha Shilingi 191,935,854,277 kinyume na kifungu cha 12 (3) cha Sheria ya Rufaa ya Mapato ya Kodi ya mwaka 2000 (Iliyorekebishwa mwaka 2006).

(c) **Usimamizi wa ukusanyaji kodi**

i. Upungufu katika usimamizi wa bidhaa zilizopo kwenye maghala na ghala za forodha za Serikali

umesababisha kukaa kwa bidhaa hizo katika maghala kwa muda mrefu kinyume na sheria ya usimamizi wa forodha kwa nchi za Afrika Mashariki zenye kodi ya thamani ya Shilingi 110,587,418,377.

**ii.** Bidhaa zenye ushuru wa forodha wenye thamani ya Shilingi 9,151,090,597 zilipelekwa kuhifadhiwa kwenye maghala kwa ajili ya kusafirishwa nje ya nchi pasipo kutozwa ushuru huo. Hata hivyo, zilionekana kuwa zimesafirishwa lakini ushahidi wa usafirishaji huo haukutolewa wakati wa ukaguzi wangu. Bidhaa huenda ziliuzwa ndani ya nchi bila kulipiwa kodi.

**iii.** Miamala 488 ya mafuta na mizigo katika bandari kavu yenye ushuru wa forodha wa Shilingi 88,667,175,447 iliyosafirishwa kwenda Uganda, Burundi na Rwanda kupitia mipaka ya Rusumo, Kabanga na Mutukula haikua na ushahidi katika muundo wa rejesta au kwenye mfumo wa kuthibitisha utokaji wake. Wakati mwingine, mfumo wa forodha (TANCIS) ulionyesha mafuta yaliyokuwa yakisafirishwa nje ya nchi kupitia hapa nchini (Transit fuel). Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi wa kuthibitisha utokaji wa mafuta hayo na maofisa wa forodha. Kiasi cha dhamana katika mafuta hayo ni Shilingi 5,774,263,079.

**iv.** Uchambuziwataarifa51katikamfumowaAsycuda++ za makampuni 8 ulionyesha dhamana zilizofutwa baada ya muda ulioruhusiwa kisheria. Hata hivyo, Mamlaka ya Mapato haikukusanya tozo ya Shilingi 1,933,580,588 kutokana na ucheleweshwaji huo. Aidha, riba ya Shilingi 47,005,629 haikukusanywa kwa makampuni yaliyochelewa kulipa ushuru wa forodha kwa bidhaa za mafuta ya petroli yaliyotakiwa kusafirishwa nje ya nchi kati ya siku mbili (2) mpaka 266 kinyume na kifungu Na. 249 cha sheria ya Usimamizi wa kodi ya forodha ya nchi za Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

v. Usuluhishi wa kiwango cha mafuta yaliyoagizwa nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na kilichotumiwa kwa matumizi mbalimbali (ikiwemo matumizi ya ndani ya nchi, kinachosamehewa kodi na kinachosafirishwa nje ya nchi) ulionyesha utofauti wa lita 123,427,592 zenye kodi ya Shilingi 9,463,254,714. Kati ya hizo, lita 113,531,317 zilibainika na kulipiwa kodi ya kiasi cha Shilingi 3,688,991,635 na kuacha kiasi cha lita 9,896,274 zenye kodi ya thamani ya Shilingi 5,774,263,079 ambazo hazikulipiwa ushuru wa forodha husika.

(x) **Deni la Taifa**

Deni la Taifa kufikia tarehe 30 Juni, 2015 lilikuwa Shilingi bilioni 33,539.8 ambapo deni la ndani lilikua Shilingi bilioni 7,990 na deni la nje bilioni 25,549.8 ikiwa ni ongezeko la bilioni 7,052.4 sawa na asilimia 27 ikilinganishwa na deni la Shilingi bilioni 26,487.4 lililoripotiwa Juni 30, 2014.

Deni la taifa limekuwa likiendelea kukua kwa kasi kila mwaka ikilinganishwa na deni lililoripotiwa mwaka wa fedha 2006/7. Sababu mbalimbali za kuongezeka kwa deni ni pamoja na mikopo mipya ya masharti nafuu na isiyo na masharti nafuu kugharimia miradi ya maendeleo, kuwapo kwa nakisi ya bajeti, kuhudumia majukumu ya serikali. Hasara zinazotokana na mbadilishano wa fedha na fedha za kigeni kutokana na kushuka kwa thamani ya Shilingi ikilinganishwa na fedha za kigeni ni sababu mojawapo ya deni.

Bila shaka, ongezeko la mikopo isiyo ya masharti nafuu na ongezeko la deni la ndani hufanya gharama ya kukopa kuwa juu. Pia, gharama za uzalishaji wa mapato ya ndani pia zimekuwa juu. Uchambuzi wangu unaonyesha kuwa malipo ya kugharamia madeni ya kiasi cha Shilingi bilioni 4,596.8 mwaka huu ni sawa na asilimia 46 ya makusanyo ya serikali ya ndani ya Shilingi bilioni 10,062.8. Gharama

hizo zikichanganywa na gharama nyingine kama vile mishahara ya wafanyakazi na likizo, serikali hubaki na kiasi kidogo cha fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na huduma nyingine za kijamii. Hii ni sambamba na tahadhari iliyotolewa na Wizara ya Fedha yenyewe katika mwongozo wa hivi karibuni wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2016/17 uliotolewa mwezi Januari 2016.

Kwa maoni yangu, kiasi kikubwa cha rasilimali kinatumika kulipia deni la Taifa ,na hii ni ishara kuwa Serikali itaendelea kutegemea mikopo ili kugharimia miradi ya maendeleo kama mapato ya ndani hayatasimamiwa kwa umakini. Kwa msingi huu, ongezeko la madeni yasiyo na masharti nafuu na deni la ndani ni kiashiria kwa watunga sera kutafuta njia mbadala za kusaidia kupunguza deni.

**(xi) Tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani**

Menejimenti ina wajibu wa kuanzisha na kusimamia mifumo wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kunakuwa na uzingatiwaji wa sheria, kanuni na mikataba katika mambo yanayohusiana na Serikali Kuu. Ukaguzi wangu katika mifumo ya udhibiti wa ndani ulijikita katika utendaji na majukumu ya Kamati za Ukaguzi, Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani, udhibiti wa tekinologia ya habari, mapitio ya vihatarishi pamoja na kuzuia udanganyifu. Nilibaini kuwa, kamati za Ukaguzi, Vitengo vya ukaguzi wa Ndani, udhibiti wa tekinolojia ya habari, mapitio ya vihatarishi pamoja na kuzuia udanganyifu vilifanya kazi chini ya kiwango. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya sita.

**(xii) Udhaifu katika Usimamizi wa rasilimali watu na taarifa za Mishahara**

Kama nilivyoripoti kwenye taarifa zangu za miaka ya nyuma, Wizara, Idara na Wakala pamoja na

Sekretarieti za Mikoa kumeendelea kuwa na udhaifu katika usimamizi wa rasilimali watu na taarifa za mishahara kama yalivyoainishwa hapa chini;

a) Kutokuwa na ushirikiano rasmi wa ki-mfumo kati ya Taasisi za Serikali, Bodi ya Mikopo ya elimu ya juu na wanufaika wa mikopo ambao ni waajiriwa wa taasisi za Serikali, imesababisha kutofanywa kwa makato kwenye mishahara kwa ajili ya kulipia madeni yao Bodi ya Mikopo.
b) Mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao hawapo kazini imeongezeka kutoka Shilingi 141,387,963 mwaka 2013/14 hadi kufikia Shilingi 392,651,036 mwaka 2014/15. Pia, kiasi cha Shilingi 61,477,664 zililipwa kwa Taasisi mbalimbali kama makato ya kisheria katika mishahara iliyolipwa kwa watumishi ambao hawapo kazini.
c) Baadhi ya Taasisi zilizokaguliwa zilikosa uthibitisho wa kupima utendaji wa watumishi wake (OPRAS) kama inavyotakiwa.
d) Kiasi cha Shilingi 707,169,904 za makato ya kisheria hazikuwa na uthibitisho wa kuwasilishwa fedha hizo kwa Taasisi husika.
e) Baadhi ya Taasisi hazikukata kodi ya mapato (PAYE) kutoka katika malipo ya kukaimu, kinyume na matakwa ya sheria ya kodi ya mapato ya mwaka 2004 (marekebisho 2008)
f) Mishahara ambayo haikulipwa kwa watumishi waliofukuzwa ya Shilingi 2,233,475,668 haikurudishwa Hazina.
g) Nilibaini mtumishi aliyestaafu kwenye ofisi ya ubalozi lakini bado yupo kazini bila kuwapo kwa mkataba. Vilevile, kuna watumishi waliokaa katika Balozi za nje ya nchi kwa kipindi cha miaka mitatu hadi mitano zaidi ya matakwa ya sheria.

Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya saba.

**(xiii) Mapungufu katika Utendaji wa Wakala za Serikali**

Sura ya nane inaelezea mapungufu mbalimbali yaliyojitokeza kwenye wakala, mifuko maalumu na taasisi nyinginezo za serikali. Mapungufu yaliyojitokeza yanajumuisha yafuatayo:

a) Ukaguzi unaonesha kuwa mapungufu yameendelea kuwapo katika kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi, hivyo kuwapo kwa usimamizi mbovu wa mikataba. Ukaguzi ulibaini kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi kama vile mabadiliko ya mikataba kutoidhinishwa na Bodi za Zabuni, ununuzi wa kivuko chenye hitilafu, ununuzi wa mabasi ya mwendo kasi zaidi ya mahitaji (DART), Kuchelewa kuanza kwa huduma ya mabasi ya mwendo kasi (DART), Magari yaliyolipiwa/nunuliwa ambayo hayajapokelewa kwa mda mrefu, manunuzi yaliyofanywa nje ya wazabuni waliothibitishwa na kuingia mikataba isiyokuwa na kikomo cha muda wa utekelezaji. Yote haya yanamaanisha kutokuwapo kwa uthibiti wa kutosha katika usimamizi wa manunuzi na mikataba.

b) Kulingana na mikataba niliyoikagua, malipo yanatakiwa kufanyika ndani ya siku 28 baada ya kuidhinishwa kwa hati ya malipo. Hata hivyo, kuna ucheleweshwaji wa malipo hadi kufikia siku 100 kuanzia siku hati ya malipo inapoidhinishwa. Kutokana na hali hiyo, TANROAD imedaiwa Shilingi 5,616,652,050 kutokana na riba ya ucheleweshaji wa malipo yaliyoidhinishwa; RITA kuna ongezeko la riba ya mkopo ya asilimia 15 hadi kufikia riba ya Shilingi 12,723,218,833 inayohusu ujenzi wa jengo la RITA.

c) Katika usimamizi wa mapato, nilibaini kuwa Wakala wa Majengo (TBA) imeshindwa kukusanya kiasi cha Shilingi 214,748,556 za mauzo ya nyumba. Pia, nilibaini kuwapo kwa udhaifu katika kupeleka mapato benki.

d) Nilibaini kiasi cha Shilingi 556,845,253.68 kimelipwa kwa wazabuni mbalimbali bila kuwapo

risiti za kielektroniki (EFD), malipo ya kodi ya zuio (withholding tax), pamoja na hasara iliyotokana na kutonunuliwa kwa kalenda na vitabu vya kumbukumbu za kila siku.

e) Pia, nilibaini kuwa fedha za matumizi ya kawaida pamoja na za maendeleo hupelekwa pungufu ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa, hivyo kuathiri utendaji katika kufikia malengo yaliyokusudiwa. Utegemezi kwa Serikali Kuu bado ni changamoto ikizingatiwa kuwa zaidi ya asilimia 90 ya wakala wa serikali wanategemea ruzuku kutoka Serikali Kuu.



**(xiv) Ukaguzi wa Vyama vya Siasa**

Kati ya vyama vya siasa 22 vyenye usajili wa kudumu, ni chama kimoja tu kilicholeta hesabu zake za kipindi cha miezi sita, kwa kipindi kinachoanzia Januari mpaka Juni, 2015. Vyama vingine 21 havikuleta vitabu vya hesabu kwa ajili ya ukaguzi kinyume na Kifungu 14 cha Sheria ya Vyama vya Siasa Na.5 ya 1992, Kifungu 25 (2) cha Sheria ya Fedha za Umma ya 2001 (marekebisho 2004) na Kanuni Na.71 Kanuni ya Ukaguzi wa Umma ya 2009. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya nane.

**(xv) Mapungufu katika Manunuzi na usimamizi wa mikataba**

Mapungufu yaliyobainishwa katika ripoti ya mwaka huu, yanajumuisha haya yafuatayo;

a) Vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Shilingi 827,046,942 vilinunuliwa zaidi ya mahitaji katika kipindi cha kuandikisha wapiga Kura kwenye daftari la kudumu, mpaka ukaguzi unafanyika vifaa vilikuwa bado havijatumika na muda wa mahitaji yake ulishapita.

b) Ununuzi wa huduma za uchapishaji inayofikia Shilingi 6,000,000,000 kuhusiana na vitabu vya katiba iliyopendekezwa kuwa na dosari kutokana

na kutofuata sheria za manunuzi. Mbali na hivyo nakala 158,003 za vitabu vya katiba iliyopendekezwa vilikuwa bado haijagawanywa kwa walengwa kwa madhumuni ya kuhamasisha umma juu ya kura ya maoni kwa Katiba inayopendekezwa.

c) Utekelezaji usioridhisha wa Mpango wa Mwaka wa Manunuzi, nilibaini Taasisi saba (7) zilifanya manunuzi yaliyofikia Shilingi 8,462,110,917 ambayo hayakuwa kwenye mpango kinyume na Kifungu 49(2) na (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011;

d) Manunuzi yenye thamani ya Shilingi 494,395,890 yalifanyika bila kuwa na idhini ya Bodi ya Manunuzi kinyume na Kanuni 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

e) Manunuzi yenye thamani ya Shilingi 27,121,224,071 yaliyofanyika bila kushindanisha wazabuni yalihusisha Taasisi nane, kinyume na Kanuni 163 na 164 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

f) Bidhaa na huduma zenye thamani ya Shilingi 15,361,328,135 zilinunuliwa katika taasisi (16) bila kuwapo ukaguzi wakati wa mapokezi, kinyume na Kanuni 244 na 245 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

g) Manunuzi ya bidhaa na huduma bila mikataba yenye thamani ya Shilingi 5,213,539,256 ilibainika katika taasisi tano, kinyume na Kanuni 10(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

h) Pia, bidhaa na huduma zenye thamani ya Shilingi 8,556,822,718 zilinunuliwa kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa katika taasisi 16, kinyume na Kanuni 131(5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013.

i) Nilibaini bidhaa na huduma zilizolipiwa kiasi cha Shilingi 3,253,650,189.09 ambazo hazijapokelewa wala huduma kutolewa katika taasisi nne.

j) Ukaguzi pia ulibaini baadhi ya Taasisi hazikusimamia kwa umakini mikataba mbalimbali iliyoingiwa na wakandarasi mbalimbali. Mapungufu yalichangia ucheleweshwaji wa ukamilishaji wa miradi mbalimbali, na miradi kuwa chini ya kiwango. Taasisi zenye mapungufu zinajumuisha Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na matengenezo ya majengo ya UBalozi kama vile Maputo Msumbuji na New York.

Nje ya ukaguzi wangu, nimejumuisha matokeo ya ukaguzi uliofanywa na Mamlaka ya Uthibiti wa Manunuzi ya Umma na Kungenzi ya Usimamizi wa Mali za Serikali (ripoti ya Mhakiki Mali). Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya tisa.

**(xvi) Mapungufu katika usimamizi wa Matumizi**

Katika mwaka huu wa fedha nimebaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa matumizi ya fedha za serikali katika maeneo yafuatayo: Malipo yaliyofanyika bila ya viambatisho vya kutosha (Kwa mfano, Hati za malipo hazikupatikana wakati wa ukaguzi, Risiti za kielectroniki hazikuambatanishwa na Malipo yasiyoambatanishwa na risiti) Shilingi 18.081 bilioni. Malipo yaliyofanyika kwenye vifungu visivyostahili Shilingi 887.012 milioni. Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti yenye thamani ya Shilingi 1.298 bilioni. Masurufu ya muda mrefu yasiyorejeshwa Shilingi 232.695 milioni, Malipo yaliziyozidi kiwango stahiki Shilingi 373.842 milioni; Malipo yasiokuwa na manufaa Shilingi 53.017 bilioni, Malipo yaliofanywa kwa kazi zisizokusudiwa Shilingi 1.788 bilioni; kodi ya zuio ambayo haijakatwa Shilingi 692.539 milioni. Mapungufu haya yameelezewa kwa kina kwenye sura ya kumi.

(xvii) **Mapungufu ya Usimamizi wa Mali**

Usimamizi wa mali za umma unajumuisha, utaratibu, mfumo mzima wa usimamiaji wa utumiaji wa Mali za Kudumu. Mapungufu yaliyobainika yameelezewa hapa chini:

a) Kuwapo kwa Rejista ya mali za kudumu isiyo timilifu kwenye taasisi 53,

b) kuchelewa kwa kazi ya kuzitambua na kuthamini Mali za Kudumu; katika Taasisi nyingi Mali za Kudumu; hazionyeshi thamani halisi;

c) Baadhi ya nyumba katika Balozi za Tanzania nje ya nchi ziko katika hali mbaya zinahitaji matengenezo, pia Balozi nne zina viwanja ambavyo havijaendelezwa;

d) Taasisi 14 zilizokaguliwa zimebainika kuwa na vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuingizwa katika vitabu vya stoo Sh.4,380,960,319;

e) Ukosefu wa Sera ya kiuhasibu ya kusimamia mali za kudumu inayoendana na mfumo mpya wa uandaaji wa taarifa za fedha katika taasisi za umma;

f) Ofisi za ubalozi nje ya Nchi kutotumia Mfumo funganifu wa Usimamizi wa Fedha -Epicor;

g) Taasisi 12 wanamiliki Ardhi bila kuwa na Hati Miliki na;

h) Ilibainika kuwa Jeshi la Zimamoto halina magari ya zimamoto ya kutosha, magari yaliyopo ni 55 wakati yanayohitajika ni 157. Pia, vifaa vya kuzima moto vilivyoko kwenye majengo ya Serikali havifanyiwi matengenezo katika baadhi ya Taasisi.

**(xviii) Mapungufu katika usimamizi wa madeni**

Nilibaini limbikizo la madeni katika Taasisi 91 ikijumuisha Wizara/Idara 52, Sekretarieti za Mikoa 25 na Balozi 14 ambazo zilikuwa na madeni ya kiasi cha Shilingi bilioni 1,443.859; kukiwa na ongezeko la Shilingi bilioni 671.351 sawa na asilimia 89 ikilinganishwa na mwaka uliopita ulioishia 30/6/2014 uliokuwa na madeni yaliyofikia Shilingi bilioni 772.508. Nilibaini malipo ambayo hayakuwapo kwenye bajeti wala kwenye orodha ya madeni ya mwaka uliopita. Hii imesababisha kuongezeka kwa limbikizo la madeni kwa sababu madeni ya miaka ya nyuma yanalipwa kwa kutumia bajeti ya mwaka mwingine.

Deni lililoonyeshwa linajumuisha kiasi cha TZS.27,800,677,740 zikiwa ni deni linalotokana na gharama ya wagonjwa wanaotibiwa katika hospitali za rufaa nchini India.

Kama madeni ya Shilingi 1,443,859,273,539.30 yangelipwa katika mwaka wa fedha 2014/15, kungekuwa na matumizi ya ziada katika matumizi ya kawaida.

Mbali na hilo kulikuwa na kesi 94 katika taasisi 11 dhidi ya makampuni na watu mbalimbali zenye jumla ya kiasi cha Shilingi 870,866,104,235 zilizokuwa zinasubiri maamuzi ya mahakama wakati ambapo kesi nyingine zilikuwa zina zaidi ya miaka kumi; na hakukuwa na taarifa za mahakama juu ya tarehe za kusikilizwa. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya kumi na moja.

**(xix) Kaguzi Maalumu**

Ulifanyika ukaguzi maalumu Wizara ya Elimu na Mafunzo, ukihusisha kufanya uhakiki wa fedha zilizotumwa kwenda taasisi zingine kutokea

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ilibainika kuwa kiasi cha Shilingi 476,820,735 zilizoripotiwa kutumwa kwenda Taasisi zilizoko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi hazikuthibitishwa matumizi yake.

Ukaguzi maalumu mwingine ulifanyika kuhusu Taarifa za Fedha za Mpango wa Maboresho wa Serikali za Mitaa Awamu II kwa mwaka ulioishia 30 Juni, 2013. Ilibainika kwamba kuna ukosefu wa uwajibikaji katika matumizi yasiyokuwa matumizi yasiokuwa kwenye bajeti, matumizi yaliyokosa nyaraka, pamoja na matumizi yasiyostahili yaliyofikia Shilingi 988,133,904. Matumizi mengine hayakuhusiana na programu husika hivyo kusababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Mapungufu mengine yaliyobainika ni kukosa uwajibikaji wa malipo ya awali ya Shilingi 903,270,394 malipo yasiyohusiana na programu Shilingi 13,040,075; malipo yasiyofuata taratibu ya posho ya mafunzo Shilingi 18,967,500. Mengine ni Malipo ya likizo, mda wa ziada, mawasiliano na posho ya vikao Shilingi 31,762,360, malipo yaliyofanywa nje ya bajeti pamoja na malipo yasiyokuwa na nyaraka Shilingi 21,093,575. Taarifa hizi zimeelezwa kwa kina katika sura ya kumi na mbili.

**(xx) Masuala mengine juu ya utekelezaji wa Sera ya Mambo ya nje na Diplomasia ya Uchumi**

Tathmini yangu alibaini changamoto kadhaa kama zilivyoainishwa; ambazo serikali inatakiwa ifanyie kazi ili kufikia ufanisi na ubora wa kazi za maBalozi nje ya Nchi. Wakati huo huo, watatakiwa kufuata sheria na miongozo ikiwa ni pamoja na ile inayotolewa na Rais. Moja ya changamoto ni kwamba, Ofisi za kidiplomasia bado hazina wafanyakazi wenye ujuzi mahususi wa kutekeleza miongozo ya Rais kutokana na ufinyu ya rasilimali

watu na fedha. Aidha, nilibaini kuwepo kwa ukosefu wa uratibu na mawasiliano na wizara. Ilibainika kwamba, hakuna uratibu uliopo kati ya Wizara ya Mambo Ya Nje na Wizara nyingine ili kuhakikisha upatikanaji wa taarifa, hatimaye kuchukua hatua zinayofaa kwa pamoja na kupanga mkakati wa pamoja.

**(xxi) Muhtasari wa Mapendekezo**

Nina mapendekezo yafuatayo ili kuboresha matumizi ya rasilimali za taifa na utoaji wa huduma bora kwa jamii:

**a) Utekelezaji wa mapendekezo ya kaguzi zilizopita**

Serikali, kupitia Mlipaji Mkuu na Maafisa Masuuli wa taasisi husika, inashauriwa kuweka bidii ya kutosha ili kufanyia kazi mapendekezo na maelekezo ya Kamati za Bunge yaliyotolewa.

Mlipaji Mkuu anashauriwa kuendelea kuwataka Maafisa Masuuli hatua katika kuboresha mifumo ya ndani ikizingatiwa kuwa mapu wachukue ngufu yaliyojitokeza yamesababishwa na mifumo dhaifu inayosababisha kushindwa kujibu baadhi ya hoja za ukaguzi.

Maafisa Masuuli wanashauriwa kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**b) Usimamizi wa Fedha za Umma**

Kasi ya makusanyo ya mapato ya ndani ni ya kuridhisha, na kwamba, changamoto zitashughulikiwa kuanzia mwaka wa fedha ujao. Changamoto hizo kama vile kupunguza bajeti, kutoa fedha katika kipindi cha mwisho wa mwaka na kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato. Hatimaye malengo ya uendeshaji na mikakati ya taifa kwa ujumla itafikiwa; mikopo

ya ndani itapungua kwa kiasi kikubwa pamoja na kutokuwapo kwa matumizi ambayo hayalipiwi kwa sababu fedha zitatolewa kulingana na bajeti zilivyoidhinishwa.

Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba, shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kwa mujibu wa ratiba. Ili kupunguza utegemezi katika misaada ya nje kwa ajili ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya taifa, serikali inashauriwa itafute vyanzo mbadala vya ndani ili kuongeza mapato.

c) **Pensheni**

Naishauri serikali kuwasilisha makato ya kisheria kwenye Mifuko ya Pensheni kwa wakati kwa kuzingatia sheriaza Mifuko ya Pensheni ili kuepukana na adhabu isiyo ya lazima. Kufanya hivyo kutaongeza ukwasi wa Mifuko, hivyo kuwezesha wanufaika wa Mifuko wa pensheni kulipwa kwa wakati.

d) **Msajili wa Hazina**

Napenda kusisitiza mapendekezo yangu yafuatayo kwa Serikali: (a) Kuanzisha mfuko wa uwekezaji na (b) Kuanzisha mfuko wa kuhifadhi fedha ambao utatumika kwa ajili ya kukusanya fedha (c) Kuharakisha utoaji wa hati fungani zisizo za fedha kwa ajili ya majukumu ya pensheni na dhamana zilizoshindwa kulipwa ili kuyawezesha madeni hayo kuingizwa kwenye deni la Taifa.

e) **Mamlaka ya Mapato Tanzania**

i. Serikali iweke mkazo katika usimamizi wa misamaha ya kodi na marejesho yatokanayo na kodi na kuimarisha ukaguzi na uendeshaji wa misamaha na marejesho yatokanayo na kodi ili kupunguza wadai hewa katika mtandao wa walipa kodi ya ongezeko la thamani, yaani VAT. Aidha, Serikali iendelee kupitia sera na kanuni za misamaha na marejesho ya kodi ili

kuimarisha maeneo hayo.

ii. Serikali itoe msamaha au kupunguza kiasi cha riba na tozo kwa wafanyabiashara watakaoweka wazi madeni yao, pia kuwapa nafasi ya kulipa kwa awamu ili kuwawezesha kumaliza madeni na kuokoa mapato ya Serikali.

iii. Serikali iharakishe usikilizwaji wa pingamizi za kodi za mda mrefu katika bodi za rufaa za kodi na mahakama ya rufaa ya Tanzania kuwezesha ukusanyaji wa kodi kwa wakati.

iv. Serikali iimarishe kaguzi na pelelezi za walipa kodi ili kuweza kubaini ukwepaji wa kodi; pia ichukue hatua kali katika kukusanya kodi zilizobainika.

v. Serikali iimarishe uendeshaji na usimamizi wa utoaji wa mizigo na mafuta yanayoingizwa nchini kwa matumizi ya ndani au kusafirishwa kwenda nje ya nchi, kuzuia kuuzwa katika soko la ndani bila kulipiwa ushuru wa forodha stahiki. Aidha, iimarishe ukusanyaji wa kodi kwa haraka endapo bidhaa hizo zitagundulika kuuzwa katika soko la ndani kinyume na sheria.

**f) Deni la Taifa**

Napendekeza yafuatayo kwa Serikali: (a) Kuongeza jitihada za ndani za kuhamasisha ukusanyaji wa mapato ya kujenga wigo mpana wa kulipa madeni kwa kuweka mkakati wa kulipa na (b) Kuweka mpango maalum wa kimkakati kuhusu fedha ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama na kuongeza mikopo yenye masharti nafuu, pamoja na kuratibu vizuri shughuli za fedha za kigeni hapa nchini.

**g) Udhibiti wa ndani**

Maafisa Masuuli wanawajibika kuanzisha Mifumo ya Udhibiti wa Ndani kama vile kusimamia uendeshaji wa shughuli na kufanya mabadiliko yanapohitajika. Huu ni mchakato endelevu wa

kulenga kuimarisha udhibiti wa ndani ili kuboresha utoaji wa huduma kwa umma.

Hatua zaidi kutoka serikalini zinahitajika katika kuhakikisha kuwa Taasisi zote zinakuwa na mfumo imara wa udhibiti wa ndani ili kutimiza kwa ufanisi majukumu yao ya kisheria.

h) **Usimamizi wa rasilimali watu na taarifa za Mishahara**

Serikali inapaswa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani ili kuhakikisha kwamba, orodha ya malipo ya mishahara inahakikiwa, makato ya kisheria yanawasilishwa kwa wakati, na kwamba, wote wanaolipwa posho ya kukaimu wanakatwa kodi ya mapato (PAYE). Kiasi cha malipo ya mishahara kwa wafanyakazi hewa kirudishwe. Aidha, nashauri Maafisa Masuuli waiarifu Tume ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) juu ya ajira ya wanufaika na wahakikishe makato yanafanyika kutoka katika mishahara yao na kuiwasilisha bodi. Vile vile, wafanye tathmini ya utendaji wa wafanyakazi mara kwa mara kulingana na kanuni za utumishi wa umma.

(xxii) **Wakala wa Serikali, mifuko maalumu na taasisi nyingine**

Nashauri kuwa wakala za serikali, taasisi za serikali na Mifuko wafuate sheria na kanuni kama vile Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake, Kanuni 24 ya EFD kanuni ya 2012, Kodi ya Mapato ya mwaka 2006, Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake na masharti ya mkataba. Kwa mfano, kivuko kilichonunuliwa bila kukidhi viwango, nashauri uongozi wa Taasisi husika kuwasiliana na wasambazaji kwa ajili ya kufanya marekebisho yote yaliyobainiwa na Kamati ya Kupokea na Kukagua Bidhaa ikiwa ni pamoja na kasi ya kiwango cha chini na juu; hatimaye, watoe Cheti

cha Kukubalika Bidhaa ili kivuko kiweze kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ninatoa wito kwa wasimamizi wa mradi wa mabasi yaendayo kasi (DART) kupitia mkataba kwa haraka ili huduma ya usafiri wa mabasi ya haraka ianze; na kuhakikisha kwamba, mabasi ya ziada yanajumuishwa na kusimamiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Pia, nashauri Wakala ziwezeshwe ili ziweze kujimudu kikamilifu kwa kutegemea vyanzo vyao vya mapato badala ya kutegemea Serikali Kuu katika kugharamia shughuli zao.

Kwenye ucheleweshwaji wa ulipwaji wa mikopo katika uuzaji wa majengo ya serikali, nashauri TBA ichukue hatua za kisheria dhidi ya wadaiwa sugu ili kuhakikisha madeni hayo yanakusanywa bila ucheleweshwaji zaidi.

TANROADs na RITA nashauri wafuatilie kwa karibu Wizara ya Fedha juu ya upatikanaji wa fedha za kukamilisha mradi.

a) **Mapungufu katika Manunuzi na Usimamizi wa mikataba**

Natoa ushauri kwa menejimenti na Taasisi za Serikali Kuu kwa kuhakikisha zinaifuata kikamilifu Sheria ya Manunuzi, hasa katika kuhakikisha kuandaa na kuutekeleza mpango wa manunuzi wa mwaka, kupata idhini ya Bodi ya Manunuzi, kuhakikisha manunuzi yanafanyika kwa idhini ya bodi ya zabuni, Vifaa na bidhaa vinafanyiwa ukaguzi kabla ya kupokelewa, na kufanya manunuzi kutoka kwa wazabuni walioidhinishwa. Maafisa Masuuli wa Taasisi za Serikali Kuu wanapaswa kuhakikisha kuwa Vitengo vya Manunuzi (PMUs) na Bodi za Manunuzi (TBs) zinaundwa kwa ukamilifu ili

kutekeleza majukumu yake kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake. Kwa upande wa kuchelewa kuanza na kukamilika kwa mikataba, nashauri uongozi wa Taasisi za Serikali Kuu ichunguze sheria na masharti katika mikataba husika na kuhakikisha wanaoshindwa kutimiza masharti ya mikataba yao wanashtakiwa kwa kushindwa masharti ya mikataba.

b) **Mapungufu katika usimamizi wa Matumizi**
Bila ya kuwapo kwa kumbukumbu na nyaraka sahihi, malipo yaliyofanyika bila kuwa na viambatisho vya kutosha hayawezi kuthibitika kuwa sahihi; hivyo, fedha za umma zinaweza kutumika bila utaratibu wa sheria na kwa njia bora. Bodi za Ushauri za Wizara za mashirika husika na Maafisa Masuuli wa Taasisi wanatakiwa waimarishe udhibiti wao wa ndani ili kuhakikisha kwamba, shughuli za usimamizi wa matumizi zinafuata Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake.

c) **Mapungufu katika Usimamizi wa Mali**
Ni matumaini yangu kwamba, Serikali inatekeleza kikamilifu mfumo mpya wa kuandaa taarifa za fedha katika sekta ya umma (IPSAS Accrual) kama ilivyoainishwa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Hesabu za Umma. Serikali inashauriwa kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji katika kuhakikisha kuwa maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Fedha yanatekelezwa na Taasisi zote. Maelekezo hayo yanahusu vipengele kama vile mpango wa utekelezaji wa mfumo mpya katika kutengeneza Rejista ya Mali za Kudumu iliyotimilifu, kuwapo kwa mpango maalumu wa kukarabati majengo na kuendeleza viwanja vinavyomilikiwa na Balozi nje ya Nchi, kuandaa muongozo maalumu wa kuondoa Mali za Kudumu ambazo hazitengenezeki, pamoja na kuliwezesha Jeshi la Zimamoto kuwa na idadi ya magari ya zimamoto inayoridhisha. Taasisi

zinashauriwa kushuhulikia Hati Miliki za maeneo yao kutoka kwa Taasisi husika.

**d) Usimamizi wa Madeni**

Kutokana na ongezeko kubwa la madeni, ninapendekeza Serikali iyaingize kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16 madeni yote ili kuondoa uwezekano wa Serikali kuingia katika mogogoro na wazabuni pamoja na wadau wengine. Kama madai ya Shilingi bilioni 1,443.859 yangelipwa katika mwaka wa fedha 2014/15, Taasisi nyingi zingekuwa na matumizi ya ziada kwenye matumizi ya kawaida na yale ya maendeleo. Hii inamaanisha kwamba, fedha ziwe zinatolewa kwa jinsi zilivyoidhinishwa na Bunge.

Kwa kuzingatia mapendekezo yangu ya awali, Serikali inashauriwa kufanya mkazo kwenye kila Taasisi kuwa na mikakati ya usimamizi wa vihatarishi ili kuhakikisha hatari ya kuwa na madeni tarajiwa inapunguzwa.

**e) Kaguzi Maalumu na mambo Mengine**

Naishauri Serikali ihakikishe kuna udhibiti wa kutosha kwenye uhamishaji wa fedha kwenda kwenye Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Zaidi, napendekeza Afisa Masuuli kufuatilia fedha zinazohamishwa na kufanya marekebisho kwenye taarifa za hesabu za mwisho.

Nashauri wadau wa utekelezaji, wakishirikiana na wadau wa maendeleo, wafanye utafiti wa kina wa mapungufu yote yaliyobainika ili kuweza kuchukua hatua za kisheria na kinidhamu.

**f) Vyama vya Siasa**

Nashauri Afisa Masuuli, kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya Siasa washughulikie suala la

uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za fedha kwa wakati kulingana na matakwa ya kisheria.

g) **Masuala mengine juu ya utekelezaji wa Sera za Kigeni na Diplomasia ya Kiuchumi**

Napendekeza mgawanyo wa watumishi katika Balozi uzingatie ujuzi na maarifa unaohitajika katika biashara, uwekezaji, utalii na utawala wa uchumi ili kuhakikisha watumishi wana uwezo wa kutoa huduma inayohitajika. Zaidi, napendekeza watumishi waajiriwe ili kujaza nafasi zilizo wazi kwa muda stahiki

Napendekeza bajeti ya kutosha itengwe ili kuhakikisha Balozi zina uwezo wa kukidhi mahitaji yao ya kifedha. Pia fedha zitolewe kwa wakati ili kuziwezesha Balozi kulipa Ankara zao kwa wakati.

Napendekeza serikali zianzishe kitengo cha kuratibu taarifa za Nchi ambacho kitawajibika kikamilifu katika kuratibu na kuwasilisha taarifa mbalimbali za Nchi kwa Balozi husika.

## Sura ya Kwanza

### 1.0 Utangulizi

Sura hii inatoa taarifa ya jumla kuhusu mchakato wa ukaguzi, hitaji la kisheria la kufanya ukaguzi pamoja na mahusiano kati ya wakaguzi na wakaguliwa.

### 1.1 Mamlaka ya ukaguzi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali

Kwa mujibu wa Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (iliyofanyiwa marekebisho mara kwa mara) na Kifungu cha 5(c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndiye mkaguzi wa mapato yote ya Serikali na matumizi. Mamlaka yake Kisheria ni kama yalivyoainishwa katika jedwali Na.1 hapa chini.

**Jedwali 2: Mamlaka ya Kisheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

| Vigezo | Mamlaka |
|---|---|
| Ibara ya 143 (2) (C) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 | Inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kufanya ukaguzi na kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu za Serikali angalau mara moja kila mwaka kwa taarifa za fedha zilizoandaliwa na Maafisa Masuuli wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, Taarfifa za fedha za Mahakama zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na taarifa za fedha za Bunge. |

| Vigezo | Mamlaka |
|---|---|
| Ibara ya 143 (3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kila mtumishi wa Serikali aliyeruhusiwa na yeye atakuwa na haki ya kukagua vitabu, kumbukumbu,taarifa za akaunti, ripoti na hati nyinginezo zote zinazohusika na aina yoyote ya akaunti iliyotajwa katika ibara ndogo (2). |
| Kifungu Na. 5 (c) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11, 2008 | Mamlaka ya kikatiba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kukagua na kutoa taarifa za Ukaguzi juu ya Taarifa za Fedha za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yaani Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Mashirika ya Umma na Miradi ya wafadhili, Serikali za Mitaa , Mahakama na Bunge |

**Chanzo:** *Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977, Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008.*

## 1.2 Madhumuni ya Ukaguzi

Madhumuni ya kufanya ukaguzi ni kuniwezesha kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kutoa maoni huru ya ukaguzi kuhusiana na hesabu za Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka ya Mapato Tanzania na Hesabu Jumuifu za Taifa kwa mwaka ulioishia Juni 30, 2015. Pia, kuthibitisha kama taarifa za fedha zimetayarishwa kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika sekta ya Umma visivyo vya msingi wa taslimu (IPSAS accrual basis of accounting) vilevile kuhakiki iwapo sheria na Kanuni zimezingatiwa.

## 1.3 Mbinu za Ukaguzi

Ukaguzi huu ulijumuisha mapitio ya taarifa mbalimbali za uhasibu pamoja na taratibu nyingine ili kukidhi malengo ya ukaguzi. Taratibu zilizotumika ni kama ifuatavyo:

- Kupanga ukaguzi ili kutambua na kutathimini viashiria hatarishi iwapo vinatokana na udanganyifu au makosa kwa kuzingatia uelewa wa Taasisi inayokaguliwa na mazingira yake pamoja na tathimini ya uthibiti wa ndani;

- Kupata vielelezo stahiki na ushahidi wa ukaguzi ulio sahihi na unaojitosheleza juu ya usahihi au kukosekana kwa taarifa muhimu katika kutathimini viashiria hatarishi;

- Kutoa maoni huru ya ukaguzi juu ya taarifa za fedha kwa kuzingatia hitimisho la ushaidi wa ukaguzi uliopatikana na;

- Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Ukaguzi yaliyotolewa miaka ya nyuma pamoja na maagizo ya Kamati ya Fedha ya Kudumu ya Bunge ili kuhakikisha hatua stahiki zimechukuliwa juu ya masuala ya hoja husika

## 1.4 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi huu ulifanyika kwa kufanya tathmini ya ufanisi wa uhasibu na mifumo ya udhibiti wa ndani juu ya shughuli mbalimbali za Taasisi za Serikali Kuu. Ukaguzi ulifanywa kwa misingi ya sampuli, Kwa hiyo, matokeo ya ukaguzi huu, kwa kiasi kikubwa, yalitegemea kumbukumbu za taarifa na nyaraka zilizoombwa na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kama Mkaguzi, si jukumu langu la msingi hasa kutafuta udanganyifu, rushwa na makosa, hivyo basi, ukaguzi wangu hauwezi kutegemewa kufichua mambo yote hayo. Hata hivyo, ukaguzi wangu ulipangwa kwa njia ya kuweza kujiridhisha kwamba, kama kungekua na makosa makubwa katika taarifa za fedha yanayotokana na kukiukwa kwa taratibu ikiwa ni pamoja na udanganyifu ningeweza kuzibaini. Wajibu wa kuchunguza, kuzuia dosari na kuweka mifumo thabiti wa udhibiti wa ndani ni jukumu la Menejimenti ya Taasisi husika.

## 1.5 Viwango na taratibu za ukaguzi zilizotumika kutoa taarifa, Idadi ya Wakaguliwa na Muundo wa ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Sehemu hii inaeleza juu ya viwango na taratibu za ukaguzi zilizotumika wakati wa ukaguzi wa mwaka wa fedha 2014/2015 kwa taarifa za hesabu za Serikali Kuu pamoja na namna ya kuwasilisha ripoti za ukaguzi, idadi ya wakaguliwa na muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi .

### 1.5.1 Viwango vya Ukaguzi vilivyotumika

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni mwanachama wa Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI), Shirika la Asasi Kuu za Ukaguzi Afrika (AFROSAI), na Shirika la Asasi Kuu za Ukaguzi Afrika – Nchi zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E). Ushirikiano na Taasisi nyingine kuu za Ukaguzi (SAI) imewezesha Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kuwa na eneo kubwa la kujifunza na kubadilishana uzoefu na utaalamu wa ukaguzi katika sekta ya Umma.

Ukaguzi huu ulifanyika kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs)

viliyotolewa na Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (INTOSAI), ili kutoa uhakika kama Taarifa za Fedha ni sahihi na hazina makosa.

### 1.5.2 Taratibu zilizotumika kutoa taarifa

Hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na kufanya mawasiliano na Menejimenti ya wakaguliwa kabla ya kutoa ripoti hii ya mwaka. Kwa hiyo basi, ni vyema kubainisha hatua zote kwa watumiaji wa ripoti hii ili waweze kufahamu taratibu zinazotumika katika kukamilisha ripoti ya ukaguzi ya mwaka kwa hesabu za Serikali Kuu Taratibu hizo za ukaguzi ni kama zinavyoonekana katika **Kielelezo Na.2** hapo chini:

**Kielelezo 1: Utaratibu Ukaguzi kwa mwaka 2014/15**




*Chanzo: Taarifa za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2014/15*

### 1.5.3 Idadi ya wakaguliwa na muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Idadi ya wakaguliwa

Katika kipindi cha mwaka 2014/15 wakaguliwa 201 kati ya ndio waliokaguliwa,Wakaguliwa 209 chini ya Serikali Kuu walikaguliwa; wakaguliwa hawa wamechanganuliwa pamoja na asilimia zao ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na.2 na kielelezo Na.3 hapa chini

Jedwali 3: Idadi ya Wakaguliwa 2014/15

| Muundo na Idadi ya Wakaguliwa kwa mwaka wa Fedha | | |
|---|---|---|
| | **Jumla** | **Asilimia** |
| Mafungu (Wizara, idara) | 63 | 30 |
| Balozi | 34 | 16 |
| Wakala | 37 | 18 |
| Taasisi nyingine | 50 | 24 |
| Sekretareti za Mikoa | 25 | 12 |
| **Jumla** | 209 | |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi kwa mwaka wa fedha*

**Jedwali Na.3** hapo juu linalohusu idadi ya wakaguliwa linaweza kuonyeshwa kwa kwa mwaka wa fedha 2014/15 katika kielezo Na. Hapa chini

**Kielelezo 2: Idadi wa Wakaguliwa**




***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2014/15*

Pamoja na hayo, sikufanikiwa kufanya au kukamilisha ukaguzi wa Taasisi nane kwa sababu tofauti kama nilivyoainisha hapa chini.

**Jedwali 4: Orodha ya Taasisi ambazo Ukaguzi wake haujahitimishwa**

| | Taasisi | Maelezo |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) | Hesabu za fedha hazikuwasishwa |
| 2 | Wakala wa Maendeleo Kigamboni (KDA) | Hesabu za fedha hazikuwasishwa |
| 3 | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania | Ukaguzi haujakamilika taarifa yake itajuishwa kaitka ukaguzi ujao |
| 4 | Shirikisho la Mabunge ya Jumuiya ya Madola | Ukaguzi haujakamilika taarifa yake itajuishwa kaitka ukaguzi ujao |
| 5 | Shirika la Uzalishaji Mali-Matrekta ya Kilimo (SUMA JKT) | Ukaguzi haujakamilika taarifa yake itajuishwa kaitka ukaguzi ujao |
| 6 | Bodi ya Mfuko wa Barabara | Ukaguzi haujakamilika taarifa yake itajuishwa kaitka ukaguzi ujao |
| 7 | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania | Ukaguzi haujakamilika taarifa yake itajuishwa kaitka ukaguzi ujao |
| 8 | Mfuko wa Maafa (NRF) | Ukaguzi haujakamilika taarifa yake itajuishwa kaitka ukaguzi ujao |

### 1.5.4 Mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Mpangilio wa muundo wa ofisi ya ukaguzi ni kwa wakaguzi kufanya kazi kwa kushirikiana na wakaguzi wenye weledi na uzoefu. Ukaguzi unafanywa na timu za ukaguzi ambazo husimamiwa na wakaguzi wa nje wa hesabu (CEA) ambao hutoa taarifa kwa Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Imekuwa muhimu kuwagawanya wakaguliwa wetu katika maeneo madogo yanayoitwa Sekta yanayongozwa na Msaidizi wa Mkaguzi Mkuu (AAGs) ambaye anatoa taarifa kwa Naibu Mkaguzi Mkuu (DAGs), ambaye anatoa taarifa moja kwa moja kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.Ripoti ya mwaka ya Serikali Kuu inajumuisha divisheni mbili; ile ya Serikali Kuu na ile ya hesabu za Taifa. Sehemu ya muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Serikali Kuu ni kama inavyoonekana katika

**Kielelezo No.3** hapo chini:

**Kielelezo 3: Sehemu ya muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Serikali Kuu**




**Kielelezo No 3** Sehemu ya Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Serikali Kuu kwa mwaka uliomalizika 2014/15

## 1.6 Majukumu ya kisheria ya taasisi zinazokaguliwa

Menejimenti za Serikali Kuu na Taasisi zake zinawajibika kuandaa taarifa za hesabu zinazozingatia Viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika sekta ya Umma (IPSAS). Pia inawajibu wa kuandaa na kuonesha kwa usahihi wa Taarifa za Fedha na kuweka mifumo ya udhibiti wa ndani ambao uongozi utaona unafaa ili kuwezesha kuandaa taarifa za hesabu ambazo hazina mapungufu na udanganyifu na makosa mengine. Wajibu wa kisheria katika maandalizi na kuwasilisha taarifa za fedha yanaweza kufafanuliwa kwa msaada wa Kielelezo Na.4 hapo chini.

**Kielelezo 4: Majukumu ya kisheria ya wakaguliwa**




**Chanzo:** *Sheria ya fedha ya Umma Na.6, 2001 nna Waraka wa Kihasibu Na.11 wa mwaka 2012/13*

### 1.6.1 Taarifa za Fedha

Taarifa kamili za fedha zinazoandaliwa kwa mujibu wa viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma kwa misingi ya fedha isiyo taslimu inajumuisha taarifa zifuatazo:

i. Mizania ya Hesabu;

ii. Taarifa ya Mapato na Matumizi/ Taarifa ya Ufanisi wa Fedha;

iii. Taarifa ya Mabadiliko ya Mtaji;

iv. Taarifa ya Mtiririko wa fedha;

v. Taarifa ya Uwiano wa Bajeti na kiasi halisi cha matumizi na

vi. Sera za Uhasibu na Maelezo ya Taarifa za fedha.

## 1.7 Matarajio ya matokeo ya ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu inategemea kutoa matokea chanya katika Taasisi zilizokaguliwa na wadau wote wanaohusishwa na Ukaguzi wangu.

- Ukaguzi huchochea uwajibikaji
- Ukaguzi huchochea utekelezaji wa nidhamu ya fedha
- Ukaguzi husaidia kutambua na kuzuia mapungufu yanayoweza kutokana na udanganyifu au makosa na matumizi mabaya ya rasilimali za Umma
- Ukaguzi hukuza mbinu bora za utunzaji wa hesabu
- Ukaguzi husaidia usimamizi imara wa rasilimali za Umma
- Ukaguzi husaidia katika kufikia utawala bora na kuainisha viashiria vya rushwa
- Ukaguzi huongeza ubora wa kiwango cha taarifa za fedha na kuwapa imani watumiaji wa taarifa za fedha na kuongeza uwajibikaji katika kusimamia Serikali kwa ujumla wake.

## Sura ya Pili

## HATI ZA UKAGUZI

### 2.0 Utangulizi

Lengo kuu la kufanya ukaguzi wa mwaka ni kutoa uhakika kwa watumiaji kama taarifa za fedha zimewasilishwa kwa usahihi, katika mambo yote muhimu, katika kipindi cha utoaji wa taarifa za fedha, kwa mujibu wa misingi inayotumika katika uandaaji wa taarifa hizo. Ukaguzi unawapa watumiaji kiwango cha uhakika namna Taarifa za Fedha za Serikali kuu zinavyoweza kuaminiwa na kutumika, kulingana na taratibu za ukaguzi uliofanyika.

### 2.1 Maana ya hati ya ukaguzi

Ripoti yangu ya ukaguzi kuhusu taarifa za fedha za Wizara,Idara na Wakala wa Serikali (MDAs) imeelezwa katika misingi ya ukweli na haki .Kwa ujumla hii inachukuliwa kumaanisha kwamba taarifa za fedha zina ukweli usiokuwa na upendeleo na huakisi hali halisi ya miamala ya kiuchumi katika taasisi husika,

Hati ya ukaguzi inatoa maoni ya kama taarifa za fedha zimeandaliwa na zimezingatia masuala yote muhimu, kulingana na mifumo inayokubalika ya uandaaji wa taarifa za fedha. Maoni hayo ya ukaguzi ni lazima yaoneshe kama taarifa husika za fedha zimetoa ufafanuzi wa kutosha kumwezesha mtumiaji wa taarifa hizo kuzielewa ama la.

Maoni ya mkaguzi katika taarifa za fedha:
Yanasaidia kuzifanya taarifa za fedha kuaminika zaidi;**hata hivyo**

- Hayatoi uhakika wa kufanikiwa kwa taasisi siku za usoni, na
- Hayatoi dhamana kwamba taasisi iko huru dhidi ya udanganyifu

## 2.2 Aina za hati za ukaguzi/Maoni ya Ukaguzi

Kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi wa Taasisi za Umma (ISSAIs).Yafuatayo ni maelezo ya aina za hati za ukaguzi kama ilivyo kwenye Jedwali hapo chini

**Jedwali 5: Aina za hati za ukaguzi**

| Hati ya Ukaguzi | Kigezo | Hali halisi ya mwaka 2014/15 |
|---|---|---|
| Hati inayoridhisha *(ISSAI 1700.16)* | Taarifa za fedha zimeandaliwa kwa kuhusisha masuala yote muhimu, kulingana na mifumo ya uandaaji wa taarifa za fedha iliyokubalika kimataifa. | Jumla ya Wakaguliwa 180 sawa na asilimia 90 zimepata hati zinazoridhisha; Angalia **Kiambatisho 1.1** |
| Hati yenye shaka *(ISSAI 1705.7)* | Taarifa za fedha zilizoandaliwa zinaonesha kutokubaliana na uongozi au kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi ambayo ni muhimu lakini si makubwa na isipokuwa kwa madhara ya mapungufu hayo,taarifa za fedha zimeandaliwa katika mambo yote kulingana na mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha unaokubalika | Jumla ya taasisi 18 sawa na asilimia 9 zimepata Hati yenye shaka. Angalia **Kiambatisho Na 1.2 (a & b)** |

| Hati ya Ukaguzi | Kigezo | Hali halisi ya mwaka 2014/15 |
|---|---|---|
| Hati isiyoridhisha *(ISSAI 1705.8)* | Madhara ya kutokubaliana ni makubwa na muhimu kwenye taarifa nzima ya fedha, na kama Mkaguzi anahitimisha kwa kutoa hati yenye mashaka kwenye ripoti ya ukaguzi kusingetosheleza katika kuonesha upotoshaji au kutokamilika kwa taarifa za fedha | Hati ya ukaguzi isiyoridhisha ilitolewa kwa Taasisi ya Mzinga sawa na Asilimia 1 ya wakaguliwa wote **Vigezo vimeoneshwa kwenye Kiambatisho Na 1.3** |
| Hati mbaya *(ISSAI 1705.9;10)* | Madhara ya kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi ni makubwa na muhimu na Mkaguzi ameshindwa kupata nyaraka za kutosha wakati wa ukaguzi ili kuweza kutoa hati sahihi na kujidhihirisha kuwa, madhara yanayoweza kutokea kutokana na mapungufu ambayo hajaweza kuyagundua yanaweza yakawa makubwa na ya muhimu sana. Katika hali hii mkaguzi anakataa kutoa hati ya ukaguzi. | Hakuna taasisi iliyopata hati mbaya. |

**Chanzo**: *ISSAI &Taarifa za hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2014/2015*

### 2.3 Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine

Aya yenye masuala ya msisitizo pamoja na aya yenye masuala mengine, kama ilivyo kwenye **Jedwali Na.5**.zinaweza kujumuishwa kwenye ripoti ya ukaguzi kulingana na hali fulani. Matumizi yake hayasababishi kubadili hati yenye shaka au isiyoridhisha kwenye taarifa za fedha

lakini zinawasilisha ujumbe wa ziada kupitia ripoti ya ukaguzi kadri Mkaguzi anavyoona ni lazima kuwafanya watumiaji kuwa makini katika jambo hilo au mambo hayo.

**Jedwali 6: Aya yenye masuala ya msisitizo na aya yenye masuala mengine**

| Aya yenye masuala ya Msisitizo | Aya yenye masuala mengine |
|---|---|
| Aya hujumuishwa wakati mambo yanayoathiri taarifa za fedha yamewasilishwa au kuoneshwa kwenye taarifa za fedha na kwamba ni ya muhimu kwa watumiaji kuelewa taarifa ya fedha.Mfano<br>• Uwalakini kutokana na madai ya kisheria ambapo haijulikani matokeo ya madai yako nje ya uwezo wa Mkaguliwa na yanaweza kuathiri taarifa ya fedha<br>• Pale ambapo kuna kiasi kikubwa cha kutooana au kuchanganyana kati ya yaliyomo kwenye ripoti ya mwaka ya wakaguliwa na taarifa za fedha, au kati ya ufafanuzi uliopo kwenye taarifa za fedha na taarifa zenyewe za fedha ambapo yalihitaji kurekebishwa lakini uongozi wa taasisi husika haukufanya hivyo.<br>• Kama kuna masuala ya Mkaguliwa kushindwa kuendeleza shughuli(Going concern) | Endapo kuma mambo zaidi ya yale yaliyowasilishwa au kuoneshwa kwenye taarifa za fedha lakini kwa mtazamo wa Mkaguzi anaona ni muhimu kwa watumiaji kuweza kuelewa Majukumu ya ukaguzi au ripoti ya ukaguzi<br>• Uwepo wa mapungufu ya udhibiti,<br>• Hali ya kutozingatia sheria na kanuni |

**Chanzo:** *Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs)*

## 2.4 Mchanganuo wa hati za ukaguzi kwa Serikali Kuu kwa miaka mitano mpaka 2014/15

Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa kipindi cha miaka mitano mpaka 2014/15 kwa upande wa Serikali kuu ni kama unavyoainishwa katika **Jedwali Na.7 hapa** chini:

**Jedwali 7: Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka mitano mpaka 2014/15**

| Mwaka | Hati za ukaguzi | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hati inayoridhisha | | Hati yenye shaka | | Hati isiyoridhisha | | Hati mbaya | | |
| | Na. | % | Na. | % | Na. | % | Na. | % | |
| 2014/15 | 180 | 90 | 18 | 9 | 1 | 1 | 0 | 0 | 199 |
| 2013/14 | 166 | 94 | 9 | 5 | 1 | 1 | 0 | 0 | 176 |
| 2012/13 | 85 | 73 | 30 | 26 | 1 | 1 | 1 | 1 | 117 |
| 2011/12 | 103 | 95 | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 108 |
| 2010/11 | 99 | 93 | 8 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 107 |

**Chanzo:** Ripoti ya Ukaguzi kwa kila Mkaguliwa 2014/15

Kutokana na Jedwali **Na.7** hapo juu mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka mitano kutoka 2010/11 mpaka 2014/15 kwa Taasisi zilizo chini ya Serikali kuu inaweza kuwasilishwa kwa kutumia **Kielelezo Na. 5** hapo chini:

**Kielelezo 5: Mwenedo wa hati za ukaguzi kwa miaka mitano**




**Chanzo:** *Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu 2014/15*

Kwa ujumla,kutokana na mchanganuo hapo juu kwa kipindi cha miaka mitano pamekuwepo na kupanda na kushuka juu ya uandaaji wa taarifa za fedha kwa Wizara,Idara na Wakala wa Serikali katika utekelezaji wa Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu za umma  usiokuwa wa taslimu (IPSAS Accrual Basis of Accounting),uzingatiaji wa Sheria na Kanuni,uboreshaji wa mifumo ya udhibiti wa ndani pamoja na kuzingatia mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## 2.5 Mchanganuo wa hati za Ukaguzi kulingana na aina ya wakaguliwa (2010/11 to 2014/15)

Mchanganuo wa hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2010/11 hadi 2014/15 kwa Taasisi zilizokaguliwa unaonyeshwa kwenye jedwali Na. 8 **hapo chini**

## Jedwali 8: Mwenendo wa hati za Ukaguzi kwa kipindi cha

| Hati | | Hati Inayoridhisha | | Hati yenye shaka | | Hati Isiyoridhisha | | Hati Mbaya | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kundi | Mwaka | Na | % | Na | % | Na | % | Na. | % | Wakaguliwa |
| Mafungu | 2014-15 | 75 | 87 | 12 | 13 | 0 | 0 | 0 | 0 | 86 |
| | 2013-14 | 79 | 91 | 7 | 8 | 1 | 1 | 0 | 0 | 87 |
| | 2012-13 | 56 | 66 | 28 | 33 | 0 | 0 | 1 | 1 | 85 |
| | 2011-12 | 73 | 96 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 76 |
| | 2010-11 | 67 | 89 | 8 | 11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 75 |
| Balozi | 2014-15 | 34 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 34 |
| | 2013-14 | 34 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 34 |
| | 2012-13 | 29 | 91 | 2 | 6 | l | 3 | 0 | 0 | 32 |
| | 2011-12 | 30 | 94 | 2 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 32 |
| | 2010-11 | 32 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 32 |
| Taasisi nyinginezo na Mifuko maalum | 2014-15 | 45 | 92 | 4 | 6 | 1 | 2 | 0 | 100 | 49 |
| | 2013-14 | 21 | 91 | 2 | 9 | 0 | 0 | 0 | 0 | 23 |
| | 2012-13 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 2011-12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 2010-11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| WAKALA | 2014-15 | 27 | 90 | 2 | 10 | 0 | 0 | 0 | 0 | 30 |
| | 2013-14 | 32 | 100 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 32 |
| | 2012-13 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 2011-12 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | 2010-11 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | | | | | | | | | | |

**Source:** *Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali 2010/11 hadi 2014/15*

## Sura ya Tatu

# UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MIAKA YA NYUMA

## 3.0 Utangulizi

Sura hii inatoa matokeo ya tathmini juu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa kwa miaka ya nyuma kwa kila Mkaguliwa,ripoti ya jumla na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC).Sura hii inatoa Muhtasari wa Mapendekezo ya Ukaguzi pamoja na tathmini ya hatua zilizochukuliwa na Wizara, Idara na Wakala wa Serikali katika kutekeleza maoni yangu.Pia, sura hii inajumuisha muhtasari wa mapendekezo juu ya ubora na kiasi cha fedha kutoka kila taarifa ya ukaguzi ambayo hayajatekelezwa kikamilifu au utekelezaji wake bado unaendelea.

Baadhi ya Wakaguliwa hawajafanya jitihaza za kutosha katika utekelezaji wa mapendekezo yangu. Kutotekeleza mapungufu yaliyoibuliwa kunaweza kuchangia makosa yaleyale kujirudia katika miaka inayofuata.Hii pia, ni ishara ya kukosa umakini na dhamira kwa Maafisa Masuuli.

## 3.1 Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa miaka iliyopita kwa kila Mkaguliwa

Ufanisi katika kufuatilia mapendekezo ya ukaguzi ni muhimu ili kupata manufaa kamili ya kazi ya ukaguzi. Kufuatia mapitio ya hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi wa mwaka uliopita kwa kila Mkaguliwa imeonekana kwamba, baadhi ya Wizara,Idara,Wakala wa Serikali zilikuwa hazijatekeleza mapendekezo kama inavyoonekana katika **kiambatisho Na.3.1**

Pia, nimefanya ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa mapendekezo yangu kuhusu taarifa za ukaguzi wa kila mkaguliwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara,Wakala wa Serikali.Jumla ya mapendekezo ya ukaguzi 2,644 yalitolewa kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara,Wakala wa Serikali. Kati ya mapendekezo ya ukaguzi 2644,mapendedkezo 1028 (39%) yalitekelezwa, mapendekezo 885 (33%) yalikuwa chini ya utekelezaji, mapendekezo 534 (20%) hayakutekelezwa, mapendekezo 126 (5%) yalitegemea matukio mengine na mapendekezo 71 (3%) yaliyokuwa yanajirudia. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na.9** na **Kiambatisho Na.3.2 mpaka 3.4**

**Jedwali 9: Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa kila Mkaguliwa**

| Hali halisi ya mapendekezo | Taasisi | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Mafungu na Balozi | Wakala | T a a s i s i Nyingine | Jumla | Asilimia |
| Yaliyo teekelezwa | 803 | 132 | 93 | 1028 | 39 |
| Yaliyo katika utekelezaji | 666 | 162 | 57 | 885 | 33 |
| Yasiyo tekelezwa | 444 | 62 | 28 | 534 | 20 |
| Yanayotegemea matukio mengine | 119 | 3 | 4 | 126 | 5 |
| Yanayojirudia | 62 | 8 | 1 | 71 | 3 |
| | **2094** | **367** | **183** | **2644** | |

**Chanzo:** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali 2014/15

Ili kuimarisha uwajibikaji na uwazi juu ya usimamizi wa rasilimali za umma, ninawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa mapendekezo yasiyoshughulikiwa yanatekelezwa kwa wakati muafaka ili kupunguza kujirudia. Maafisa Masuuli wanashauriwa kuandaa mpango kazi na kuandaa majibu ya kila ripoti ya Ukaguzi.

### 3.2 Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi kwa miaka ya nyuma kuhusu ripoti ya mwaka ya Ukaguzi

Ripoti yangu ya mwaka jana ilikuwa na mapendekezo 46 yasiyoshughulikiwa ikiwa ni limbikizo la mapendekezo hadi mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2014 ambayo yalihitaji utekelezaji wa Serikali. Nilipokea majibu kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali tarehe 20 Julai , 2015 kupitia barua yenye kumbukumbu LH.276 / 692/01/11 juu ya majibu ya Serikali.Kati ya mapendekezo 46 mapendekezo 8 (17%) yalitekelezwa, mapendekezo 37 (63%) yanaendelea kutekelezwa na 1 (2% ) hayakutekelezwa. Hali ya utekelezaji wa mapendekezo ni kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali Na.10 na Kiambatisho Na 3.5

**Jedwali 10: Muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa miaka ya nyuma**

| Hali halisi ya Mapendekezo | Mwaka wa fedha | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2006/7 | 2008/9 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | Jumla | Asilimia |
| Yaliyotekelezwa | - | - | - | - | 6 | 2 | 8 | 17 |
| Yaliyo katika hatua ya utekelezaji | 2 | 1 | 2 | 2 | 14 | 8 | 37 | 81 |
| Yasiyotekelezwa | - | - | - | - | 1 | - | 1 | 2 |
| Jumla | 2 | 1 | 2 | 2 | 21 | 18 | 46 | |

**Chanzo:** Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali

Kutokana na **Jedwali Na.10** hapo juu, imebainika kwamba, majibu ya Serikali juu ya mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali siyo ya kuridhisha. Malengo ya kutoa mapendekezo hayo ni kuboresha usimamizi wa fedha katika Wizara,Idara na Wakala Serikali hivyo Serikali inahitaji kuchukua

hatua kuhakikisha kuwa mapendekezo hayo yanatekelezwa ipasavyo kwa ajili ya kuboresha utendaji bora na uwajibikaji.

### 3.3 Kufuatilia utekelezaji wa maelekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge (PAC)

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati juu ya msaada ninaopata kutoka Kamati ya Kudumu ya Bunge (PAC), kwa kutoa maelekezo muhimu kwa serikali ili kutekeleza mapendekezo ninayotoa katika taarifa zangu za Ukaguzi.Hivyo PAC imesaidia majukumu yangu ya kisheria kuwa na manufaa. Ni muhimu sana maagizo yote yaliyotolewa na PAC kutekelezwa kwa wakati. Katika utekelezaji wa maelekezo ya PAC, Serikali itakuwa katika nafasi ya kuongeza makusanyo ya mapato, kudhibiti bajeti na matumizi na kuleta uwajibikaji bora wa rasilimali za Umma.

Katika ripoti ya mwaka 2013/14, kulikuwa na maelekezo tisa (9) yaliyotolewa na PAC ambayo yalihitaji usikivu wa serikali kwa ajili ya utekelezaji. Mapendekezo sita(6) yalikuwa ya mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2012 na matatu(3) yalikuwa ya mwaka wa fedha uliooishia tarehe 30 Juni, 2013.

Hakukuwa na maelekezo zaidi yaliyotolewa na PAC juu ya taarifa ya CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2014 kwani ni mwaka ambao Bunge lilivunjwa kikatiba na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 9Julai , 2015. kwa maana hiyo PAC haikufanya mkutano wowote na Mlipaji Mkuu wa Serikali. Kwa sababu hiyo maelekezo ya PAC ya mwaka 2013/2014 yataingizwa kwenye ripoti ya jumla ya ukaguzi wa mwaka 2015/16.

Maelezo ya hali halisi ya utekelezaji yanapatikana kwenye Jedwali Na.10 na Kiambatisho Na 3.6

**Jedwali 11: Muhtasari wa utekelezaji wa maelekezo ya PAC ya miaka iliyopita**

| Hali halisi ya mapendekezo | 2011/12 | 2012/13 | Jumla | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Yaliyotekelezwa | 0 | 1 | 1 | 11 |
| Yaliyo katika hatua ya utekelezaji | 1 | 4 | 5 | 56 |
| Yasiyotekelezwa | 2 | 1 | 3 | 33 |
| Jumla | | | 9 | 100 |

**Chanzo:** Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali juu ya maelekezo ya PAC ya mwaka 2013/14

Kutoka kwenye **Jedwali Na. 11** inaweza kuhitimishwa kuwa kuna kasi ndogo na mikakati duni juu ya utekelezaji bora wa maelekezo ya PAC juu ya mapendekezo ninayoishauri Serikali katika taarifa zangu za kila mwaka.

## Sura ya Nne

## USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA

### 4.0 Utangulizi

Sura hii inaonyesha muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi na mapendekezo husika kutokana na makisio ya mapato na matumizi ya Serikali yaliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2014/15.

### 4.1 Mapitio ya Bajeti

Bajeti ya Serikali hupitishwa na Bunge kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia tarehe 1 Julai – 30 Juni ya mwaka unaofuata. Bajeti ya Serikali ipo katika misingi ya fedha taslimu. Hata hivyo, matumizi na mapato ya Serikali hufanyika kwa misingi isiyo ya fedha taslimu tangu kuanzishwa kwa matumizi ya Viwango vya Kimataifa visivyo vya Misingi ya Fedha Taslimu (IPSAS Accrual basis of Accounting). Kwa sasa, Serikali Kuu iko katika kipindi cha mpito ikitegemea kutumika kwa ukamilifu ifikapo mwaka wa fedha 2017/18.

Vyanzo vya fedha za kutekeleza bajeti ya Serikali vimebakia vile vile vikiwa na tofauti kidogo huku bajeti ya Serikali ikiongezeka kila mwaka. Vyanzo vikuu vya fedha vya Serikali ni pamoja na Kodi, Misaada ya Wahisani/Wadau wa Maendeleo pamoja na mikopo ya Ndani na Nje. Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/15 iliyoidhinishwa na Bunge iliongezeka kutoka shilingi bilioni 18,248.98 katika kwa mwaka 2013/14 hadi kufikia shilingi bilioni 19,853.3 katika mwaka 2014/2015 ongezeko la takriban asilimia 8.8 kama inavyoonekana katika kielelezo na. 7 hapa chini;

**Kielelezo 6: Mwenendo wa bajeti dhidi ya mapato halisi**




## 4.2 Mwenendo wa ujumla wa Ukusanyaji wa Mapato

Serikali ilipanga kukusanya mapato ya shilingi bilioni 19,853.3 katika mwaka wa fedha 2014/15, ambapo shilingi bilioni 13,408.22 zitumike katika matumizi ya kawaida (ongezeko la 6.6% ikilinganishwa na shilingi bilioni 12,574.95 zilizotengwa mwaka 2013/14) na shilingi bilioni 6,445.11 zitumike kwenye shughuli za maendeleo (ongezeko la 13.6% ikilinganishwa na shilingi bilioni 5,674.03 mwaka 2013/14).

**Kutofikia lengo la mapato kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,091.27**

Jumla ya mapato halisi yaliyokusanywa kutoka vyanzo vilivyoainishwa ilifikia shilingi bilioni 19,111.68 na kufanya kiasi cha shilingi bilioni 1,091.27, sawa na 5.40% kutokusanywa ukiondoa mapato kutoka Serikali za Mitaa. Kati ya fedha zilizokusanywa shilingi bilioni 14,144.31 zilitolewa kwa Wizara, Idara za Serikali, Wakala wa Serikali, na Sekretarieti za Mkoa, shilingi bilioni 11,190.11 kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2,954.20 kwa ajili ya shughuli za maendeleo.






Hata hivyo, kati ya fedha zilizotolewa, kiasi cha Shilingi bilioni 5,178.13 za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 165.41 kwa miradi ya maendeleo zilitolewa katika robo ya nne ya mwaka wa fedha (Kati ya Aprili na Juni 2015) sawa na 26.92% ya bajeti yote ya Serikali na kiasi cha shilingi bilioni 134.29 zilizotolewa kwa Wizara ya Ujenzi hazikupokelewa Wizarani katika mwaka wa fedha husika na hivyo kuathiri utekelezaji mzima wa bajeti ya Wizara hiyo.

**Mapato yatokanayo na Kodi**

Katika mwaka wa fedha 2014/15 mapato halisi yaliyokusanywa kutokana na kodi yalikuwa shilingi bilioni 10,773.22 (88.88%) dhidi ya makisio ya shilingi bilioni 12,121.19 na kuonyesha kutofikiwa kwa lengo kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,347.97 (11.12%) ya jumla ya makisio yaliyopitishwa. Mapato hayo yaliyotokana na kodi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

**Mapato yasiyotokana** na **Kodi**
Mapato yasiyotokana na kodi yaliyokusanywa kwa mwaka 2014/15 yalikuwa shilingi bilioni 616.73 (86%) dhidi ya makisio ya shilingi bilioni 717.11, hivyo kutofikia lengo la makusanyo kwa shilingi bilioni 100.38, sawa na 14% ya makisio yaliyoidhinishwa.

**Mapato halisi** ya **fedha za gawio**
Mapato halisi kutokana na fedha za gawio kama yalivyoripotiwa katika taarifa za fedha za ofisi ya Msajili wa Hazina yalikuwa shilingi bilioni 159.87 (98%) yakilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 163.36, ambapo shilingi bilioni 3.49 (2%) ya makisio yaliyopitishwa hazikuweza kukusanywa.

**Mapato yatokanayo na mikopo ya ndani**
Mapato yatokanayo na Mikopo ya ndani ambayo ni kwa ajili ya **kugharamia** bajeti na kulipia mikopo iliyofikia muda wake yalikuwa shilingi bilioni 3,978.95 (134.64%) dhidi ya makisio idhinishwa ya shilingi bilioni 2,955.20 ikionesha kukopa zaidi ya makisio kwa kiasi cha shilingi bilioni 1,023.75 sawa na 34.64% juu ya makisio. Deni la Ndani limekuwa likikua kila mwaka huku wawekezaji wakubwa wakiwa mabenki ya biashara. Jambo hili lina athari za kiuchumi, kwani hali hii inasababisha viwango vya riba inayotozwa katika mikopo inayotolewa na mabenki ya biashara kuendelea kupanda ili kuwavunja moyo wakopaji. Athari za jambo hili ni kwamba, hatimaye, huchangia kuongezeka kwa gharama za maisha ya wananchi.

**Mikopo ya nje, misaada ya Wahisani/wadau wa maendeleo**
Mapato halisi **yaliyotokana** na Misaada ya Wahisani/ Wadau wa Maendeleo na mikopo ya nje kwa Mwaka wa Fedha 2014/15 **yalikuwa** shilingi bilioni 3,601.95 (84.5%) dhidi ya makisio yaliyopitishwa ya shilingi bilioni 4,261.60, hivyo kusababisha

misaada kiasi cha shilingi bilioni 659.65 sawa na 15.47% kutopokelewa.

Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa miaka mitatu mfululizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 12 hapo chini:

**Jedwali 12:** Mwenendo wa makusanyo ya mapato kwa miaka mitatu (kiasi katika shilingi bilioni)

| 2014/2015 | | | |
|---|---|---|---|
| **Aina ya Mapato** | **Makisio TZS** | **Halisi TZS** | **Tofauti zaidi/(Pungufu)** |
| Kodi | 12,121.19 | 10,773.22 | (1,347.97) |
| Yasiyo ya Kodi | 701.60 | 597.70 | (103.90) |
| Fedha za Gawio | 163.36 | 159.87 | (3.49) |
| Mikopo ya Ndani | 2,955.20 | 3,978.95 | 1,023.75 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 4,261.60 | 3,601.95 | (659.65) |
| **JUMLA** | **20,202.95** | **19,111.68** | **(1,091.27)** |
| **2013/2014** | | | |
| **Aina ya Mapato** | **Makisio TZS** | **Halisi TZS** | **Tofauti zaidi/(Pungufu) TZS** |
| Kodi | 10,412.95 | 9,289.00 | (1,123.95) |
| Yasiyo ya Kodi | 639.68 | 532.24 | (107.44) |
| Fedha za Gawio | 123.75 | 108.71 | (15.04) |
| Mikopo ya Ndani | 1,699.87 | 3,289.41 | 1,589.54 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 5,011.60 | 3,084.93 | (1,926.67) |
| **JUMLA** | **17,887.84** | **16,304.30** | **(1,583.55)** |
| **2012/2013** | | | |
| **Aina ya Mapato** | **Makisio TZS** | **Halisi TZS** | **Tofauti zaidi/(Pungufu) TZS** |
| Kodi | 8,432.29 | 8,052.29 | (380.01) |
| Yasiyo ya Kodi | 644.58 | 419.56 | (225.02) |
| Fedha za Gawio | 72.26 | 61.59 | (10.66) |
| Mikopo ya Ndani | 1,632.00 | 2,492.71 | 860.71 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 4,410.81 | 3,992.17 | (418.64) |
| **JUMLA** | **15,191.94** | **15,018.33** | **(173.62)** |

**Vyanzo:** *Taarifa ya ukaguzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, taarifa ya ukaguzi ya Deni la Taifa, Taarifa ya ukaguzi ya Wizara ya fedha za 2014/2015 na Taarifa ya jumla ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka 2013/2014.*

Kutoka katika jedwali Na. 13 inaonesha yafuatayo:- Mwenendo wa makisio ya mapato kutokana na kodi katika mwaka wa fedha 2014/15 umeongezeka

kwa 14.86% na 30.43% ikilinganishwa na makisio kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2012/13 kwa mfuatano huo. Vilevile, kumekuwa na ongezeko la mapato halisi kwa 13.78% na 25.26% ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa katika mwaka wa fedha 2013/14 na 2012/13 kwa mfuatano huo. Ongezeko la mwaka 2014/15 kwenye makisio ya mapato ya Kodi na halisi linatokana na jumuisho la Zanzibar ambapo miaka mingine lilikuwa halijumuishwi.

- Katika mwaka 2014/15, makisio ya mapato yasiyotokana na kodi yaliongezeka kwa 11.76% na 8.13% ikilinganishwa na makisio kwa mwaka wa fedha 2013/14 na 2012/13 kwa mfuatano huo. Vilevile, ukusanyaji maduhuli kutoka katika vyanzo visivyo vya kodi yaliongezeka kwa 14.66% na 29.80% yakilinganishwa na yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2013/14 na 2012/13 kwa mfuatano huo.
- Makisio ya mapato ya Fedha za gawio katika mwaka wa fedha 2014/2015 yaliongezeka kwa 24.25% na 55.77% yakilinganishwa na makisio yaliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2013/14 na 2012/13 kwa mfuatano huo. Mapato halisi yaliongezeka kwa 32% na 61.47% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013/14 na 2012/13 kwa mfuatano huo.
- Mapato yatokanayo na mikopo ya ndani yaliongezeka kwa 17.33% huku mikopo ya nje na misaada ikiongezeka kwa 14.35% katika mwaka wa fedha 2014/15 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013/14.

**Uwiano kati ya makisio na mapato halisi**

Kumekuwa na ongezeko katika makisio ya mapato na matumizi kila mwaka, na ongezeko kidogo katika ukusanyaji maduhuli. Deni la Ndani na Nje limekuwa likiongezeka kila mwaka wakati mapato kutokana kodi na yasiyo ya kodi yanaongezeka

taratibu sana licha ya mapendekezo mbalimbali ambayo nimekuwa nikiyatoa mara kwa mara.

**Jedwali 13: Mwenendo wa uchambuzi wa bajeti kwa miaka mitatu (Kiasi katika bilioni za shilingi)**

| Aina ya Mapato | Makisio TZS | | | D | E | % ya D | % ya E |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2014/2015 (A) | 2013/2014 (B) | 2012/2013 (C) | Tofauti (A-B) | Tofauti (A-C) | | |
| Kodi | 12,121.19 | 10,320.16 | 8,432.29 | 1,801.04 | 3,688.90 | 14.86 | 30.43 |
| Yasiyo ya Kodi | 701.60 | 619.06 | 644.58 | 82.54 | 57.02 | 11.76 | 8.13 |
| Fedha za Gawio | 163.36 | 123.75 | 72.26 | 39.61 | 91.10 | 24.25 | 55.77 |
| Mikopo ya Ndani | 2,955.20 | 2,947.82 | 1,632.00 | 7.38 | 1,323.20 | 0.25 | 44.78 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 4,261.60 | 3,855.20 | 4,410.81 | 406.40 | (149.21) | 9.54 | -3.50 |
| **JUMLA** | **20,202.95** | **17,865.98** | **15,191.94** | **2,336.97** | **5,011.01** | | |
| | | | | | | | |
| **Aina ya Mapato** | **Halisi TZS** | | | **D** | **E** | **% ya D** | **% ya E** |
| | **2014/2015 (A)** | **2013/2014 (B)** | **2012/2013 (C)** | **Tofauti (A - B)** | **Tofauti (A - C)** | | |
| Kodi | 10,773.22 | 9,289.00 | 8,052.29 | 1,484.23 | 2,720.94 | 13.78 | 25.26 |
| Yasiyo ya Kodi | 597.70 | 510.09 | 419.56 | 87.61 | 178.13 | 14.66 | 29.80 |
| Fedha za Gawio | 159.87 | 108.71 | 61.59 | 51.15 | 98.27 | 32.00 | 61.47 |
| Mikopo ya Ndani | 3,978.95 | 3,289.41 | 2,492.71 | 689.54 | 1,486.24 | 17.33 | 37.35 |
| Mikopo ya Nje na Misaada ya Wahisani | 3,601.95 | 3,084.93 | 3,992.17 | 517.02 | (390.23) | 14.35 | -10.83 |
| **JUMLA** | **19,111.68** | **16,282.15** | **15,018.33** | **2,829.54** | **4,093.35** | | |

**Vyanzo:** *Taarifa ya ukaguzi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, taarifa ya ukaguzi ya Deni la Taifa, Taarifa ya ukaguzi ya Wizara ya fedha za 2014/2015 na Taarifa ya jumla ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ya mwaka 2013/2014.*

Ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuanza kufuatilia na kupunguza mianya mbalimbali iliyopo katika Sheria ya Kodi na maeneo mengine ambayo yanahitaji maboresho ili kuboresha vyanzo vyetu vya ndani vya mapato. Kufanya hivyyo kutatusaidia kuondokana na kuendesha bajeti ya Serikali kwa kutegemea mikopo na misaada ya wahisani.

### 4.2.1 Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida zikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa

Makisio ya matumizi ya kawaida katika mwaka husika wa ukaguzi kwa Wizara, Idara, na Sekretarieti za Mikoa yalikuwa shilingi bilioni 11,646.20 yakionesha ongezeko la shilingi bilioni 1,686.38 (16.93%) ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2013/14 ya shilingi bilioni 9,959.81.

Mapitio ya taarifa za fedha za Wizara na Sekretarieti za Mkoa yalibainisha kuwa shilingi bilioni 11,190.11 zilitolewa kama matumizi ya kawaida ikiwa ni 96.06% ya makisio yaliyoidhinishwa, hivyo, shilingi bilioni 456.08 hazikutolewa; hiyo ni sawa na 3.92% ya makisio yaliyoidhinishwa.

Pia, kuna ongezeko la fedha zilizotolewa, kiasi cha shilingi bilioni 1,630.56 (17.06%), ikilinganishwa na fedha zilizotolewa mwaka 2013/14. Fedha zilizotolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2013/14 zilikuwa shilingi bilioni 9,559.56 zikilinganishwa na bajeti ya shilingi bilioni 9,959.81.

**Jedwali 14: Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida dhidi ya Makisio (Kiasi katika Shilingi).**

| Makisio yaliyoidhinishwa na Fedha zilizotolewa | | | |
|---|---|---|---|
| **Mwaka wa Fedha** | **Makisio** | **Halisi zilizotolewa** | **Fedha zisizotolewa** |
| 2014/15 (A) | 11,646,196,605,462 | 11,190,114,440,646 | 456,082,164,816 |
| 2013/14 (B) | 9,959,812,919,274 | 9,559,557,777,044 | 400,255,142,230 |
| 2012/13 (C) | 8,599,992,738,758 | 8,284,419,655,467 | 315,573,083,291 |
| 2011/12 (D) | 9,214,885,955,263 | 8,687,230,788,550 | 527,655,166,713 |
| Tofauti kati ya (A-B) | 1,686,383,686,188 | 1,630,556,663,602 | |
| Asilimia ya Kuongezeka/Kupungu | 16.93 | 17.06 | |

**Chanzo:** *Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Fedha zisizotolewa na zinazotolewa kwa kuchelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zinakwamisha utendaji wa shughuli za Serikali.

Jedwali Na. 14 hapo juu linaonyesha makisio yaliyoidhinishwa na fedha halisi zilizotolewa na Serikali kwa matumizi ya kawaida kwa kipindi cha miaka minne. Mchanganuo zaidi unaonyesha makisio na mapato halisi kwa kila Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa zinapatikana katika kiambatisho Na: 4.1

### 4.2.2 Uwiano wa fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa na matumizi halisi

Matumizi halisi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2014/15 yalifikia shilingi bilioni 11,156.43 dhidi fedha zilizotolewa kiasi cha shilingi bilioni 11,190.11 na kusababisha kiasi cha shilingi bilioni 33.68 sawa na 0.30% ya fedha iliyotolewa kutotumika.

Kuna ongezeko la matumizi halisi la shilingi bilioni 1,605.14 sawa na 16.81% katika mwaka wa fedha 2014/15 ikilinganishwa na matumizi halisi yaliyoripotiwa katika mwaka wa fedha 2013/2014. Jedwali Na.15 linaonyesha fedha zilizotolewa na matumizi halisi. Mchanganuo zaidi unaoonyesha mapato halisi na matumizi kwa kila Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa ni kama unavyoonekana katika kiambatisho Na.4.1:

**Jedwali 15: Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida na matumizi halisi (Kiasi katika shilingi)**

| | Fedha zilizotolewa dhidi ya Matumizi | | |
|---|---|---|---|
| Mwaka wa Fedha | Halisi zilizotolewa | Halisi zilizotumika | Fedha zisizotumika |
| 2014/15 (A) | 11,190,114,440,646 | 11,156,432,036,782 | 33,682,403,864 |
| 2013/14 (B) | 9,559,557,777,044 | 9,551,289,609,949 | 8,268,167,095 |
| 2012/13 (C) | 8,284,419,655,467 | 8,249,278,491,861 | 35,141,163,606 |
| 2011/12 (D) | 8,687,230,788,550 | 8,685,275,162,094 | 1,955,626,456 |
| Tofauti kati ya (A-B) | 1,630,556,663,602 | 1,605,142,426,833 | |
| Asilimia ya Kuongezeka/Kupungua | 17.06 | 16.81 | |

**Chanzo:** *Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Kwa jumla, kumekuwepo na ongezeko la matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2014/15 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013/14. Hata hivyo, kuwapo kwa fedha zisizotumika kunamaanisha baadhi ya shughuli zilizopangwa hazikutekelezwa kama zilivyopangwa.

### 4.2.3 Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo zikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa

Makisio yaliyoidhinishwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika mwaka husika wa ukaguzi yalikuwa shilingi bilioni 4,389.02. Fedha hizo zikionyesha kupungua kwa kiasi cha shilingi 646.92 bilioni sawa na (12.85%) ikilinganishwa na bajeti ya mwaka uliopita ya shilingi bilioni 5,035.94.

Mapitio ya taarifa za fedha za Wizara na Sekretarieti za mikoa yalibainisha kuwa shilingi bilioni 2,954.20 zilizotolewa kwa matumizi ya maendeleo sawa na 67.31% dhidi ya makisio yaliyoidhinishwa na kufanya kiasi cha shilingi bilioni 1,434.83 pungufu sawa na 32.69% dhidi ya makisio.

Hata hivyo, fedha zilizotolewa zilipungua kwa shilingi bilioni 192.84 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013/14. Rejea jedwali Na. 17 hapo chini. Mchanganuo zaidi unaoonesha mapato halisi na makisio kwa kila Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa ni kama unavyoonekana katika kiambatisho na.4.2:

**Jedwali 16: Uwiano wa fedha zilizotolewa kwa shughuli za maendeleo dhidi Makisio (Kiasi katika Shilingi)**

| Makisio yaliyoidhinishwa na Fedha zilizotolewa | | | |
|---|---|---|---|
| Mwaka wa Fedha | Makisio | Halisi zilizotolewa | Fedha zisizotolewa |
| 2014/15 (A) | 4,389,023,185,915 | 2,954,195,303,772 | 1,434,827,882,143 |
| 2013/14 (B) | 5,035,944,055,546 | 3,147,036,199,330 | 1,888,907,856,216 |
| 2012/13 (C) | 4,225,474,934,851 | 3,247,527,081,386 | 977,947,853,465 |
| 2011/12 (D) | 4,311,009,394,737 | 3,384,431,758,346 | 926,577,636,391 |
| Tofauti kati ya (A-B) | (646,920,869,632) | (192,840,895,558) | |
| Asilimia ya Kuongezeka/Kupungua | (12.85) | (6.13) | |

**Chanzo:** *Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Fedha zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo ambazo hazikutolewa zina athari kwenye shughuli hizo kama vile kuongezeka kwa gharama ya utekelezaji wa miradi iliyokuwa imetengewa fedha hizo; na inaweza ikasababisha kuongezeka kwa riba kwa ile miradi iliyokuwa imeanza kutekelezwa na ambayo madai yake kwa kazi zilizokwishafanyika yameshaidhinishwa na wakandarasi na kusababisha mzigo mkubwa wa kifedha kwa Serikali katika siku zijazo.

### 4.2.4 Uwiano wa fedha za matumizi ya maendeleo zilizotolewa na matumizi halisi

Fedha zilizotolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika mwaka wa fedha 2014/15 zilifikia shilingi bilioni 2,954.20 ikiwa ni pungufu kwa 6.13% ikilinganishwa na fedha zilizotolewa kwa mwaka 2013/14. Kati ya hizi, kiasi cha shilingi bilioni 165.41 zilitolewa katika robo ya nne, na hivyo, kuathiri utekelezaji wa bajeti. Matumizi halisi yalikuwa shilingi bilioni 2,916.18 na kusababisha kiasi cha shilingi bilioni 38.02 sawa na 1.29% kutotumika kati ya fedha zilizotolewa.

Matumizi halisi ya fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha 2014/15 yalipungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 228.90 sawa na 7.28% ikilinganishwa na matumizi ya mwaka 2013/14. Jedwali Na. 17 hapo chini linaonesha uwiano wa fedha zilizotolewa dhidi matumizi halisi. Mchanganuo zaidi unaoonesha mapato halisi na matumizi kwa kila Wizara, Idara za Serikali na Sekretarieti za Mikoa ni kama inavyoonekana katika kiambatisho na.4.2:

**Jedwali 17: Uwiano wa fedha zilizotolewa na matumizi halisi kwa fedha za maendeleo (Kiasi katika Shilingi)**

| Fedha zilizotolewa dhidi ya Matumizi | | | |
|---|---|---|---|
| Mwaka wa Fedha | Halisi zilizotolewa | Halisi zilizotumika | Fedha zisizotumika |
| 2014/15 (A) | 2,954,195,303,772 | 2,916,177,331,940 | 38,017,971,832 |
| 2013/14 (B) | 3,147,036,199,330 | 3,145,081,736,220 | 1,954,463,110 |
| 2012/13 (C) | 3,247,527,081,386 | 3,203,098,332,184 | 44,428,749,202 |
| 2011/12 (D) | 3,384,431,758,346 | 3,376,296,146,186 | 8,135,612,160 |
| Tofauti kati ya (A-B) | (192,840,895,558) | (228,904,404,281) | |
| Asilimia ya Kuongezeka/Kupungua | (6.13) | (7.28) | |

**Chanzo:** *Hesabu za Wizara na Sekretarieti za Mikoa zilizokaguliwa*

Kwa ujumla, kuongezeka kwa mapato ya Serikali, hasa ya ndani yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi, yatasaidia utengamo mzuri wa shughuli za Serikali na kwa kiasi kikubwa kupunguza Serikali kutegemea misaada kutoka nje pamoja na mikopo ya kuendeshea shughuli zake. Kuimarisha na kuboresha maeneo ya uwezo wa uchumi kama mipakani, Bandari, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sekta ya Madini, Utalii na sekta ya Kilimo kutasaidia kukuza Pato la Taifa la ndani na kupunguza utegemezi wa Serikali na itasaidia kuboresha maisha ya wananchi. Kuhimiza uwajibikaji juu ya Sheria na Kanuni na waraka tofauti zinazotolewa na Serikali na kurekebisha mfumo wa bajeti kunaweza

kuchangia katika kufikia shabaha tunazojiwekea.

Serikali inatakiwa kuandaa bajeti yenye uhalisia, kupeleka fedha kama zinavyoidhishwa na bunge ili kuwezesha utengamano katika utekelezaji wa bajeti, na kupunguza kufanya mapitio ya bajeti ya mara kwa mara. Maboresho zaidi yanahitajika katika makisio ya mapato yote ya ndani na nje ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na Washirika wa Maendeleo waweze kutoa misaada yao kwa wakati.



### 4.2.5 Ulinganifu wa makusanyo yasiyo ya Kodi ya Mapato na bajeti iliyoidhinishwa

Bajeti ya mapato yasiyotokana na kodi kwa Wizara/Idara/Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, na Balozi kwa mwaka wa fedha 2014/15 yalikuwa shilingi milioni 701,558, shilingi milioni 40 na shilingi milioni 15,510 kwa mfuatano huo. Makusanyo halisi yalikuwa shilingi 597,607 milioni, shilingi milioni 89 na shilingi milioni 19,029 kwa Wizara/Idara/Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Balozi mfuatano huo.

Wizara hazikuweza kufikia malengo ya makusanyo kwa kiasi cha shilingi milioni 103,951 (14.82%), wakati Balozi zilikusanya zaidi ya malengo kwa shilingi milioni 3,520 (22.69%). Sekretarieti za Mkoa zilivuka malengo kwa kiasi cha shilingi 49 milioni (124.68%) ya bajeti.

Bajeti ya mapato yasiyotokana na kodi kwa Wizara/Idara/Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Balozi kwa mwaka wa fedha 2013/14 ilikuwa shilingi milioni 639,631, shilingi milioni 49 na shilingi milioni 17,152 kwa mfuatano huo. Makusanyo halisi yalikuwa shilingi milioni 532,221, Sh. Milioni 14 na shilingi milioni 21,069 kwa Wizara/Idara/Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa,na Balozi mfuatano huo.

Bajeti kwa mapato yasiyo ya kodi kwa Wizara/ Idara/Wakala wa Serikali, Balozi na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2012/13 ilikuwa shilingi milioni 644,515, shilingi milioni 15,968 na shilingi milioni 65, kwa mtiririko huo. Makusanyo halisi yalikuwa shilingi bilioni 461,138, shilingi bilioni 19,918, na Shilingi bilioni 2.13, kwa mfuatano huo.

**Jedwali 18: Mwenendo wa mapato yasiyo ya kodi kwa miaka mitatu (Kiasi katika Sh. Milioni)**

| Mwaka wa Fedha | Husika | Makisio | Halisi | Zaidi/Pungufu ya Makusanyo | Asilimia ya Halisi Dhidi ya Makisio | Asilimia ya kisichokusanywa |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2014/15 | Wizara/Idara | 701,558 | 597,607 | (103,951) | 85.18 | (14.82) |
| | Sekretarieti za Mikoa | 40 | 89 | 49 | 224.68 | 124.68 |
| | Balozi | 15,510 | 19,029 | 3,520 | 122.69 | 22.69 |
| 2013/14 | Wizara/Idara | 639,631 | 532,221 | (107,410) | 83.21 | (16.79) |
| | Sekretarieti za Mikoa | 49 | 14 | (35) | 28.57 | (71.43) |
| | Balozi | 17,152 | 21,069 | 3,917 | 122.84 | 22.84 |
| 2012/13 | Wizara/Idara | 644,515 | 461,138 | (183,377) | 71.55 | (28.45) |
| | Sekretarieti za Mikoa | 65 | 2,128 | 2,063 | 3,273.85 | 3,173.85 |
| | Balozi | 15,968 | 19,918 | 3,950 | 124.74 | 24.74 |

**Kielelezo 7: Mapato yasiyotokana na kodiWizara,Idara, Balozi na Sekretarieti za Mikoa**




**Chanzo:** *Hesabu za Wizara Sekretarieti za Mikoa na Balozi zilizokaguliwa*

## 4.3 Masuala Yanayohusiana na Mpango wa Kubakiza Makusanyo

Sehemu hii ya ripoti inaelezea masuala yaliyojitokeza kuhusu mpango wa kubakiza makusanyo kwa baadhi ya Wizara na Idara za Serikali kwa mwaka 2014/15.

**Kushindwa kurejesha pesa za Mpango wa kubakiza makusanyo kiasi cha Shilingi bilioni 21.04**

Serikali imeweka utaratibu kwa baadhi ya Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kukusanya mapato yao ya ndani na kuyaweka katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kisha kiasi cha fedha hizo zitarejeshwa kama walivyokubaliana kwa mpango wa kubakiza.

Wizara na Idara hizo ni pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto. Kwa upande wa Idara, nazo ni: Idara ya Huduma za Uhamiaji, Jeshi la Polisi na Idara ya Huduma za Magereza.

Nilibaini wakati wa ukaguzi kuwa kiasi cha shilingi bilioni 21.04 hazikurejeshwa kwa Idara ya Huduma za Uhamiaji kulingana na makubaliano juu ya mpango wa kubakiza. Baadhi ya Wizara na Idara hazikukusanya mapato yao kama yalivyoidhinishwa na fedha walizokusanya ziliwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na taratibu zilifuatwa. Mchanganuo zaidi ni kama unavyoonekana katika jedwali la hapo chini:

**Jedwali 19: Uchambuzi wa mkusanyiko yasiyo ya kodi kwa Wizara na Idara chini ya mpango wa kubakiza (Shilingi)**

| Wizara/Idara | Makisio | Makusanyo Mapato Halisi | (Pungufu)/zaidi ya Makusanyo | % ya zaidi/(pungufu ya Makusanyo |
|---|---|---|---|---|
| Elimu na Mafunzo ya Ufundi | 9,502,818,100 | 7,460,697,372 | (2,042,120,728) | -21.49 |
| Aridhi, Nyumba na Makazi | 61,320,000,000 | 53,832,959,191 | (7,487,040,809) | -12.21 |
| Maendeleo ya Jamii Wanawake na Watoto | - | 1,841,434,357 | 1,841,434,357 | 100.00 |
| Nishati na Madini | 269,385,983,999 | 211,255,402,708 | (58,130,581,291) | -21.58 |
| Mali asili na Utalii | 114,656,850,557 | 75,825,462,808 | (38,831,387,749) | -33.87 |
| Mambo ya Ndani - Polisi | 22,980,396,000 | 32,945,937,275 | 9,965,541,275 | 43.37 |
| Mambo ya Ndani - Magereza | - | 1,645,143,527 | 1,645,143,527 | 100.00 |
| Idara ya Uhamiaji | 95,536,675,000 | 105,501,616,430 | 9,964,941,430 | 10.43 |

Isipokuwa Wizara za Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mambo ya Ndani - Jeshi la Polisi, Magereza pamoja na Idara ya Uhamiaji, Wizara nyingine chini ya mpango wa kubakiza zilishindwa kutimiza malengo yao kwa kati ya asilimia 12.21 na asilimia 33.87 kama inavyoonekana katika jedwali na. 19 hapo juu.

Ninatoa wito kwa Wizara na Idara chini ya mpango

wa kubakiza kukusanya mapato yasiyo ya kodi ili kufikia hayo malengo wanayojiwekea, hii ni pamoja na kutengeneza bajeti kwa wale ambao hawakuwa na bajeti na waliweza kukusanya zaidi ya bilioni moja (kwa mfano, Idara ya Huduma za Magereza na Wizara ya Maendeleo ya Jamii chini ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii).

# Sura ya Tano

# HESABU ZA TAIFA

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea masuala yaliyojiri kutokana na ukaguzi wa Hesabu za Taifa, Usimamizi wa uwekezaji na maslahi ya Serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Deni la Taifa na Kitengo cha Ukaguzi wa Awali cha Malipo ya Pensheni

## 5.1 Uandaaji wa Taarifa za Hesabu za Majumuisho

Kufuatia uamuzi wa serikali kurasimisha matumizi ya Kanuni za Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS accrual basis of accounting) kuanzia tarehe 1 Julai, 2012, serikali inalazimika kuandaa taarifa ya hesabu zake na za taasisi inazomiliki kulingana na Kanuni Na.6 za IPSAS na Kifungu cha 25 cha Sheria za Fedha ya mwaka 2001(marekebisho 2004).

Pamoja na nia ya dhati ya serikali katika kuboresha uwazi na uwajibikaji, ujumuishwaji wa taasisi za umma kwenye Taarifa za Hesabu za Majumuisho umeendelea kukumbwa na changamoto kadha wa kadha katika utekelezaji. Changamoto hizo ni pamoja na:

### 5.1.1 Kuandaa Hesabu za Majumuisho kwa Taasisi zinazofunga Hesabu kwa Tarehe Tofauti Bila Kufanya Marekebisho

Ukaguzi wa Hesabu za Majumuisho za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazoishia tarehe 30 Juni 2015 ulibaini kuwa taarifa za hesabu za Majumuisho zinazohusisha Taasisi za Umma haziwiani katika tarehe za kufunga hesabu. Hii ni kinyume na aya ya 47 ya IPSAS Na. 6 na Waraka wa Hazina Na.12 wa 2014/2015 uliotolewa tarehe 9 Januari 2015.

Pia, nilibaini kuwa hakuna marekebisho yaliyofanyika katika hesabu ili kuoanisha tarehe. Hali hii inatia shaka kwenye uhalisia wa hesabu za majumuisho na inakinzana na aya ya 48 ya IPSAS Na. 6. Orodha ya Taasisi hizo ipo kwenye **kiambatisho Na.5.1**

Kuna haja ya serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina ifuatilie kwa ukaribu jitihada zake ili kuhakikisha kwamba, taasisi za umma zinafunga hesabu zao katika vipindi sawa ili kupunguza muda unaotumika kufanya masahihisho ya hesabu zao. Kutokana na hali hii, naishauri serikali isimamie miongozo inayotolewa ili taasisi zote za umma zifunge hesabu zake mwishoni mwa mwaka wa serikali. Pia kupunguza changamoto zinazoweza kutokea wakati wa kusuluhisha vipindi tofauti vya hesabu na kuzingatia IPSAS Na. 6.

### 5.1.2 Utofauti Katika Uandaaji wa Taarifa za Mtiririko wa fedha (Cash Flows)

Waraka wa hazina Na.11 uliotolewa na Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali kuandaa Taarifa za mtiririko wa fedha (cash flows statements) unaelekeza Taasisi zote, ikiwemo Serikali za Mitaa, kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha kwa kutumia njia ya moja kwa moja (Direct Method).Hata hivyo ,ukaguzi wa Hesabu za Majumuisho ulibaini kuwa Halmashauri ziliandaa Hesabu kwa kutumia njia isiyo ya moja kwa moja (Indirect Method) kinyume na waraka Na.11 wa 2014/2015.

Kupitia mahojiano na Mhasibu Mkuu wa Serikali, nilibaini kuwa Halmashauri zilipewa maelekezo kutumia njia isiyo ya moja kwa moja kuandaa taarifa za mtiririko wa fedha. Agizo hili lililotolewa na Ofisi ya Waziri Mkuu Serikali za Mitaa (PMO-RLAG) linakinzana na kifungu cha 25 cha Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (Ilivyorekebishwa 2004) na Kanuni ya 10(3) na 4(a).

Ninaelewa utata uliopo kati ya kifungu cha 4(a) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa,2009 kinachompa mamlaka Waziri husika na Serikali za Mitaa kutoa maelekezo ya namna bora ya kusimamia fedha za Halmashauri.

Nionavyo, matakwa ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2009 haimzuii Mhasibu Mkuu wa Serikali kutoa muongozo kwa Halmashauri kuhusu namna bora ya kuandaa hesabu. Hivyo, kutoa maelekezo yenye kuleta utata hufanya uandaaji wa hesabu Jumuifu kuwa mgumu kwani viwango vinaelekeza kufanya marekebisho taarifa zinapokinzana.

Ninaishauri Serikali ihakikishe kuwa maelekezo yanayoongoza uandaaji wa hesabu yatolewe na Mhasibu Mkuu wa serikali kupitia kwa Katibu Mkuu Hazina ili kuondoa utata unaojitokeza wakati wa kuandaa Hesabu.

### 5.1.3 Kuandaa Hesabu za Majumuisho za Wizara,Idara zinazojitegemea,Wakala wa serikasli, Serikali za mitaa na Taasisi za Serikali zinazofanya biashara kwa Kutumia Mfumo Usiojiendesha

Wakati wa ukaguzi wa Hesabu Jumuifu, nilibaini kuwepo kwa uandaaji wa hesabu bila kuwa na mfumo maalum unaojiendesha ingawataasisi zote Serikali kuu na Serikali za Mtaa, zinatumia mfumo wa EPICOR

Kupitia mahojiano niliyofanya, nilibaini kuwa:

(a) Balozi ambazo ziko chini ya Wizara ya Mambo ya Nje na Mahusiano ya Kimataifa hazijaunganishwa kwenye mfumo wa EPICOR ,

(b) Mifumo ya EPICOR ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa haijaunganishwa pamoja ingawa wote wanatumia EPICOR 9.05 ambayo kama ingetumika ipasavyo ingewezesha kuandaa taarifa za hesabu kwa ufasaha zaidi.

Nilibaini kuwa baadhi ya Taasisi zina mifumo ya kipekee ingawa zinatumia EPICOR kulingana na aina ya shughuli zinazofanywa. Hii pia inachangia kutokuwa na mfumo wa majumuisho ya pamoja wa kuandaa Hesabu Jumuifu za Taifa.

Utumiaji wa njia za mfumo usiojiendesha wenyewe katika kuandaa Hesabu Jumuifu huweza kusababisha makosa ya kibinadamu; ambayo hatimaye yanaweza kusababisha kuandaa hesabu zisizo sahihi .Hii husababisha majumuisho ya hesabu na marekebisho kuchukua muda mrefu.

Wakati nakubaliana na changamoto mbalimbali katika kuandaa Hesabu Jumuifu za Taifa, hususani taasisi za Serikali zinzfabya Biashara ambazo hazitumii EPICOR na IPSAS ,Ninaamini kuwa nafasi bado ipo kwa serikali kuweka mfumo unaojiendeshakuandaa katika kuandaa hesabu za Serikali kuu, Serikali za Mitaa na Taasisi Nyinginezo . Hivyo kupunguza makosa ya kibinadamu na kufanya marekebisho na kuyafuatilia na kuandaa taarifa sahihi wakati wote.

Narudia mapendekezo yangu yafuatayo, Serikali (a) Iandae mfumo unaojiendesha katika kuandaa hesabu za Wizara, Serikali za Mitaa na taasisi zinazofanya biashara; (b) Iongeze kasi ya jitihada zake za kuunganisha Balozi za Tanzania katika mfumo wa EPICOR

ili kuimarisha udhibiti wao wa bajeti na uaminifu katika taarifa zao za fedha; (c) Ioanishe taarifa ya Serikali za Mitaa na Wizara,Idara zinazojitegea na Wakala wa Serikali ili kuwa na uwezo wa moja kwa moja wa kuandaa taarifa zao za fedha kutokana na mfumo wa EPICOR; hivyo, kuwa na njia bora ya kuunganisha taarifa za fedha za vyombo vya serikali kwa kutumia EPICOR ingawa utendaji wao umegawanywa.

Kukosekana kwa vigezo vya uthaminishaji kwa ajili ya utoaji wa Pensheni za Serikali shilingi bilioni 597.4 Aya ya 59 ya IPSAS 25 inaeleza ugumu wa kihasibu katika kuonyesha stahili kwa sababu wanatakiwa kupima wajibu na gharama; na kuna uwezekano wa kuwepokwa faida na hasara. Pia, majukumu hupimwa kwa misingi ya punguzo, kwa sababu inaweza kuchukua miaka mingi baada ya wafanyakazi kutoa huduma

Ukaguzi wa Hesabu Jumuifu kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2015 ulibainisha kuwa shilingi bilioni 616.1 zilitolewa na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa ajili ya shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kulipa mafao kwa wastaafu, malipo ya likizo, kesi za kisheria na dhamana ya kifedha. Ukaguzi umebaini kuwa asilimia 97 ya fedha hizo ilikuwa ni kwa ajili ya mifuko ya pensheni kwa wastaafu, wakati kiasi kilichobaki kilikuwa kwa ajili ya likizo za wafanyakazi, kulipa kesi za kisheria, dhamana za fedha na mengineyo.

Ukaguzi zaidi wa hesabu Jumuifu na za taasisi moja moja umebaini kuwa Serikali hutoa mafao yaliyopangwa kwa mpango

maalum. Katika ukaguzi nilibaini kuwa Serikali ilitenga shilingi. 597.4 bilioni kama mafao kwa wastaafu. Hata hivyo, hakuna tathmini ya fedha za mafao iliyofanyika; hivyo, kuna uwezekano kuwa kiasi cha fedha kilichotengwa kinaweza kisiwe sahihi. Hivyo, kukosekana kwa tathmini ya gharama halisi inaweka walakini wa gharama halisi kwani haijulikani kama fedha zilizotengwa ni sawa au sio sawa.

Hivyo ninaishauri Serikali izingatie IPSAS 25 kwa kufanya tathmini na kujua madeni halisi ambayo Serikali inadaiwa.

### 5.1.4 Mali za kibaiolojia hazijabainishwa shilingi bilioni 83.993

Aya ya 39 ya IPSAS Na.27 inaeleza kwamba, "Taasisi itatoa maelezo ya mali za kibaiolojia na kutofautisha kati ya mali za kutumiwa na mali za matumizi ya muda zaidi ya mara moja au zaidi ya mwaka; na kati ya mali za kibiolojia zilizohifadhiwa kwa ajili ya kuuzwa na zilizohifadhiwa kwa ajili ya kusambazwa bila malipo.

Pia, aya ya 42 inasema kwamba, "Katika kuonyesha matakwa ya aya 39, Taasisi inatakiwa kutofautisha kati ya mali za kibaiolojia zilizokomaa na ambazo hazijakomaa kama inavyotakiwa. Tofauti hizi hutoa taarifa ambazo zinaweza kuwa na manufaa katika kutathmini majira ya mtiririko wa fedha na uwezo wa huduma. Taasisi huweka wazi vigezo vya kuonyesha tofauti.

Katika mwaka wa ukaguzi, mali za kibaiolojia ikiwa ni pamoja na ng'ombe wa maziwa,

mizabibu, misitu, miti ya matunda na misitu ya mashamba vilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 84.0. Hata hivyo, taarifa ya mali za kibaiolojia hazikugawanywa kama inavyotakiwa na aya ya 39 ya IPSAS 27. Hata hivyo, ilibainika kuwa, hakuna mwongozo uliotolewa kuhusu namna ambayo Taasisi zinaweza kutaja mali za kibaiolojia. Bila shaka, ukosefu wa mwongozo unaibua wasiwasi juu ya jinsi ya kutoa taarifa ya mali za kibaiolojia katika makundi kwa usahihi; hivyo, kuna mashaka kama taarifa za mali za kibaiolojia zimeelezewa ipasavyo.

Napendekeza kwa serikali: (a) Itoe taarifa za mali za kibaiolojia kwa kufuata IPSAS 27; na (b) Iingize taratibu za kutoa taarifa ya mali za kibaiolojia kwa taratibu za uhasibu na kutoa mwongozo kuongoza Taasisi namna ya kutaja mali za kibiolojia.

## 5.2 Usimamizi wa uwekezaji na maslahi ya Serikali

### 5.2.1 Utangulizi

Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kusimamia uwekezaji na maslahi ya serikali katika mashirika ya umma na taasisi nyingine. Ofisi ya Msajili wa Hazina ilianzishwa kwa Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) sura ya 370 ya mwaka 2002 (marekebisho 2010). Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa jukumu la kudumu la kusimamia uendeshaji wa biashara na mambo ya watumishi na bodi ambapo Msajili wa Hazina anamiliki au ana maslahi napo. Hivyo, Msajili wa Hazina ana wajibu wa kusimamia mitaji ya serikali kwenye uwekezaji ndani ya Mashirika ya Umma na ya Binafsi ambako serikali inamiliki hisa kwa niaba ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hivyo, Serikali imeipa Ofisi ya Msajili wa Hazina jukumu la kufanya kazi kwa kujitegemea kama shirika binafsi kuanzia Julai 2013 kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi uliopo badala ya kufanya kazi kama kitengo chini ya Wizara ya Fedha.

Hoja ya kuiimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina ina lengo la kuimarisha ufanisi katika utendaji na usimamizi wa mashirika ya umma na ya Binafsi ambako serikali inamiliki hisa ili biashara zinazomilikiwa na umma zikusanye rasilimali za kutosha, zifanye matumizi kwa umakini na kwa uwajibikaji zaidi kuliko ilivyokuwa awali.

Ukaguzi wangu kuhusu jinsi Ofisi inavyotekeleza majukumu yake katika kusimamia uwekezaji wa serikali ulibaini changamoto kadhaa kama inavyoonekana hapa chini:

### 5.2.2 Usimamizi usioridhisha wa uwekezaji na maslahi mengine ya serikali

Wakati wa ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, nilibaini kupungua kwa uwekezaji wa serikali na vipaumbele vyake katika mashirika na taasisi nyingine, na wakati mwingine, kupungua kwa hisa zake; na hata mwishowe kuwa hatarini kupoteza hisa hizo.

Hii ilitokana na Serikali kushindwa kuongeza mtaji wakati ulipohitajika kwenye mashirika na taasisi ilizowekeza kama inavyodhiirishwa hapa chini:

a) Ukaguzi wangu wa uwekezaji wa serikali katika makampuni binafsi ulibaini kuwa hisa za serikali zilizopo kwenye baadhi ya makampuni zilipungua kwa sababu serikali

kupitia kwa Msajili wa Hazina ilishindwa kuongeza mtaji wa kupitia fursa ya haki ya kununua hisa za ziada na mpya ilivyopaswa kufanya hivyo. Hivyo, kusababisha umiliki na nguvu ya serikali katika kufanya maamuzi kupungua,hatimaye kupungua kwa uwezo wa serikali kupata gawio. Tatizo hilo la kupungua kwa umiliki lilibainika katika Kiwanda cha kusindika Kahawa (TANICA), Kampuni ya gesi Tanzania (Tanzania Oxygen Ltd) na Tanzania Development Finance Limited katika mwaka huu. Nilibaini kuwa upungufu wa hisa za serikali TDFL ulipunguza umiliki wa Benki ya ABC lakini si moja kwa moja, umiliki ambao ulifanywa kupitia Tanzania Development Finance Limited. Jedwari 20 hapo chini linaonyesha kiwango ambacho hisa za serikali zilipungua kwenye makampuni hayo na mtaji wa nyongeza ambao serikali ilishindwa kuweka.

**Jedwali 20: Orodha ya makampuni ambayo hisa zake zimepungua**

| S/N | Kampuni (Sh. milioni) | Thamani ya awali ya hisa | % ya umiliki | Thamani ya sasa ya hisa | Umiliki | Hasara baada ya hisa kupungua | Mtaji uliohitajika |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kiwanda cha kusindika Kahawa (TANICA) | 188.72 | 10% | 145 | 8% | 43.97 | Hatukupatiwa Taarifa |
| 2 | Tanzania Oxygen Ltd | 526.68 | 9% | 357 | 6% | 169.71 | 428 |
| 3 | Bank ABC via TDFL | 1,060.26 | 6% | - | 3% | - | 2,700 |

Chanzo: Taarifa ya hesabu iliyokaguliwa 2014/2015

b) Wakati wa ukaguzi, nilipitia utendaji wa hisa zilizowekezwa na Serikali kwa washirika wa mradi wa pamoja (Joint ventures), mashirika ambayo Serikali ina hisa chache (associates) na matawi (subsidiaries) na kubaini kuwepo

kwa Taasisi kumi na tisa (19) ambazo uwekezaji wake unatengeneza hasara ambapo Serikali haipati faida. Hasara ya muda mrefu na mapungufu katika Taasisi zimeondoa mtaji wa Serikali kwenye uwekezaji huo. Uwekezaji ndani ya Mashirika ya Umma kama vile Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL), Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), Kampuni ya Reli Tanzania (TRL), Shirika la Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASCO) na Twioga Bancorp umekabiliwa na uhaba mkubwa wa mtaji na kuwafanya washindwe kujiendesha bila ruzuku ya Serikali. Ijapokuwa kinachosababisha hali ya sasa kinaweza kushughulikiwa, lakini umuhimu wa kimkakati kwa nchi ni jambo lisilopingika, hivyo uwezeshwaji wa kifedha kutoka Serikalini unahitajika. Kiambatisho Na.5.2 kinaonyesha orodha ya Taasisi ambazo uwekezaji wake unatengeneza hasara.

c) Kwa ujumla, ukosefu wa Mfuko kwa ajili ya Uwekezaji huathiri uwekezaji wa Serikali na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Kwa mwenendo huu, wanahisa makini katika makampuni mengine wanaweza kushawishika kutumia fursa ya ufinyu wa bajeti Serikalini na kuamua kuwekeza wakati Serikali haina fedha na kupelekea umiliki wa Serikali kwenye makampuni kupungua. Kwa maoni yangu, ukosefu wa Mfuko wa Uwekezaji huathiri urekebishaji (restructuring) wa Mashirika ya Umma na kusababisha hisa za Serikali kupungua pale ambapo Serikali ina umiliki.

### 5.2.3 Ushiriki hafifu wa Msajili wa Hazina katika Mkutano Mkuu wa mwaka katika Taasisi ambazo kuna uwekezaji wa Serikali

Kwa kutambua jukumu la Msajili wa Hazina la kusimamia uwekezaji, nilifanya tathmini ya uwezo wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kifedha na nilibaini kuwa Msajili wa Hazina anategemea ruzuku kutoka Serikalini ambayo haikidhi mahitaji ya kuweza kusimamia vema mashirika ya umma na binafsi ambapo Serikali ina umiliki wenye thamani ya shilingi bilioni 22,678.16 hadi tarehe 30 Juni, 2015. Ofisi ya Msajili wa Hazina hukusanya gawio, mapato mengineyo, na michango kutoka katika makampuni wanayoyasimamia. Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, jumla ya shilingi bilioni 161.14 (2014: bilioni 108.71) zilikusanywa ikilinganishwa na makisio ya Shilingi bilioni 142.39, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18. Hata hivyo, mapato yote kutoka kwenye mashirika yalipelekwa Serikalini kwa sababu Msajili wa Hazina hayupo kwenye mpango wa bakizo (retention scheme) kwa sasa. Kwa hiyo, uwezo wa Msajili wa Hazina kutekeleza majukumu yake ni mdogo.

Kukosekana kwa Mfuko wa Serikali kwa ajili ya uwekezaji kumesababisha mapungufu yaliyojitokeza na kuifanya Ofisi ya Msajili wa Hazina kushindwa kuongeza mtaji kwenye makampuni ambayo Serikali ina uwekezaji pale inapohitajika. Ukosefu wa fedha husababisha maslahi na uwekezaji wa Serikali kwenye mashirika hayo kuwa kwenye hatari ya kupata hasara au kupungua, hatimaye kupoteza umiliki wa Serikali na taifa kwa ujumla. Kwa maoni yangu, ili Serikali iweze kujikwamua kwenye changamoto zilizojitokeza katika kusimamia hisa zilizowekezwa pamoja na maslahi mengine

hatua zifuatazo zinapaswa kuchukuliwa:

a) Serikali ianzishe Mfuko kwa ajili ya uwekezaji kutokana na mapato yanayopokelewa yatokanayo na gawio pamoja na mapato mengineyo na kuunda Mfuko wa uwekezaji kwa ajili ya mtaji wa kuwekeza pale ambapo makampuni ambayo Serikali imewekeza yanahitaji kuongezewa mtaji au kushiriki kuwekeza katika fursa nyingine. Hii inahusisha Serikali kuruhusu Msajili wa Hazina kubakiza makusanyo kwa muda utakaopangwa (kwa mfano kwa miaka minne hadi mitano);na hivyo, na hivyo kujiendesha kama ninavyoshauri hapa chini.

b) Serikali kupitia Wizara ya Fedha ianzishe mpango wa bakizo (retention scheme) kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ili Mfuko wa Uwekezaji nili0pendekezwa uanzishwe. Mpango huo utatumika kama chombo cha kupima utendaji wa Msajili wa Hazina na kuwezesha Serikali kutathmini uwezo wa Msajili wa Hazina kupata mapato kutokana na uwekezaji.

c) Menejimenti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ianzishe mfumo ambao utahakikisha Serikali inawakilishwa vema na inashiriki katika kufanya maamuzi ya makampuni ambayo Serikali ina hisa kwa ajili ya manufaa ya umma. Hii itasaidia kuhakikisha Serikali inashiriki kikamilifu kwenye Mikutano mikuu ya mwaka na vikao vingine vya kufanya maamuzi.

### 5.2.4 Usimamizi wa Madeni yaliyo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina

Nilifanya ukaguzi wa majukumu ya kifedha ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2015. Pia, nilipitia namna ofisi inavyosimamia mikopo na dhamana iliyotolewa na Serikali kwa Mashirika ya umma na makampuni, madaftari

ya madeni, kumbukumbu za uwekezaji wa Taasisi za Serikali na uwezo wa kurejesha madeni yake.

Pia nilibaini kuwa dhamana nyingi zilishindwa kurejeshwa, na madeni mengi yasiyotokana na uwekezaji ambayo Serikali ina mkataba nayo hatimaye yalihamishiwa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Madeni yanayotokana na fidia, pensheni na maamuzi ya mahakama yasiyohusiana na uwekezaji yalihamishiwa Ofisi ya Msajili wa Hazina kutoka Wizara ya Fedha. Pia, dhamana zilizokwisha muda wake ambazo kimsingi ni deni la Taifa hazikuweza kuhamishiwa katika idara sahihi ambayo inasimamia madeni ya Serikali.

Pia, nilibaini kuwa madeni yote yasiyo ya uwekezaji ambayo yanahudumiwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina, yalihudumiwa kupitia Mfuko mkuu wa Serikali. Madeni hayo jumla yake ilifikia kiasi cha shilingi bilioni 674.95 ukiondoa dhamana zilizokwisha muda wake kiasi cha Dola za Kimarekani bilioni 139.9, deni la shilingi bilioni 473.4 kwa Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (PSPF) na madeni mengine ya shilingi bilioni 61.7. Hivyo, napata wasiwasi kuhusu uwezo wa Ofisi ya Msajili wa Hazina kushughulikia madeni makubwa ambayo hayahusiani na kazi ya msingi ya Ofisi hiyo wala hayaendani na bajeti ya Msajili wa Hazina. Kwa maoni yangu,kulingana na asili ya madeni haya yanastahili kuwekwa chini ya Ofisi ya Deni la Taifa (Idara ya Usimamizi wa Madeni). Kwa msingi huu, napendekeza hatua zifuatazo kuchukuliwa:

Serikali irekebishe na kuweka madeni katika mafungu yasiyo ya uwekezaji na dhamana

zilizopita muda wake kisha kuyahamisha Ofisi ya Deni la Taifa ili kuiwezesha Serikali kuunda usimamizi na muundo wa ulipaji wake. Hili linaweza kufanyika kwa Serikali kutoa dhamana (bonds) ambazo zitatumika kama chombo kwa ajili ya kurekodi na kulipa madeni hayo chini ya fungu sahihi.

a) Ofisi ya Msajili wa Hazina ipitie taarifa za madeni yake na kuandaa bajeti ya kutosha kila mwaka ili kulipa madeni yake yaliyobaki ambayo yanahusiana na uwekezaji pale yanapohitajika kulipwa. Hii itaepusha mkusanyiko zaidi wa madeni.

## 5.3 Ukaguzi Mamlaka ya Mapato Tanzania

### 5.3.1 Utangulizi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria Na.11 ya mwaka 1995 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na.8 ya mwaka 1996 ikiwa na majukumu ya kusimamia na kukusanya mapato ya kodi kwa niaba ya Serikali.

Mamlaka inatayarisha aina mbili za Taarifa za Fedha; Taarifa za Mapato na Taarifa ya Hesabu ya Matumizi. Taarifa ya Hesabu za Matumizi inaandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma visivyo vya misingi na taslimu (IPSAS Accrual basis of accounting) wakati zile za Mapato zinaandaliwa kwa kutumia Viwango vya Kimataifa vya kihasibu katika Sekta ya Umma kwa misingi ya fedha taslimu.

### 5.3.2 Mwelekeo wa Utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita

Katika barua ya mapungufu iliyopita 2013/2014, mapendekezo thelathini na tano (35) yalitolewa kwa mwaka wa fedha unaoisha

tarehe 30 Juni 2014 na mapendekezo sabini na tisa (79) hayajafanyiwa kazi toka mwaka wa fedha 2001/2002 mpaka 2012/2013. Nimepitia hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa jumla ya mapendekezo mia moja na kumi na manne (114). Kati ya hayo 59 (52%) yanahusiana na kitengo cha forodha na ushuru wa bidhaa, 26 (23%) yanahusiana na kitengo cha walipakodi wakubwa na 29 (25%) kitengo cha mapato ya ndani kama ilivyoainishwa hapa chini:

| Na. | Mwaka | Kitengo cha Forodha na Ushuru wa Bidhaa | Kitengo cha walipakodi wakubwa | Kitengo cha mapato ya ndani | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2001/2002 | 1 | 0 | 0 | 1 |
| 2 | 2002/2003 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 3 | 2003/2004 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| 4 | 2004/2005 | 2 | 0 | 0 | 2 |
| 5 | 2005/2006 | 4 | 0 | 0 | 4 |
| 6 | 2006/2007 | 3 | 0 | 0 | 3 |
| 7 | 2007/2008 | 5 | 1 | 1 | 7 |
| 8 | 2008/2009 | 2 | 2 | 2 | 6 |
| 9 | 2009/2010 | 4 | 2 | 2 | 8 |
| 10 | 2010/2011 | 3 | 4 | 3 | 10 |
| 11 | 2011/2012 | 5 | 5 | 0 | 10 |
| 12 | 2012/2013 | 13 | 6 | 8 | 27 |
| | **Jumla ndogo** | **42** | **20** | **17** | **79** |
| 13 | 2013/2014 | 17 | 6 | 12 | 35 |
| | **Jumla kuu** | **59** | **26** | **29** | **114** |

Kati ya mapendekezo 114, arobaini na tatu (38%) yalitekelezwa, arobaini na tatu (38%) yalikua chini ya utekelezaji na ishirini na nane (24%) hayakutekelezwa kabisa. Muhtasari wa mwelekeo wa utekelezwaji wa mapendekezo kwa vitengo vyote vitatu umeonyeshwa katika Jedwali 21 hapo

chini. Aidha maelezo zaidi kuhusu mapendekezo na mwelekeo wa utekelezaji yametolewa katika kiambatisho namba 1 katika barua ya mapungufu.

**Jedwali 21: Muhtasari wa utekelezaji wa mapendekezo ya miaka iliyopita**

| Mwelekeo | Kitengo cha Forodha na Ushuru wa Bidhaa | Kitengo cha Walipakodi wakubwa | Kitengo cha Mapato ya ndani | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Yaliyotekelezwa | 28 | 1 | 14 | 38 |
| Chini ya utekelezaji | 11 | 20 | 12 | 38 |
| Hayajatekelezwa | 20 | 5 | 3 | 24 |
| **Jumla** | **59** | **26** | **29** | **100** |

Jumla ya Mapendekezo yakiyoko chini ya utekelezaji na yale ambayo hayajatekelezwa ni sabini na moja (71). Mapitio zaidi ya utekelezaji wa mapendekezo yaligundua kuwa, kati ya jumla ya mapendekezo yaliyotolewa, kesi ishirini na tisa (29) sawa na asilimia 41 yanahiitaji maamuzi ya mamlaka nje ya Mamlaka ya mapato Tanzania kama vile Bodi za rufaa ya kodi, Mahakama ya rufaa ya Tanzania na Bunge kwa madeni ya kodi yaliyopendekezwa na Hazina kwa ajili ya kufutwa. Maamuzi ya kesi hizo na kufutwa kwa madeni kumesubiriwa kwa muda toka mwaka wa fedha 2001/2002. Aidha, kiasi cha kesi arobaini na mbili (42) sawa na asilimia 59 kilichobaki kinashughulikiwa na menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.
Kulingana na uhalisia wa mapendekezo husika, mwelekeo wa utekelezaji unaridhisha, ila menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania inatakiwa kuongeza jitihada katika utekelezaji wa mapendekezo yaliyoko chini ya utekelezaji ili kukomboa mapato yaliozuiwa kutokana

na mapungufu yaliyoainishwa na kukuza upatikanaji wa mapato zaidi.

### 5.3.3 Mwelekeo wa Mapato Tanzania

Katika ukaguzi huu, Mamlaka ya Mapato ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 10,744 dhidi ya malengo yaliyowekwa ya Shilingi bilioni 12,078. Hii inayoonesha upungufu katika ukusanyaji wa shilingi bilioni 1,334 ambazo ni sawa na asilimia 11 ya jumla ya makisio au malengo. Jumla ya makusanyo mbali na shilingi bilioni 29 zinazojumuisha misamaha ya kodi iliyotolewa na serikali, mapato halisi ya mwaka wa fedha 2014/2015 ni shilingi bilioni 10,773. **Jedwali Na.22** linaonyesha jumla ya makisio na makusanyo ya mapato toka Tanzania bara na visiwani:

**Jedwali 22: Jumla ya makusanyo kwa mwaka 2014/15 (Shilingi kwa mamillion)**

| Idara | Lengo- Tanzania bara na visiwani | Makusanyo halisi kwa Tanzania bara na visiwani | Makusanyo pungufu | Makusanyo pungufu kwa asilimia | Asilimia ya makusanyo kwa Idara |
|---|---|---|---|---|---|
| Mapato ya ndani | 2,120,063 | 1,974,958 | 145,106 | 7 | 18 |
| Walipakodi wakubwa | 5,489,128 | 4,611,058 | 878,071 | 16 | 43 |
| Forodha na ushuru wa bidhaa | 4,468,823 | 4,157,749 | 311,073 | 7 | 39 |
| **Jumla** | **12,078,015** | **10,743,765** | **1,334,250** | **11** | **-** |
| **Vocha** | 43,179 | 29,459 | 13,719 | 32 | 0.27 |
| **Jumla kuu** | **12,121,193** | **10,773,224** | **1,347,969** | **11** | **100** |

**Chanzo:** Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu za mwaka *2014/15*

Kwa ujumla, makusanyo yote katika idara zote tatu hayakufikia malengo kwa mwaka huu. Hata hivyo, Idara ya Walipa kodi wakubwa ndiyo iliyoshindwa kufikia lengo kwa kiasi kikubwa kwa asilimia 16. Idara hii ilishindwa kufikia

lengo kwa asilimia 16 ikilinganishwa na idara ya Forodha na Ushuru wa bidhaa na idara ya kodi za ndani zilizoshindwa kufikia lengo kwa asilimia 7.

**Kielelezo Na. 8** kinachofuata kinaonyesha kwamba, Idara ya walipakodi Wakubwa ilikusanya asilimia 43 ya makusanyo halisi ambayo ndiyo sehemu kubwa kuliko zote; ikifuatiwa na Idara ya Forodha yenye asilimia 39; na kodi za ndani asilimia 18 ambayo ndiyo ya mwisho kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ukitoa hati za malipo ya Hazina.

**Kielelezo 8: Asilimia ya Makusanyo halisi Kwa Idara kwa mwaka 2014/15**




### 5.3.4 Ufanisi wa Kodi na Mwelekeo wa Mapato

Mwelekeo wa makusanyo ya mapato kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, kwa wastani, ulikuwa chini ya makadirio yaliyoidhinishwa, isipokuwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ambapo makusanyo halisi yalikuwa chini ya

makadirio kwa asilimia 4. Kwahiyo kulikuwa na mwelekeo wa ongezeko la ufanisi wa mapato (uwiano wa kodi dhidi ya pato la jumla la ndani (GDP)) kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita hadi kufikia asilimia 17 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kabla ya kupungua na kufikia asilimia 13 mwaka huu. Kupungua Kwa uwiano wa kodi dhidi ya pato la jumla la ndani kumesababishwa na mabadiliko kwenye mfumo wa ukokotoaji wa zao la jumla la ndani ambapo limeongezeka kwa asilimia 17 ukilinganisha na mwaka 2013/14.

Kwa ujumla, uwiano wa kodi dhidi ya pato la ndani bado liko chini ya asilimia 19.9 ya lengo lililowekwa na Mamlaka ya Mapato kufikia mwaka 2018. **Jedwali Na.23** hapo chini linaonyesha mwelekeo wa makusanyo na uwiano wa kodi dhidi ya pato la ndani kwa kipindi cha miaka mitano kwa Tanzania na nchi nyingine za Afrika Mashariki.

**Jedwali 23: Ufanisi kwa ujumla katika makusanyo ya mapato Tanzania (shilingi kwa milioni)**

| Maelezo | Mwaka wa fedha | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 |
| Lengo | 5,721,831 | 6,329,413 | 7,978,158 | 10,957,001 | 12,078,015 |
| Makusanyo halisi | 5,443,592 | 6,586,585 | 7,912,304 | 10,026,659 | 10,743,765 |
| Tofauti ya lengo na makusanyo | -278,239 | 257,172 | -65,854 | -930,342 | -1,334,250 |
| Tofauti ya lengo na makusanyo kwa asilimia | -5 | 4 | -1 | -8 | -11 |
| **Uwiano wa kodi dhidi ya zao la jumla la ndani (Tax/GDP)** | | | | | |
| **Tanzania** | 15.54% | 15.80% | 16.00% | 16.90% | 12.78% |
| **Uganda** | | | | 13.30% | 12.77% |
| **Kenya** | | | | 22.10% | 16.34% |
| **Rwanda** | | | | 14.90% | 14.20% |

***Chanzo: Takwimu za Mamlaka ya Mapato Tanzania, 2014/2015***

Kutokana na uchambuzi wa malengo dhidi ya makusanyo, makusanyo halisi katika asilimia ya makadirio yalikuwa ni asilimia 96 kwa wastani kwa muda wa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Hii ipo chini ya malengo kwa asilimia 4 mbali na mwaka 2011/12. Hata hivyo, makusanyo ya mwaka wa fedha 2014/2015 yapo chini kwa asilimia 11 ya makadirio, kiwango cha juu zaidi kuripotiwa katika miaka mitano iliyopita.

Kwa upande mwingine, mchanganuo linganifu wa ufanisi wa kodi kwa nchi za Afrika Mashariki unaonyesha kwamba, Tanzania iko nafasi ya tatu nyuma ya Kenya na Rwanda, na mbele ya Uganda katika uwiano wa zao la kodi dhidi ya zao la ndani la jumla. Kwa kuzingatia mwelekeo linganifu wa Kenya na Rwanda, ninaonelea kwamba, ufanisi wa kodi wa Tanzania kwa pande zote mbili za zao halisi na zao lengwa, zinaacha fursa ya maboresho zaidi ya kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato.

### 5.3.5 Mambo yanayokwaza kutofikia malengo ya makusanyo Tanzania

Ufuatiliaji wa misamaha ya kodi na majeresho ya kodi kwa walipa kodi waliosamehewa ni mdogo sana. Hii inasababisha walipa kodi wasio waaminifu kutumia vibaya fursa hii na kuisababishia serikali kupoteza mapato. Sababu kuu ni hizi zifuatazo:

(a) Misamaha ya kodi haijalenga moja kwa moja mikakati ya kiuchumi, hivyo kusababisha misamaha mingine kulenga maslahi ya mtu au kundi la watu na siyo kazi au taasisi husika ili kukuza uchumi au kusaidia jamii kiuchumi kama ilivyokusudiwa. Hii inasababisha mifumo wa ulipaji kodi kukosa

usawa na kuwa na mifumo wa kiubaguzi.

(b) Suala la misamaha ya kodi na motisha ya ulipaji halijamafanikiwa;kuna misamaha ambayo imewalenga zaidi watu binafsi au makampuni kuliko sguhghuli za kiuchumi kama ilivyopaswakuwa.Hali hii hudhoofisha dhana nzima ya misamaha;pia hujenga matabaka katika mfumo wa ulipaji kodi.

(c) Kaguzi na uchunguzi huhusu kodi haufanyiki ipasavyo na hata muda mwingine ukifanyika, ufuatiliaji na ukusanyaji wa kodi zilizopatikana haukuweka msisitizo unaostahili. Nimegundua kuwa Mamlaka imeshindwa kukusanya riba na faini stahiki kwa walipa kodi waliochelewa kulipa kodi zilizotokana na kaguzi na chunguzi zilizofanyika.

(d) Aidha, nimebaini udhaifu kwenye mifumo ya ufuatiliaji wa walipa kodi wasiofaili mapato yao ya mwezi na ya mwaka, uuzianaji wa bidhaa kwa makampuni yenye uhusiano (transfer pricing arrangements), uwepo wa biashara bubu au zisizo rasmi na vyanzo vidogo vya mapato. Tumeona pia kiwango kidogo cha ufuatiliaji na usimamizi wa matumizi yam ashine za kielekroniki “Electronic Fiscal Devices (EFD)” kwa walipakodi wanaokidhi vigezo na hata walio na kifaa hicho hawavitumii wakati wote kama inavyohitajika.

(e) Udhaifu kwenye mifumo na ufuatiliaji wa utoaji wa mizigo iliyoingizwa nchini na ile inayosafirishwa kwenda nchi nyingine kupitia nchi yetu (in transit), mifumo ya upekuzi wa forodha na maghala ya mali. vifurushi na makontena.

(f) Mapungufu kwenye utaratibu wa ukaguzi wa mafuta ya petrol yanayoingia nchini na yanayoenda nchi zingine kupitia bandari yetu (transit fuel) na ukosekanaji wa kifaa madhubuti cha kupimia mafuta "flow meters" na tenki la akiba la Serikali bandarini vimeonekana kuwa moja ya visababishi vya upotevu wa mapato kwa serikali katika sekta ya mafuta.

(g) Walipa kodi hawana utamaduni wa kuhifadhi taarifa ya kodi; makampuni ya Kimataifa huamisha faida kupitia kuongeza bei na kuhamisha bei za bidhaa.

Napendekeza Serikali ihakikishe kuwa mikakati ya usimamizi madhubuti wa kodi inaimarishwa na inapewa kipaumbele ili kuongeza wigo wa mapato ili hatimaye iongeze ufanisi kwenye makusanyo hasa katika maeneo yafuatayo;

#### 5.3.6.1 Usimamizi wa Misamaha na Marejesho ya kodi

(a) Serikali iendelee kupitia sera na kanuni za kodi ili kuondoa misamaha isiyo na tija kwa nchi. Hii inaweza kufanyika kwa Mamlaka ya mapato kuongeza ufanisi kwenye uchunguzi na usimamizi madhubuti wa mifumo ya ulipaji wa misamaha ya kodi, pia iongeze ufanisi kwenye ufuatiliaji na uchunguzi kwa walengwa wa misamaha ya kodi ili kujiridhisha kama ilitumika ilivyokusudiwa.

(b) Serikali iendelee kusisitiza uwazi kwenye misamaha ya kodi kupitia machapisho ya misamaha ya kodi na ripoti ya mwaka ya

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuuu wa Hesabu za Serikali.

(c) Serikali iimarishe usimamizi wa marejesho ya kodi na kuongeza mifumo dhabiti ya ukaguzi wa nyaraka za kudai marejesho ili kuondokana na madai batili kutoka kwa mtandao wa walipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT network). Pia isisitize utoaji na matumizi ya mashine za kielekitroniKI (EFD) kwa wafanyabishara wanaostahili.

**5.3.6.2 Kaguzi na pelelezi za walipakodi**

(a) Serikali iimarishe ukaguzi na kuweka mikakati madhubuti ili kupunguza ukwepaji wa kodi.

(b) Serikali isamehe sehemu ya riba na faini kwa walipa kodi walioradhi kulipa madeni yao na kuweka mbadala wa kuyalipa kwa vipindi ili kuwawekea mazingira mazuri ya kuwa waaminifu na kuendelea kulipa kodi zijazo kwa wakati.

**5.3.6.3 Usimamizi madhubuti wa bidhaa na mafuta yanayoingizwa nchini**

(a) Serikali iimarishe upekuzi na ukaguzi wa bidhaa zinazoingia kwa matumizi nchini na zinazokwenda nchi zingine kupitia nchini hazitumika nchini kinyemela bila kulipa kodi stahiki; na endapo zimeuzwa katika soko la ndani, mamlaka ikusanye kodi stahiki kwa mujibu wa sheria.

(b) Serikali iendelee kusisitiza matumizi ya “off-bond meters” na kuweka

au kujenga Tenki la akiba la mafuta (National Reserve Tank (RT)) kwa kila bandari ya kuingilia ili kuhakikisha kuwa taarifa za mafuta yanayoingizwa nchini zinaandikwa sawasawa na usimamizi wa utoaji mafuta unaimarishwa sambamba na ulipaji wa kodi zinazotakiwa. Matumizi ya "flow meters" na tenki la akiba (Reserve tank) yatasaidia Mamlaka kuwa na taarifa sahihi ya mafuta yaliyoingia na yanayotoka; na hatimae kuimarisha makusanyo kwenye mafuta yanayoagizwa.

**5.3.6.4 Masuala maalum yaliyoonekana katika ukaguzi wa mwaka 2014/15**

Sehemu hii inatoa taarifa juu ya maeneo makuu matatu ambayo yanahitaji usimamizi na uangalifu wa karibu wa menejimenti ya Mamlaka ya Mapato ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato. Maeneo hayo muhimu ni; Usimamizi wa pingamisi za Kodi, Usimamizi wa Misamaha ya Kodi na Usimamizi wa Makusanyo ya Kodi.

**5.3.6.5 Usimamizi wa Pingamizi za Kodi: Kesi za muda mrefu katika bodi za rufaa ya kodi sshilingi bilioni 6850**

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kwamba, Mamlaka ya Mapato ina kesi zilizo katika bodi za rufaa na Mahakama ya rufaa za kodi kwa muda mrefu zenye jumla ya shilingi bilioni 6850; ambapo kiasi cha shilingi bilioni 187 kimekwama katika Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, shilingi bilioni 2,780 kimekwama katika Mahakama ya Rufaa za Kodi, na kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 3,883

kinasubiri maamuzi katika bodi ya rufaa za kodi kama taarifa inavyoonekana kwenye Jedwali Na.24 hapo chini:

**Jedwali 24: Muhtasari wa kesi zilizo katika Bodi ya Rufaa za Kodi na Mahakama ya Rufaa Tanzania**

| Na. | Mwaka | Bodi ya rufaa za kodi (Tax Appeals Board) | | Mahakama ya Rufaa za Kodi ( Tax Appeals Tribunal) | | Mahakama ya rufaa Tanzania ( Court of Appeals) | | Jumla Kuu | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | USD ("000") | TZS. ("000'000") | USD ("000") | TZS. ("000'000") | USD ("000") | TZS. ("000'000") | USD ("000") | TZS. ("000'000") |
| 1 | 2001 | - | 65 | - | - | - | - | - | 65 |
| 2 | 2002 | - | 26,863 | - | 85,071 | - | - | - | 111,934 |
| 3 | 2003 | - | 10,178 | - | 22,444 | - | - | - | 32,622 |
| 4 | 2004 | 15,009 | 165,069 | - | 472 | - | - | 15,009 | 165,541 |
| 5 | 2005 | 11,763 | 8,863 | 20,595 | 1,420 | - | 21,357 | 32,358 | 31,640 |
| 6 | 2006 | 6 | 18,531 | 53,980 | 6,244 | - | 234 | 53,986 | 25,009 |
| 7 | 2007 | 60 | 55,270 | 9,669 | 25,945 | - | 2,880 | 9,729 | 84,095 |
| 8 | 2008 | 40 | 54,775 | - | 2,389 | 3,198 | 22,609 | 3,238 | 79,773 |
| 9 | 2009 | - | 106,491 | - | 14,393 | - | - | - | 120,884 |
| 10 | 2010 | 4,037 | 267,553 | - | 2,462,166 | - | - | 4,037 | 2,729,719 |
| 11 | 2011 | 215,211 | 49,333 | 107,888 | 6,877 | - | 35,363 | 323,099 | 91,573 |
| 12 | 2012 | 15,931 | 128,429 | 35,740 | 30,977 | - | 30,821 | 51,671 | 190,227 |
| 13 | 2013 | 112,998 | 179,459 | 220,919 | 85,424 | - | 50,114 | 333,917 | 314,997 |
| 14 | 2014 | 4,899 | 390,993 | - | 16,407 | - | 9,384 | 4,899 | 416,784 |
| 15 | 2015 | 63,291 | 355,824 | 45,956 | 48,866 | - | 7,672 | 109,247 | 412,362 |
| | **Total** | **443,245** | **1,817,696** | **494,747** | **2,809,095** | **3,198** | **180,434** | **941,190** | **4,807,225** |
| | Kiwango cha kubadilisha fedha kilichotumika: TZS. 2170/USD | | | | | | | | |
| Jumla TZS. | | 2,779,537,650,000 | | 3,882,695,990,000 | | 187,373,660,000 | | 6,849,607,300,000 | |
| A | Jumla ya mapato yaliyokwama katika kesi (TZS. Milioni ) | | | | | | | **6,849,607** | |
| B | Bajeti ya mwaka 2014/15 (Sh. Milioni ) | | | | | | | 22,769,100 | |
| C | Sehemu ya mapato ya kodi kwa asilimia ya bajeti (A/B*100) | | | | | | | 30% | |
| D | Pato la jumla la ndani kwa mwaka 2014/15 (Sh. Milioni ) | | | | | | | 84,279,922 | |
| E | Sehemu ya mapato ya kodi kwa asilimia ya zao la ndani (GDP) (A/D*100) | | | | | | | 8% | |

**Chanzo: Ripoti za mapato za Mamlaka ya Mapato Tanzania na daftari la kesi, 2014/15.**

Ikilinganishwa na taarifa yangu ya mwaka wa fedha uliopita, mapato yaliyokwama katika rufaa yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1,716 hadi shilingi bilioni 6,850 kwa mwaka 2014/15 ambayo ni ongezeko la shilingi milioni 5,133,607 sawa na asilimia 299. Uchanganuzi wangu unaonyesha mapato yaliyokwama katika rufaa ni asilimia thelathini (30%) ya bajeti ya mwaka 2014/2015 na asilimia nane ya zao la jumla la ndani (GDP). kwa mwaka 2014/2015. Hivyo thamani ya kodi inayobishaniwa katika bodi ya rufaa ya kodi na mahakama ya rufaa za kodi iko juu na serikali inaingia gharama katika kuendesha kesi hizi kwa muda mrefu, na hasara kwenye mapato pale mrufani atakapofilisika kabla ya kesi kuamuliwa.

Nasisitiza kuhusu utekelezwaji wa mapendekezo yangu niliyoyatoa katika ripoti ya mwaka wa fedha 2013/14 kwamba: (a) usikilizwaji wa kesi hizi ufanyike haraka na Mahakama (b) Kwa suluhisho la kudumu, napendekeza kwa serikali kuunda kamati huru ya kusikiliza rufani, na (c) menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kuongeza nguvu na kuboresha mchakato wa ukaguzi na uchunguzi ili kupunguza malalamiko kati ya Mamlaka na walipakodi.

### 5.3.6.6 Kasoro zilizoonekana katika mapingamizi ya Kodi na Mifumo ya ushawishi ya ulipaji Kodi

Ukaguzi wangu wa mapingamizi za kodi na mifumo ya ushawishi ya ulipaji kodi ulibaini kasoro zifuatazo:

**Kesi za muda mrefu dhidi ya mapingamizi za shilingi 580,718,607,384**

Katika mwaka wa fedha 2014/15, jumla ya mapingamizi 211 ya kodi kutoka kwa walipa kodi zenye thamani ya shilingi 782,457,354,243 yailiwasilishwa katika Mamlaka ya Mapato yakipinga kiasi cha kodi kilichokokotolewa na kufanyiwa tathmini na Kamishna wa kodi. Katika idadi hiyo, mapingamizi 55 sawa na asilimia ishirini na sita (26%) yenye thamani ya shilingi 201,738,746,859 yalifanyiwa upembuzi yakinifu na kushughulikiwa ipasavyo na Kamishna wa Kodi. Mapingamizi yaliyobaki 156 sawa na asilimia sabini na sita (76%) yenye thamani ya shilingi 580,718,607,384 hayakushughulikiwa ipasavyo na kutolewa maamuzi hadi tarehe 31 Juni, 2015. Kuwepo kwa mapingamizi mengi ya kodi ambayo hayashughulikiwi kwa wakati na kutolewa maamuzi unatokana na upungufu wa wataalamu na rasilimali watu katika Mamlaka ya Mapato wa kushughulikia mapingamizi ya kodi ikilinganishwa na idadi ya mapingamizi yaliyoletwa na walipa kodi.

**Fedha za Amana ambazo hazikukusanywa kutokana na mapingamizi ya Kodi shilingi 191,935,854,277**

Ukaguzi wa maombi ya mapingamizi ya kodi kutoka kwa walipa kodi katika mwaka wa fedha wa ukaguzi ulibaini kuwa, Mamlaka ya Mapato ilishindwa kukusanya shilingi 191,935,854,277 ambazo ni fedha za amana zinazotokana na malipo yaliyotakiwa kulipwa ikiwa ni moja ya tatu ya kiasi cha kodi kilichofanyiwa tathmini na kutakiwa kulipwa na walipa kodi au kiasi cha kodi ambacho hakipo katika pingamizi, chochote kitakachokuwa kikubwa kinyume na Kifungu Na. 12 (3) ya Sheria ya Rufaa ya Mapato ya Kodi ya mwaka 2000 (Iliyorekebishwa mwaka 2006).

Kutokukusanywa kwa fedha hizi kunachangia kwa kiasi kikubwa walipa kodi kutumia mwanya huu kukwepa kulipa kodi. Hii inatokana na kutokuwepo kwa ufanisi katika kushughulikia mifumo ya pingamizi za kodi, hivyo kusababisha mapato ya serikali kutokukusanywa kwa wakati. Hii inasababisha kutokufikiwa kwa makadirio ya makusanyo ya mapato ya Serikali, hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango ya Serikali.

Ninaishauri Serikali;

(a) Kuongeza jitihada za kushughulikia kesi za mapingamizi aa kodi yaliyoletwa na walipa kodi kwa wakati ili kutoa maamuzi sahihi juu ya kodi sahihi inayopaswa kulipwa kwa wakati. Hili

linawezekana kwa kuongeza idadi ya watumishi wenye utaalamu na ujuzi pamoja na kuwaongezea mafunzo ya kimbinu watumishi wote walio katika kitengo cha Huduma za Kiufundi ili kuboresha hatua za kutoa tathmini ya kodi inayopaswa kulipwa kwa Wakati, hivyo kupunguza idadi kubwa ya kesi za pingamizi za kodi ambazo zinachelewa kushughulikiwa.

(b) Kuangalia mahitaji ya kisheria ya kukusanywa kwa amana ya kodi inayotokana na ama moja ya tatu ya kiasi cha kodi kilichofanyiwa tathmini na kutakiwa kulipwa na walipa kodi au kiasi cha kodi ambacho hakipo katika pingamizi chochote kitakachokuwa kikubwa kabla mlipakodi hajaleta pingamizi la kulipa kodi kwa ajili ya kusikilizwa.

**5.3.6.7 Usimamizi wa Misamaha ya Kodi**

Serikali kwa kupitia Mamlaka ya Mapato, ilitoa misamaha ya kodi kwa ajili ya shughuli maalum zilizoainishwa katika sharia za kodi mbalimbali kama vile uwekezaji katika bidhaa za mtaji kwa kipindi maalum ili kuvutia uwekezaji kutoka nje ya nchi. Pamoja na kukuza sera maalum za kiuchumi kama vile kuhamasisha uwekezaji katika sekta maalum, kuendeleza uhusiano na mataifa mengine kwa kutoa misamaha kwa shughuli za kidiplomasia na kwa sababu za kibinadamu.

Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2014/15 zinaonyesha misamaha ya kodi yenye jumla ya shilingi bilioni 1,627 ikiwa ni punguzo la shilingi

bilioni 207 (asilimia 11) ikilinganishwa na misamaha ya kodi iliyotolewa mwaka 2013/14 yenye thamani ya shilingi bilioni 1,834 (**Kiambatanisho Na. 5.3**)

Ingawa kiasi cha misamaha ya kodi iliyotolewa katika mwaka huu wa fedha kimepungua, kiasi kilichotolewa bado ni kikubwa kwani ni asilimia mbili (2) ya pato la ndani (GDP) kwa mwaka 2014/15 ikilinganishwa na malengo ya Serikali ya kupunguza misamaha ya kodi kuwa chini ya asilimia moja (1) ya pato la ndani (GDP). Jitihada za kupunguza misamaha ya kodi itasaidia Mamlaka ya Mapato kuongeza uwezo wake wa kukusanya kodi, hivyo kufikia malengo yaliyowekwa. Mwenendo wa misamaha ya kodi iliyotolewa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 25** hapo chini;

**Jedwali 25: Mwenendo wa Misamaha ya Kodi kuanzia mwaka 2010-2015 (shilingi kwa Milioni)**

| Mwaka | Pato la mwaka | Jumla ya Misamaha ya Kodi | Asilimia ya Misamaha ikilinganisha na pata la Taifa |
|---|---|---|---|
| 2010/11 | 35,026,679 | 1,016,320 | 2.9 |
| 2011/12 | 41,125,313 | 1,806,204 | 4.39 |
| 2012/13 | 48,385,100 | 1,515,607 | 3.13 |
| 2013/14 | 55,619,077 | 1,834,097 | 3.3 |
| 2014/15 | 84,279,922.20 | 1,627,012 | 1.93 |

Kutokana na mchanganuo hapo juu, kiasi cha misamaha ya kodi cha asilimia ya pato la Taifa la jumla (GDP) kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kilikuwa asilimia 3 ya GDP, kwa wastani, ambacho bado kiko juu ikilinganishwa na lengo la

asilimia moja ya pato la Taifa au asilimia tano ya makusanyo yote (Rejea bajeti kuu ya Serikali ya mwaka 2013/14). Misamaha iliyotolewa ilifikia kiwango cha chini cha asilimia 1.93 ya GDP katika mwaka wa fedha wa ukaguzi lakini hali ya kiuchumi kwa mwaka 2014/15 imechangia kushuka kwa kiasi hicho.

Nimebaini kuwa, usimamizi usioridhisha wa misamaha ya kodi zinazotolewa inatoa mianya ya kutumia vibaya motisha hii, hivyo kuisababishia Serikali kukosa mapato. Kwa mfano, misamaha ya kodi ilitolewa ikimlenga mtu/kikundi cha watu badala ya kulenga shughuli za kiuchumi zilizokusudiwa, hivyo kukiuka lengo la kutolewa kwa misamaha hiyo na kujenga mfumo wa kodi za kibaguzi. Hivyo, uthibiti wa kina unatakiwa ili kuziba mianya yote iliyopo katika sheria, njama na vitendo vya makusudi vya ukwepaji kulipa kodi,pamoja na kutokuwepo usimamizi na uangalizi makini katika kusimamia upotevu wa mapato ya Serikali. Hata hivyo, jitihada za hivi karibuni zilizochukuliwa na Serikali ikijumuisha kuanzishwa kwa Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 2014 na Sheria ya Utawala wa Kodi ya mwaka 2014 inaonyesha maboresho ya hatua zinazochukuliwa katika kuthibiti upotevu huo wa mapato ya Serikali.

Ninaishauri Serikali:

(a) Kuendelea kupitia upya motisha za kodi zinazotolewa kwa lengo la kupunguza viwango vya misamaha ya kodi hadi kufikia asilimia moja (1%) au chini ya zao la ndani (GDP) na kuongeza kiwango cha makusanyo ya mapato.

(b) Kuendelea kupitia sera za kiuchumi na kodi kwa lengo la kuondoa misamaha yote ya kodi isiyokuwa na tija Hili

linawezekana kwa kuboresha kaguzi na udhibiti wa motisha za kodi, kuimarisha usimamizi na uchunguzi dhidi ya matumizi ya motisha za kodi.

### 5.3.6.8 Usimamizi wa Ukusanyaji Kodi

Usimamizi usioridhisha wa bidhaa zilizohifadhiwa katika maghala kabla ya kulipiwa ushuru wa forodha

Ukaguzi wa Forodha na maghala ya mali (customs bonded warehouses) ambazo hazijalipiwa kodi ulibaini mapungufu yafuatayo;

**Bidhaa zilizokaa muda mrefu katika maghala kabla ya kulipiwa ushuru wa forodha Shiling 110, 587, 418,377**

Ukaguzi wa taarifa zilizopo katika mfumo wa forodha (TANCIS) pamoja na nyaraka muhimu za forodha ulibaini bidhaa 137 ambazo hazikulipiwa kodi ya thamani ya shilingi 110, 587,418,377 zikiwa zimeshikiliwa katika Forodha na maghala ya mali (Customs Bonded Warehouses) kwa zaidi ya miezi sita bila kuhamishwa katika ghala la Forodha la serikali au iliyoidhinishwa na serikali. Hii ni kinyume na Kifungu Na. 57(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ambayo inahitaji bidhaaa zilizo kwenye Forodha na maghala ya mali kuondolewa ndani muda wa miezi sita kutokea muda zilivyoingizwa kwenye ghala hilo au kibali kiwe kimetolewa na Kamishina wa Forodha kwa maandishi cha kuomba kuendelea kutunza bidhaa hizo kwenye maghala kwa miezi mitatu zaidi. Kwa mtazamo wangu, kuwepo kwa bidhaa zilizokaa mda mrefu zaidi ni ishara kuwa mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa bidhaa zilizopo kwenye maghala, bidhaa zilizo njiani

(in transit) kwenda nchi zingine, Forodha na maghala ya mali (customs bonded warehouses) ni dhaifu.

Kadhalika, ukaguzi wa uhakiki uliofanyika katika ofisi za Ushuru wa forodha za mikoa na mipakani ulibaini kuwa, bidhaa 237 (Jedwali Na. 4) zilikuwa hazijalipiwa kodi kwa zaidi ya miaka saba (7) zikisubiri taratibu na hatua za utoaji mizigo inayotakiwa kulipiwa ushuru wa forodha. Kipindi hiki ni zaidi ya kipindi kilichowekwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 42(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 ambacho kinahitaji bidhaa zote ambazo zimekaa katika Forodha na maghala ya mali (customs bonded warehouses) kwa zaidi ya siku 60 ziuzwe kwa njia ya mnada wa wazi au kwa njia yoyote ambayo Kamishna ataona inafaa. Jedwali Na.26 linaonyesha orodha ya idadi ya bidhaa zilizokaa mda mrefu kwa mikoa na mipaka.

**Jedwali 26: Bidhaa zilizokaa zaidi kwenye Forodha na maghala ya mali (customs bonded warehouses)**

| Na | Mahali | Idadi ya Bidhaa Zilizopo katika Maghala |
|---|---|---|
| 1 | Moshi service center | 16 |
| 2 | KIA airport | 34 |
| 3 | Arusha customs service center | 17 |
| 4 | Namanga | 5 |
| 5 | Tarakea | 22 |
| 6 | Tanga | 11 |
| 7 | Horohoro | 1 |
| 8 | Bagamoyo | 131 |
| | **Jumla** | **237** |

### Utoaji wa bidhaa nje ya nchi wenye mashaka shilingi 9,151,090,597

Ukaguzi wangu ulibaini kuwepo kwa bidhaa zilizohifadhiwa katika maghala ya kuhifadhia bidhaa kwa ajili ya kuuzwa nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2014/15 ambazo zilipewa msamaha wa kodi wa shilingi 9,151,090,597. Bidhaa hizi ziliuzwa nje ya nchi kupitia vituo tofauti mipakani. Hatahivyo ushahidi unaoonyesha mauzo ya bidhaa hizi nje ya nchi haukuweza kupatikana wakati wa ukaguzi. Kwa sababu hiyo sikuweza kujiridhisha kwa kina kuwa bidhaa hizi ziliuzwa nje ya nchi au ziliingizwa kwenye soko la ndani ya nchi na hivyo kujua uhalali wa msamaha wa kodi uliotolewa kama ni sawa kwa mujibu wa Kifungu Na. 115 (a) & (b) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

(a) Serikali ichukue hatua za haraka za kunadi na kuuza bidhaa zote zilizokaa zaidi katika Forodha na maghala ya mali (customs bonded warehouses ili kuepuka kuharibika kwa bidhaa hizo, hivyo kusababisha hasara ya mapato Serikali.

(b) Serikali iboreshe mifumo ya usimamizi na ukaguzi wa Forodha na maghala ya mali (customs bonded warehouses) ili kuendana na matakwa ya Kifungu Na. 42 (1) ya Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

(c) Serikali iwasilishe ushahidi kwa ajili ya ukaguzi unaohusu bidhaa zilizouzwa nje ya nchi na kupewa msamaha wa kodi wenye thamani ya shilingi 9,151,090,597. Ikishindikana, ushahidi wa kukusanya kodi hiyo uwasilishwe. Kadhalika, Serikali iongeze mifumo ya udhibiti ya bidhaa zote zinazopita bila

ya kutumiwa ndani ya nchi na uuzwaji wa bidhaa nje ya nchi ili kuepuka uuzwaji wa bidhaa usio wa halali, hivyo kuisababishia hasara ya mapato Serikali.

**Mifumo isiyoridhisha ya Udhibiti wa mafuta yanayosafirishwa nje ya nchi na bandari kavu**
Katika ukaguzi wa mwaka 2014/15, nilibaini nyaraka 488 zenye thamani ya kodi ya forodha ya shilingi 42,734,929,515 katika kipindi cha mwezi Januari hadi Disemba 2014 zinazohusiana na mafuta yaliyouzwa katika nchi ya Uganda, Burundi na Rwanda kupitia mipaka ya Rusumo, Kabanga na Mutukula kwa mtawalia.Pia nilibaini nyaraka 177 zenye thamani ya kodi ya forodha ya shilingi 45,932,245,932.47 katika kipindi cha Julai 2013 hadi Mei 2015 zinazohusiana na mizigo katika bandari kavu zilizouzwa kupitia mipaka ya Kasumulu na Tunduma hazikuwa na ushahidi katika muundo wa rejista au mfumo wa kuhakiki kwamba, bidhaa hizo zilitolewa kupitia mipaka hiyo. Jumla ya thamani ya mafuta na mizigo ambayo haikuweza kutolewa ushahidi ni shilingi 88,667,175,447. Hii inaonyesha hali ya kutokuzingatiwa kwa mifumo ya udhibiti wa forodha ambayo inaweza kutoa mianya ya mafuta/mizigo kuweza kuuzwa ndani ya nchi bila ya kulipiwa kodi stahiki, hivyo kuipa Serikali hasara ya mapato.

Ukaguzi wangu wa kina wa taarifa zilizotoka katika mfumo wa forodha (TANCIS) umebaini utolewaji wa mafuta nje ya nchi yenye thamani ya shilingi 5,259,606,714. Mfumo wa forodha (TANCIS) unaruhusu afisa kodi katika mpaka/kituo cha kutokea nje ya nchi kuweka na kuidhinisha alama ya utolewaji wa mafuta katika mfumo. Uchambuzi wangu wa taarifa zilizotoka katika mfumo wa forodha (TANCIS)

katika mpaka wa Tunduma kwa kutumia makampuni matatu ya mafuta katika kipindi cha mwezi Novemba 2014, Disemba 2014 na Januari 2015 ilibaini kuwa, magari 263 hayakuweza kuonekana kama yameidhinishwa kutoka nchini. Jedwali Na. 27 linaonyesha maelezo zaidi;

**Jedwali 27: Magari yasiyoonekana kutoka nchini (Novemba 2014 – Januari 2015)**

| Jina la Kampuni ya Mafuta | Jumla ya magari yaliyoingia (T1 entries) | Jumla ya magari ambayo hayajatoka (un-carried out T1) | Dhamana ya magari ambayo hayajatoka (SHS) |
|---|---|---|---|
| Dalbit petroleum | 825 | 244 | 4,857,251,251 |
| Olympic | 114 | 10 | 232,060,639 |
| Lake Oil | 150 | 9 | 170,294,824 |
| **Total** | **1089** | **263** | **5,259,606,714** |

(a) Serikali iongeze usimamizi wa kutii matakwa ya taratibu za utoaji na udhibiti wa mafuta yanayokwenda nje ya nchi ili kuhakikisha makusanyanyo sahihi ya kodi za forodha.

(b) Serikali ichunguze mafuta yote ambayo hayakuidhinishwa na kukusanya kodi zote kama mafuta hayo yalitumika ndani ya nchi.

**Kutokukusanywa kwa faini zilizotokana na ucheleweshwaji wa malipo ya dhamana zilizoisha (Cancelled bond) na kuchelewa kulipa kodi za mafuta yaliyotumika nchini bila kulipa kodi kwa kisingizio cha kwamba, yapo njiani kwenda nchi za nje.**

Kanuni Na. 104 (17) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2010 inasema kuwa, endapo ikitokea ushahidi wa mauzo yaliyofanywa nje ya nchi yakifanyika

baada ya kupita siku 30 kutoka tarehe ya mauzo yalipofanyika, mmiliki wa bidhaa anatakiwa kulipa faini ya asilimia 3 kwa mwezi au katika kiwango cha asilimia sawa ikiwa muda utakuwa ni chini ya mwezi mmoja.

Kadhalika, Kifungu Na. 249 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004 kinasema, "Ikitokea kiasi cha kodi kinachotakiwa kulipwa kwa mujibu wa Sheria hii hakijalipwa katika kipindi kilichopaswa kulipwa, riba ya asilimia 2 kwa kila mwezi ya kiasi ambacho hakijalipwa inatakiwa kulipwa". Uchambuzi wa taarifa zilizotoka katika mfumo wa Asycuda++ ulibaini taarifa 51 za makampuni 8 ambazo ziliidhinishwa katika mda wa zaidi ya mda unaotakiwa kisheria lakini Mamlaka ya Mapato haikuweza kukusanya tozo inayotokana na ucheleweshaji huo. Hali hii imesababisha kutokukusanywa kwa mapato ya serikali yatokanayo na tozo yenye thamani ya shilingi 1,886,574,959.39. Jedwali Na. 28 linaonyesha tozo ambazo hazijakusanywa na makampuni yaliyohusika;

**Jedwali 28: Tozo kutokana na ucheleweshaji wa dhamana zilizofutwa/kuisha- Orodha ya Makampuni**

| Na | Jina la Wakala | Jumla ya Tozo (SHS.) |
|---|---|---|
| 1 | Camel Oil (T) LTD | 151,497,254.70 |
| 2 | ENGEN PETROLEUM TANZANIA LIMITED | 29,314,812.38 |
| 3 | HASS PETROLEUM (T) LIMITED | 102,612,235.81 |
| 4 | LAKE OIL LIMITED | 203,389,711.98 |
| 5 | MOGAS TANZANIA LIMITED | 134,652,340.90 |
| 6 | Oil com(T) LTD | 261,089,111.71 |
| 7 | OLYMPIC ENERGY (T) LIMITED | 60,298,312.61 |
| 8 | ORYX OIL COMPANY LTD | 114,985,997.48 |
| 9 | PUMA ENERGY TANZANIA LIMITED | 712,781,316.18 |
| 10 | SHIRE PETROLEUM (T) LTD | 8,205,676.51 |
| 11 | TOTAL TANZANIA LIMITED | 107,748,189.12 |
| | **Jumla** | **1,886,574,959.39** |

Ukaguzi wangu wa kina wa tathmini ya makusanyo ya mapato kutoka katika bidhaa za mafuta za ndani ya nchi yanayosafirishwa ulibaini ucheleweshaji wa siku mbili (2) hadi 266 kutokea siku ambayo taarifa ya hitaji la kulipwa kodi ilipotolewa kwa makampuni ya biashara hadi siku malipo yalipofanyika. Hata hivyo, hakukuwa na ushahidi uliotolewa ukionyesha mapato yaliyotokana na riba ya kiasi cha shilingi 47,005,629 kutoka kwenye mafuta yaliyocheleweshwa kulipiwa kinyume na Kifungu Na. 249 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004. Jedwali Na. 29 hapo chini linaonesha orodha ya riba ambazo hazikukusanywa na makampuni yaliyohusika:

**Jedwali 29: Muhtasari wa riba ambazo hazijakusanywa na makampuni**

| Na | Kampuni | Tozo (SH) |
|---|---|---|
| 1 | HASS PETROLEUM (T) LTD | 22,913,608.66 |
| 2 | HASHI ENERGY (T) LTD | 1,385,920.97 |
| 3 | GAPCO (T) LTD | 12,367,471.55 |
| 4 | TOTAL TANZANIA LIMITED | 1,346,976.70 |
| 5 | OLYMPIC ENERGY (T) LTD | 2,933,614.20 |
| 6 | UNITED GROUP LTD | 1,759,246.57 |
| 7 | SOCIETE PETROLIERE TANZANIA | 3,118,475.63 |
| 8 | AUGUSTA ENERGY | 1,180,314.74 |
| | **Jumla** | **47,005,629.02** |

Kushindwa kusimamia sheria juu ya ulipaji wa riba inayotokana na ucheleweshaji wa malipo ya bidhaa za nje zinazosafirishwa pamoja na tozo kunainyima Serikali nafasi ya kukusanya mapato zaidi ili kuweza kugharamia mipango katika bajeti yake. Vile vile, kushindwa kusimamia adhabu inayopaswa kutekelezwa

kwa kushindwa kufuata matakwa ya sheria kunakwamisha jitihada za Serikali za kukusanya mapato kwa wakati na kusimamia utekelezaji wa sheria.

Ninaishauri Serikali;

(a) Kuhakikisha kuwa riba na tozo zinazotokana na ucheleweshaji wa malipo ya kodi za mafuta yanayosafirishwa na baadaye kutumiwa nchini zinakusanywa na kuhakikisha kodi ya shilingi 47,005,629 inakusanywa kwa mujibu wa Kifungu Na. 249 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2004.

(b) Kukusanya tozo zote zilizotokana na ucheleweshaji wa ulipaji wa dhamana zilizoisha (bond cancellations) yenye thamani ya shilingi 1,886,574,959.39 kama ilivyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni 104 (17) ya Kanuni za Usimamizi wa Kodi ya Forodha ya Afrika Mashariki ya mwaka 2010.

**Kutokukusanywa kwa Kodi na Ushuru wa forodha unaotokana na mafuta yaliyoingizwa nchini Sh.5,774,263,079**

Usuluhishi wa kiwango cha mafuta kilichoagizwa kutoka nchi za nje kwa mwaka wa fedha 2014/15 kiasi cha lita 4,150,317,080 na kiasi cha mafuta kilichotumika kwa matumizi ya ndani ya nchi, mafuta yaliyosamehewa kodi, na mafuta yaliyopita nchini kuelekea nchi nyingine cha lita 4,026,889,488 umeonyesha tofauti ya lita za mafuta 123,427,591 zenye ushuru wa forodha wa kiasi cha Shilingi 9,463,254,714. Mpaka wakati wa kuandika ripoti hii ni kiasi cha lita 113,531,317 chenye thamani ni ya kodi ya shilingi 3,688,991,635 tu ndicho kimelipiwa

ushuru wa forodha na kuacha kiasi cha lita 9,896,274 ambacho bado hakijalipiwa kodi yenye thamani ya shilingi 5,774,263,079. Tofauti hizo zimetokana na mafuta aina ya AGO, Mogas/PMS, IK/JET A1 na HFO.

Ninaishauri Serikali:

(a) Kuchunguza tofauti wa mafuta uiyobainika kwa lengo la kujiridhisha ili kujua kama mafuta hayo yalitumiwa ndani ya nchi kwa njia zisizokuwa halali, na kuhakikisha kodi za forodha pamoja na tozo na riba zinakusanywa.

(b) Kuhakikisha udhibiti wa mafuta yanayonunuliwa kutoka nchi za nje unaimarishwa kwa lengo la kuzuia vitendo vinavyosababisha upotevu visijirudie tena hapo baadaye.

**Kodi zilizokokotolewa na kutokukusanywa kwa wakati TZS. 297,296,619,239**

Ukaguzi wa daftari linalotunza taarifa za uchunguzi wa kodi, daftari la kodi ambazo hazijalipwa pamoja na nyaraka nyinginezo za kodi ulibaini kiasi cha kodi cha shilingi 297,296,619,239 kilichofanyiwa tathmini kwa ajili ya kulipwa ambaco hakijakusanywa hadi wakati wa kipindi cha ukaguzi mwezi Novemba 2015. Ukaguzi ulibaini kuwa. Kuwepo kwa kodi ambazo zimekaa muda mrefu bila ya kukusanywa kumechangiwa na mifumo isiyoridhisha ya ukusanyaji kodi, hasa katika ofisi za mikoa za Mamlaka ya Mapato.

**Jedwali 30: Kodi zilizofanyiwa tathmini na kutokukusanywa shilingi 297,296,619,239**

| Na | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1. | Kodi zinazolipwa kwa awamu lakini hazijalipwa ndani ya tarehe zinazotakiwa | 15,823,636,084 |
| 2. | Makusanyo ya riba isiyokusanywa hadi tarehe 30 Septemba 2015 | 10,542,829,114 |
| 3. | Kodi isiyokusanywa kutoka kwa wafanyabiashara waliopewa misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani | 26,057,123,910 |
| 4. | Kodi ya ongezeko la thamani isiyokusanywa kutoka kwa wafanyabiashara wenye mashaka | 504,108,317 |
| 5. | Kodi isiyokusanywa hadi tarehe 30 Juni, 2015 kutoka mikoa mbalimbali ya Kodi | 216,825,432,311 |
| 6. | Kodi iliyoonyeshwa imekusanywa wakati haijathibitishwa kukusanywa | 858,829,897 |
| 7. | Kodi isiyokusanywa kwa mujibu wa mfumo wa ITAX kutoka kwa M/S Kaskazi Catering Services Ltd | 714,162,773 |
| 8. | Notisi za hitaji la malipo ya kodi zisizolipwa | 882,514,319 |
| 9. | Tozo zisizolipwa na walipa kodi waliokiuka sheria | 182,287,150 |
| 10. | Kodi zilizokokotolewa na Idara ya Uchunguzi wa kodi ambazo hazijakusanywa | 22,349,200,474 |
| 11. | Kodi zilizokokotolewa na kutokukusanywa kutokana na mapato waliyoyapata wanufaika wa akaunti ya IPTL Escrow | 2,556,494,890 |
| | **Jumla** | **297,296,619,239** |

Ninaishauri Serikali kuongeza nguvu katika uwekaji wa mifumo sahihi ya ukusanyaji kodi ili kuhakikisha kodi zote zinazotokana na tathmini zilizofanywa na maafisa kodi wa idara ya uchunguzi wa kodi, kitengo cha uchunguzi wa kodi na kitengo cha ukaguzi wa kodi zinakusanywa.

**Kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi halisi shilingi 43, 911,472,701**

Ukaguzi wa baadhi ya nyaraka za walipa kodi na taarifa za hesabu zilizoandaliwa na walipa kodi, taarifa za wanufaika waliopewa misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani, taarifa za malipo ya kodi ya ongezeko la thamani pamoja na nyaraka mbalimbali za kodi ulibaini kuwepo kwa kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi halisi yenye thamani ya shilingi 43,911,472,701. Upungufu katika ukokotoaji wa kodi hiyo ulisababishwa na taarifa zisizokuwa sahihi kuhusiana na makadirio ya juu au ya chini ya mapato ya mlipa kodi pamoja na malipo ya kodi ya ongezeko la thamani yanayotokana na ukokotoaji binafsi unaofanywa na walipa

kodi, mapitio yasiyoridhisha ya taarifa za kodi, uchambuzi na ulinganifu wa ukokotoaji binafsi uliofanywa na walipa kodi na taarifa za ukokotoaji wa kodi zinazotunzwa na Mamlaka ya Mapato.

Kwa mtazamo wangu, uzembe katika kufanya mapitio ya kodi iliyokokotolewa unaweza kutoa fursa ya ukwepaji kodi kwa njia shirikishi ya makubaliano, hivyo kuathiri mfumo wa ukokotoaji binafsi wa kodi kwa watu wasio waaminifu na kuikosesha Serikali mapato yake stahiki. Jedwali Na. 31 linaonyesha Kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi halisi kilichobainika wakati wa ukaguzi wangu:

**Jedwali 31: Kodi iliyokokotolewa pungufu ya kiasi halisi**

| Na | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| | Kodi zilizokokotolewa kutoka Mikoa mbalimbali | 17,224,348,334 |
| | Kodi iliyokokotolewa kutoka Kampuni ya M/S WU ZHO | 279,500,230 |
| | Kodi ya kipato kwa wafanyabiashara waliosamehewa kodi ya ongezeko la thamani | 26,057,123,910 |
| | Kodi iliyokokotolewa kutoka Kampuni ya M/S CMC Automobile Ltd | 350,500,227 |
| | **Total** | **43,911,472,701** |

Ninaishauri Serikali:

(a) Kuboresha ukaguzi na uchunguzi wa ukokotoaji wa kodi ili kupunguza udanganyifu wa madai ya kodi zinazotokana na mauzo ya bidhaa kutoka kwa wafanyabiashara waliopo katika mfumo wa kodi ya ongezeko la thamani na kuzuia udanyanyifu wa utoaji wa taarifa zinazoonyesha makadirio ya chini ya mapato katika

taarifa za mapato ya walipa kodi.

(b) Kufanya uchunguzi wa kodi zilizobainika kuwa pungufu katika ukokotoaji na kuhakikisha tofauti ya kodi hizo zinakusanywa pamoja na riba na tozo kama inavyotakiwa katika Sheria za Kodi.

**Taarifa za mapato ya kodi ya ongezeko la thamani zisizowasilishwa katika Mamlaka ya Mapato na walipa Kodi 51,792**

Kifungu Na. 26 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997 (Iliyorekebishwa mwaka 2006) elekeza kuwa, kila mlipa kodi ya kodi ya ongezeko la thamani anatakiwa kupeleka taarifa za mauzo ya bidhaa na huduma anazozifanya katika kila mwezi; Kifungu Na. 27 na 45 kinatoa hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa wale watakaoshindwa kutekeleza jukumu la utoaji taarifa. Hata hivyo, ukaguzi wangu wa sampuli za taarifa za walipa kodi waliojiandikisha katika kodi ya ongezeko la thamani kwa mwaka wa fedha 2014/15 katika baadhi ya mikoa ilibaini wafanyabiashara waliojiandikisha katika mfumo wa kodi ya ongezeko la thamani wapatao 51,792 ambao hawakuweza kuleta taarifa zao za mauzo ya bidhaa na huduma walizozifanya katika mwaka wa fedha wa ukaguzi. Jumla ya taarifa 2,549 za mapato ya kodi ya ongezeko la thamani hayakuweza kuwasilishwa na wafanyabiashara waliojiandikisha katika mfumo wa kodi ya ongezeko la thamani kama inavyotakiwa na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997.

Kadhalika, uchunguzi wangu wa taarifa ya Z-ripoti katika sampuli 5 za walipa kodi katika usimamizi wa mashine za kiielekironiki kutoa

stakabadhi za mauzo kwenye mkoa wa kodi wa Iringa ulibaini kuwa, biashara hizo zilikuwa zinafanya kazi na kodi ya ongezeko la thamani ya shilingi 504,108,314 haikukusanywa. **Jedwali Na. 32** linaonyesha orodha ya walipa kodi ambao hawakutoa taarifa kwa mikoa;

**Jedwali 32: Taarifa ya fomu za mrejesho wa kodi ya ongezeko la thamani ambazo hazikuwasilishwa Mamlaka ya Mapato**

| Na | Mkoa wa Kodi | Wafanyabiashara walioandikishwa | Idadi ya Taarifa ambazo hazikuwasilishwa |
|---|---|---|---|
| 1. | Arusha | 31 | 92 |
| 2. | Kilimanjaro | 20 | 176 |
| 3. | Manyara | 77 | 0 |
| 4. | Temeke | 153 | 927 |
| 5. | Kinondoni | 50,164 | 0 |
| 6. | Shinyanga | | 1,043 |
| 7. | Ruvuma | | 286 |
| 8. | Tanga | 254 | 0 |
| 9. | Dodoma | 50 | 25 |
| 10. | Mwanza | 1043 | 0 |
| 11. | Iringa | | 969 |
| | **Jumla** | **51,792** | **2,549** |

Ninaishauri menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ianzishe mfumo wa ufuatiliaji wa taarifa za mapato ya kodi ya ongezeko la thamani kwa wafanyabiashara wasioleta taarifa hizo ili kuhakikisha kuwepo kwa taarifa za hesabu ulio sahihi na uwasilishwaji wa mapato ya kodi ya ongezeko la thamani kwa wakati.

## 5.4 Ukaguzi na Usimamizi wa Deni la Taifa

### 5.4.1 Utangulizi

Deni la Taifa linahusu majukumu ambayo Serikali Kuu na Taasisi nyingine wanayo. Deni la Taifa linasimamiwa na Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebisha 2004) na Kulingana na vifungu namba 3 na 6 vya

sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali, 1974 Waziri wa Fedha ndiye mwenye dhamana ya kukopa na kutoa dhamana kwa niaba ya Serikali.

### 5.4.2 Mseto wa Deni la Taifa

Deni la Taifa kufikia tarehe 30 Juni, 2015 lilikuwa shilingi bilioni 33,539.8 ambapo deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 7,990 na deni la nje bilioni 25,549.8 ikiwa ni ongezeko la bilioni 7,052.4 sawa na asilimia 27 ikilinganishwa na deni la shilingi bilioni 26,487.4 lililoripotiwa 30 Juni 2014. Kielelezo 9 unaonyesha mseto wa deni hadi kufikia Juni 2015.

**Kielelezo 9: Mseto wa Deni la Taifa**




Katika mwaka huu wa fedha, malipo kutoka kwa wafadhili yalikuwa shilingi bilioni 7,884.8 ikilinganishwa na bilioni 6,374.3 mwaka 2013/214. Hii ni nyongeza ya shilingi bilioni 1,510.5 sawa na asilimia 24.

Deni la taifa limekuwa likiendelea kukua kila mwaka kutokana na kuwepo kwa nakisi ya mapato ya serikali na matumizi, ubadilishwaji wa hati za ukwasi kugharamia bajeti ya serikali, na pia ukopaji kwa ajili ya shughuli za maendeleona hasara katika kubadilisha fedha za kigeni ikisababishwa na kushuka

kwa kasi kwa thamani ya shilingi ikilinganishwa na fedha nyingine za kigeni ambazo ni imara. Jedwali Na. 33 na Mchoro Na. 10 zinaonyesha mwenendo wa ukuaji wa deni kwa miaka mitano iliyopita;

**Jedwali 33: Mwenendo wa Ukuaji wa Deni kwa Miaka Mitano**

| **Mwaka( Kiasi Sh.Bilioni)** | **2010/11** | **2011/12** | **2012/13** | **2013/14** | **2014/15** |
|---|---|---|---|---|---|
| Deni la Ndani | 3,707 | 4,076 | 5,775 | 7,145 | 7,990 |
| Deni la Nje | 10,735 | 12,430 | 15,634 | 19,343 | 25,550 |
| **Jumla ya Deni** | **14,442** | **16,506** | **21,409** | **26,488** | **33,540** |

**Kielelezo 10 : Mwenendo wa Ukuaji wa Deni kwa Miaka Mitano**




### 5.4.3 Mseto wa Deni la Ndani

Mseto wa deni la ndani unajumuisha dhamana zinazouzwa sokoni, na zisizouzwa zenye ukomo tofauti kama vile dhamana za muda mrefu na hati fungani. Hadi kufikia Juni 2015, Deni la ndani lilifikia shilingi bilioni 7,990.0 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 7,114.5 zilizofikiwa mwishoni mwa Juni, 2014.Deni la

ndani limeongezeka kwa shilingi bilioni 845.4 sawa na asilimia 12 ya nyongeza ya deni la ndani lililorekodiwa mwaka jana.Mikopo ya ndani katika mwaka ilifikia shilingi bilioni 4,282.8 ; ambapo shilingi bilioni 3,157.6 ilikuwa kwa ajili ya kukopea kipindi kingine, shilingi bilioni 586.5 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo na shilingi bilioni 538.7 ilikuwa ni kwa ajili ya hati fungani na dhamana.

Kimsingi, deni la ndani linachangiwa na utaratibu wa kukopa na kulipa madeni yaliyoiva bila kuweka utaratibu wa kibajeti kulipa madeni hayo kwa mapato ya ndani ya Serikali. Kwa maoni yangu, kukopa na kulipa ndani ya nchi husaidia Serikali kulipa madeni yaliyoiva.

### 5.4.4 Mseto wa Deni la Nje

Deni la nje linahusisha mikopo kutoka, Taasisi za Kimataifa na Washirika wa Maendeleo. Hadi tarehe 30 Juni 2015 Deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 25,549.8 sawa na asilimia 73.1% ya deni la Taifa .Deni hili liliongezeka kwa bilioni 6,206.9 sawa na asilimia 32.7 ya deni la nje la bilioni 19,342.9 lililoripotiwa mwaka 2013/2014. Mlinganisho wa Madeni ya nje kwa aina tofauti ya vyanzo ni kama ilivyo katika Kielelezo Na 11 hapa chini;

**Kielelezo 11: Vyanzo vya deni la Nje hadi tarehe 30 Juni 2015**




Ukaguzi wangu umebaini kwamba, ongezeko la deni la nje limechangiwa na ukopaji kutoka Mashirika ya Kimataifa kama vile IDA ambako tumepokea jumla ya shilingi .1,164 kwa ajili ya miradi ya maendeleo na ya kijamii kusaidia maendeleo mbalimbali na miradi ya kijamii ikiwa ni pamoja Mradi wa kuhawilisha fedha kwa jamii masikini (shilingi bilioni 201.4), na Usimamizi wa fedha za Umma (shilingi bilioni 201.0), Miradi ya Usafiri (shilingi bilioni 82.1) na Uboreshaji wa Mipango na Serikali za Mitaa (shilingi bilioni 76.8).

Vilevile, Serikali ilipokea fedha kutoka nchi wahisani (Ufaransa, UAE,na Japan) shilingi bilioni 108.1, Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara (ENCB) katika mfumo wa Mpangilio wa Mkopo wa nje kiasi cha shilingi bilioni 897.2;Mkopo kutoka ENCB ambao hutolewa na Benki ya Korea, China na India zilielekezwa kwenye miradi muhimu kama vile Bomba la gesi asilia (Shilingi bilioni 444.3), Mpango wa kuokoa nishati Tanzania (shilingi bilioni 144.5); mradi wa maji Dar Es Salaam mpaka Chalinze (shilingi bilioni 54.6), na Ujenzi wa kituo cha kuhifadhi takwimu (bilioni 24.0).

Pia, Serikali ilipokea fedha kutoka Benki za biashara kiasi cha shilingi bilioni 1,004.1 ikiwa ni shilingi bilioni 512.1 na shilingi bilioni 414.4 kutoka Benki ya China kwa Mkataba wa Miundombinu. Credit Suisse AG ilitoa mkopo wa shilingi bilioni 17.4, na Benki ya Hong Kong Shanghai HSBC shilingi bilioni 60.2 kwa Ujenzi wa Jengo Na. III la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere.

### 5.4.5 Kuhudumia Deni na Uchambuzi wa Deni la Taifa

Deni la Taifa limekuwa likiongezeka kwa madeni yote ya nje na ndani baada ya kushuka kwa kasi mwaka 2007/8 wakati nchi ilipopata msamaha kutoka Nchi wahisani na Mashirika ya Kimataifa. Ukaguzi wangu ulibainisha kuongezeka kwa kasi kwa deni ambako kulitokana na kuongezeka kwa ukopaji mpya kwa masharti nafuu na yasiyo nafuu kugharamia miradi ya maendeleo. Bila shaka, hasara ya fedha za kigeni (2014/15 peke yake: shilingi bilioni 2,943) kutokana na kuzorota kwa shilingi ya Tanzania dhidi ya fedha imara ni moja ya sababu za ukuaji wa deni la nje. Ongezeko la mikopo ya ndani isiyo ya masharti nafuu imesababisha gharama ya kukopa kuwa juu,Inatoa wito kwa watunga sera kuchukua tahadhari.

Hata hivyo, ukaguzi wa deni ulibainisha kuwa Wizara ya Fedha haikufanya tathmini ya uhimilivu wa deni kwa mwaka 2014 kama inavyotakiwa na Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebisha 2004); ingawa Shirika la Fedha la Duniani lilifanya uchambuzi na kutoa ripoti yake Juni 19, 2015. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa deni la taifa limebaki himilivu likiwa na viashiria vya hatari

vichache na havijavuka uwiano unaokubalika. Naamini matokeo ya tathmini ya deni itabakia sawa hata kama madeni ya shilingi bilioni 550.39 ambayo bado yanahakikiwa yataingizwa kwenye deni la Taifa.

Madeni ambayo hayajaingizwa yanajumuisha shilingi bilioni 348.5 ambazo ni malipo ambayo yapo kwenye mchakato kaitka ofisi ya malipo Hazina, bilioni 0.34 ambalo ni deni la GEPF, dhamana ambazo hazijalipwa bilioni 139.9, Deni la PSPF bilioni 473.4 na madeni mengine bilioni 61.7 chini ya msajili wa Hazina. Hii pia ni dalili kwamba, usimamizi wa deni la taifa Tanzania umegawanyika; kwani kuna taasisi nyingi ambazo zinasimamia madeni kwa sasa. Hivyo natoa wito kwa Serikali kuweka utaratibu wa usimamizi wa deni la Taifa sehemu moja .

Kwa kuangalia gharama ya deni naona kuwa gharama za huduma kwa ajili ya makusanyo ya ndani ziko juu.Tathmini yangu ya malipo ya mkopo na gharama zake,ikiwemo riba na malipo mengine nilibainisha kuwa jumla ya shilingi bilioni 4,596.8 zililipwa katika mwaka huu. Hii ni sawa na asilimia 46 ya makusanyo ya serikali ya ndani ya mapato ya shilingi bilioni 10,062.8. Gharama za kulipa madeni zikichanganywa na gharama nyingine kama vile mishahara ya wafanyakazi ni gharama ambazo zinaiacha Serikali na kiasi kidogo cha fedha za kugharamia miradi ya maendeleo na huduma nyingine za kijamii. Hii ni sambamba na tahadhari iliyotolewa na Wizara ya Fedha katika mwongozo wa hivi karibuni wa Mpango wa Mwaka na Bajeti kwa mwaka 2016/17 uliyotolewa mwezi Januari 2016. Hivyo, kutokana na rasilimali kuelekezwa katika kulipa madeni, ni kiashiria kuwa serikali

itaendelea kutegemea mikopo ili kuwezesha utekelezaji wa bajeti na miradi ya maendeleo kama mapato ya ndani hayatasimamiwa kwa umakini.

Kwa upande mwingine, kuongezeka kwa mikopo ya nje isiyo na masharti nafuu (ECB) na mikopo ya kibiashara ni ishara kuwa deni litaendelea kuwa mzigo kwa Taifa. Hii ni kutokana na vipindi vifupi vinavyotolewa katika kulipa deni ambapo mara nyingi miaka mitatu na riba kubwa (Six Month USD Libor + asilimia 5.55); na muda mfupi wa deni kuiva wengi wao wakiwa miaka kumi. Jedwali 34 na Kielelezo 12 kuonyesha deni la nje kati ya mwaka 2010/11 na 2014/15.

**Jedwali 34: Deni la nje Juni 30 2011 hadi Juni 30 2015**

| **Maelezo** | **2010/2011** | | **2014/2015** | |
|---|---|---|---|---|
| **Details (shilingi bilioni)** | **Kiasi** | **Asilimia %** | **Kiasi** | **% Asilimia** |
| **Mashirika** ya **Kimataifa** | 7,494.**56** | 70% | 4,485.44 | 57% |
| Madeni ya Nchi Wahisani | 2,585.33 | 24% | 3,229.47 | 12% |
| Madeni ya kuuza bidhaa | 346.67 | 3% | 3,767.39 | 15% |
| Madeni ya Kibiashara | 307.75 | 3% | 4,067.52 | 16% |
| **Jumla** | 10,734.31 | **100%** | **25,549.82** | **100%** |

**Kielelezo 12: Ulinganifu wa deni la nje kwa kuonyesha wadai kufikia 30 Juni 2011 mpaka 2015**




**Kielelezo 13: Ulingamfu wa deni la nje kwa kuonesha wadai kufikia 30 Juni 2015**




Uchambuzi wangu kutokana na takwimu hapo juu unaonyesha uwiano wa madeni ya kibiashara na kuingiza na kusafirisha bidhaa umeongezeka kutoka asilimia tatu mpaka asilimia 16 na asilimia 15. Katika mwaka 2014/15 kutokana na takwimu zilivyoripotiwa mwaka 2010/11, Ongezeko hilo ni uwiano wa mikopo yenye masharti nafuu kutoka nchi wahisani na Mashirika ya kimataifa.

Ni wazi kwamba, mashirika ya kimataifa yalikuwa yanadai asilimia 70 ya deni hadi tarehe 30 Juni, 2011 ikilinganishwa na asilimia 57 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2014/15. Uwiano wa Mikopo umepungua kutoka asilimia 24 hadi asilimia 12 katika kipindi hicho. Hivyo, serikali imelazimika kuingia madeni yasiyo na masharti nafuu ili kupata fedha za kugharamia Bajeti ya Maendeleo.

Mapendekezo:

a) Serikali iongeze juhudi za ndani katika kukusanya mapato ili kupata fedha ya kutosha kulipia madeni kutokana na kukosekana kwa mkakati wa vyanzo vya mapato. Mkakati utawezesha kulipia deni badala ya kulipa deni kwa kukopa (rollover) kama ilivyo sasa.

b) Serikali iweke mkakati wa matumizi bora ya raslimali fedha, ikiwa ni pamoja na kupunguza matumizi na kukopa mikopo yenye masharti nafuu na usimamizi wenye ufanisi na kuratibu shughuli za kigeni nchini na kuboresha juhudi za kuuza bidhaa nje ili kuimarisha shilingi ya Tanzania dhidi ya fedha za kigeni ambazo ni imara; hivyo, kupunguza hasara inayopatikana kutokana na fedha na kupunguza hasara ambayo inaongezeka kwa kasi.

c) Serikali kupitia Mkakati wa Taifa wa Madeni ihhakikishe Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Deni inatekelezwa

d) Serikali iongeze kasi ya marekebisho Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974

(iliyorekebisha 2004) ili kukabiliana na changamoto ya madeni ya umma na usimamizi wa deni

e) Serikali ihakikishe kwamba, kuna Mkakati wa Madeni wa kati na wa mwaka, na Uchambuzi wa Deni unafanyika kama inavyotakiwa na Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2004).

### 5.4.6 Kutoingizwa kwa dhamana za Serikali kwenye Deni la Taifa

Katika ukaguzi nilibaini kuwa dhamana za serikali zilizotolewa kwa taasisi za utoaji wa huduma zilishindwa kulipwa na Taasisi kama vile Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Shirika la ndege Tanzania (ATCL), Bunge, Kampuni ya simu (TTCL) na Bodi ya Mikopo kutaja kwa uchache, ambayo ilifikia shilingi bilioni 139.9 ambazo hazikuingizwa kwenye taarifa ya deni la Taifa hadi kufikia 30 Juni 2015. Ukaguzi wangu pia alibainisha madeni mengine ya shilingi bilioni 61.7 na deni la PSPF kiasi cha shilingi bilioni 473.4 liliripotiwa na Msajili wa Hazina bila kuingizwa kwenye hesabu za fungu. Hata hivyo, ninafahamu kuwa Serikali ipo katika mchakato wa kutoa hati fungani zisizo za fedha kwa mifuko ya pensheni ikiwemo PSPF. kiasi cha shilingi bilioni 201.6 kinabaki chini ya usimamizi wa Msajili wa Hazina na kuwa nje ya kumbukumbu za Deni la Taifa.

Aidha, kulikuwa na shilingi bilioni 348.5 chini ya ofisi ya malipo Hazina (CPO) na madeni mengine ya pensheni ambayo yalikua bado yanahakikiwa na Serikali. Katika mahojiano ofisi ya Hazina ilinipa taarifa kuwa Serikali itatoa hati fungani zisizo za fedha kwa ajili ya madeni ya pensheni

pamoja na dhamana za serikali ambazo zimepita muda wake na madeni yaliyo chini ya CPO kujumuishwa kwenye deni la Taifa hadi Juni 2015.

Kwa maoni yangu, dhamana na madeni katika hali halisi ya kiuchumi yanafuzu kuwa madeni halisi ya Serikali na kuonyeshwa kwenye deni la Taifa.Hivyo, deni la Taifa linaweza kuwa chini ukilinganisha na uhalisia.

Hivyo naishauri Serikali iharakishe utoaji wa hati fungani zisizo za fedha taslimu kwa Mifuko ya Pensheni na dhamana zisizoweza kulipika ili kuweza kutambulika na kuingizwa kwenye deni la Taifa kwenye fungu 22 kama deni la Taifa na huduma za kawaida.

### 5.4.7 Kukosekana kwa usuluhishi wa malipo kati ya Serikali na Benki Kuu

Uhakiki wa malipo ya Serikali kwenda Benki Kuu kwa ajili ya kulipia gharama za Ukwasi (liquidity Management costs) pamoja na riba inayotozwa na Serikali kwenye Nakisi yake katika kipindi cha mwaka 2014/15 umebaini kuwepo kwa tofauti ya shilingi bilioni 56.1 ambazo ni malimbikizo kwenye hesabu za Benki Kuu.

Pia, nilibaini kuwa hesabu za hali ya kifedha ya Benki Kuu hadi kufikia Juni 2015 ilionyesha bilioni 409.0038 kama nakisi ya Serikali wakati deni la Taifa lilionyesha kuwa shilingi bilioni 401.67 katika tarehe hiyo.Hivyo, takwimu kutofautiana kwa shilingi bilioni 7.333

Kwa maoni yangu, kiasi cha madeni kilichoonyeshwa kama gharama halisi, gharama za usimamizi na riba ya Serikali kilikuwa pungufu kwa jumla ya shilingi bilioni 64.153

Hivyo, napendekeza Serikali ihakikishe inafanya ulinganisho wa hesabu mara kwa mara na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepuka tofauti kama hizo katika siku zijazo.

**5.4.8 Sheria ya Deni na Mpango Mkakati wa Deni la Taifa vilivyopitwa na Wakati**

Shughuli za deni la Taifa zinapaswa kuwa zimeainishwa vizuri na sheria, kanuni na taratibu, ambazo zitakuwa zikifanyiwa tathmini ya mara kwa mara ili kuendana na wakati wa sasa. Mkakati wa Deni la Taifa (NDS) wa mwaka 2002 unaeleza malengo kadhaa ikiwa ni pamoja na kuwa na mkakati endelevu wa sera ya deni baada ya kukamilika kwa mpango wa Nchi Masikini zenye Madeni Makubwa (HIPC) ambao ulimalizika Novemba 2001 na kusainiwa kwa makubaliano ya Paris Club VII Januari 2002.

Hali ya uchumi wakati wa kuanzishwa kwa sheria na Mkakati wa Deni (NDS) imebadilika mno kutokana na mabadiliko ya kiuchumi ambayo yametokea Tanzania na duniani kwa ujumla.

Ninafahamu kwamba, Mkakati wa deni(NDS) haujawahi kufanyiwa marekebisho; na mabadiliko ya mwisho yalifanyika Novemba 2004. Hivyo, kutokana na kukua kwa deni na kuongeza kukopa kila mwaka ni muhimu kuwa na sheria na miongozo inayoendana na maendeleo hayo ya wakati uliopo.

Pia, nafahamu kwamba, Serikali ilianza kuandaa Mpango wa Muda wa Kati (MTDS) kwa kushirikiana na Shirika la Fedha duniani (IMF) na Benki ya Dunia. Serikali ilitoa rasimu ya mkakati Juni 2011 Katika mjadala wangu na

Hazina, ilibainika kuwa Mpango wa Muda wa Kati uliandaliwa kwenye nafasi ya Mpango wa deni wa Taifa ingawa Serikali ina mpango wa kuwa na Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Deni la taifa huku mpango wa kati ukitolewa kwa mwaka kusaidia sera. Wakati nikipongeza juhudi hizi, Mpango wa Kati wa deni (MTDS) na Sera ya Deni la Taifa havipo kwenye Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2004).

Natoa wito kwa Serikali ipitie upya Mkakati wa Taifa wa Madeni; pia kuhakikisha Sera ya Usimamizi wa Deni la Taifa inatekelezwa na mabadiliko yanafanyika katika Sheria ya Madeni, Dhamana na Misaada ya Serikali ya mwaka 1974 (iliyorekebishwa 2004) ili kutatua changamoto zilizopo.

### 5.4.9 Madeni Mfu Yasiyolipwa kwa Muda Mrefu Bilioni 2,090

Tathmini ya mseto wa deni kufikia Juni 30, 2015 ulibainisha madeni saba (7) kutoka nchi sita wahisani kwa madeni ya shilingi bilioni 2,090.0; ambazo zilihusu fedha za deni ambazo hazikutolewa shilingi bilioni 721.5; ambazo ni asilimia 35 na malimbikizo ya riba shilingi bilioni 1,368.5 au asilimia 65 .Madeni haya yamekua mfu kwa miaka 23 na mengine hawajawahi kuhudumiwa. Menejimenti ilitoa maelezo kwamba, malipo ya mikopo hiyo iyalisimama ili kusubiri majadiliano ya marekebisho au kusitishwa madeni na nchi husika. Ni maoni yangu kua uwepo wa akaunti hizi unasababisha riba kuongezeka bila sababu zozote za msingi na hivyo kuongeza deni la Taifa.

Napendekeza Serikali kuharakisha mazungumzo na Nchi husikaTaasisi kwa lengo la kutoa msimamo wa madeni husika na kuanza

kuhudumia madeni hayo.

### 5.4.10 Kuchelewesha Makato ya Kisheria ya Mafao na Kusababisha Adhabu ya Shilingi Bilioni 52.8

Tathmini yangu ya makato ya kisheria ilibaini kuwa Hazina ilichelewesha makato ya michango ya fedha za pensheni kwa kipindi cha miezi miwili (2) hadi kumi na miwili (12) baada ya mwisho wa mwezi. Ucheleweshaji huu ulisababisha adhabu ya shilingi bilioni 52.8 kutokana na kukiuka matakwa ya sheria za pensheni.

Natoa wito kwa Serikali kutoa michango ya makato ya kisheria kwa Mifuko ya Pensheni kwa wakati muafaka ili kuepuka adhabu zisizo za lazima na kuzingatia matakwa ya sheria. Pia napendekeza makato ya kisheria ambayo hayajalipwa  yalipwemara moja ili kuboresha ukwasi wa fedha na kuepusha usumbufu kwa walengwa wa pensheni.

## 5.5 Ukaguzi wa Awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu

Sehemu hii ya ripoti inawasilisha mambo ya msingi yaliyojitokeza kwenye ukaguzi wa awali wa Malipo ya Mafao ya Wastaafu (Pensheni) katika kipindi cha mwaka 2014/15.

### 5.5.1 Utangulizi

Ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao ya wastaafu hufanyika kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 (marekebisho 2005) na Kifungu cha 29 na 5 (a) cha Sheria ya Ukaguzi No. 11 ya mwaka 2008 ambayo inamtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujiridhisha na kuidhinisha malipo yafanyike kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali na kuhakikisha kwamba, Ibara ya 136 ya Katiba imezingatiwa.

Hivyo ni muhimu kufanya ukaguzi wa awali kwenye malipo yote ya Serikali ambayo sio rahisi kuyatabiri na kutengewa fedha.

### 5.5.2 Lengo la kufanya Ukaguzi wa Awali

malipo ya mafao ya kustaafu kwa kuwezesha kutambua mapema makosa kwa nia ya kuhakikisha kwamba, wastaafu wanalipwa kile wanachostahili. Kiasi chochote kitakacholipwa kimakosa ni vigumu kurejeshwa kutoka kwa mstaafu.

Kwa upande mwingine, madhumuni ya ya uhakiki wa mafao ni kuhakikisha kuwa sheria husika na kanuni za mafao ya kazi na sera na miundo ya utumishi wa umma na muundo wa mishahara vinazingatiwa.

### 5.5.3 Mawanda ya Ukaguzi

Ukaguzi kabla ya mafao ya pensheni huhusisha Watumishi wa Umma ambao mafao yao hulipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali; na ukaguzi hahihusishi Watumishi wa umma ambao mafao yao yanashughulikiwa na PSPF, PPF na makato mengine ya huduma. Ukaguzi wa awali wa mafao ulifanyika kwa kuhusisha :-

- Watumishi wa umma, watoa huduma mchanganyiko, wanajeshi na viongozi wengine, walimu, na maafisa usalama.
- Malipo ya kimkataba kwa viongozi wa kisiasa, wageni toka nje, wastaafu waliorejeshwa kwenye utumishi, na raia waliopewa ajira wakiwa na umri wa zaidi ya miaka 45
- Kiinua mgongo kwa watumishi wasiokuwa na mafao, na pia
- Malipo kwa viongozi wa juu, na askari polisi

### 5.5.4 Ufafanuzi wa Hoja za Ukaguzi na Mapendekezo

Sehemu hii ya ripoti inaeleza mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa awali wa malipo ya mafao kwa mwaka wa fedha 2014/2015;

#### 5.5.4.1 Utekelezaji wa Mwaka (Ufanisi wa Kiutendaji)

Katika kipindi cha mwaka 2014/15, Ofisi ya Ukaguzi ilifanya ukaguzi wa awali wa mafao na ofisi ilianza ukaguzi ikiwa na majalada 44 yaliyotokana na ukaguzi wa kipindi cha mwaka 2013/14.Katika kipindi hiki, majalada ya wastaafu 4,777 yaliletwa kwa ajili ya kukaguliwa. Majalada 4,683 yalikaguliwa na kuidhinishwa, majalada 138 yalirejeshwa kwa Maafisa Masuuli wahusika kwa ajili ya masahihisho, na yalikuwa bado yakiendelea na ukaguzi wakati wa kufunga mwaka wa fedha 30 Juni, 2015 kama inavyoonyeshwa katika **jedwali Na 35** hapo chini:

**Jedwali 35: Mafaili ya wastaafu yaliyokaguliwa**

| Maelezo | Majalada |
|---|---|
| Idadi ya Majalada 1 Julai,2014 | 44 |
| Majalada yaliyopokelewa | 4,777 |
| Jumla ya majalada kwa ukaguzi | 4,821 |
| Majalada yaliyokaguliwa | **4,683** |
| **Majalada yaliyobakia 30 Juni,2015** | **138** |

#### 5.5.4.2 Ukokotoaji Usio Sahihi wa Mafao ya Wastaafu

Ukaguzi wa awali wa majalada kabla ya malipo ya Mafao ya Wastaafu ulibaini kwamba, baadhi ya majalada ya wastaafu yaliyowasilishwa kwa ukaguzi wa awali kwa ajili ya malipo malipo ya wastaafu yalikokotolewa isivyo sahihi.

Kati ya majalada 4,683 ya wastaafu yaliyokaguliwa, malipo ya majalada 268

yalibainika yamezidishwa kwa kiasi cha Sh.1,053,777,358.07 huku majalada 200 yakiwa yamepunjwa malipo ya TZS.385,304,481.69. Ukaguzi ulibaini kuwa majalada ya wastaafu hayakupitiwa kwa umakini na Taasisi husika kabla ya kuwasilisha majalada kwa ukaguzi wa awali. Hali hii ilitokana na kukosa umakini, utaalam wa masuala ya mafao na kutozifahamu vizuri sheria za mafao kama inavyoonyeshwa katika **Jedwali Na.36** na **Jedwali Na. 37** hapa chini:

**Jedwali 36: Mafao ya Wastaafu yaliyozidishwa**

| Na | Maelezo | Idadi ya kesi | Kiasi(TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kipindi kilichozidishwa | 126 | 607,234,896.01 |
| 2 | Mishahara iliyozidishwa | 70 | 335,472,992.32 |
| 3 | Makosa katika Ukokotoaji | 11 | 36,174,009.05 |
| 4 | Mapunjo NSSF | 61 | 74,895,460.69 |
| | | 268 | 1,053,777,358.07 |

**Jedwali 37: Mafao ya Wastaafu yaliyopunjwa**

| Na | Maelezo | Idadi ya kesi | Kiasi(TZS) |
|---|---|---|---|
| 1 | Kipindi kilichozidishwa | 97 | 207,193,954.57 |
| 2 | Mishahara iliyozidishwa | 60 | 121,704,508.58 |
| 3 | Makosa katika Ukokotoaji | 9 | 1,938,822 |
| 4 | Mapunjo NSSF | 34 | 54,467,196.54 |
| | | **200** | **385,304,481.69** |

Uchangazi wa hapo juu unadhihirisha umuhimu wa ukaguzi wa awali katika malipo ya Mafao ya Wastaafu, kwani bila kufanyika, serikali ingepoteza jumla ya TZS.1,053,777,358.07 au wastaafu wangeweza kupunjwa mafao yao kwa kiasi cha TZS.385,304,481.69 ambayo ingeleta hasara halisi ya TZS.668,472,876.38 kwa Serikali.

Uokoaji wa fedha hizo ni mojawapo ya mchango

wa Ofisi yangu kwa ukaguzi wa awali kwa mafao yanayolipwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na kuonyesha umuhimu wa kuimarisha mifumo ya ndani katika Taasisi za Serikali, kwani mapungufu ya Maafisa Masuuli yangeweza kuigharimu Serikali na Wastaafu endapo ukaguzi wa awali wa mafao usingefanyika.

### 5.5.6 Ucheleweshwaji Usiokuwa na Tija katika Kuandaa Mafao ya Wastaafu

Ukaguzi wangu wa malipo ya awali ya Wastaafu umebaini baadhi ya malipo ya wastaafu yamekuwa yakichelewa kuwasilishwa PSPF na waajiri.Ucheleweshwaji huu ulibainika pia katika mifuko mingine ya hifadhi.Ucheleweshaji huu umesababisha baadhi ya wastaafu kushindwa kuandaliwa malipo yao na pia kuigharimu Serikali tozo (Penalty). Kwa maoni yangu, fedha za adhabu na ugumu wa maisha wanaoupata wastaafu vingeweza kuepukika endapo michango ya watumishi ingekuwa ikiwasilishwa kwa wakati. Jedwali Na. 38 hapo chini linaonyesha makato ya kisheria kiasi cha shilingi 213,609,402,639 ambayo hazikuwasilishwa kwenye mifuko kwa baadhi ya miezi iliyokaguliwa ya Mei, Juni na Agosti 2015.

**Jedwali 38: Mafao ambayo hayakupelekwa kwa wakati**

| Mfuko | Mei-15 | Juni-15 | Ag-15 | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| PSPF | 35,888,648,135 | 36,279,839,100 | 41,762,030,310 | **113,930,517,545** |
| LAPF | 11,916,307,581 | 12,324,061,781 | 14,340,946,885 | 38,581,316,247 |
| PPF | 3,241,676,495 | 3,255,560,980 | 3,512,617,120 | 10,009,854,595 |
| GEPF | 1,957,961,870 | 2,432,555,584 | 2,908,843,903 | 7,299,361,356 |
| NSSF | 1,740,826,979 | 1,754,920,186 | 1,946,246,277 | 5,441,993,442 |
| NHIF | 12,086,618,883 | 12,191,273,148 | 14,068,467,423 | 38346359453 |
| **Jumla** | **66,832,039,942** | **68,238,210,779** | **78,539,151,918** | **213,609,402,639** |

Mbali na ucheleweshaji katika kuwasilisha michango,ukaguzi pia ulibaini kuwa baadhi ya waajiri waliwasilisha majalada ambayo hayakuwa na taarifa sahihi zitakazowezesha malipo. Katika hali kama hiyo, ofisi yangu iliwataka waajiri kuwasilisha nyaraka zinazokosekana, na wakati mwingine, ilisababisha kurudia rudia mchakato; hivyo kuchelewesha malipo ya pensheni kwa walengwa.

Napendekeza majalada ya mafao yaandaliwe vizuri kabla ya kuwasilisha katika ofisi yangu kwa ajili ya ukaguzi wa awali ili kupata taarifa sahihi na maelezo yenye usahihi na kuzuia waajiriwa kulipa mafao zaidi au kidogo kutokana na taarifa zisizo sahihi. Ni muhimu , waajiri welewa umuhimu wa kuwasilisha majalada ya pensheni ambayo ni kamili, kwa wakati, na taarifa sahihi ambazo zitawezesha kufanyika kwa malipo sahihi ya mafao ya wastaafu.

Napenda kusisitiza Mapendekezo yangu kwa Serikali;

- Serikali ihakikishe inapeleka kwa wakati makato ya michango ya kisheria ya pensheni kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ili kuepuka ucheleweshaji katika kuandaa mafao pamoja na kuzuia adhabu.
- Maafisa Masuuli wahakikishe waandaaji wa mafao wanafuata kanuni na sheria. Wanapaswa pia kuhakikisha mafaili ya pensheni yanayowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi wa awali ni kamili, sahihi na yanawasilishwa kwa wakati ili kuepuka ucheleweshaji wa malipo ya mafao ya wastaafu.

- Serikali itoe mafunzo ya mara kwa mara kwa waandaaji wa mafao ya pensheni ili

kuongeza uelewa wao kuhusu sheria za pensheni na mambo mengine.

ukomo tofauti kama vile dhamana za muda mrefu na hati fungani. Hadi kufikia Juni 2015,Deni la ndani lilifikia Shilingi bilioni.7,990.0 ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi bilioni 7,114.5 zilizofikiwa mwishoni mwa Juni, 2014. Deni la ndani limeongezeka kwa Shilingi bilioni 845.4 sawa naasilimia 12 ya nyongeza ya deni la ndani lililorekodiwa mwaka jana.Mikopo ya ndani katika mwaka ilifikia Shilingi bilioni 4,282.8 ambapo Shilingi bilioni 3,157.6 ilikuwa kwa ajili ya kukopea kipindi kingine, Shilingi bilioni 586.5 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo na Shilingi bilioni 538.7 ilikuwa ni kwa ajili ya hati fungani na dhamana.

## Sura ya Sita

## Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

### 6.0 Utangulizi

Mfumo wa udhibiti wa ndani unahusisha taratibu zote za usimamizi zilizopitishwa na menejimenti ya Taasisi zote za Serikali kutekeleza majukumu na kutoa huduma kwa wateja. Hii ni pamoja na kuzingatia sheria, kanuni na sera katika kulinda mali kuwa na taarifa sahihi za kihasibu, kubaini na kuzuia mapungufu na udanganyifu pamoja na kuwa na taarifa sahihi kwa wakati.

Jukumu kuu la Afisa Masuuli katika Taasisi ni kuhakikisha mifumo ya udhibiti ya ndani inafanya kazi ipasavyo na kwa ufanisi. Katika ukaguzi niliofanya, nilizingatia kukagua mifumo ya ndani ili kujiridhisha kama inafanya kazi kulingana na taratibu zilizowekwa na kutoa ushauri. Katka ukaguzi wangu nilizingatia baadhi ya mifumo ya udhibiti inayoniwezesha kutambua mapungufu, hivyo, inawezekana nisitoe uhakika kwamba mapungufu yote niliyabaini.

Umuhimu wa kipekee ulizingatiwa katika kuangalia jinsi vyombo vya usimamizi na udhibiti wa mifumo ya ndani kama vile: Kamati ya Ukaguzi, Ukaguzi wa ndani, Mifumo ya TEHAMA na mifumo ya kudhibiti udanganyifu wa mali za Taasisi inafanya kazi.

### 6.1 Tathmini ya Ukaguzi wa Ndani katika Taasisi

Kulingana na Kanuni ya 28(1) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inamtaka kila Afisa Masuuli kuanzisha kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kutoa uhakika iwapo mifumo ya ndani ya Taasisi inafanya kazi ipasavyo.

Hata hivyo, tathmini ya ukaguzi iliyofanyika kuhusu ukaguzi wa ndani ilibaini kuwa kwa ujumla, hali imeboreka kwa asilimia 24 ikilinganishwa na mwaka

jana ambapo Taasisi 10 ziliboresha vitengo vya ukaguzi wa ndani kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:

**Jedwali 39: Mapungufu katika utendaji wa ukaguzi wa ndani**

| **Tathmini ya Mifumo ya Ndani** | **Mapungufu Yaliyobainika** |
|---|---|
| *Kuwapo kwa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani* | Kwa mujibu wa kanuni, baadhi ya Taasisi zilianzisha Vitengo vya ukaguzi wa ndani baadhi bado. |
| *Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kufuata sheria na kanuni na maagizo mbalimbali* | • Baadhi ya Vitengo vya ukaguzi wa ndani havikutekeleza majukumu yote waliyojipangia kutokana na uhaba wa watumishi na fedha<br>• Kulikua na ufatiliaji wa mapendekezo yaliyotolewa na ukaguzi wa ndani usioridhisha<br>• Baadhi ya vitengo vya ukaguzi wa ndani vilitumia hati idhini (**charter**) ambazo hazijaidhinishwa.<br>• Baadhi hawakuwa na vitendea kazi kama magari<br>• Baadhi ya mipango ya ukaguzi wa ndani haikupitiwa na kuidhinishwa na Kamati ya Ukaguzi |

*Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti 2014/2015*

Orodha ya Taasisi zenye Mapungufu kwenye kitengo cha ukaguzi wa ndani zimeonyeshwa kwenye kiambatisho 6.1

**Kielelezo 14: Taasisi zenye mapungufu kwenye vitengo vya ukaguzi wa ndani**

| Taasisi | 2014/15 | 2013/14 | Ongezeko/ Punguzo | Asilimia ya Ongezeko/ punguzo |
|---|---|---|---|---|
| Fungu | 22 | 27 | 5 | 19 |
| Wakala | 6 | 6 | 0 | 0 |
| Taasisi Nyinginezo | 3 | 3 | 0 | 0 |
| Balozi | 1 | 6 | 5 | 83 |
| **Jumla** | **32** | **42** | **10** | **24** |

*Chanzo: Taarifa za Ukaguzi kwa Menejimenti 2014/2015*

Kama Taasisi haitakuwa na kitengo cha ukaguzi wa ndani ambacho ni madhubuti kuna hatari ya kuwa na mifumo ya ndani ambayo ni dhaifu, kutofuatwa kwa taratibu, maagizo, na sera za kazi

Maafisa Masuuli wanashauriwa kuhakikisha kuwapo kwa Kitengo cha ukaguzi wa ndani katika Taasisi na kipewe raslimali za kukiwezesha kufanya kazi ikiwamo kupitia mifumo ya ndani na kubainisha mapungufu na kutoa mapendekezo na ushauri utakaoleta tija.

### 6.2 Tathmini ya Kamati ya Ukaguzi

Kanuni ya 30 ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 inaitaka kila Taasisi kuwa na Kamati ya Ukaguzi. Uanachama na majukumu ya kamati ya ukaguzi vimeainishwa kwenye Kanuni ya 31 na 32 ya Sheria ya Fedha. Majukumu ya Kamati ya Ukaguzi ni pamoja na kuwa na vikao vya kila robo mwaka, Kupitisha mpango wa mwaka wa ukaguzi wa ndani, kutoa ushauri kwa Afisa Masuuli katika masuala muhimu yaliyobainishwa na Mkaguzi wa ndani au katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuandaa taarifa ya mwaka.

Ikilinganishwa na ripoti ya mwaka jana kumekuwa na ongezeko la kuimarika kwa Kamati za Ukaguzi kwa asilimia 28 ambapo taasisi 12 zimeongezeka kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.40 hapa chini.

**Jedwali 40: Mapungufu katika utendaji wa Kamati za Ukaguzi**

| Mfumo wa Ndani Uliopitiwa | Mapungufu |
|---|---|
| *Kamati ya Ukaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, mipango na Maagizo mbalimbali* | • Baadhi ya Kamati za Ukaguzi hazikukaa vikao vya robo mwaka kwa mujibu wa sheria<br>• Baadhi ya Kamati za Ukaguzi hazikujadili taarifa za ukaguzi wa ndani kwa mujibu wa sheria.<br>• Baadhi ya Kamati hazikuandaa taarifa za mwaka.<br>• Baadhi ya Kamati za Ukaguzi hazikupitia muundo na utekelezaji wa mifumo ya ndani inayoangalia usimamizi wa mali, matumizi, mapato, na usimamizi wa taratibu za manunuzi.<br>• Baadhi ya Kamati za Ukaguzi hazikualika Mkaguzi Mkuu wa Nje katika vikao vya kila robo mwaka kinyume na kifungu 32(3) cha Sheria ya Fedha ya Umma ya mwaka 2001.<br>• Kamati nyingine hazikupitia hesabu za Taasisi zao za mwaka wa fedha ulioishia Juni 30 2015<br>• Baadhi ya wajumbe wa Kamati za Ukaguzi hawakupewa Mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kufanya kazi zao kwa ufanisi. |

Takwimu ya Taasisi ambazo zilikutwa na mapungufu zimeonyeshwa kwenye Kiambatisho 6.1 na Kielelezo Na.15 linaonyesha mgawanyo wa Taasisi

**Kielelezo 15: Mgawanyo wa Taasisi na mapungufu katika kamati za ukaguzi**

| Taasisi | 2014/15 | 2013/14 | Zilizoongezeka | % ya Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| Fungu | 21 | 30 | 9 | 30 |
| Wakala | 5 | 9 | 4 | 44 |
| Taasisi Nyinginezo | 5 | 2 | -3 | (150) |
| Balozi | 0 | 2 | 2 | 100 |
| **Jumla** | **31** | **43** | **12** | **28** |

Ninapendekeza kwamba, Maafisa Masuhuli wahakikishe Kamati za Ukaguzi zinafanya kazi walizopangiwa kama zilivyoainishwa kwenye sheria ya Fedha za Serikali ili kuhakikisha uwajibikaji unajengeka na kuboresha utoaji wa huduma bora kwa kuimarisha mifumo ya ndani.

### 6.3 Mapungufu katika usimamizi wa vihatarishi

Pia, katika ukaguzi nilifanya mapitio ya usimamizi wa vihatarishi katika Taasisi kwa nia ya kutathmini uwezo wake wa kuonyesha athari kabla hazijatokea ambazo endapo hazitazuiliwa zitaleta athari katika kutoa huduma kwa umma. Pia niliangalia kama taasisi zimejizatiti na vihatarishi vya kurithi na kama njia sahihi za kuzuia vihatarishi hivyo zimezingatiwa.

Kwa tathmini niliyoifanya, nimeona hali imeboreka kwa asilimia 65 ukilinganisha na mwaka jana ambapo taasisi 20 zimeboresha taratibu za kusimamia vihatarishi.Katika ukaguzi, bado nilibaini kuwabaadhi ya taasisi hazizingatii kuboresha namna ya kusimamia vihatarishi. Mapungufu yafuatayo yalibainika:

- Baadhi ya Taasisi hazikuwa na Sera ya kudhibiti vihatarishi iliyoidhinishwa

- Baadhi ya Taasisi hazikuwa na Rejista ya Vihatarishi na

- Baadhi ya Taasisi zilikuwa na rejista pamoja na sera ya vihatarishi lakini hazikurekebishwa kulingana na wakati uliopo kwa kuzingatia matukio mapya.

Taasisi zenye Mapungufu zimeonyeshwa kwenye kiambatisho 6.1 na jedwali na 41. Linaonyesha Mgawanyo wa Taasisi

**Kielelezo 16: Mapungufu katika kudhibiti Vihatarishi**

| Taasisi | 2014/15 | 2013/14 | Ongezeko | % ya Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| Fungu | 9 | 22 | 13 | 59 |
| Wakala | 1 | 6 | 5 | 83 |
| Taasisi Nyinginezo | 1 | 2 | 1 | 50 |
| Balozi | 0 | 1 | 1 | 100 |
| **Jumla** | **11** | **31** | **20** | **65** |

Ili kuweza kutoa huduma bora kwa umma kwa mwingiliano usio na matukio yenye athari, maafisa Masuuli wanashauriwa kuboresha taratibu za kusimamia na kudhibiti vihatarishi kwa kuhakikisha kuwapo kwa taratibu zilizoandikwa vizuri za kuzuia vihatarishi na kufikia malengo yaliyowekwa.

### 6.4 Kupitia Mifumo ya TEHAMA

Ikiwa ni sehemu ya ukaguzi, tathmini ilifanyika kwenye mifumo ya TEHAMA ili kujiridhisha kama Taasisi zimeweka mifumo madhubuti ya TEHAMA ili kudhibiti usiri na uwepo wa taarifa sahihi za kihasibu na nyinginezo. Ukaguzi umebaini kuwa kumekuwa na mapungufu katika TEHAMA kwa asilimia 26 ikilinganishwa na mwaka jana kama inavyoonekana kwenye jedwali Na. 41 hapa chini:

**Jedwali 41: Mapungufu katika TEHAMA**

| Eneo lililofanyiwa tathmini | Mapungufu |
|---|---|
| Sera na taratibu za TEHAMA | • Baadhi ya Taasisi zina mifumo dhaifu ya usalama ya kutunza taarifa dhaifu ambayo inaweza kusababisha taarifa zake kuingiliwa.<br>• Baadhi ya Taasisi kuna wakati zinapata matatizo ya mtandao ambayo husababisha kushindwa kutoa taarifa za fedha kutoka katika mfumo wa Epicor kwa wakati. |
| Wajibu na Majukumu | • Baadhi ya Taasisi hazikuwa na Kamati za kujadili Masuala ya TEHAMA |
| Usimamizi wa watumishi wa Tehama | • Hakukuwa na sera za kuonyesha mgawanyo wa kazi kwa wafanyakazi chini ya kitengo cha TEHAMA. |
| Usalama wa TEHAMA | • Baadhi ya Taasisi hazikuwa na mpango wa kuzuia maafa ya TEHAMA ili kuruhusu mwendelezo wa biashara<br>• Baadhi ya Taasisi hazikubuni mifumo ya kudhibiti<br>• Baadhi ya Taasisi hazikuwa na ofisi mbadala za kutunzia taarifa |
| Kompyuta inavyofanya kazi | • Mfumo wa Epicor haujaunganishwa na mifumo mingine kama vilewa madeni,madai na mali za kudumu.Taarifa huingizwa bila kutumia mfumo wa tehama.<br>• Kutotumia mfumo wa EPICOR ipasavyo.<br>• Balozi hazijaunganishwa na mfumo wa Epicor |

**Chanzo:** *Taarifa ya ukaguzi kwa menejimenti 2014/2015*

Taasisi zenye mapungufu zimeonyeshwa kwenye kiambatisho 6.1 na kielelzo 17 linaonyesha Mgawanyo wa Taasisi

**Kielelezo 17: Mgawanyo wa Taasisi zenye mapungufu katika TEHAMA**

| Taasisi | 2014/15 | 2013/14 | Ongezeko/ Pungufu | % Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| Fungu | 30 | 31 | 1 | 3 |
| Wakala | 10 | 8 | (2) | (25) |
| Taasisi Nyinginezo | 6 | 1 | (5) | (500) |
| Balozi | 12 | 6 | (6) | (100) |
| **Jumla** | **58** | **46** | **(12)** | **(26)** |

Wakati mifumo mingi ya Taasisi imeunganishwa na TEHAMA ili kuendana na dunia ya sasa inayobadilika ya teknolojia, naishauri Serikali kufuata taratibu zifuatazo ili kuwa na uhakika wa usiri, usalama, uaminifu na uwepo wa taarifa sahihi:

- Kufafanua na kuwezesha mifumo ya TEHAMA ambayo itawezesha kupangilia na kuunganisha maamuzi ya kimkakati, vitega uchumi na kuweka mipango ya kuhakikisha kuwa mifumo ya TEHAMA inadhibitiwa ipasavyo.
- Mifumo inapaswa kuweka kipaumbele katika uundaji wa Kamati ya Uendeshaji, Mpango mkakati wa TEHAMA na muundo wa TEHAMA katika taasisi utakaowezesha kufanikisha mipango na mikakati ya Taasisi.

## 6.5 Tathmini ya Kugundua na Kuzuia Udanganyifu

Kama sehemu ya ukaguzi, tathmini ilifanyika ili kuhakikisha iwapo Taasissi zina mfumo wa udhibiti unaoweza kutambua na kuzuia aina yoyote ya udanganyifu na siyo kusubiri hadi utokee. Kwa ujumla, udanganyifu ni kitendo cha makusudi kinachofanywa na sehemu ya menejimenti na wale wanaohusika na utawala,

wafanyakazi au watu wengine ambao hutumia udanganyifu ili kupata isiyo haki au faida haramu. Ndani ya Serikali udanganyifu unaweza kuwa utoaji wa taarifa za ulaghai wa fedha na matumizi mabaya ya mali za umma ikiwa ni pamoja na ubadhirifu wa fedha taslimu.

Uongozi wa Taasisi una jukumu la msingi la kuunda mfumo madhubuti wa udhibiti wa ndani kwa ajili ya kugundua, pamoja na kuzuia udanganyifu na ubadhirifu katikaTaasisi inayokaguliwa.

Kutokana na tathmini hii, nilibainisha kuzorota kwa hali ambapo mafungu 2 zaidi yalizembea katika eneo la udanganyifu ikilinganishwa na mwaka jana. Yafuatayo yalibainika:

- Kukosekana kwa sera ya usimamizi wa udanganyifu ambayo itaonyesha viashiria hatarishi.
- Tathmini ya vihatarishi hazikufanyika mara kwa mara
- Hakuna ushahidi wa maandishi wa kutambua udhibiti maalum ambao utasaidia kupunguza hatari ya makosa kutokana na udanganyifu.
- Hakuna tathmini yoyote ya usimamizi wa mifumo ya ndani iliyofanyika.
- Uelewa mdogo wa udanganyifu kutokana na ukosefu wa tathmini yoyote ya vihatarishi uliofanywa:

| **Taasisi** | **2014/15** | **2013/14** | **Zilizoongezeka** | **% ya ongezeko** |
|---|---|---|---|---|
| Fungu | 9 | 7 | (2) | (29) |
| **Jumla** | **9** | **7** | **(2)** | **(29)** |

Hivyo, nazishauriTaasisi ‘kuanzisha utaratibu wa kuchunguza na kuzuia vitendo vya ulaghai na kuweka viashiria vya hatari ambayo vitasaidia kupunguza matukio ya udanganyifu.

Kwa ujumla, tathmini juu ya mifumo ya udhiti ya ndani ya Taasisi inaonekana kuwa bora kwa asilimia 17 ikilinganishwa na kipindi cha taarifa iliyopita kama inavyoonekana katika takwimu za jedwali Na. xx hapa chini:

**Kielelezo 18: Tathmini kwa ujumla ya Mifumo ya udhibiti ya Ndani ya Taasisi**

| | 2014/15 | 2013/14 | Ongezeko | % ya ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| Utendaji wa Ukaguzi wa Ndani | 32 | 42 | 10 | 24 |
| Utendaji wa Kamati ya Ukaguzi | 31 | 43 | 12 | 28 |
| Tathmini ya TEHAMA | 58 | 46 | -12 | (26) |
| Tathmini ya vihatarishi | 11 | 31 | 20 | 65 |
| Tathmini ya Udanganyifu | 9 | 7 | -2 | (29) |
| **Jumla** | **141** | **169** | **28** | 17 |

**Chanzo:** *Ripoti ya CAG kwa menejimenti 2014/15*

Wakati baadhi ya Taasisi zimeonyesha maboresho hasa kwenye eneo la kuanzishwa na kufuatwa kwa Sheria na Kanuni zinazohusiana na ukaguzi wa ndani, Kamati ya Ukaguzi na Tathmini ya Vihatarishi, nayo imeonyesha kudorora katika eneo la kujenga ufanisi wa mazingira ya TEHAMA ili kuhakikisha usiri, usalama na uadilifu wa shughuli za umma. Pamoja na kuimarika, hatua zaidi zinahitajika ili kuhakikisha kwamba Taasisi zote zinaweka mifumo madhubuti ya ndani ili kutimiza ufanisi wa majukumu yaliyopo kisheria

## Sura ya Saba

## USIMAMIZI WA RASILIMALI WATU NA MISHAHARA

### 7.0 Utangulizi

Sura hii ya ripoti inaonyesha masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa rasilimali watu na mishahara kwa taasisi za Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Masuala muhimu yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa usimamizi wa rasilimali watu na mishahara ni haya yafuatavyo:

### 7.1 Mambo muhimu yaliyobainika katika ukaguzi wa usimamiaji wa rasilimali watu na mishahara

#### 7.1.1 Ukiukwaji wa utaratibu wa urejeshwaji wa mikopo kwa mujibu wa Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Wakati wa ukaguzi nilibaini kutokuzingatiwa kwa masharti ya mikopo ya wanafunzi katika Wizara, Idara na Wakala ikiwa ni pamoja na Kifungu cha 20(1)(a) – (c) cha Sheria namba 9 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ya mwaka 2004.

Ukaguzi niliofanya pamoja na mahojiano na Maafisa Masuuli nimebaini kuwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu hawakuwa na mawasiliano na wanufaika wa mikopo mara baada ya kuhitimu mafunzo yao.

Maafisa Masuuli (Waajiri) wa Wizara, Idara na Wakala hawakukagua wala kutoa mwongozo wa kutosha kwa wafanyakazi kuhusiana na urejeshwaji wa mikopo pindi inapotumwa. Katika mwaka huu, nimekagua Wizara/Idara nne (4) na Sekretariati za Mikoa mbili (2) kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.42** na yafuatayo ndio mapungufu yaliyobainika:-

**Jedwali 42: Mapungufu yaliyobainika katika urejeshwaji wa mikopo ya elimu ya juu**

| Fungu | Taasisi | Matokeo ya ukaguzi |
|---|---|---|
| 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | Desemba 14, 2001 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilitoa Waraka Na AB. 71/348/01/8 kwa Taasisi zote za elimu ya juu ambao ulizitaka taasisi hizo zionyeshe aina ya udhamini wa mwanafunzi kwenye cheti cha mhitimu ili kuwawezesha waajiri kuwatambua wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu. Taasisi nyingi za elimu ya juu zilishindwa kutekeleka Agizo hilo la Wizara. |
| 72 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | Sekretarieti ya Mkoa haijawahi kuwasiliana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuhusu waajiriwa wapya ili kuiwezesha Bodi kufuatilia wafanyakazi hao kwenye masijala yake ya takwimu. Katika mwaka huu wa ukaguzi, Sekretarieti ya Mkoa iliajiri wafanyakazi wapya 78, hata hivyo, hakuna ushahidi kwamba, utaratibu ulifanywa kwa wafanyakazi wapya ili kuhakikisha kila mnufaika wa mkopo wa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu anarejesha mkopo kwa makato ya kila mwezi na kutumwa Bodi. |
| 89 | Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa | Wafanyakazi watatu wa Sekretarieti ya Mkoa walinufaika na mkopo kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu. Hata hivyo, Sekretarieti ya Mkoa haijatuma marejesho yao ya mkopo kwenda Bodi yenye jumla Sh. 72,060,407.36 ambazo ni mkopo wa kiasi cha shilingi 65,509,461.24 na adhabu ya Sh. 6,550,946.12. |
| 43 | i ya Kilimo, Chakula na Ushirika | Wafanyakazi sita wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika walishindwa kulipa mkopo kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Wakati walipotakiwa kurejesha mikopo hiyo, tayari walikuwa na mikopo mingine kutoka Taasisi za Fedha. |

| Fungu | Taasisi | Matokeo ya ukaguzi |
|---|---|---|
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandika barua mbili, yenye kumbukumbu Na. AB.67/456/01/50 ya tarehe 16/07/2015 kwa Foster Auctioneers and General Traders ambaye ni Wakala wa kukusanya madeni na nyingine yenye kumbukumbu Na. AB.112/352/01/08 ya tarehe 07/03/2012 kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kuiomba Bodi kuthibitisha mikopo ya wanafunnzi ili kupanga marejesho ya kila mwezi kutoka kwenye mishahara yao. Hata hivyo, hadi mwezi Novemba, 2015 hakuna majibu yaliyotolewa na bodi ili kuthibitisha mikopo ya wanafuzi wa elimu ya juu. |
| 31 | Ofisi ya Makamu wa Rais | Kinyume na masharti ya Sheria namba 9 ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, 2004, Ofisi ya Makamu wa Rais imeajiri wafanyakazi 25 kuanzia Julai, 2007 hadi Agosti, 2015. Hata hivyo, Menejimenti haikuitaarifu Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu juu ya ajira hizo. |

Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

Nawashauri Maafisa Masuuli (Waajiri) kuitaarifu Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuhusu kuwaajiri wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu na kutuma marejesho ya mikopo kutoka kwenye mishahara au marupurupu ya wanufaika wa mikopo ya Bodi ndani ya siku kumi na tano (15) baada ya mwisho wa mwezi. Pia, wanufaika wa mikopo (waajiriwa) kupanga na waajiri kuhusu makato ya kila mwezi kutoka kwenye mishahara yao na kuhakikisha malipo ya makato ya kila mwezi yanatumwa na mwajiri kwenda Bodi.

### 7.1.2 Malipo kwa wafanyakazi ambao hawapo kwenye Utumishi wa Umma Shilingi 392,651,036

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa kiasi cha Shilingi 392,651,036 kililipwa kama mishahara kwa watumishi walioacha kazi, waliofukuzwa, waliofariki na waliostaafu kama inavyoonekana kwenye **jedwali Na.43** Hii inaonyesha kutozingatiwa kwa matakwa ya Kanuni ya 112 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inayosema mapitio ya mara kwa mara ya watumishi yafanyike ili kuondoa kwenye orodha wafanyakazi ambao hawapo kwenye utumishi wa umma. Malipo kwa wafanyakazi ambao hawapo kwenye utumishi wa umma husababisha hasara kwa taifa, hivyo, natoa wito kwa viongozi wa taasisi za umma kushughulikia suala hii.

**Jedwali 43: Mishahara iliyolipwa kwa wafanyakazi ambao hawapo kwenye Utumishi wa Umma**

| Fungu | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 77 | Sekretarieti ya Mkoa- Mara | 8,054,080 |
| 70 | Sekretarieti ya Mkoa- Arusha | 16,507,788 |
| 72 | Sekretarieti ya Mkoa- Dodoma | 2,302,660 |
| 47 | Sekretarieti ya Mkoa- Simiyu | 878,825 |
| 86 | Sekretarieti ya Mkoa -Tanga | 10,762,700 |
| 81 | Sekretarieti ya Mkoa -Mwanza | 5,941,708 |
| 89 | Sekretarieti ya Mkoa -Rukwa | 6,841,700 |
| 82 | Sekretarieti ya Mkoa- Ruvuma | 5,236,033 |
| 85 | Sekretarieti ya Mkoa -Tabora | 27,084,000 |
| 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | 76,782,367 |
| 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani | 2,360,000 |
| 53 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto | 21,881,000 |
| 43 | Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika | 32,294,689 |

| Fungu | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 28 | Jeshi la Polisi | 158,855,537 |
| 79 | Sekretarieti ya Mkoa-Morogoro | 16,181,046 |
| 83 | Sekretarieti ya Mkoa -Shinyanga | 686,903 |
| | Jumla | 392,651,036 |

*Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015*

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 kumekuwa na Taasisi kumi na sita (16), hili ni ongezeko la Taasisi tisa (9) kutoka Taasisi saba (7) zilizoripotiwa mwaka wa fedha 2013/2014. Hili ni tatizo la kimfumo serikalini.

Zaidi ya hayo, ilibainika kuwa Sekretariati ya Mkoa Rukwa ina mfanyakazi mmoja mwenye Namba ya Mshahara 9790184 ambaye hayupo kazini kwa zaidi ya miaka miwili kutoka tarehe 20 Julai, 2013 na hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa ili kusitisha ajira yake. Kwa upande mwingine, Sekretarieti iliendelea kumlipa mishahara yake kupitia akaunti yake ya benki.

Nawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa fedha zilizolipwa zinarejeshwa Wizara ya Fedha. Pia, nawashauri Maafisa Masuuli kuimarisha udhibiti katika urekebishaji wa kumbukumbu za wafanyakazi kwenye mfumo wa LAWSON na uboreshwaji wa kumbukumbu uwe endelevu katika Taasisi zote za Serikali Kuu.

Pia, nawashauri Maafisa Masuuli kuwaondoa wafanyakazi walioacha kazi kwa wakati kwenye orodha ya mishahara ili kuepusha hasara kwa serikali na pia kuhakikisha wafanyakazi walioacha kazi na kulipwa mishahara wanarejesha fedha walizolipwa.

### 7.1.3 Makato ya kisheria kwenye Mishahara yalifanywa kwa wafanyakazi walioacha kazi Shilingi 61,477,664

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, Sekretariati za Mikoa sita (6) zilibainika kufanya makato ya Shilingi 61,477,664 kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi waliostaafu, waliofariki na walioacha kazi na kuyatuma kwa taasisi mbalimbali kama vile Mifuko ya Pensheni, Taasisi za Fedha, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mishahara halisi ya watumishi waliokatwa haikurejeshwa Hazina kama mishahara isiyolipwa au kulipwa kwa wafanyakazi ambao hawapo kwenye utumishi wa umma. Mwenendo huo husababisha kuwepo kwa malipo ambayo si sahihi. **Jedwari Na. 44** linaonyesha orodha ya taasisi zilizofanya makato kwa wafanyakazi ambao hawapo kwenye utumishi wa umma

**Jedwali 44: Makato yaliyolipwa kwa niaba ya wafanyakazi ambao hawapo kwenye utumishi wa Umma**

| Fungu | Taasisi | Makato (Sh.) |
|---|---|---|
| 77 | Sekretarieti ya Mkoa- Mara | 3,998,040 |
| 70 | Sekretarieti ya Mkoa -Arusha | 7,819,412 |
| 89 | Sekretarieti ya Mkoa- Rukwa | 23,383,196 |
| 82 | Sekretarieti ya Mkoa- Ruvuma | 2,379,967 |
| 85 | Sekretarieti ya Mkoa -Tabora | 23,897,049 |
| | **Jumla** | **61,477,664** |

Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

Nawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa Taasisi za Fedha na Mifuko ya Pensheni zinarejesha makato yaliyolipwa kwa makosa. Kwa siku zijazo, Taasisi za Umma zijidhatiti

kuzuia mapungufu yaliyojitokeza, ambayo husababisha ongezeko la gharama za mishahara bila sababu.

### 7.1.4 Upungufu wa Watumishi wa Umma

Ukaguzi wangu wa miundo ya utumishi kwa sampuli ya Taasisi arobaini (40) za serikali ulibaini nafasi 16,643 ambazo zilikuwa hazijajazwa kwa kuzingatia miundo iliyopitishwa kama inavyoonekana kwenye **kiambatisho Na.7.1.** Upungufu wa watumishi huathiri utoaji wa huduma katika Taasisi za Serikali.

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa Ofisi ya Rais ya Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Kipaumbele una upungufu wa watumishi kumi na wanane (18), Ubalozi wa Tanzania Kampala una upungufu wa watumishi sita (6), Ubalozi wa Tanzania Hague una upungufu wa watumishi watatu (3) na Ubalozi wa Tanzania Cairo una upungufu wa watumishi wawili (2).

Mapungufu kama haya yalijitokeza pia kwenye taarifa yangu ya mwaka uliopita. Suala hili ni kubwa na halizuiliki katika Taasisi za Umma. Jitihada za makusudi zinahitajika ili kuongeza idadi ya wafanyakazi.

Nawashauri Maafisa Masuuli wakishirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhakikisha nafasi zote zilizo wazi zinajazwa au Serikali ipitie upya Miundo ya Utumishi ili iendane na mahitaji halisi.

### 7.1.5 Wafanyakazi ambao hawajathibitiswa baada ya muda wa majaribio kumalizika

Kanuni ya D.40 (1) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema kuwa pale ambapo mtumishi ameajiriwa kwenye ofisi ya umma katika masharti ya kudumu na pensheni, mtumishi huyo atakuwa kwenye kipindi cha majaribio cha miezi kumi na miwili.

Kanuni ya D.45 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema mtumishi wa umma anayo haki ya kuthibitishwa katika cheo chake baada ya kipindi cha majaribio kinapomalizika iwapo mwenendo na utendaji wake vinaridhisha.

Kinyume na matakwa hayo ya Kanuni za Utumishi wa Umma, mapitio ya orodha kuu ya wafanyakazi wa taasisi za umma waliopo kwenye Sekretariati za Mikoa mitatu (3) na Wizara moja (1) umebaini kuwa watumishi 356 hawajathibitishwa kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.45** ingawa wengi wao wamefanya kazi kwa zaidi ya miaka thelathini (30) hadi tarehe 30 Juni, 2015. Mwamko wa utendaji kazi huwa mdogo pale ambapo mtumishi huwa hajathibitishwa.

**Jedwali 45: Taasisi zenye watumishi ambao hawajathibitishwa**

| Fungu | Taasisi | Idadi ya Wafanyakazi |
|---|---|---|
| 77 | Sekretarieti ya Mkoa Mara | 133 |
| 70 | Sekretarieti ya Mkoa Arusha | 115 |
| 89 | Sekretarieti ya Mkoa Rukwa | 96 |
| 99 | Wizara ya Mifugo na Maendeleo ya Uvuvi | 12 |
| | Jumla | 356 |

Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

Ninashauri kwamba Maafisa Masuuli wahakikishe wafanyakazi wanathibitishwa mara baada ya kipindi cha majaribio kukamilika na taarifa zao zilizopo kwenye mfumo wa LAWSON zinarekebishwa.

### 7.1.6 Kukosekana kwa ushahidi wa kupima na kutathimini utendaji wa wafanyakazi kwa uwazi

Kanuni ya D.62 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema kuwa taasisi zote ziwe na mfumo wa uwazi wa kutathimini utendaji kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni ya 22 ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003.

Kanuni ya 22(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003 inasema kuwa kila taasisi iliyopo kwenye utumishi wa umma iwe na mfumo wa uwazi wa kutathmini utendaji wa wafanyakazi wake wote; matakwa haya ni kwa mujibu wa kanuni ya D.62 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009.

Zaidi ya hayo, Kanuni ya 22(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2003 inasema kuwa lengo la kutathmini utendaji ni kubainisha, kupima na kuweka kumbukumbu za uwezo na mapungufu ya kila mfanyakazi ili kuweza kuchukua hatua za kuboresha ufanisi katika utumishi wa umma kama lengo endelevu.

Ukaguzi wangu kwa sampuli ya Sekretariati za Mikoa mitano (5) na Wizara mbili (2) ulibaini kuwa kati ya majalada 187 yaliyokaguliwa, majalada 119 hayakuwa na ushahidi kwamba, utendaji ulipimwa na kutathminiwa kwa uwazi katika mwaka huu wa ukaguzi kama inavyoonekana kwenye **jedwali Na.46** hapo chini. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa ubalozi wa Tanzania London hawakufanya tathmini na kupima utendaji wa wafanyakazi wake.

Kushindwa kutathimini utendaji wa wafanyakazi husababisha uongozi kushindwa kutambua mapungufu ya kiutendaji ya wafanyakazi wake ili kutengeneza mikakati ya kuyashungulikia. Mbali na hayo, ni vema kuwa na mfumo wa

wazi wa kupima na kutathmini utendaji ambao utazingatia utendaji wa mtumishi katika kupanda vyeo, mafunzo na uhamisho.

**Jedwali 46: Kutofanyika kwa tathmini ya uwazi ya utendaji kazi**

| Fungu | Taasisi | Majarada yaliyopitiwa | Majarada yenye Mapungufu |
|---|---|---|---|
| 70 | Sekretarieti ya Mkoa -Arusha | 10 | 7 |
| 75 | Sekretarieti ya Mkoa -Kilimanjaro | 25 | 8 |
| 84 | Sekretarieti ya Mkoa -Singida | 11 | 9 |
| 86 | Sekretarieti ya Mkoa -Tanga | 30 | 19 |
| 82 | Sekretarieti ya Mkoa- Ruvuma | 35 | 2 |
| 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani | 15 | 13 |
| 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 61 | 61 |
| | **Jumla** | **187** | **119** |

Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

Nawashauri Maafisa Masuuli wapime na kutathimini utendaji wa wafanyakazi mara kwa mara kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009.

### 7.1.7 Wakuu wa Vitengo kukaimu nafasi zilizo wazi kwa zaidi ya miezi sita

Kanuni ya 24(3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inasema kuwa pale inapowezekana, wafanyakazi wa umma wasikaimu kwenye nafasi kwa kipindi kinachozidi miezi sita. Mamlaka ya uteuzi ifanye mchakato wa uteuzi kwa nafasi iliyo wazi ndani ya kipindi cha miezi sita.

Ukaguzi wangu juu ya usimamizi wa rasilimali watu katika taasisi zilizopo chini ya Serikali Kuu ulibaini kuwa Taasisi saba (7) zenye jumla ya watumishi ishirini (20) zilikuwa na watumishi wanaokaimu kwenye nafasi mbalimbali kama inavyooneka kwenye **jedwali Na. 47**

Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa watumishi hao wanakaimu kwa kipindi kinachozidi miezi sita bila kuthibitishwa. Wafanyakazi wasipothibitishwa kwa muda mrefu huweza kukosa ari ya kufanya kazi na hatimaye ufanisi kupungua.

**Jedwali 47: Wakuu wa Vitengo wanaokaimu katika nafasi mbalimbali**

| Na. | Fungu | Taasisi | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa -Arusha | 1 |
| 2 | 72 | Sekretarieti ya Mkoa -Dodoma | 5 |
| 3 | 95 | Sekretarieti ya Mkoa -Manyara | 1 |
| 4 | 36 | Sekretarieti ya Mkoa- Katavi | 2 |
| 5 | 82 | Sekretarieti ya Mkoa -Ruvuma | 4 |
| 6 | 85 | Sekretarieti ya Mkoa -Tabora | 4 |
| 7 | 66 | Ofisi ya Rais – Tume ya Mipango | 3 |
| | | **Jumla** | **20** |

Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

Nashauri Maafisa Masuuli kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma wajaze nafasi zilizo wazi kwa kutumia wafanyakazi wenye sifa.

### 7.1.8 Kuchelewa kutuma makato ya Mishahara kisheria - Shilingi 707,169,904

Nilibaini kuwa makato ya Mishahara kisheria ya shilingi 707,169,904 kama inavyoonekana kwenye **jedwali Na.48** yalikatwa kutoka kwenye mishahara ya wafanyakazi wa Sekretarieti za Mikoa miwili (2), lakini hatuna ushahidi kama fedha hizo zilipelekwa kwa taasisi husika, ikiwemo Mfuko ya Hifadhi ya Jamii, Mfuko wa Pensheni kwa watumishi wa Umma, Mfuko wa Pensheni wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zingine za Fedha. Ucheleweshaji wa makato ya Kisheria husababisha faini na tozo kutoka kwa Taasisi husika.

**Jedwali 48: Taasisi zilizochelewesha kutuma makato kwenda mifuko ya Hifadhi ya Jamii**

| Fungu | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 75 | Sekretarieti ya Mkoa -Kilimanjaro | 590,670,916 |
| 36 | Sekretarieti ya Mkoa -Katavi | 116,498,988 |
| | **Jumla** | **707,169,904** |

Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

Naishauri Serikali kuhakikisha makato ya kisheria yanatumwa kwenda katika Taasisi husika kwa wakati.

### 7.1.9 Kodi ya Mapato kutolipwa kutoka kwenye posho za kukaimu Shilingi 78,187,048

Kwa mujibu wa Kanuni D.18 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 kuteuliwa kukaimu hutokea pale ambapo mfanyakazi atapangwa kwa muda kutekeleza majukumu ya nafasi inayohitaji uteuzi.

Kifungu Na. 7 (2) (a) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa 2008) inahitaji mapato yote yanayotokana na ajira yakatwe kodi isipokuwa posho ya kujikimu, safari, ukarimu au posho zinginezo anazolipwa mtumishi ili kumwezesha kufanya kazi itakayomfanya apate kipato katika ajira yake au kutoa huduma kama inavyotakiwa chini ya Kifungu 7 (3) (d) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa 2008).

Ukaguzi wangu kwenye sampuli ya Taasisi za Serikali tatu (3) ulibaini kuwa posho ya kukaimu ya Shilingi 78,187,048 kama inavyoonekana kwenye **jedwali Na.49** hapo chini kililipwa bila kukatwa kodi ya mapato, hivyo, wafanyakazi

hao walilipwa sehemu ya kodi ya mapato badala ya kuipeleka Mamlaka ya Mapato Tanzania kama inavyotakiwa na kifungu Na. 7(2)(a) cha Sheria ya kodi ya Mapato ya mwaka 2004 (iliyorekebishwa 2008).

Nashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha posho ya kukaimu inakatwa kodi ya mapato. Pia, Maafisa Masuuli wahakikishe kodi ambayo haikukatwa inalipwa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

**Jedwali 49: Posho ya kukaimu iliyolipwa bila kukatwa kodi ya mapato**

| Fungu | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 81 | Sekretariati ya Mkoa- Mwanza | 39,569,000 |
| 89 | Sekretariati ya Mkoa- Rukwa | 36,311,000 |
| 32 | Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma | 2,307,048 |
| | Jumla | 78,187,048 |

**Chazo:** Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

### 7.1.10 Watumishi walio na mikataba ubalozini hawakulipwa kiinua mgongo - Shilingi 17,980,539

Nilibaini kuwa watumishi wa mikataba katika Ubalozi wa Tanzania Cairo hawakulipwa Shilingi 17,980,539 ikiwa ni kiinua mgongo kwa mwaka unaoishia Desemba, 2015. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,990,270 ni kwa ajili ya kipindi kinachoishia tarehe 30 Juni, 2015 na shilingi 8,990,270 ni ya kipindi cha kuanzia Julai, 2015 hadi Desemba, 2015. Kulingana na utaratibu kulipa kiinua mgongo inapaswa kulipwa mwezi Desemba kila mwaka .

Naishauri Serikali kuhakikisha watumishi wa mikataba balozi mbalimbali wanalipwa kiinua mgongo kwa mujibu wa mikataba yao ya kazi.

### 7.1.11 Mishahara isiyolipwa ambayo haijarejeshwa Hazina - Shilingi 2,233,475,668

Kanuni na.133 (1) na (2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inasema kama amana ambayo itaendelea kutodaiwa kwa zaidi ya miaka mitano inaweza, kwa idhini ya Mhasibu Mkuu, kuhesabiwa kama mapato ya Serikali na Mhasibu Mkuu atarejesha fedha hizo kwa mtu yeyote anayestahili, endapo atajiridhisha kuwa madai ni halali. Na, marejesho yote baada ya amana iliyohamishiwa kwenye mapato lazima itoke kwenye matumizi yaliyopangwa (voted expenditures).

Ukaguzi wangu wa orodha ya mishahara na nyaraka nyinginezo katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kipindi cha miaka saba kuanzia 2007 hadi 2014 ulibaini mishahara ambayo haikulipwa kwa maafisa na askari ambao walisimamishwa kazi yenye jumla ya Shilingi 2,233,475,668 ilikuwa haijatumwa Hazina. Badala yake, mishahara ambayo haikulipwa iliendelea kuwa kwenye akaunti ya muda ya Mkuu wa Majeshi. Hivyo kuna hatari mishahara hiyo ikatumika vinginevyo.

Nashauri Maafisa Masuuli wazingatie Kanuni na. 133 (1) na (2) ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004). Pia, warejeshe mishahara ambayo haijalipwa Hazina.

### 7.1.12 Watumishi wa umma kupokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria

Kifungu cha 3 cha sheria ya kurejesha madeni ya mwaka 1970 - na waraka wenye Kumb. C / CE.45 / 271/01 / I / 87 wa Machi, 2009 uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma kinawaelekeza Makatibu wakuu wote kuhakikisha makato ya mishahara kwa watumishi kwa ajili kurejesha mikopo

katika mwezi hayazidi theluthi mbili ya mshahara.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwa wafanyakazi 875 kutoka katika taasisi mbili (2) za serikali walilipwa mishahara chini ya kiwango kilichokubalika kisheria. Watumishi wanaopata mishahara midogo hukosa ari ya kufanya kazi na kupelekea utendaji duni na kutoa huduma chini ya viwango, taasisi zenye watumishi hao ni kama inavyoonekana kwenye **jedwali Na.50**

**Jedwali 50: Taasisi ambazo watumishi wake wanapata mishahara chini ya kiwango kilichopitishwa kisheria**

| Fungu | Taasisi | Idadi ya Watumishi |
|---|---|---|
| 82 | Sekretariati ya Mkoa Ruvuma | 4 |
| - | Mamlaka ya Mapato Tanzania | 871 |
| | Jumla | 875 |

Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

Kama ilivyojitokeza kwenye miaka iliyopita, tatizo hili bado limeendelea kuwa kubwa kwenye Taasisi za Umma kwani bado kuna ukiukwaji wa utaratibu. Wakati jumla ya wafanyakazi wanaopokea mishahara chini ya kiwango kinachokubalika kisheria ikiongezeka kutoka 314 mwaka jana hadi 875 mwaka huu, ikiwa ni ongeze wafanyakazi 561; idadi ya taasisi zimepungua kutoka kumi na mbili (12) hadi mbili (2).

Nashauri Maafisa Masuuli waimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani katika kuthibitisha mikopo ya watumishi kwa kushirikiana na watoa mikopo ili kuhakikisha kuwa makato hayazidi theluthi mbili ya mshahara wa mwezi kwa mujibu wa

kifungu cha 3 cha sheria ya kurejesha madeni ya mwaka 1970 - na waraka wenye Kumb. C / CE.45 / 271/01 / I / 87 wa Machi, 2009 uliotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

**7.1.13 Watumishi waliostaafu kufanya kazi bila kuwa na mikataba ya ajira**

Ubalozi wa Tanzania Washington DC una mtumishi mmoja ambaye amestaafu tarehe 14 Machi, 2015 lakini bado anaendelea na kazi ubalozini bila mkataba wa kazi unaotambulika kutokana na ukosefu wa fedha za kusafirishia mizigo kutoka Washington DC. Hii ni kinyume cha Kanuni F.43 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009 inayohusu masharti ya kustaaafu kwa lazima.

Pia, nilibaini kuwa TZS 105,135,200 zililipwa kama posho za kuhudumu nje ya nchi kwa kipindi cha kuanzia 14 Machi, 2015 hadi Januari, 2016.

Naishauri serikali kupitia Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuwa iwe inawapa mkataba wa ajira wastaafu wakati wakisubiria upatikanaji wa fedha za kuwarejesha. Pia, Maafisa Masuuli wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa waandae mpango wa kuwezesha kuwarejesha nyumbani watumishi waliostaafu.

**7.1.14 Kufanya kazi ubalozini zaidi ya muda ulioidhinishwa**

Kifungu cha 31(1) na (2) cha Kanuni za Tanzania za kuhudumu nje ya nchi za mwaka 2013 ***(of the Tanzania Foreign services Regulations of 2013)*** kinasema afisa anaweza kupelekwa kituo chochote, ambapo anahitajika kufanya kazi, vinginevyo iwe imeelezwa kwenye fomu ya kazi ila itakuwa ni kipindi cha miezi arobaini na nane. Pia, barua za uteuzi wa wafanyakazi

huwapa muda wa miaka minne kufanya kazi ubalozini.

Ukaguzi wangu wa usimamizi wa rasililmali watu na mishahara kwa sampuli ya balozi tisa (9), ulibaini watumishi ishirini na watatu (23) wamehudumu zaidi ya muda ulioidhinishwa. Watumishi hao walikaa zaidi ya muda ulioidhinishwa ikiwa ni kati ya miaka mitatu hadi miaka mitano. Hii inatokana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kutowarejesha kutoka ubalozini. Maelezo ya watumishi waliokaa ubalozini zaidi ya muda uliothibitishwa ni kama yanavyoonekana kwenye **jedwali Na.51** hapo chini.

**Jedwali 51: Orodha ya ofisi za balozi zenye watumishi waliofanya kazi ubalozini zaidi ya muda ulioidhinishwa**

| Kasma | Ubalozi | Idadi ya watumishi |
|---|---|---|
| 2032 | Ubalozi wa Tanzania Brasilia | 1 |
| 2012 | Ubalozi wa Tanzania Ottawa | 2 |
| 2018 | Ubalozi wa Tanzania Washington DC | 2 |
| 2011 | Ubalozi wa Kudumu katika Umoja wa Mataifa --UN - New York | 5 |
| 2005 | Ubalozi wa Tanzania Abuja | 1 |
| 2001 | Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa | 3 |
| 2014 | Ubalozi wa Tanzania Beijing | 5 |
| 2004 | Ubalozi wa Tanzania Kinshasa | 1 |
| 2021 | Ubalozi wa Tanzania Kampala | 3 |
| | | **23** |

Chazo: Taarifa za ukaguzi kwa Menejimenti za Taasisi kwa mwaka 2014/2015

Namshauri Afisa Masuuli wa Wizara ya Mambo ya Nje

na Ushirikiano wa Kimataifa kuzingatia kanuni Na. 31(1) na (2) ya Kanuni za Tanzania za kuhudumu nje ya nchi za mwaka 2013 ***(of the Tanzania Foreign services Regulations of 2013)*** katika kufanya uhamisho wa watumishi.

## Sura ya Nane

## WAKALA WA SERIKALI NA TAASISI NYINGINE ZA SERIKALI

### 8.0 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo ya ukaguzi wa Wakala wa Serikali thelathini na mbili (32), Mifuko Maalumu ya Fedha (12) na Taasisi nyingine za Serikali (24) na vyama vya Siasa.

Sura hii inaonyesha masuala mahususi yanayohitaji kushughulikiwa na Serikali, Bunge, Bodi ya Ushauri ya Wizara na usimamizi wa taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli zao.

### 8.0 Masuala Muhimu Yaliyojitokeza kwenye ukaguzi

Yafutayo ni matokeo muhimu ya ukaguzi kwenye ukaguzi wa Wakala za Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

#### 8.1.1 Udhaifu katika Bajeti na Fedha

#### 8.1.1.1 Utegemezi wa Serikali

Vyanzo vya fedha kwa ajili ya bajeti ya Wakala wa Serikali ni pamoja na vyanzo vya ndani na misaada ya serikali (kawaida na ya maendeleo). Hali halisi ya upatikanaji wa fedha kutoka katika kila moja ya vyanzo hivi una athari juu ya utendaji wa jumla wa bajeti ya Wakala.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, jumla ya makisio ya mapato ya Wakala yalifikia kiasi cha shilingi 1,949,385,061,572, ikiwa ni pungufu ya shilingi 46,428,235,058 (2%) ikilinganishwa na makisio ya mwaka wa fedha 2013/2014 ya kiasi cha Shilingi 1,995,813,296,630. Katika jumla ya makisio yote kiasi cha Shilingi 1,655,629,610,241(85%)kilitarajiwakufadhiliwa

na ruzuku kutoka serikalini; na kiasi cha Shilingi 293,755,451,331 (15%) kutoka vyanzo vya ndani vya mapato. Kati ya ruzuku kutoka serikalini, kiasi cha Shilingi 685,760,849,482 (41%) kilikuwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 969,868,760,759 (59%) kwa ajili ya shughuli za maendeleo.




Kielelezo hapo juu kinaonesha uwezo wa Wakala kuendesha shuguli zake kwa kutegemea vyanzo vya ndani vya mapato; Wakala moja(3%) kati ya 32 imeweza kujiendesha kwa kutegemea vyanzo vyake vya ndani vya mapato kwa 100%, Wakala (11)(34%) kwa zaidi ya 50% na Wakala (20)(63%) kwa chini ya 50%. Wakala zinazojitegemea kwa zaidi ya 50% kutoka vyanzo vya ndani vya mapato, iwapo zitawezeshwa zitaweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka serikalini. Nimebaini kwamba Wakala mbili kati ya Wakala zinazojitemea kwa chini ya 50% ni Wakala zinazojiendesha kwa kutegemea ruzuku kutoka serikalini tu; kwa hiyo uwezo wa Wakala hizo kutegemea vyanzo vyake vya ndani kuendesha shughuli zake bado ni mdogo sana. Kwa ujumla inaonesha kwamba, kwa kiasi kikubwa, mpaka sasa Wakala zinategemea ruzuku kuendesha shughuli zake.

Makusanyo halisi yalikuwa jumla ya Shilingi

1,202,910,236,048 (62%) dhidi ya makisio yaliyoidhinishwa ya kiasi cha Shilingi 1,949,385,061,572; hivyo, kulikuwa na mapungufu ya makusanyo kiasi cha Shilingi 746,474,825,524 sawa na asilimia 39 ya jumla ya makisio yote. Hii ni upungufu wa kiasi cha Shilingi 171,341,522,409.68 (13%) ya makusanyo ikilingalishwa na makusanyo halisi ya mwaka 2013/2014 ya kiasi cha Shilingi 1,360,424,225,204.

Makisio ya Wakala yaliyoidhinishwa dhidi ya makusanyo halisi yameoneshwa katika jedwali Na. 52:

**Jedwali 52: Makisio yaliyoidhinishwa na Makusanyo halisi**

| S/N | Wakala | Jumla ya Makisio Shs. | Jumla ya Makusanyo Shs. |
|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa serikali Mtandao | 10,074,626,857 | 5,114,824,724 |
| 2 | Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi | 8,742,439,033 | 6,601,667,897 |
| 3 | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania | 81,228,596,000 | 88,271,762,518 |
| 4 | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa | 1,983,278,000 | 1,552,072,858 |
| 5 | Chuo cha Utumishi wa Umma | 22,576,110,000 | 19,493,979,775 |
| 6 | Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania | 1,453,376,000 | 1,079,765,148 |
| 7 | Wakala wa Mbegu za Kilimo | 8,919,630,408 | 5,814,013,612 |
| 8 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa | 13,261,413,809 | 11,064,881,940 |
| 9 | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo | 3,259,203,800 | 2,525,611,414 |
| 10 | Wakala wa Utafiti wa Miamba | 12,234,598,300 | 5,911,151,110 |
| 11 | Chuo cha Mafunzo ya Mifugo | 7,329,514,210 | 6,494,481,712 |
| 12 | Wakala wa Akiba ya Chakula Taifa | 154,600,547,950 | 188,370,098,469 |
| 13 | Wakala wa Majengo Tanzania | 22,573,755,813 | 14,448,354,348 |
| 14 | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi | 53,881,438,514 | 44,425,571,750 |
| 15 | Wakala wa Ndege za Serikali | 21,571,957,000 | 16,399,374,687 |
| 16 | Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa | 23,919,514,422 | 16,270,980,167 |
| 17 | Wakala wa Barabara Tanzania | 1,116,334,213,000 | 481,759,738,304 |
| 18 | Wakala wa Maabara za Mifugo | 3,580,503,400 | 1,991,582,009 |
| 19 | Chuo cha Maendeleo  na Usimamizi wa Maji | 8,471,433,097 | 4,591,325,785 |
| 20 | Wakala wa Vipimo | 20,868,033,728 | 18,186,885,122 |
| 21 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | 3,258,518,000 | 1,839,870,786 |
| 22 | Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu | 3,459,011,040 | 2,584,323,639 |
| 23 | Wakala wa Maabara za Serikali | 3,551,420,000 | 10,155,207,380 |
| 24 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni - Bagamoyo | 2,046,984,000 | 1,258,655,753 |
| 25 | Wakala wa Usalama na Afya Kazini | 7,582,079,370 | 6,996,180,528 |
| 26 | Wakala wa Huduma za Ajira | 1,823,833,600 | 1,133,708,687 |
| 27 | Wakala wa ukaguzi wa Uchimbaji Madini Tanzania | 11,178,436,000 | 10,886,222,000 |
| 28 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam | 6,880,542,440 | 4,376,537,266 |
| 29 | Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi | 13,629,422,000 | 7,555,166,694 |
| 30 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania | 21,044,452,000 | 20,317,203,448 |
| 31 | Wakala wa Umeme Vijjini | 269,457,877,881 | 191,887,823,176 |
| 32 | Chuo cha Taifa cha Utalii | 8,608,301,900 | 3,551,213,342 |
| | | **1,949,385,061,572** | **1,202,910,236,048** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015*

Katika mwaka 2014/2015 kiasi cha Shilingi 879,855,434,819 (73%) ya makusanyo

yotekilitokana na ruzuku kutoka serikalini na kiasi cha Shilingi 323,054,801,229 (27%) kilitoka vyanzo vya ndani vya mapato; kati ya ruzuku ya kutoka Serikalini, kiasi cha shilingi 389,572,100,385 (44%) kilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha Shilingi 490,283,334,434 (56%) kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Kielelezo hapo chini kinaonesha makusanyo halisi kutoka vyanzo vya ndani na ruzuku serikalini:




Kielelezo hapo juu kinaonesha makusanyo halisi kutoka serikalini na vyanzo vya ndani vya mapato. Kutokana na Kielelezo Na.16, kiasi cha 73% ya makusanyo yalitokana na ruzuku serikalini na 27% yalitokana na vyanzo vya ndani vya mapato; hivyo, makusanyo kutoka vyanzo vya ndani yameongezeka kwa kiasi cha Shilingi 26,352,696,008 sawa na asilimia tisa kilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2013/2014 ya kiasi cha Shilingi 296,702,105,221; ruzuku kutoka serikalini imepungua kwa kiasi cha Shilingi 183,866,685,164 sawa na asilimia 17 kilinganishwa na ruzuku ya mwaka 2013/2014 ya kiasi cha shilingi 1,063,722,119,983.

#### 8.1.1.2 Fedha iliyoidhinishwa na Serikali kwa Matumizi ya Kawaida na Maendeleo haikutolewa Shilingi 775,774,175,422

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya Shilingi 879,855,434,819 ilitolewa na serikali kama

ruzuku ya maendeleo na matumizi ya kawaida, ikiwa ni pungufu ya Shilingi 775,774,175,422 (47%), ya fedha zilizoidhinishwa kiasi cha Shilingi 1,655,629,610,241. Kiasi cha Shilingi 296,188,749,097 (38%) kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na kiasi cha Shilingi 479,585,426,325 (62%) kwa ajili ya shughuli za maendeleo hazikutolewa; hivyo kusababisha shughuli za kawaida na maendeleo kukwama kutokana na upungufu wa fedha zilizotolewa.

Makisio ya fedha za Wakala zilizoidhinishwa na fedha zilizotolewa yameoneshwa kwenye jedwali Na. 53 hapo chini:

**Jedwali 53: Makisio yaliyoidhinishwa na Fedha zilizotolewa**

| S/N | Wakala | Jumla ya Makisio Shs. | Fedha Zilizotolewa Shs. |
|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa serikali Mtandao | 8,631,264,857 | 4,831,543,960 |
| 2 | Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi | 3,311,242,912 | 2,594,601,793 |
| 3 | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania | - | - |
| 4 | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa | 290,878,000 | 182,425,086 |
| 5 | Chuo cha Utumishi wa Umma | 5,016,730,000 | 3,550,736,150 |
| 6 | Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania | 1,015,476,000 | 477,917,895 |
| 7 | Wakala wa Mbegu za Kilimo | 4,944,630,408 | 4,077,827,614 |
| 8 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa | 4,950,421,004 | 2,562,915,424 |
| 9 | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo | 1,850,114,800 | 848,403,536 |
| 10 | Wakala wa Utafiti wa Miamba | 11,551,098,300 | 5,625,747,885 |
| 11 | Chuo cha Mafunzo ya Mifugo | 2,453,857,260 | 1,172,757,501 |
| 12 | Wakala wa Akiba ya Chakula Taifa | 111,656,840,000 | 111,533,816,548 |
| 13 | Wakala wa Majengo Tanzania | 6,372,715,600 | 2,880,848,058 |
| 14 | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi | 23,920,867,250 | 16,875,672,119 |
| 15 | Wakala wa Ndege za Serikali | 15,882,797,000 | 10,290,857,076 |
| 16 | Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa | 17,594,514,422 | 10,809,270,328 |
| 17 | Wakala wa Barabara Tanzania | 1,109,673,890,000 | 471,502,591,304 |
| 18 | Wakala wa Maabara za Mifugo | 2,812,003,400 | 1,499,008,775 |
| 19 | Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji | 7,435,062,297 | 3,535,544,655 |
| 20 | Wakala wa Vipimo | 2,809,630,000 | 3,043,705,450 |
| 21 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | 2,394,998,000 | 745,004,947 |
| 22 | Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu | 1,754,566,040 | 766,461,764 |
| 23 | Wakala wa Maabara za Serikali | 3,551,420,000 | 1,949,281,289 |
| 24 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni - Bagamoyo | 1,831,984,000 | 756,885,903 |
| 25 | Wakala wa Usalama na Afya Kazini | 2,781,539,370 | 1,438,620,733 |
| 26 | Wakala wa Huduma za Ajira | 1,743,833,600 | 969,580,208 |
| 27 | Wakala wa ukaguzi wa Uchimbaji Madini Tanzania | 10,978,436,000 | 10,705,544,000 |
| 28 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam | 6,880,542,440 | 4,376,537,266 |
| 29 | Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi | 4,735,000,000 | 2,564,772,000 |
| 30 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania | 3,654,352,000 | 3,489,900,788 |
| 31 | Wakala wa Umeme Vijjini | 269,440,305,381 | 191,870,250,676 |
| 32 | Chuo cha Taifa cha Utalii | 3,708,599,900 | 2,326,404,089 |
| | **JUMLA KUU** | **1,655,629,610,241** | **879,855,434,819** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

### 8.1.1.3 Makusanyo kutoka vyanzo vya ndani

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 mapato halisi kutoka vyanzo vya ndani yalikuwa kiasi cha Shilingi 323,054,801,229 ikilinganishwa na makisio yaliyoidhinishwa kiasi cha Shilingi

293,755,451,331. Kwa ujumla, kulikuwa na ongezeko la Shilingi 29,299,349,898 (10%) ya makisio ya mapato ya ndani yaliyoidhinishwa. Licha ya jumla ya ongezeko la makusanyo ya mapato ya ndani, Wakala 15 zilikusanaya chini ya makisio yaliyoidhinishwa kwa kiasi cha Shilingi 26,419,696,565 (20%); wakati Wakala 15 zilikusanya zaidi ya makisio yaliyoidhinishwa kwa kiasi cha Shilingi 55,719,046,463 (35%). Hii inaashiria kwamba Wakala 15 zilizokusanya zaidi ya makisio yao yaliyopitishwa bajeti zao hazikuwa na uhalisia.

Ninashauri serikali iandae utaratibu ambao utaziwezesha Wakala kuboresha mapato yake ya ndani na kuweza kujiendesha zenyewe pasipo kutegemea ruzuku kutoka serikalini.



### 8.1.2 Mapungufu yaliyojitokeza katika manunuzi na mikataba

#### 8.1.2.1 Manunuzi yaliyofanywa kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa Shilingi 165,583,183

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 wakala tatu zilikiuka sheria ya manunuzi namba 131(5), ya mwaka 2013 ambayo inazitaka taasisi za Serikali kufanya manunuzi kwa wazabuni waliodhinishwa. Taasisi ambazo zilifanya manunuzi kwa wazabuni ambao hawakuidhinishwa na Wakala wa ugavi na huduma za manunuzi (GPSA) ni Chuo cha Taifa cha Utalii ambacho kilinunua bidhaa zenye thamani ya shilingi 125,384,200; Wakala wa huduma za misitu Tanzania kiasi cha shilingi 25,494,460 na kiasi cha shilingi 14,704,523 ni matengenezo ya magari yaliyofanywa na Wakala wa vizazi, vifo na ufilisi (RITA) bila kupitia Wakala wa umeme, mitambo na ufundi (TEMESA).

Ninashauri Wakala zote zifuate sheria ya Umma ya manunuzi ili kuweka uwazi katika shughuli

za manunuzi.

**8.1.2.2 Kuchelewa kuanza huduma ya usafiri wa mabasi**

Nimebaini kwamba Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) iliingia mkataba na UDA-RT (ISP) kwa ajili ya utoaji huduma ya usafiri wa mabasi wa mpito (Interim Bus Service); mpaka kufikia Desemba 2015, huduma ya usafiri ilikuwa haijaanza kutolewa na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa na Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam dhidi ya UDA –RT.

Napendekeza Wakala wa usafiri wa mabasi yaendayo kasi kufuata masharti yaliyowekwa kwenye mikataba ili kuepuka mikataba kuchelewa zaidi.

**8.1.2.3 Ununuzi wa mabasi uliozidi mahitaji**

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 nilibaini kwamba Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) uliingia mkataba na UDA-RT ambao uliitaka UDA-RT kutoa huduma ya usafiri wa mpito wa kuendesha mabasi 76 kulingana na vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba. Kwa kuzingatia sheria ya manunuzi ya Umma, Mkataba umetoa ongezeko la mabasi kufikia 84 kulingana na matakwa ya Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART). Kwa kupitia nyaraka mbalimbali wakati wa ukaguzi nimebaini kwamba UDA walinunua jumla ya mabasi 140 ikiwa ni zaidi ya mabasi 54 yaliyoidhinishwa kwenye mkataba. Pia, nilibaini kwamba mabasi yaliyonunuliwa yalikuwa na nembo ya UDA-RT badala ya DART kinyume na vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba.

Nimebaini kwamba UDA-RT ilifanya ununuzi wa mabasi uliozidi mahitaji ya Wakala. Napendekeza kwamba uongozi wa Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) uhakikishe kwamba uendeshwaji wa UDA-RT

unazingatia kanuni na tararibu zilizoainishwa kwenye mkataba.

#### 8.1.2.4 Mkataba usiokuwa na muda

Rondo Forest Plantation iliingia mkataba Machi 9, 2015 na PRIME TIMBER LTD chini ya Wakala wa huduma ya misitu Tanzania wa uvunaji wa mita za mraba 6,766.9 za mitiki katika mwaka wa fedha 2014/2015; mkataba huo haukuonesha muda uliotakiwa kutumiwa na PRIME TIMBER LTD kukamilisha zoezi zima la uvunaji; hii inaweza kusababisha kuchelewesha katika uvunaji na upandaji au kuongeza garama kwa Wakala.

Napendekeza mikataba yote inayoingiwa chini ya Wakala wa huduma za misitu Tanzania iainishe muda ili kuepukana na ucheleweshwaji wa kuanza na kumaliza mkataba.

#### 8.1.2.5 Mkataba kwa ajili ya Supply and assembling of Tunnel Formwork System ulikuwa nje ya mpango wa manunuzi

Novemba 22, 2012 Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iliingia mkataba wa mwaka mmoja na M / S Mesa Imalat San. VE TIC wa **Supply and assembling of Tunnel Formwork System** kwa gharama ya dola 500,000 za Kimarekani sawa na shilingi 971,000,000. Manunuzi hayo hayakuwa kwenye mpango wa manunuzi ambapo ni kinyume na kifungu Na. 49 (3) cha sheria ya manunuzi, 2011; baada ya kupitia mkataba huo nilibaini kwamba Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) imelipa malipo ya ziada kiasi cha shilingi 147,585,464 kutokana na kuchelewa kutoa mzigo bandarini; pia nilibaini kwamba Mzabuni hakulipa dhamana ya utendaji kazi (Performance Security Bond) kiasi cha Dola 50,000 za kimarekani sawa na Shilingi 79,100,000 (10% ya gharama za mkataba) ambayo ilitakiwa kulipwa ndani ya siku 30 baada ya kupokea taarifa ya kuanza mkataba(notification of contract award).

Napendekeza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) izingatie sheria ya Manunuzi ili kuepuka kukosekana kwa ufanisi katika kutekeleza taratibu za manunuzi.

**8.1.2.6 Mikataba usotekelezwa**

Matokeo ya ukaguzi yanaonyesha kuwa Agosti 21, 2013 Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) iliingia mkataba kwa ajili ya manunuzi na ufungaji wa lifti katika Ujenzi wa jengo la Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) lililopo kitalu na. 5 na 7 mtaa wa Moshi Avenue mkoani Dodoma kwa gharama ya shilingi 131,762,380. Wakati wa ukaguzi nilibaini kwamba mpaka kufikia Julai 2015 mkandarasi alishindwa kukamilisha ujenzi wa lifti ingawa muda wa kumalizika kwa kazi hiyo uliisha tangu Januari 21, 2014; sambamba na hilo nilibaini pia kwamba Wakala wa Majengo Tanzania hakutoza tozo ya ucheleweshaji kazi (Liquidated Damages) ya asilimia 0.1 ya gharama ya mkataba kwa siku.

Napendekeza Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kuzingatia vigezo na masharti ilivyoainishwa katika mkataba.

Tarehe 30, Oktoba 2014 Wakala wa umeme, mitambo na ufundi (TEMESA) iliingia mkataba na M/s Navy Command wa matengenezo ya ghati kwa gharama Shilingi 180,000,000. Nilibaini kwamba dhamana ya utedaji kazi haikulipwa na mkandarasi wakati malipo ya awali ya kiasi cha Shilingi 90,000,000 yalipofanyika; pia nilibaini kwamba Wakala wa umeme, mitambo na ufundi (TEMESA) haikutoza tozo la ucheleweshaji kazi wala haikusimamisha mkataba licha ya mkandarasi kutowajibika kulingana na taratibu zilizoainishwa kwenye mkataba.

Wakala wa umeme, mitambo na ufundi (TEMESA) ihakikishe kwamba malipo ya awali yaliyolipwa

kwa makandarasi yanarejeshwa sambamba na tozo la ucheleweshaji kazi.

#### 8.1.2.7 Mapungufu ya ununuzi wa kivuko Shilingi 7,916,955,000

Wizara ya ujenzi kupitia Wakala wa umeme, mitambo na ufundi (TEMESA) iliingia mkataba na M/s Johs.Gram-Hanssen Bergensgade 10, DK 2100 Copenhagen Oe Denmark wa ununuzi wa kivuko cha Dar es salaam -Bagamoyo chenye thamani ya Dola za Kimarekani 4,980,000 bila Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT).Mapungufu yafutayo yalibainika katika manunuzi hayo:

**Kasi ya kivuko haikuzingatia matakwa ya mnunuzi**

Ripoti ya mtaalam wa ukaguzi ilibainisha kwamba kiwango cha juu na chini cha kasi ya kivuko wakati wa majaribio kilikuwa na kiwango kati ya 19.45 na 17.25 kinyume na makubaliano yaliyoainishwa kwenye mkataba ya kasi ya kiwango cha 20 .

**Hati ya makabidhiano haikutolewa**

Kivuko kilikabidhiwa bila hati ya makabidhiano (Goods Acceptance Certificate) Novemba 17, 2014 baada ya ucheleweshwaji wa siku 16; pia nilibaini kwamba mpaka wakati wa ukaguzi, Augusti 2015, hati ya makabidhiano ilikuwa haijatolewa na mzabuni kinyume na kanuni ya 248 ya mwaka 2013 ya manunuzi ya umma.

Napendekeza TEMESA awasiliane na Mzabuni kufanya marekebisho ya mapungufu yote yaliyobainishwa kwenye kivuko cha Dar es Salaam Bagamoyo; pia, hati ya makabidhiano itolewe kulingana na Kanuni ya manunuzi ya umma ya mwaka 2013.

#### 8.1.2.8 Gari lililo lipiwa halijapokelewa Shilingi 144,150,000

Nilibaini kwamba Wakala wa mafunzo ya mifugo (LITA) kililipa Wakala wa ugavi na huduma za

manunuzi (GPSA) kiasi cha Shilingi 144,150,000 kwa ajili ya ununuzi wa gari; mpaka kufikia Juni 30, 2015 gari lililolipiwa halikufika. Kutokana na kutofika kwa gari hilo, nimeshindwa kuthibitisha matumizi ya kiasi cha Shilingi 144,150,000; hivyo kuna uwezekano fedha hizo hazikutumika kwa matumizi yaliyopangwa.

Napendekeza menejimenti ya LITA ifuatilie kwa ukaribu ili kuhakikisha kwamba gari lililolipiwa linafika bia kuchelewa zaidi

**8.1.2.9 Kuchelewa kukamilika kwa kazi ya ujenzi**

Wakala wa Barabara (TANROADS) iliingia mikataba mbalimbali ya ujenzi wa barabara na madaraja. Wakati wa ukaguzi nilibaini kwamba, baadhi ya mikataba haikukamilika kwa muda uliopangwa kutokana na kuchelewa kwa ulipaji wa fedha kama ilivyoainishwa kwenye jedwali Na. 54; pia, nilibaini kwamba ucheleweshwaji wa malipo ya kati (Interim Payment Certificates) ya mikataba 16 ulisababisha ulipaji wa riba kiasi cha shilingi 5,616,652,022 na Dola za kimarekani 686,174.86

## Jedwali 54: Riba kwa kuchelewesha malipo

| SN | Maelezo ya Mkataba | Thamani ya Mkataba(Shs) | Tarehe Kuanza | Kumaliza | Riba (Shs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Daraja la Kilombero | 53,214,395,756 | 21.1.2013 | 20.1.2015 | 414,815,917 |
| 2 | Kuweka lami barabara ya Makutano-Natta(50 KM) | 46,138,083,789 | 17.5.2013 | 3.3.2016 | 90,358,036 |
| 3 | Kuweka lami barabara ya Kibondo-Nyakanazi(50 KM) | 45,985,780,766 | 13.6.2014 | 13.6.2016 | 128,297,105 |
| 4 | Kuweka lami barabara ya Kidahwe-Kasulu(50 KM) | 50,908,095,566 | 4.6.2014 | 4.6.2016 | - |
| 5 | Mkataba Namba TRD/HQ/1007/2009/10 wa Kuweka lami barabara ya Bariadi - Lamadi (71.8 km) | 67,408,991,569 | 9.9. 2009 | 23.12.2014 | 513,594,431.83 na Dola za Kimarekani 686,174.86 |
| 6 | Ujenzi wa Daraja la Sibiti(82M) na Barabara zake 25 KM | 16,302,313,479 | 01.11.2012 | 30.4.2014 | |
| 7 | Mkataba Namba TRD/HQ/1022/2013/14wa Kuweka lami barabara ya Nyamuswa - Bunda - Kisorya - Nansio (121.9 km) | 51,281,285,533 | 5.11.2013 | 11.11. 2015 | 1,138,713,393 |
| 8 | Mkataba Namba TRD/HQ/1040/2008/2009 wa Kuweka lami barabara ya azi - Kizi - Kibaoni(76.6 Km) | 82,841,779,607 | 15.12.2012 | 14.12.2014 | 139,841,385 |
| 9 | Kuweka lami barabara yaTabora - Sikonge (Uselula) (30Km) | 28,645,048,253 | 15.8.2014 | 14.4.2016 | 1,673,901,938 |
| 10 | Mkataba Namba TRD/HQ/1029/2012/13wa Kuweka lami barabara ya Usagara - Kisesa (16 Km) | 20,828,392,743 | 2.5.2013 | 30.12.2015 | - |
| 11 | Magole - Turiani - Mziha - Handeni Sehemu 1 Magole-Turiani | 41,890,858,201 | 3.3.2010 | 10.2.2012 | 1,517,129,845 |
| | **Jumla** | **505,445,025,261** | | | **5,616,652,051** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti kwa Mwaka unaoishia Juni 30, 2015*

Napendekeza Wakala wa Barabara (TANROADS) ifuatilie fedha Wizara ya Fedha ili kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati; pia napendekeza mikataba itolewe kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha; hii itasababisha Serikali kuepukana na gharama zisizo za lazima (riba) zinazotokana na ucheleweshwaji wa malipo ya wakandarasi.

### 8.1.2.10 Mikopo kiasi cha Shilingi 180,637,375 haikurejeshwa

Ukaguzi wa mwaka wa fedha 2014/2015 ulibaini Wizara tatu zilishindwa kurejesha mikopo kiasi cha jumla ya Shilingi 180,637,375 iliyopewa na Wakala zilizo chini yao. Wizara Hizo ni

Wizara ya Kilimo na Chakula kiasi cha Shilingi 103,377,375.18(57%) kutoka Wakala wa Akiba ya Chakula Taifa (NFRA) Wizara ya Maji kiasi cha Shilingi 55,760,000 (31%) kutoka Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa (DDCA) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kiasi cha Shilingi 21,500,000(12%) kutoka Wakala wa Maendeleo ya Elimu na Usimamizi (ADEM).

Wizara Kushindwa kurejesha mikopo iliyotolewa na Wakala inazozisimamia huchangia kuathiri utendaji wa Wakala husika.

Napendekeza Wakala husika zifuatilie na kuhakikisha mikopo yote iliyotolewa kwa Wizara husika inarejeshwa bila kuchelewa.

### 8.1.3 Mapungufu katika usimamizi wa Mali

#### 8.1.3.1 Magari yaliyotelekezwa na taasisi za serikali

Nimebaini kwamba katika mwaka wa fedha 2014/2015 karakana ya TEMESA Mwanza ilikuwa na magari 44 yaliyotelekezwa na taasisi mbalimbali za Serikali kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu hadi mitano. Taasisi za serikali na magari yaliyotelekezwa zimeainishwa kwenye jedwali Na. 55 hapo chini:

## Jedwali 55: Magari yaliyotelekezwa

| S/N | Namba ya Gari | Muundo wa Gari | Taasisi za Serikali | Karakana | Tarehe |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | STK 4333 | Suzuki Vitara | Ofisi ya Bunge | MT DEPOT | 18-05-10 |
| 2 | DFP 1090 | Toyota L/C | Wizara ya Fedha | MT DEPOT | 18-04-10 |
| 3 | STJ 3956 | Toyota L/C | Wizara ya Kazi na Ajira | MT DEPOT | 21-05-12 |
| 4 | STK 2624 | Toyota L/C | Wizara ya Afrika Mashariki | MT DEPOT | 20-01-14 |
| 5 | STK 411 | Nissan Patrol | Wizara ya Fedha | MT DEPOT | 24-10-12 |
| 6 | STJ 3012 | Prado | Wizara ya Ujenzi | MT DEPOT | 20-05-13 |
| 7 | STK 1972 | Nissan Patrol | Wizara ya Kazi na Ajira | MT DEPOT | 31-01-12 |
| 8 | STJ 2409 | Hyundai | TEMESA | MT DEPOT | 24-06-10 |
| 9 | STK 5142 | Toyota L/C V-8 | Halmashauri ya Mpanda | MT DEPOT | 03-10-13 |
| 10 | STJ 7336 | Nissan Patrol | Wizara ya Fedha | MT DEPOT | 25-03-13 |
| 11 | STK 702 | L/Rover 110 | Wizara ya Fedha | MT DEPOT | |
| 12 | DFP 3059 | Discover | Wizara ya Fedha | MT DEPOT | |
| 13 | STH 2785 | Tata Lory | TEMESA | MT DEPOT | |
| 14 | STJ 1810 | M/Benz | Ofisi ya Bunge | MT DEPOT | |
| 15 | STJ 2727 | Toyota L/C | TEMESA Makao Makuu | MT DEPOT | 06-02-11 |
| 16 | STJ 2411 | Hyundai | TEMESA | MT DEPOT | 24-06-10 |
| 17 | STJ 9888 | Nissan H/Body | Wakala wa Hali ya Hewa Tanzania | MT DEPOT | |
| 18 | STK 8275 | Toyota L/C V-8 | Wakala wa Barabara Tanzania | MT DEPOT | |
| 19 | STK 5478 | Toyota L/C V-8 | Halmashauri ya Nanyumbu | MT DEPOT | |
| 20 | DFP 7399 | Toyota Rav 4 | Cma | MT DEPOT | |
| 21 | STL 2632 | Toyota L/C | Ofisi ya Msajili wa Hazina | MT DEPOT | |
| 22 | STH 5812 | Isuzu Tipper | Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi | MT DEPOT | |
| 23 | STH 7388 | Tata Bus | TEMESA Makao Makuu | MT DEPOT | |
| 24 | STJ 8384 | Isuzu D/Cabin | TEMESA | MT DEPOT | |
| 25 | STJ 9333 | Toyota Rav 4 | Ofisi ya Msajili wa Hazina | MT DEPOT | |
| 26 | STJ 1673 | Toyota L/C | Wizara ya Fedha | MT DEPOT | |
| 27 | STJ 7800 | M/Benz | Gta-Temesa | MT DEPOT | |
| 28 | ST 137 A | Toyota L/C | Ofisi ya Rais Ikulu | MT DEPOT | Nov-13 |
| 29 | STJ 853 | Kia | Ofisi ya Rais Ikulu | MT DEPOT | Nov-13 |
| 30 | ST 68 A | Isuzu Bus | Ofisi ya Rais Ikulu | MT DEPOT | Nov-13 |
| 31 | | Tractor | Ofisi ya Rais Ikulu | MT DEPOT | Nov-13 |
| 32 | STJ 3107 | Toyota L/C | BRELA | MT DEPOT | 11-02-13 |
| 33 | STJ 9751 | Prado | BRELA | MT DEPOT | 26-06-14 |
| 34 | STJ 9602 | Toyota Hilux | BRELA | MT DEPOT | 25-06-14 |
| 35 | DFP 209 | Toyota L/Cruiser Hard Top | TAFIRI -Mwanza | MWANZA | 29-11-12 |
| 36 | DFP 2240 | Nissan Ternal | Kituo cha Kuleana Mwanza | MWANZA | 04-12-12 |
| 37 | DFP 2289 | Suzuk Escudo | Kituo cha Kuleana Mwanza | MWANZA | 04-12-12 |
| 38 | DFP 194 | Toyota Hilux | Uvuvi-Mwanza | MWANZA | 30-11-12 |
| 39 | DFP 187 | Toyota Prado | TAFIRI -Mwanza | MWANZA | 29-11-12 |
| 40 | STJ 447 | Mitsubishi Canter | TEMESA-Mwanza | MWANZA | |
| 41 | STG 9474 | Tata LWB Lorry | TEMESA-Mwanza | MWANZA | |
| 42 | STK 345 | Ford Ranger/Cabin | TEMESA-Mwanza | MWANZA | |
| 43 | STH 7898 | Mitsubishi P/UP | TEMESA-Mwanza | MWANZA | |
| 44 | STH 2789 | Layland Comet Tanker | TEMESA-Mwanza | MWANZA | |

**Chanzo:** ***Taarifa ya ukaguzi kwa Menejimenti***

Kutochukuliwa kwa hatua za haraka kuchukuliwa dhidi ya magari yaliyotelekezwa kunasababisha kuendelea kushuka thamani kwa magari hayo kufikiahadi hali ya kutouzika.

Nashauri Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi (TEMESA) kuwasiliana na taasisi zote za Serikali kuokoa magari yaliyotelekezwa kutoendelea kuharibika zaidi.

### 8.1.3.2 Magari yaliyoegeshwa bila matengenezo kwa muda mrefu

Katika ukaguzi wa Mwaka 2014/2015 nilibaini magari 31 yaliyoegeshwa bila matengenezo katika wakala tatu; Wakala wa kuchimba visima na mabwawa (DDCA) magari 28, Wakala wa umeme, mitambo na ufundi (TEMESA) magari mawili, na Wakala wa akiba ya chakula Taifa (NFRA) gari moja; pia nilibaini vifaa chakavu vyenye gharama ya Shilingi 83,301,000 katika Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA). Mpaka kufikia Juni 30, 2015 taratibu za uuzaji wa magari na vifaa hivyo haijachukuliwa na Afisa masuuli katika Wakala husika; hii ni kinyume na kanuni ya fedha ya umma Namba 254(1) ya mwaka 2001.

Napendekeza Wakala husika iuze vifaa vyote chakavu ili kuepuka hasara zaidi. Magari yaliyoegeshwa bila matengenezo na vifaa chakavu vimeainishwa katika Kiambatisho Na. 8.1.

### 8.1.3.3 Ukosefu wa hati miliki

Katika ukaguzi wa Mwaka 2014/2015 nilibaini kwamba Shirika la Magereza linamiliki mali zenye thamani ya Shilingi 522,727,935 bila hati miliki; hii ni kutokana na uhamisho wa mali kutoka Idara ya huduma ya Magereza (Prison Service Department) kwenda Shirika la Magereza. Nimebaini kwamba wakala mbili zinamiliki jumla ya viwanja 52 (Wakala wa akiba ya chakula Taifa-NFRA viwanja 10 na Wakala wa mbegu za miti-TTSA viwanja 42) pasipo hati miliki. Kutokana na kukosekana kwa nyaraka kwa umiliki, sikuweza kuthibitisha umiliki halali wa viwanja hivyo.

Nashauri wakala husika apate hati miliki ya viwanja inavyovimiliki ili kulinda mali za Serikali.

### 8.1.3.4 Hasara kutokana na kutouza Shajara na Kalenda zenye thamani ya Shilingi 42,536,880

Katika ukaguzi wa mwaka 2014/2015 nilibaini kwamba Wakala wa ugavi na huduma za manunuzi (GPSA) ilipata hasara ya shilingi 42,536,880 kutokana na kutouza Shajara na Kalenda zenye thamani ya Shilingi 42,536,880. Hasara ilisababishwa na kuchelewa kuwasilishwa kwa Shajara na Kalenda kulikosababishwa na mabadiliko ya Sera ya Serikali, ambapo nyaraka zote za Serikali zilitakiwa kuchapishwa na Mpiga chapa wa Serikali; pia nilibaini kwamba Wizara na Taasisi nyingine za Serikali zilichapisha shajara na Kalenda zao, hivyo kusababisha kupungua kwa mahitaji ya Shajara na Kalenda zilizochapishwa na Wakala wa ugavi na huduma za manunuzi (GPSA).

Napendekeza Wakala wa ugavi na huduma za manunuzi (GPSA) kuweka utaratibu ambao utahakikisha wazabuni wanawajibishwa kutokana na hasara wanayosababisha.

### 8.1.3.5 Rejista ya mali za kudumu kutokwenda na wakati na mali zisizokuwa na alama za utambulisho

Mapitio ya mfumo wa udhibiti wa ndani umebaini kwamba rejista ya mali za kudumu za Wakala nane hazikwenda na wakati; pia nimebaini kwamba Wakala tatu zilikuwa na mali ambazo hazikuwa na alama za utambulisho. Hii ni kinyume na Kanuni ya Fedha za Umma 265(2) ya mwaka 2001.

**Jedwali 56: Wakala zenye Rejista ya mali za kudumu isiyokwenda na wakati na mali zisizo na alama za utambulisho**

| S/N | Wakala | Rejista ya mali za kudumu isiyokwenda na wakati | Mali zisizo na alama za utambulisho |
|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) | v | |
| 2 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | v | |
| 3 | Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT) | v | |
| 4 | Wakala wa Maabara za serikali (GCLA) | v | v |
| 5 | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi (TEMESA) | v | |
| 6 | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo | v | |
| 7 | Wakala wa Akiba ya Chakula Taifa (NFRA) | v | |
| 8 | Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania(TTSA) | v | |
| 9 | Taasisi ya Sanaa na utamaduni - Bagamoyo | | v |
| 10 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | | v |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Napendekeza kuwa Wakala zizingatie kanuni ya fedha za umma Na.265(2) ya mwaka 2001

kwa kuhakikisha Rejesta ya mali za Wakala inaenda na wakati ili kuweka usahihi wa takwimu za mali za kudumu zinazomilikiwa na Wakala; pia, wakala zinatakiwa kuweka alama za utambulisho katika mali zake ili kuimarisha udhibiti wa mali zinazomilikiwa na Wakala.

**8.1.3.6 Madeni yasiyokusanywa Shilingi 688,022,407,694**

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 nimebaini Wakala 28 hazikuweza kukusanya madeni kiasi cha Shilingi 688,022,407,694; hii ni ongezeko la Shilingi 442,555,951,209 (180%) ikilinganishwa na madeni ya mwaka 2013/2014 kiasi cha Shilingi 245,466,456,485. Kati ya madeni yasiyokusanywa, kiasi cha Shilingi 501,909,054,611 (73%) kilikuwa ni madeni yaliyodumu zaidi ya miezi 12 na kiasi cha Shilingi 186,113,353,083 (27%) kilikuwa ni madeni yaliyodumu kwa miezi 12; zaidi, nimebaini kwamba Wakala wa barabara (TANROADS) imebeba 56% ya madeni yasiyokusanywa ikifuatiwa na Wakala wa akiba ya chakula Taifa (NFRA) 25% na Wakala wa umeme vijjini ( REA) 7%

Orodha ya Wakala zenye Madeni yasiyokusanywa imeainishwa kwenye jedwali na. 57 hapo chini:

Jedwali 57: Madeni yasiyokusanywa

| S/N | Wakala | Kiasi Shs. |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa serikali Mtandao | 233,336,923 |
| 2 | Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi | 1,850,563,850 |
| 3 | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa | 118,841,000 |
| 4 | Chuo cha Utumishi wa Umma | 281,740,053 |
| 5 | Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania | 900,000 |
| 6 | Wakala wa Mbegu za Kilimo | 1,616,546,834 |
| 7 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa | 1,834,955,424 |
| 8 | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo | 38,546,500 |
| 9 | Wakala wa Utafiti wa Miamba | 11,831,000 |
| 10 | Chuo cha Mafunzo ya Mifugo | 216,140,004 |
| 11 | Wakala wa Akiba ya Chakula Taifa | 173,650,642,457 |
| 12 | Wakala wa Majengo Tanzania | 30,885,241,650 |
| 13 | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi | 13,441,603,867 |
| 14 | Wakala wa Ndege za Serikali | 23,229,512,368 |
| 15 | Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa | 981,573,580 |
| 16 | Wakala wa Barabara Tanzania | 382,319,084,991 |
| 17 | Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji | 46,938,596 |
| 18 | Wakala wa Vipimo | 1,021,977,317 |
| 19 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | 19,138,466 |
| 20 | Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu | 94,393,122 |
| 21 | Wakala wa Maabara za Serikali | 1,476,299,928 |
| 22 | Wakala wa Usalama na Afya Kazini | 1,641,500,474 |
| 23 | Wakala wa ukaguzi wa Uchimbaji Madini Tanzania | 1,485,111,000 |
| 24 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam | 45,647,635 |
| 25 | Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi | 3,271,833,648 |
| 26 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania | 1,000,829,195 |
| 27 | Wakala wa Umeme Vijjini | 47,097,093,000 |
| 28 | Chuo cha Taifa cha Utalii | 110,584,813 |
| | **JUMLA** | **688,022,407,694** |

**Chanzo**: *Ripoti ya CAG*

Kuwapo kwa kiasi kikubwa cha madeni yasiyokusanywa hupunguza shughuli za kiutendaji za Wakala.
Napendekeza Wakala husika kufuatilia madeni yasiyokusanywa ili kuepuka uchelewaji wa Wakala kutekeleza malengo yake

### 8.1.4 Udhaifu kwenye madeni yasiyolipwa

#### 8.1.4.1 Kesi za Madai dhidi ya Wakala TZS 3,984,442,970

Nimebaini kwamba Wakala Tano (5) zilikuwa na kesi Mahakamani ambazo zina athari za kifedha kwa Wakala kiasi cha shilingi 3,984,442,970 iwapo maamuzi hayatakuwa upande wa Wakala; pia nimebaini kwamba Wakala wa mbegu za kilimo (ASA) na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) hazikutenga fedha za kulipa madeni hayo iwapo Wakala hizo zitalazimika kulipa madeni hayo kulingana na maamuzi ya mahakama. Orodha ya Wakala zenye kesi mahakamani zinazotegemea matukio zimeainishwa kwenye jedwali Na. 58 hapo chini:

**Jedwali 58: Wakala zenye kesi za Madai**

| S/N | Wakala | Kiasi Sh |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Mbegu za Kilimo | 2,751,850 |
| 2 | Wakala wa Mbegu za Kilimo | Kesi mbili zinategemea maamuzi ya mahakama |
| 3 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam | 2,570,062,176 |
| 4 | Wakala wa Majengo Tanzania | 1,368,188,944 |
| 5 | Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi | 43,040,000 |
| | **Jumla** | **3,984,042,970** |

**Chanzo:** *Taarifa ya ukaguzi kwa Menejimenti*

Napendekeza Wakala zifuatilie kwa ukaribu Kesi zilizopo mahakamani ili kuhakikisha zinamalizika kwa wakati; pia wakala zitenge fedha kwa ajili ya ulipaji wa madeni ya kesi za madai iwapo wakala zitalazimika kulipa madeni hayo kulingana na maamuzi ya mahakama.

#### 8.1.4.2 Ongezeko la riba katika 15% mkopo Shilingi 12,723,218,833

RITA ilisaini mkataba na Bodi ya Wadhamini wa NSSF ya mkopo wa kiasi cha Shilingi

24,153,638,530 April 19, 2011 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Wakala wa vizazi, vifo na ufilisi (RITA). Kufikia Juni 30, 2015 RITA ilikuwa na jumla ya riba kiasi cha shilingi 12,723,218,833 sawa na asilimia 52.68 ya mkopo.

Kiasi hicho kikubwa cha riba kingeweza kuepukika iwapo RITA ingelipa deni kwa wakati.

Napendekeza RITA ilipe mkopo bila kuchelewa zaidi ili kupunguza mzigo kwa Serikali kutokana na riba inayozidi kuongezeka.

#### 8.1.4.3 Madeni yasiyolipwa Shilingi 1,585,462,664,305

Katika mwaka 2014/2015 Wakala 26 zilibainika kuwa na madeni kiasi cha Shilingi 1,585,462,664,305; ongezeko la kiasi cha Shilingi 666,328,896,602 (72%) ikilinganishwa na na madeni ya mwaka 2013/2014 ya kiasi cha Shilingi 919,133,767,703. Kati ya madeni yasiyolipwa, kiasi cha Shilingi 1,312,571,520,270 (83%) yalikuwa ni madeni ya zaidi ya mwaka mmoja, na kiasi cha shilingi 272,891,144,035 (17%) ni madeni yaliyodumu kwa miezi 12. Zaidi ya hayo, nimebaini kwamba Wakala wa barabara (TANROAD) ilikuwa na kiasi kikubwa cha madeni cha 73% ya madeni yote. Kiasi kikubwa cha madeni kinapunguza uwezo wa Wakala kutekeleza majukumu yake; pia uaminifu wa Wakala wa Serikali kwa watoa huduma unapungua.

Orodha ya Wakala zenye madeni yasiyolipwa imeoneshwa kwenye jedwali namba 59 hapo chini

**Jedwali 59: Wakala zenye Madeni yasiyolipwa**

| S/N | Wakala | Kiasi Shs |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi | 1,407,935,742 |
| 2 | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania | 335,926,280 |
| 3 | Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa | 334,768,000 |
| 4 | Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania | 87,511,184 |
| 5 | Wakala wa Mbegu za Kilimo | 1,144,528,716 |
| 6 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa | 182,798,475 |
| 7 | Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo | 89,962,937 |
| 8 | Wakala wa Utafiti wa Miamba | 328,679,577 |
| 9 | Chuo cha Mafunzo ya Mifugo | 195,562,296 |
| 10 | Wakala wa Akiba ya Chakula Taifa | 3,275,740,163 |
| 11 | Wakala wa Majengo Tanzania | 3,551,905,010 |
| 12 | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi | 11,695,999,695 |
| 13 | Wakala wa Ndege za Serikali | 2,939,302,106 |
| 14 | Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa | 1,928,679,827 |
| 15 | Wakala wa Barabara Tanzania | 1,159,229,494,045 |
| 16 | Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji | 1,044,323,274 |
| 17 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | 8,180,000 |
| 18 | Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu | 2,108,736,121 |
| 19 | Wakala wa Usalama na Afya Kazini | 31,106,662 |
| 20 | Wakala wa Huduma za Ajira | 220,534,959 |
| 21 | Wakala wa ukaguzi wa Uchimbaji Madini Tanzania | 341,708,000 |
| 22 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam | 123,866,399 |
| 23 | Wakala wa Ugavi na Huduma za Manunuzi | 2,371,696,011 |
| 24 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania | 1,491,583,493 |
| 25 | Wakala wa Umeme Vijjini | 390,826,808,000 |
| 26 | Chuo cha Taifa cha Utalii | 165,327,333 |
| | **JUMLA** | **1,585,462,664,305** |

**Chanzo:** *Ripoti ya CAG*

Ninashauri maafisa masuuli wa Wakala za Serikali watenge fedha kwa ajili ya ulipaji wa madeni; pia bajeti za Wakala ziongezwe ili kukidhi mahitaji ya Wakala.

### 8.1.5 Udhaifu ulioonekana katika matumizi

#### 8.1.5.1 Malipo yasiyoambatana na risiti za Kielektroniki(EFD) shilingi 976,282,947

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 nimebaini Wakala Tano (5) wamelipa kiasi cha Shilingi 976,282,947 kwa Wazabuni bila kudai risiti za Kielektroniki (EFD); hii ni kinyume na kanuni 24 ya EFD ya mwaka 2012. Kutokutumia risiti za kielektroniki kunaashiria ukwepaji wa kodi, hivyo kusababishia Serikali upotevu wa mapato.
Orodha ya Wakala zilizofanya malipo bila kudai

risiti za Kielekroniki zimeainishwa kwenye jedwali Na. 60 hapo chini:

**Jedwali 60: Malipo yasiyoambatana na risiti za Kielektroniki**

| S/N | Wakala | Kiasi kwa Sh. |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam (DART) | 14,144,420 |
| 2 | Wakala wa kuchimba Visima na Mabwawa (DDCA) | 170,938,360 |
| 3 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo (NHBRA) | 196,980,403 |
| 4 | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) | 265,389,402 |
| 5 | Wakala wa Umeme, Mitambo na Ufundi (TEMESA) | 328,830,362 |
| | **Jumla** | **976,282,947** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Ninashauri Wakala za Serikali zidai risiti za kielektroniki wakati wa kufanya malipo; pia Wakala za Serikali zinashauriwa kufanya manunuzi kwa wafanyabiashara wanaotoa risiti za kielektroniki.

### 8.1.5.2 Malipo bila kukata kodi ya zuio Shilingi 21,210,107

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, nimebaini Wakala Tano (5) zimelipa bila kukata kodi ya zuio kiasi cha Shilingi 21,210,107; hii ni kinyume na kifungu cha 83 cha Kodi ya Mapato ya mwaka 2006 ambayo inazitaka taasisi za Serikali kukata kodi ya zuio kiasi cha 2% ya gharama za bidhaa zilizonunuliwa. Kushindwa kukata kodi ya zuio kunaashiria upotevu wa mapato ya Serikali.

Orodha ya Wakala ambazo hazikukata kodi ya zuio imeainishwa kwenye jedwali Na. 61 hapo chini:

**Jedwali 61: Wakala zisizotoza kodi ya zuio**

| S/N | Wakala | Kiasi Shs |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Usafiri wa Mwendo Kasi Dar es Salaam | 7,404,717 |
| 2 | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni - Bagamoyo | 5,100,000 |
| 3 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa | 1,133,412 |
| 4 | Wakala wa Majengo Tanzania | 1,580,978 |
| 5 | Wakala wa Vizazi, Vifo na Ufilisi | 5,991,000 |
| | **Jumla** | **21,210,107** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Napendekeza kwamba Maafisa Masuuli wa Wakala husika wazingatie Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2006.

### 8.1.5.3 Masurufu Yasiyorejeshwa Shilingi 402,706,732

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, nimebaini Wakala sita (6) zenye masurufu yasiyorejeshwa kiasi cha shilingi 402,706,732. Hata hivyo, hadi Juni 30, 2015 masurufu yao yalikuwa hayajarejeshwa kinyume na Kanuni Na. 103 (1) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) ambayo inahitaji masurufu kurejeshwa ndani ya siku 14 baada ya kukamilika kwa shughuli husika. Orodha ya Mashirika pamoja na masurufu yasiyorejeshwa yameainishwa katika jedwali Na. 62

**Jedwali 62: Wakala zenye Masurufu Yasiyorejeshwa**

| S/N | Wakala | Kiasi Shs |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Maabara za Mifugo | 5,415,000 |
| 2 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa | 115,433,629 |
| 3 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | 256,745,503 |
| 4 | Wakala wa Majengo Tanzania | 10,000,000 |
| 5 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania | 8,972,600 |
| 6 | Bonde la Ruvuma na Ukanda wa Kusini | 6,140,000 |
| | **Jumla** | **402,706,732** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Napendekeza Wakala za Serikali zizingatie Kanuni za Fedha za Umma kwa kuhakikisha masurufu yanarejeshwa baada ya kazi husika kukamilika.

#### 8.1.5.4 Malipo yasiyokuwa na viambatisho shilingi 556,845,254

Nimebaini kwamba katika mwaka 2014/2015 wakala sita (19%) kati ya 32 zilikuwa na malipo ya kiasi cha shilingi 556,845,254 ambayo hayakuwa na viambatisho ambapo ni kinyume na Kanuni 95 (4) ya fedha za umma ya mwaka 2001 ambayo inataka malipo yote kuwa na viambatisho.

Orodha ya Wakala zenye malipo yasiyo na viambatisho yameainishwa kwenye jedwali na. 63 hapo chini:

**Jedwali 63: Wakala zenye malipo yasiyo na viambatisho**

| S/N | Wakala | Kiasi Shs |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania | 44,781,809 |
| 2 | Chuo cha Utumishi wa Umma | 138,988,913 |
| 3 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | 275,166,457 |
| 4 | Wakala wa Majengo Tanzania | 78,123,075 |
| 5 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania | 8,545,000 |
| 6 | Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji | 11,240,000 |
| | **Jumla** | **556,845,254** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Napendekeza Afisa Masuuli kwa wazingatie mahitaji ya Kanuni ya 95 (4) kuhakikisha malipo yote yanakuwa na viambatisho vya kutosha.

### 8.1.5.5 Mikopo kwa Watumishi isiyorejeshwa shilingi 78,690,084

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 nilibaini Wakala Tatu (3) zilitoa mikopo kwa watumishi wake kiasi cha Shilingi 78,690,084; zaidi, nimebaini kuwa hakukuwa na jitihada zozote zilizofanywa na Wakala husika kuhakikisha fedha hizo zinarejeshwa. Hali ya Wakala kushindwa kurejesha mikopo hiyo kutoka kwa Watumishi huchangia kurudisha nyuma shughuli za Wakala.

Orodha ya Wakala zenye mikopo kwa Watumishi isiyorejeshwa zimeainishwa kwenye kwenye jedwani Na. 64 hapo chini;

**Jedwali 64: Wakala zenye Mikopo kwa Watumishi ambayo haijarejeshwa**

| S/N | Wakala | Kiasi Shs |
|---|---|---|
| 1 | Chuo cha Mafunzo ya Mifugo | 8,482,982 |
| 2 | Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | 7,842,272 |
| 3 | Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji | 62,364,830 |
| | **Jumla** | **78,690,084** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Ninashauri Maafisa Masuuli wahakikishe fedha hizo zinarejeshwa na Watumishi kutoka kwenye mishahara yao.

### 8.1.5.6 Makato ya watumishi hayakuwasilishwa Mamlaka husika

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 nimebaini kwamba makato ya watumishi ya kisheria kiasi cha shilingi 35,642,900 hayakuwasilishwa mamlaka husika. Wakala ambazo hazikupeleka

makato ya watumishi katika mamlaka husika ni Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa (DDCA) kiasi cha Shilingi 27,023,876 na Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA) kiasi cha Shilingi 8,619,024. Kushindwa kurejesha makato ya lazima kwa Mamlaka husika kunasababisha Watumishi kutokupata pensheni na kiinua mgongo wakati wa kustaafu

Wakala zenye makato yasiyowasilishwa mamlaka husika yameainishwa kwenye jedwali Na. 65 hapo chini:

**Jedwali 65: Wakala zenye makato yasiyowasilishwa mamlaka husika**

| SS/N | Wakala | Kiasi Shs |
|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Kuchimba Visima na Mabwawa (DDCA) | 27,023,876 |
| 2 | Wakala wa Huduma za Ajira (TaESA) | 8,619,024 |
| | **Jumla** | **35,642,900** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Nashauri Afisa Masuuli wa Wakala za Serikali waanzishe utaratibu wa kuhakikisha kwamba makato yote ya kisheria yanarejeshwa kwa mamlaka husika.

### 8.1.6 Udhaifu ulioonekana katika Usimamizi wa Mapato

#### 8.1.6.1 Mapato yasiyokusanywa kwenye Mauzo ya nyumba za Serikali shilingi 214,748,556

Wakala wa majengo Tanzania (TBA) haikukusanya ipasavyo mapato yaliyotokana na uuzaji wa nyumba kwa watumishi wa Serikali. Malipo ya nyumba hizo yalitakiwa kumalizika Januari, 2015 (miaka kumi toka kuuziwa nyumba); mpaka Juni, 2015 wadaiwa 199 walikuwa wakidaiwa kiasi cha shilingi 214,748,556; zaidi, nilibani kwamba Afisa Masuuli wa Wakala wa Majengo Tanzania

alishindwa kuwakumbusha wadaiwa kulipa madeni yao.

Mapato yasiyokusanywa kwenye mauzo ya nyumba za Serikali yameainishwa kwenye jedwali Na. 66 hapo chini:

**Jedwali 66: Mapato yasiyokusanywa kwenye Mauzo ya nyumba**

| S/N | Mkoa | Idadi ya Wadaiwa | Kiasi Shs |
|---|---|---|---|
| 1 | Morogoro | 89 | 99,031,850 |
| 2 | Dodoma | 59 | 55,605,762 |
| 3 | Mbeya | 51 | 60,110,944 |
| | **Jumla** | **199** | **214,748,556** |

**Chanzo:** *Taarifa ya ukaguzi kwa Menejimenti*

Napendekeza Wakala wa majengo Tanzania zichukue hatua za kisheria dhidi ya wadaiwa wote.

### 8.1.6.2 Mapato ambayo hayakupelekwa benki kwa usahihi

Wakala tatu (3) kati ya thelathini na mbili zilizokaguliwa zilikuwa na mapungufu katika ukusanyaji wa mapato. Nimebaini mapato yaliyokusanywa kiasi cha Shilingi 51,465,623 hayakupelekwa benki; na mapato kiasi cha Shilingi 14,162,800 hayakupelekwa katika akaunti sahihi ya benki. Hii ni kinyume na Kanuni na.78(1) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 ambayo inataka mapato yote yaliyokusanywa yapelekwa Benki bila kuchelewa.
Taasisi ambazo mapato yake hayakupelekwa benki kwa usahihi zimeoneshwa kwenye jedwali Na. 67 hapo chini:

**Jedwali 67: Mapato yasiyopelekwa benki kwa usahihi**

| Mkoa | Wakala | Kiasi Shs. | Maelezo |
|---|---|---|---|
| Morogoro | TBA | 6,335,000 | Haikupelekwa Benki |
| Dodoma | TBA | 5,460,000 | Haikupelekwa Benki |
| Arusha | TBA | 9,513,800 | Akaunti si sahihi |
| Mwanza | TBA | 4, 649,000 | Akaunti si sahihi |
| Morogoro | TTSA | 39,670,623 | Haikupelekwa Benki |
| | RITA | 103,882,962 | |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Napendekeza Wakala wa Serikali zihakikishe mapato yote yanapelekwa benki kuhifadhiwa mara tu baada ya kukusanywa.

## 8.1.7 Usimamizi wa rasilimali watu

### 8.1.7.1 Uhaba wa watumishi

Nimebaini Wakala Nane (8) zilikuwa na uhaba wa wa jumla ya watumishi 2554 katika idara mbalimbali, sawa na 52% ya watumishi wanaohitajika. Wakala yenye kiasi kikubwa cha uhaba wa Watumishi ni Wakala wa huduma za misitu Tanzania (80%) ikifuatiwa na Wakala wa vizazi, vifo na ufilisi (6%) na Wakala wa maabara za mifugo (5%). Uhaba wa watumishi unaathiri ufanisi wa Wakala katika utendaji kazi. Zaidi, nimebaini Wakala tatu zilikuwa na wakuu wa vitengo wanaokaimu kwa muda mrefu kinyume na Kifungu D.42(3) cha Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma ya mwaka 2009.

Taasisi zenye uhaba wa watumishi na watumishi wanaokaimu muda mrefu zimeoneshwa kwenye jedwali Na. 68 hapo chini:

**Jedwali 68: Uhaba wa watumishi na wanaokaimu**

| S/N | Wakala | Wanaokaimu | Idadi ya Watumishi Wanaohitajika | Watumishi Waliopo | Mapungufu |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wakala wa Usimamizi na Maendeleo ya Elimu (ADEM) | | 4 | 1 | 3 |
| 2 | Wakala wa maabara za mifugo (TVLA) | | 318 | 200 | 118 |
| 3 | Wakala wa huduma za misitu Tanzania (TFSA) | | 3891 | 1840 | 2051 |
| 4 | Wakala wa usalama na Afya Kazini (OSHA) | 1 | 30 | 7 | 23 |
| 5 | Wakala wa akiba ya chakula Taifa (NFRA) | | 239 | 128 | 111 |
| 6 | Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) | | 128 | 33 | 95 |
| 7 | Wakala wa vizazi, vifo na ufilisi (RITA) | 1 | 308 | 155 | 153 |
| 8 | Wakala wa huduma za ajira (TAESA) | 5 | | | |
| | **JUMLA** | **7** | **4918** | **2364** | **2554** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Napendekeza Wakala za Serikali kuwasiliana na Sekretarieti ya Utumishi wa Umma kuhakikisha kwamba watumishi wenye sifa wanaajiriwa kujaza nafasi. Pia, Wakala zinatakiwa kuwathibitisha watumishi wanaokaimu kwa zaidi ya miezi sita au kuajiri watumishi wengine iwapo watabaini watumishi wanaokaimu hawakidhi vigezo.

## 8.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Taasisi nyingine za Serikali

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi kwa taasisi nyingine 31 za Serikali zilizokaguliwa mwaka 2014/2015:

### 8.2.1 Kuchelewa kwa ujenzi wa jengo la kudumu la Taasisi ya Uongozi

Wakati wa ukaguzi nilibaini kuwa Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) ilipewa ekari 490 na Serikali kwa ajili ya kujenga jengo la ofisi la kudumu katika kijiji cha Kondo, Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo, tangu mwaka 2011; lakini hadi Desemba 2015 ujenzi ulikuwa bado haujaanza kutokana na kuchelewa kutoa fidia kiasi cha shilingi 589,388,000 kwa wanakijiji 68 ambao mali zao zitaathiriwa na ujenzi wa Kilomita 5 za barabara ya lami kuelekea ulipo mradi huo.

Nashauri menejimenti ya Taasisi ya Uongozi wa Maendeleo Endelevu ifuatilie kwa fedha za kuwalipa watakaoathirika na mradi huo ili mradi uweze kuanza.

### 8.2.2 Samani zilizonunuliwa ambazo hazitumiki Shilingi 94,344,119

Kutokana na makisio ya juu zaidi ya mahitaji wakati wa maandalizi ya Bunge la Katiba; samani zilizonunuliwa zilikuwa zaidi ya mahitaji, hivyo kusababisha samani zenye thamani ya Shilingi 94,344,119 kukosa matumizi na kuhifadhiwa ghalani.

Nashauri mamlaka zihakikishe kuwa ugavi na mahitaji ya vifaa unafanyika kwa umakini kuanzia wakati wa maandalizi ya mpango wa manunuzi wa mwaka ili kuepuka upotevu wa fedha na manunuzi ya vifaa visivyohitajika. Nashauri Bunge litafute matumizi mbadala wa samani hizi.

Shule Kuu ya Sheria ya Tanzania iliingia mkataba wa shilingi 213,561,400 ikijumisha Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT) na Invention Technology Company Limited kwa ajili ya manunuzi ya vifaa na ufungaji wa

kiungo cha kuwezesha kufanya mikutano kwa kutumia nyenzo ya runinga Hata hivyo, vifaa vilivyofungwa havijaanza kufanya kazi, kwani hakukuwa na makubaliano kati ya Shule Kuu ya Sheria na Mahakama ili kuwawezesha wanachuo kuweza kufuatilia mienendo ya kesi kama ilivyokusudiwa.

Ninashauri Shule Kuu ya Sheria ifuatilie mkataba huo ili kuhakikisha kuwa malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa ili kufikia thamani ya fedha.

Kitendo cha kushindwa kuweka kiungo husika na kuwezesha matumizi ya vifaa vilivyonunuliwa kunaashiria kutofikiwa kwa thamani ya fedha kama ilivyokusudiwa.

### 8.2.3 Makato kisheria ambayo hayajapelekwa Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA) Shilingi 89,286,386

Mpango wa Kujitathimini kwa Nchi za Africa (APRM) ulishindwa kuwasilisha kiasi cha shilingi 89,286,386 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Fedha hizo, kiasi cha shilingi 61,734,761, zilikuwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2013/2014 na Shilingi 27,551,625 kwa mwaka 2014/2015.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mpango wa Kujitathimini kwa Nchi za Afrika ulipokea shilingi 681,221,236 kama ruzuku ya Serikali. Mpango wa Kujitathimini kwa Nchi za Africa (APRM) ulianzishwa Tanzania tarehe 26 Mei 2004 baada ya kusaini makubaliano na Serikali na kuridhiwa bunge tarehe 1 Februari 2005. Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi Desemba 2015 Sekretarieti ilikuwa inafanya kazi bila kutangazwa katika gazeti la Serikali hivyo kukosa hadhi ya kisheria.

Nashauri Afisa Masuuli wa APRM kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kwamba makato ya kisheria (PAYE) yanawasilishwa Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa wakati ili kuepuka adhabu kwa malipo ya kuchelewesha malipo.

### 8.2.4 Kutotumika kwa Mfumo wa Utunzaji Taarifa (MIS)

Nilibaini kuwa NYUMBU (TATC) ilisaini mkataba na MS DATA HOUSE tarehe Juni 22, 2011 ukiwa na jumla ya shilingi 187,729,645 na malipo yafanyike kwa muda wa miezi tisa. Mkataba ulikuwa ni kwa ajili ya kuwezesha moduli ndogo tisa zilizomo katika Mfumo wa Kutunza Taarifa (MIS) ziweze kufanya kazi. Hadi Juni 2015 ni moduli moja tu (Integrated Financial Management) kati ya moduli tisa ndio uliokuwa unatumika, hasa kwa matumizi ya kutengeneza Hati za malipo na kuandikia stakabadhi, huku moduli nyingine nane zikiwa hazitumiki. Mfumo huo umechakaa (depreciated) kwa kiasi cha Shilingi 62,513,972 bila kufikia faida za kiuchumi zilizokusudiwa na Kituo. Hata hivyo, TATC bado haitumii mfumo wa kompyuta katika uandaaji wa taarifa za fedha licha ya kuwepo kwa mfumo tangu mwaka 2011.

Nashauri TATC itumie Mfumo wa utunzaji taarifa kama ilivyokusudiwa katika Mkataba ili kufaidika ikiwa ni pamoja na kutambua thamani ya fedha ya fedha zilizotumika kutekeleza mradi huo.

### 8.2.5 Mabadiliko ya bei ya Mkataba bila idhini

Kanuni Na.61 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inataka mabadiliko ya mkataba yakizidi asilimia 15 ya Mkataba wa awali yaidhinishwe na Afisa Masuuli. Nilibaini kuwa shilingi 279,504,931 (15.53% ya bei ya awali) zililipwa na Bodi ya Maji Bonde la Ziwa

Victoria kwa M/s Prince General Investment Ltd kama ongezeko la bei ya mkataba bila idhini ya mamlaka inayoidhinisha bajeti.

Matumizi ya fedha bila idhini ya mamlaka inayoidhinisha bajeti huonyesha matumizi mabaya ya fedha.

Napendekeza usimamizi wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria kwa kuzingatia mahitaji ya kanuni Na. 61 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013.

**8.2.6 Utendaji Hafifu katika Kituo cha Kuunda Mitambo na Magari Tanzania (TATC)**

Nilibainisha upungufu mkubwa wa ruzuku za Serikali toka 2012/2013 hadi mwaka 2014/2015 kwa ajili ya Nyumbu. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, shs 3,337,468,000 zilipokelewa na Kituo cha Nyumbu (TATC) kama Ruzuku ya Serikali; upungufu wa shilingi 1,082,336,000 na shilingi 1,050,987,000 ikilinganishwa na ruzuku za mwaka 2013/2014 na 2012/2013 za kiasi cha shilingi 4,419,804,000 na shilingi 4,388,455,000 mtawalia. Katika kipindi cha miaka mitatu mfululizo TATC iliipokea kiasi cha shilingi 1,030,000,000 fedha za maendeleo katika mwaka wa fedha 2013/14.

Nilibaini pia kuwa, hakuna juhudi zozote zilizochukuliwa na Serikali ili kuhamasisha bidhaa za ndani zinazozalishwa na TATC, hasa zana za kilimo (matrekta madogo, mashine za matofali, na pampu za maji za uwezo wa kati) ambazo zingeweza kununuliwa na taasisi za Serikali na watumiaji wengine wa ndani, hivyo kuokoa fedha za Serikali ambazo zingetumika kuagiza zana hizo kutoka nje ya nchi.

Pia, kulikuwa na msukumo mdogo kwa upande

wa Serikali katika kuongeza tafiti katika kutengeneza Magari ya Jeshi ambapo TATC iliweza kutengeneza Gari la Upelelezi la kivita Nyumbu (ARV) na magari ya kubeba askari wa kivita (APC); ambapo, tafiti zingeweza kuendelea na kuboreshwa, wangeweza kutengeneza vitu vingi ambavyo vingeweza kuipunguzia Serikali gharama za kuagiza toka nje ya nchi.

Nashauri Serikali kuiwezesha TATC kwa kuipatia fedha za kutosha ili kuwezesha kituo hicho kutekeleza majukumu yake ya msingi kama ilivyoainishwa katika Kanuni na. 1 ya Machi, 6 1986.

### 8.2.7 Mikopo ambayo haijalipwa kiasi cha Shilingi 80,900,000

Shirika Binafsi la Uzalishaji mali la Magereza lilitoa kiasi cha mkopo wa shilingi 80,900,000 kwa ajili ya matengenezo ya samani za wabunge, fedha ambazo zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mikoani. Hata hivyo, hadi Juni 30, 2015 fedha hizo zilikuwa bado hazijalipwa na ofisi za Bunge. Kutorejesha fedha hizo kumezuia kufanyika kwa shughuli zilizokusudiwa mikoani.

Ninapendekeza Shirika Binafsi la Uzalishaji mali la Magereza, makao makuu lirudishe kiasi cha shilingi 80,900,000 katika akaunti husika ziweze kutumika kama zilivyokusudiwa.

### 8.2.8 Manunuzi yasiyozingatia taratibu kiasi cha shilingi 60,536,600

Nilibaini kuwa Chuo cha Serikali za Mitaa kilinunua bidhaa na huduma kutoka KAREN GENERAL SUPPLY na NEHOS GENERAL SUPPLIES kiasi cha shilingi 24,747,000 na shilingi 35,789,600 mtawalia. Bidhaa na huduma hizo

zilikuwa ni kwa ajili ya mkutano wa siku tatu wa viongozi wa Mkoa na Wilaya uliofanyika mjini Dodoma kuanzia tarehe 01/03/2014 hadi 03/10/2014. Hata hivyo, sikuweza kuona ushahidi juu ya manunuzi yaliyofanyika na kama huduma husika zilitolewa kwa washiriki wa mkutano.

Hati za malipo zilizowasilishwa zinatofautiana kati ya tarehe ya mapokezi ya bidhaa na huduma; ambapo tarehe katika hati ya mapokezi ya bidhaa inaonesha bidhaa zilipokelewa siku tano baada ya kufungwa kwa mkutano. Aidha, idadi ya bidhaa zilizoletwa zilikuwa zinakinzana; hivyo basi, hatukuweza kuthibitisha uhalali wa matumizi haya.

Napendekeza Maafisa Masuuli wa Taasisi waimarishe udhibiti juu ya matumizi yote katika ya Taasisi wanazoziongoza.

**8.2.9 Mali zilizohifadhiwa kwa zaidi ya miezi 35 bila kutumika wala kuwekwa wazi katika taarifa za fedha Shilingi 5,130,665,997**

Usimamizi mzuri wa mali ni pamoja na kuhakikisha kuwa mtaji wa kuendeshea shughuli za mara kwa mara haukai bila kuzalisha bidhaa za kuuza kwa muda mrefu ili kupata mapato yaliyokusudiwa.

Wakati wa ukaguzi wa nyaraka pamoja na mikataba, niliona kuwa Shirika la Mzinga lilinunua shehena ya vifaa kutoka China North Industries Corporation (NORINCO) yenye thamani ya dola za Marekani 3,154,962 mwaka 2012 sawa na shilingi 5,130,665,997 kama ilivyokuwa tarehe 30/06/2015.

Bidhaa hizo zilipokelewa na Shirika la Mzinga tangu Februari 2013, lakini hadi Februari 2016

bidhaa hizo zilikuwa hazijakaguliwa wala kuwekwa katika kumbukumbu za stoo za Shirika na zilikuwa hazijatolewa kwa ajili ya uzalishaji ikiwa ni miezi 35 tangu zinunuliwe.

Niliona pia kuwa vifaa hivi havikuhusishwa katika zoezi la kuhakiki mali za Shirika uliofanyika Juni mwaka 2015.

Ninashauri manunuzi yafanyike kulingana na mpango wa manunuzi na pale uhitaji unapokuwepo, na uanzie kwa mtumiaji. Kukaa na shehena ya vifaa kwa zaidi ya miezi 35 bila kutumika inamaanisha kwamba bidhaa hizo zilinunuliwa bila kuwapo na mahitaji toka kwa mtumiaji.

**8.2.10 Matumizi yasiyothibitika kiasi cha Shilingi.48,480,300**

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Waziri Mkuu ilihamisha jumla ya kiasi cha shilingi 48,480,300 kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara hundi Na.247760 ya 6/2/2015 kwa ajili ya gharama za usafirishaji wa mahindi ya misaada. Hata hivyo, mapitio ya nyaraka katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara sikuweza kuona uthibitisho wa Matumizi ya fedha hizo kiasi cha shilingi 48,480,300.

Nawasihi wale waliokabidhiwa majukumu wazingatie Sheria ya Fedha za Umma na Sheria nyinginezo wakati utekelezaji majukumu yao. Nimeshawasilisha hili jambo kwa taasisi husika na nitafuatilia wakati wa ukaguzi ujao.

**8.2.11 Madeni ya yasiyolipwa Shilingi 13,006,575,507**

Katika mwaka 2014/2015 Taasisi za Serikali 20 na zilikuwa na madeni ambayo hayakulipwa hadi mwisho wa mwaka wa fedha kiasi cha

shilingi 13,006,575,507. Kuwa na kiasi kikubwa cha madeni yasiyolipwa hupunguza sifa ya Taasisi kwa wauzaji.

Orodha ya Taasisi za Serikali zenye madeni imeoneshwa katika jedwali Na. 69 hapo chini;

**Jedwali 69: Taasisi zenye madeni yasiyolipwa**

| S/N | Taasisi | Kiasi Shs |
|---|---|---|
| 1 | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania | 47,577,079 |
| 2 | Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA) | 450,760,298 |
| 3 | Shule Kuu ya Sheria Tanzania | 10,695,760 |
| 4 | Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi | 146,129,636 |
| 5 | Mpango wa kujitathimni kwa Nchi za Afrika | 34,981,950 |
| 6 | Ofisi za Bunge la Katiba | 2,186,981,048 |
| 7 | Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru | 99,461,275 |
| 8 | Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela(NM-AIST) | 1,180,243,510 |
| 9 | Bonde la Ruvuma na Ukanda wa Pwani ya Kusini | 44,344,780 |
| 10 | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 1,800,000 |
| 11 | Bonde la Mto Wami/Ruvu | 144,719,083 |
| 12 | Bonde la Mto Rufiji | 1,853,315,036 |
| 13 | Bonde la Ziwa Tanganyika | 94,450,900 |
| 14 | Kituo cha Kuunda Mitambo na Magari Tanzania | 479,893,306 |
| 15 | SUMA JKT Idara ya Kilimo na Viwanda | 1,715,851,000 |
| 16 | Internal Drainage Basin Water Board | 41,658,300 |
| 17 | Shirika la Uzalishaji Mali la SUMA JKT | 1,297,814,421 |
| 18 | SUMA JKT Idara ya Ulinzi | 146,857,000 |
| 19 | SUMA JKT Idara ya Ujenzi | 2,421,307,000 |
| 20 | Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa | 607,734,126 |
|  | **Jumla** | **13,006,575,507** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya Mwaka 2014/2015*

Napendekeza Maafisa Masuuli watenge fedha kwenye bajeti zijazo kwa ajili ya kulipa madeni.

### 8.2.12 Madai yasiyokusanywa kiasi cha Shilingi 30,655,370,268

Katika mwaka wa fedha 2014/15 niliona Taasisi za Serikali 24 zilizokuwa zinadai kiasi cha shilingi 30,655,370,268. Kuwa na fedha nyingi tunazodai hupunguza ukuaji wa uwezo wa Taasisi za Serikali na kuwalazimisha kutotekeleza kikamilifu shughuli zilizopangwa.

Orodha ya Taasisi za Serikali zenye madai imeonyeshwa katika jedwali Na. 70 hapa chini:

**Jedwali 70: Taasisi zenye madeni yasiyokusanywa**

| S/N | Taasisi | Kiasi Shs |
|---|---|---|
| 1 | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania | 49,950,427 |
| 2 | Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA) | 94,721,100 |
| 3 | Shule Kuu ya Sheria Tanzania | 176,859,238 |
| 4 | Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi | 17,582,500 |
| 5 | Mpango wa kujitathimni kwa Nchi za Afrika | 4,050,000 |
| 6 | Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa | 76,855,000 |
| 7 | Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru | 109,914,097 |
| 8 | Taasisi ya kuthibitisha ubora wa Mbegu | 743,932,757 |
| 9 | Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST) | 1,165,487,228 |
| 10 | Bonde la Ruvuma na Ukanda wa Pwani ya Kusini | 51,892,068 |
| 11 | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 6,900,265,069 |
| 12 | Shirika Binafsi la Uzalishaji Mali la Magereza | 6,592,506,042 |
| 13 | Bonde la Mto Wami/Ruvu | 749,172,750 |
| 14 | Bonde la Mto Rufiji | 3,322,137,013 |
| 15 | Bonde la Ziwa Tanganyika | 316,275,431 |
| 16 | Kituo cha Kuunda Mitambo na Magari Tanzania | 277,504,000 |
| 17 | Kituo cha Mafunzo ya Takwimu Afrika Mashariki | 328,815,573 |
| 18 | SUMA JKT Idara ya Kilimo na Viwanda | 1,043,158,000 |
| 19 | Bonde la Mto Pangani | 289,655,000 |
| 20 | Internal Drainage Basin Water Board | 54,052,688 |
| 21 | SUMA JKT Idara ya Ulinzi | 1,023,830,000 |
| 22 | Shirika la Uzalishaji Mali la SUMA JKT | 1,184,654,327 |
| 23 | SUMA JKT Idara ya Ujenzi | 3,754,239,000 |
| 24 | Shirika la  Mzinga | 2,327,860,960 |
| | **Jumla** | **30,655,370,268** |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi Kwa Menejimenti ya Mwaka 2014/2015*

Nazisihi Taasisi Serikali zifuatilie kwa umakini fedha wanazodai ili ziweze kuwasaidia kutimiza malengo mkakati yao kwa wakati.

### 8.2.13 Udhaifu katika Usimamizi wa Manunuzi

Ukaguzi wangu juu ya manunuzi ulibaini kuwa Taasisi za Serikali tatu zilizonunua bidhaa zenye thamani ya shilingi 660,939,835 bila ya kupata nukuu ya bei kutoka kwa wauzaji na idhini ya Bodi ya Zabuni. Hii ni kinyume na kifungu na. 164 (1) na 55 (2) cha kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya

mwaka 2013.

Kushindwa kupata nukuu ya bei kutoka kwa wauzaji angalau watatu inamaanisha kuwa mchakato wa ununuzi haukuwa na ushindani; hivyo bei iliyotumika inaweza isitoe thamani bora ya fedha. Nashauri uongozi wa taasisi husika ushiriki katika mchakato wa zabuni ambao una uwazi na kupitia njia sahihi na kufuata sheria za manunuzi. Jedwali Na. 71 linaonyesha Taasisi za Serikali ambazo hazikufuata taratibu za manunuzi.

**Jedwali 71: Taasisi ambazo hazikuzingatia taratibu za Manunuzi**

| SN | Taasisi | Kiasi Shs | Mapungufu Yaliyobainika |
|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza | 40,000,000 | Manunuzi ya huduma za ushauri wa kihandisi na mpango wa biashara wa shamba la Magereza la Kitengule- Kagera bila kufanya ushindani wa kizabuni |
| 2 | SUMA JKT Idara ya Kilimo na Viwanda | 36,910,000 | Manunuzi yaliyofanyika bila |
| 3 | Bonde la mto Pangani | 10,195,200 | ushindani wa nukuu za bei |
| 4 | SUMA JKT Idara ya Ujenzi | 98,069,100 | Manunuzi ya bidhaa na huduma yaliyofanywa na SUMA JKT Idara ya Ujenzi bila bila kuidhinishwa na Bodi ya Wazabuni |
| 5 | SUMA JKT Idara ya Kilimo na Viwanda | 63,836,300 | Manunuzi ya Bidhaa na huduma bila kuidhinishwa na Bodi ya wazabuni |
| 6 | SUMA JKT Idara ya Ujenzi | 240,500,277 | Manunuzi ya vifaa bila nukuu za bei |
| 7 | SUMA JKT Idara ya Ujenzi | 44,792,375 | Kukodisha magari bila ushindani wa bei |
| 8 | Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknoloj | 14,250,000 | Manunuzi ya bidhaa bila kupitia kitengo cha manunuzi |
| 9 | Shirika la Uzalishaji Mali la SUMA JKT | 17,426,440 | Manunuzi ya bidhaa bila kufuata taratibu za manunuzi |
| 10 | SUMA JKT Idara ya Ulinzi | 72,782,643 | Manunuzi ya bidhaa bila kufuata taratibu za manunuzi |
| 11 | Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa | 22,177,500 | Manunuzi ya bidhaa bila ushindani |
| | **Jumla** | **660,939,835** | |

**Chanzo:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya Juni 30, 2015*

Ninashauri Taasisi za Serikali kwa kuzingatia Kifungu cha 164 (1) cha Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ili kuhakikisha ushindani wa mchakato wa manunuzi ndani ya Taasisi unafuatwa. Pia, manunuzi yasifanyike bila idhini ya Bodi ya Zabuni kama inavyotakiwa na Kanuni ya 55 (2) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013.

### 8.2.14 Madai ya kisheria yanayosubiri maamuzi ya kesi shilingi 191,502,000

Wakati napitia madeni sanjari ya Taasisi mbalimbali za Serikali nilibaini kuwa Shirika la Umma la Uzalishaji Mali lilikuwa na kesi katika mahakama; ambapo iwapo zitafanyiwa maamuzi kuna uwezekano wa kuwapo na athari ya kifedha kiasi cha shilingi 191,502,000 iwapo maamuzi hayo yatakuwa na neema kwa upande wa Shirika.

Nashauri Shirika la Umma la Uzalishaji Mali lifanye kazi karibu na mahakama kwa ajili ya kukamilisha mapema ya kesi.

### 8.2.15 Matumizi yasiyo na viambatisho vya kutosha

Tathmini yangu ya matumizi ya taasisi nilibaini kuwa malipo yenye jumla ya shilingi 5,189,261,546 yalifanywa bila nyaraka sahihi katika mwaka 2014/15. Kwa hiyo, sikuweza kuhakiki usahihi na wa matumizi hayo. Hii inajumuisha kukosekana kwa hati za malipo, matumizi yasiyo na viambatisho vya kutosha, malipo yaliyolipwa stakabadhi za kielektroniki, kodi ya zuio isiyokatwa pamoja na masurufu yasiyorejeshwa. Muhtasari wa taasisi zenye mapungufu hayo ni kama unavyoonekana katika jedwali na. 72 hapa chini.

## Jedwali 72: Taasisi zenye Malipo yasiyo na viambatisho vya kutosha

| Sheria/Kanuni | Hoja | | Kiasi Shs |
|---|---|---|---|
| Kanuni 94(4) ya kanuni za fedha za Umma, 2001 | Hati za malipo zilizokosekana | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania | 5,944,150 |
| | | Baraza la Famasia Tanzania | 181,478,440 |
| | | Shirika la Mzinga | 1,096,314,480 |
| Kanuni 95(4) ya kanuni za fedha za Umma, 2001 | Malipo yasiyokuwa na viambatisho | Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi | 102,031,934 |
| | | Shirika la Uzalishaji Mali la SUMA JKT | 78,482,800 |
| | | Bonde la Mto Wami/Ruvu | 5,848,000 |
| | | Bonde la ziwa Rukwa | 22,726,295 |
| | | Baraza la Wakunga na Wauguzi Tanzania | 21,004,000 |
| | | Baraza la Famasia Tanzania | 500,490,405 |
| | | Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa | 410,910,499 |
| | | Shirika la Mzinga | 95,226,828 |
| **Jumla Ndogo** | | | **2,520,457,830** |
| Kanuni 24 ya Kanuni ya Mashine za kielektroniki ya 2012 | Malipo yasiyoambatana na risiti za kielekroniki(EFD Receipts) | Taasisi ya Uongozi wa Sheria Lushoto (IJA) | 216,736,043 |
| | | Bonde la Ruvuma na Ukanda wa Pwani ya Kusini | 7,216,800 |
| | | Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa | 34,035,448 |
| | | Shirika la uzalishaji mali la Magereza | 113,051,288 |
| | | Bonde la Mto Wami/Ruvu | 15,868,750 |
| | | Bonde la Mto Rufiji | 471,877,540 |
| | | Bonde la Mto Pangani | 650,079,481 |
| | | Bonde la ziwa Rukwa | 22,761,575 |
| | | Internal Drainage Basin Water Board | 21,308,000 |
| | | Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa | 498,403,700 |
| | | Shirika la Mzinga | 355,540,504 |
| **Jumla Ndogo** | | | **2,406,879,129** |
| Kifungu 83 ya sheria ya kodi ya mapato, 2006 | Malipo bila makato ya kodi ya zuio | Chuo cha Uongozi | 18,897,855 |
| | | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania | 3,552,083 |
| | | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 3,183,447 |
| | | Bonde la Ziwa Victoria | 504,547 |
| **Jumla Ndogo** | | | **26,137,931** |
| Kanuni 103(1) ya kanuni za fedha za Umma 2001(iliyorejewa 2004) | Masurufu yasiyorejeshwa | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania | 16,041,455 |
| | | Taasisi ya Mafunzo ya Wanyamapori Pasiansi | 17,067,500 |
| | | Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela(NM-AIST) | 160,806,300 |
| | | Bonde la Mto Wami/Ruvu | 17,519,400 |
| | | Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa | 24,352,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **235,786,655** |
| **Jumla Kuu** | | | **5,189,261,546** |

**Chanzo**: *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti*

Kuhusu malipo yasiyo na viambatisho vya kutosha na kukosekana kwa hati za malipo, napenda kuwakumbusha wasimamizi wa taasisi za Serikali kuzingatia mahitaji ya Kanuni ya 95 (4) ya Kanuni ya Fedha za Umma yam waka 2001 na kuanzisha mifumo madhubuti ya ndan ya usimamizi wa fedha na kuhakikisha kwamba nyaraka zote muhimu ikiwa ni pamoja na hati za malipo zinatunzwa vizuri.

Kuhusu suala la malipo yasiyokuwa Stakabadhi za Kielectroniki, nashauri Serikali kutoa maelekezo kwa taasisi zote za Serikali ziache kushughulika na

wauzaji ambao hawatumii mashine za Stakabadhi za Kielektroniki.

Kuhusu suala la malipo bila kukata kodi ya zuio, ninatoa wito kwa Maafisa Masuuli wote wa Taasisi za Serikali wazingatie Sheria za Kodi ya Mapato.

Kuhusu suala la masurufu yasiyorejeshwa, Nashauri Taasisi za Serikali zizingatie Kanuni za Fedha za Umma kuhusu kurejesha mapema masurufu baada ya kukamilika kwa shughuli iliyokuwa imeombewa masurufu.

### 8.2.16 Mapungufu katika usimamizi mali

Wakati wa ukaguzi nimebaini Taasisi za Serikali tano zina magari yaliyoegeshwa muda mrefu bila kufanyiwa matengenezo, tano zina daftari la mali za kudumu ambalo halina uhalisia wa sasa, na mali zenye thamani ya shilingi 9,850,000 zinazomilikiwa na MKURABITA hazikuwa na alama za utambulisho. Muhtasari wa taasisi ambazo zina upungufu katika usimamizi mali ni kama zinavyoonekana katika jedwali Na. 73 hapa chini:

**Jedwali 73: Taasisi zenye mapungufu katika usimamizi wa Mali**

| Kanuni/Sheria | Hoja | Taasisi | Kiasi Shs |
|---|---|---|---|
| Kanuni 265(2) ya kanuni za fedha 2001 | Rejesta ya mali isiyoenda na wakati | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania | |
| | | Taasisi ya kuthibitisha ubora wa Mbegu | |
| | | SUMA JKT Idara ya Ujenzi | |
| | | SUMA JKT Idara ya Ulinzi | |
| | | SUMA JKT Idara ya Kilimo na Viwanda | |
| | Mali zisizo na alama za utambulisho | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania | 9,850,000 |
| Kanuni 254(1) ya kanuni za fedha 2001 | Magari yaliyoegeshwa bila kufanyiwa Matengenezo | Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru | STG 6336 |
| | | Stoo ya Maji | STA 1654, STJ 4944, na STJ 6500 |
| | | Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela(NM-AIST) | Toyota Land Cruiser GX V8 200R. Yenye Namba ya usajili; SU 38375 |
| | | Bonde la Ziwa Tanganyika | DFP 2649 na DFP 2648 |
| | | Internal Drainage Basin Water Board | DFP 2651 |
| | | | STH 8627 |
| | | | STH 8254 |
| | | | STG 6145 |
| Kanuni 68(2) ya kanuni ya manunuzi ya Umma | Manunuzi yaliyofanyika bila kupitia kitengo cha | Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela(NM-AIST) | 14,250,000 |

**Source:** *Taarifa ya Ukaguzi kwa Menejimenti ya mwaka unaoishia Juni 30, 2015*

Kuhusu suala la kutokuwa na rejista ya Mali za Kudumu; nashauri Taasisi za Serikali zizingatie kanuni namba 265 (2) ya Kanuni za Fedha za Umma, 2001 kwa kuhakikisha kwamba, rejista ya Mali za kudumu zinafanyiwa usuluhishi wa mara kwa mara na mizani katika leja kuu na thamani ya Mali na Mitambo zinazooneshwa kwenye Taarifa za Fedha zinafanane na zile zinazoonekana katika rejista ya mali za kudumu.

Kuhusu suala la Mali za kudumu ambazo hazina alama za utambulisho, nashauri Taasisi za Serikali ili zihakikishe kwamba mali zote zimewekewa alama za utambulisho.

Kuhusu suala la magari yaliyoegeshwa muda mrefu bila matenengezo. Nashauri Taasisi za Serikali ziuze mali ambazo hazitengenezeki ili kuepuka hasara zaidi.

## 8.3 Matokeo ya Ukaguzi wa Mifuko Maalmu ya Fedha

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 mapungufu yafuatayo yamebainika katika Mifiko Maalumu ya Fedha:

### 8.3.1 Msaada walichangia kwa walengwa bila idhini ya TANDREC shilingi 70,680,000

Baada ya kupitia malipo yaliyofanyika kwa waathirika wa majanga nimebaini kwamba Shilingi 70,680,000 zililipwa kwa waathirika wa majanga bila kuidhinishwa na Kamati ya Maafa na uokoaji Tanzania (TANDREC). Hii ni kinyume na maelekezo ya Mfuko wa Maafa wa Taifa yanayoelekeza kwamba misaada yote kutoka mfuko wa Maafa wa Taifa iidhinishwe na Kamati ya Maafa na Uokoaji kabla na baada ya malipo.

Napendekeza wahusika wa mfuko wa maafa wazingatie sheria na maelekezo yote ya Mfuko wa Maafa.

### 8.3.2 Mikopo isiyorejeshwa na Wakulima Shilingi 130,745,000

Ukaguzi wa Mfuko wa Pembejeo za Kilimo umebaini kwamba, Mfuko wa pembejeo za kilimo ulitoa mikopo kiasi cha shilingi 212,720,000 kwa wakulima Tisa (9) iliyopaswa kurejeshwa njani ya mwka 2013 na 2014; Mpaka kufikia 30, Juni 2015 kiasi cha shilingi 130,745,000 (61%) za mikopo iliyotolewa haikurejeshwa kutoka kwa wakulima.

Kushindwa kurejesha mikopo kwa wakati kunazuia mfuko kutekeleza majukumu yake.

Napendekeza Mfuko wa Pembejeo za Kilimo kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wakulima walioshindwa kurejesha mikopo yao kwa wakati.

### 8.3.3 Makosa mengine yaliyobainishwa kwenye Ukaguzi wa Mifuko Maalumu ya Fedha

Mifuko Maalumu ya Fedha ambayo matumizi yake hayakuzingatia sheria na kanuni za fedha na manunuzi zimeainishwa kwenye Jedwali hapo chini;

**Jedwali: Makosa mengine yaliyobainishwa kwenye Ukaguzi wa Mifuko Maalmu ya Fedha**

| Sheria/Kigezo | Hoja iliyojitokeza | Jina la Mfuko | Kiasi Shs |
|---|---|---|---|
| Kanuni 103(1) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 iliyorekebishwa 2005 | Masurufu Yasiyorejeshwa | Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale | 3,222,000 |
| **Jumla Ndogo** | | | **3,222,000** |

| Sheria/Kigezo | Hoja iliyojitokeza | Jina la Mfuko | Kiasi Shs |
|---|---|---|---|
| Kanuni 95(4) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 | Malipo yasiyokuwa na viambatisho | Mfuko wa Pembejeo za Kilimo | 19,050,000 |
| | | Maji mfuko wa (MCRF) | 232,315,637 |
| | | Mfuko wa Hifadhi ya wanyama pori | 133,139,089 |
| **Jumla Ndogo** | | | **384,504,726** |
| Kanuni 265(2) ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 | Kukosekana kwa Rejesta ya Mali | Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale | 969,659,151 |
| **Jumla Ndogo** | | | **969,659,151** |
| Kanuni Namba 24 ya kanuni za Mashine za Risiti (EFD)ya mwaka 2012 | Malipo yasiyoambatana na stakabadhi za Kielektroniki (EFD) | Maji mfuko wa (MCRF) | 539,771,253 |
| **Jumla Ndogo** | | | **539,771,253** |

Katika suala la malipo yasiyokuwa na viambatisho nashauri Maafisa Masuuli wazingatie na kufuata masharti ya Kanuni ya Fedha za Umma 95 (4) ya 2001.

Katika suala la malipo pasipo stakabadhi za mashine za kielekroniki (EFD Receipts) napendekeza Serikali itoe maelekezo kwa Taasisi za Serikali kuacha kufanya manunuza kwa wauzaji wasiotumia mashine za kielektroniki.

Katika suala la kutokuwa na Rejesta ya mali, napendekeza Mifuko Maalumu ya Fedha izingatie

Kanuni Na. 265(2) ya kanuni za Fedha, 2001 kwa kuhakikisha Rejesta ya mali inaadaliwa.

**8.4 Matokeo ya ujumla ya ukaguzi wa vyama vya siasa**

Ukaguzi wa vyama vya siasa unafanyika kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu 14(1) cha sheria ya vyama vya Siasa Namba 5 ya 1992. Ukaguzi wa taarifa za fedha za vyama vya siasa kwa mwaka unaoishia Juni 30, 2015 unaonesha kuwa, kati ya vyama vya siasa 22 vyenye usajili wa kudumu, chama kimoja tu ndicho kilichowasilisha taarifa za fedha kwa kipindi cha miezi sita (kuanzia Januari mpaka Juni 2015); vyama vingine 21 havikuwasilisha taarifa za fedha kama ilivyopaswa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Siasa na Sheria ya Fedha ya Umma, 2001.

Katika mwaka 2013/2014 vyama vitatu tu ndivyo vilivyowasilisha taarifa za fedha kwa ajili ya ukaguzi.

Sikuweza kuthibitisha usahihi wa taarifa za fedha za vyama vya Siasa ambavyo havikuwasilisha taarifa za fedha kwa mujibu wa sheria.

## Sura ya Tisa

## USIMAMIZI WA MANUNUZI NA MIKATABA

### 9.0 Utangulizi

Dhumuni la kufanya Manunuzi na mikataba katika Wizara,Idara,Wakala na Sektretarieti za Mikoa ni kuhakikisha upatikanaji wa bidhaaa na huduma kwa namna ambavyo huongeza ufanisi,ushindani, haki na thamani halisi ya fedha kwa faida ya ujumla ya Taasisi husika.

Sura hii inaonyesha matokeo ya mapitio ya taratibu za Manunuzi ya Umma na usimamizi wa mikataba kutokana na kaguzi za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka huu wa fedha husika. Katika ripoti yangu nimejumuisha ripoti ya Mamlaka ya Udhibiti ya Manunuzi ya Umma na Taarifa ya Kurugenzi ya Uhakiki mali za Serikali.

### 9.1 Sheria na udhibiti katika Manunuzi ya Umma

Manunuzi ya Umma katika Tanzania yanaongozwa na Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 pamoja na Kanuni zake za Mwaka,2013 kupitia tangazo la Serikali (GN 446) la tarehe 20 Desemba 2013, ambayo imerasimisha mfumo wa Manunuzi kwa kutoa Mamlaka kwa kila Taasisi ya Umma kufanya maamuzi ya manunuzi ndani ya bajeti yake iliyopitishwa na kuwajibika katika yote yaliyofanyika.

Katika kuhakikisha kuwa taratibu za manunuzi zinafuatwa nchini Tanzania, Kifungu na 48(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 kinaeleza bayana kumtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya tathmini na kutoa taarifa katika Ripoti yake ya mwaka kuwa Taasisi iliyokaguliwa kama imezingatia au kutozingatia Sheria za Manunuzi na Kanuni zake.

### 9.1.1 Mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka Sh. 8,462,110,917

Katika Ukaguzi wa Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa imebainika kuwa kati ya Taasisi 121 zilizokaguliwa, imebainika kuwa Taasisi saba (7) zilifanya Manunuzi yenye thamani ya Sh. 8,462,110,917 nje ya Mpango wa Manunuzi wa mwaka kinyume na Kifungu na 49(2)(3) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka, 2011 ambacho kinataka Mamlaka husika kuidhinisha Mpango wa Manunuzi wa Mwaka kulingana na bajeti ya Taasisi iliyopitishwa. Kutokana na manunuzi haya kufanyika nje ya Mpango wa Manunuzi wa mwaka ilipelekea kutumia fedha za bajeti kwa kazi zisizokusudiwa.Manunuzi yaliozidi bajeti yanaweza kusababisha bajeti ya Taasisi kutotekelezeka.Ni maoni yangu mapungufu haya yalitokana na udhaifu katika mipango hivyo, ninashauri Taasisi husika kufanya utafiti wa kutosha kabla ya kuandaaa mpango kamilifu wa Manunuzi wa mwaka. Jedwali Na. 74 hapa chini linaonesha Taasisi zilizofanya Manunuzi kinyume na Mpango wa Manunuzi wa mwaka.

**Jedwali 74: Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi**

| S/N | Fungu | Taasisi | Hoja | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 29 | Idara ya Magereza | Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi. | 911,906,006 |
| 2 | 72 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | Kazi za Mikataba ambazo hazikujumuishwa katika Mpango wa Manunuzi | 45,538,560 |
| 3 | 73 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | Matumizi yaliyofanyika zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa katika Mpango wa Manunuzi | 9,215,700 |

| S/N | Fungu | Taasisi | Hoja | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 4 | 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | Sekretarieti kuingia mikataba bila kuwepo fedha za kutosha | 54,902,400 |
| 5 | 34 | Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa | Manunuzi yaliofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi wa mwaka | 4,617,947,311 |
| 6 | 56 | TAMISEMI | Manunuzi yaliofanyika bila ya kufuata utaratibu | 1,995,557,870 |
| 7 | 23 | Mhasibu Mkuu wa Serikali | Manunuzi yaliofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi wa mwaka | 827,043,070 |
| | **Jumla** | | | **8,462,110,917** |

***Chanzo:*** *Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Katika utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa mwaka, matokeo ya ukaguzi yamebainisha kuwa Manunuzi yanayofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi yameongezaka kulinganisha na mwaka wa fedha uliopita. Katika mwaka wa fedha uliopita, jumla ya Taasisi nne zilifanya Manunuzi nje ya Mpango wa Manunuzi yenye thamani ya Sh. 204,346,797 ikilinganishwa na mwaka husika ambapo Manunuzi yenye thamani ya Sh 8,462,110,917 hayakufuata Mpango wa Manunuzi. Hii ni ongezeko la asilimia 75 la Taasisi zisizofuata Mpango wa Manunuzi.

Nazishauri Taasisi kuzingatia Mpango wa Manunuzi wa mwaka na vile vile natoa wito kwa Menejimenti ya Taasisi husika kufanya utafiti ili kupata taarifa za kutosha katika kuandaa Mpango wa Manunuzi wa mwaka unaoendana na bajeti ya Taasisi husika. Pia nasisitiza Menejimenti husika kuomba kibali

katika Mamlaka husika ili kuhalalisha manunuzi hayo. zaidi, Taasisi husika zinatakiwa kufanya manunuzi kwa kufuata Sheria ya Manunuzi ya Umma.

### 9.1.2 Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni Sh. 494,395,890

Katika kupitia uzingatiaji wa Kifungu na35(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 pamoja na Kanuni na 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inayotaka Manunuzi kuidhinishwa na Bodi ya Zabuni nilibaini kuwa jumla ya Taasisi za Serikali Kuu tatu zilifanya Manunuzi yenye thamani ya Sh. 494, 395,890 bila kupata idhini ya Bodi ya Zabuni. Taasisi mbalimbali zilizofanya Manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni husika zimeorodheshwa kwenye jedwali na. 75 hapa chini

**Jedwali 75: Taasisi zilizofanya Manunuzi bila idhini ya Bodi ya Zabuni**

| Na | Fungu | Taasisi | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 29 | Idara ya Magereza | 348,500,000 |
| 2 | 72 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | 124,274,335 |
| 3 | 68 | Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia | 21,621,555. |
| | **Jumla** | | **494,395,890** |

***Chanzo:*** *Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Katika ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini kuimarika katika uzingatiaji wa Sheria hii na Kanuni zake katika Taasisi nilizokagua. Manunuzi yasiyoidhinishwa na Bodi ya Zabuni yamepungua kwa asilimia 35 kutoka Sh. 760,868,514 hadi Sh. 494,395,890 ikilinganishwa na ukaguzi wa mwaka jana. Nashauri menejimenti ya Taasisi husika kuzingatia kikamilifu Sheria ya Manunuzi

ya Umma ili bodi za zabuni ziweze kufanya kazi yake ya kuidhinisha manunuzi kama Sheria inavyoagiza.

### 9.1.3 Manunuzi yaliyofanyika bila ushindanishi Sh. 27,121,224,071

Kanuni ya 163 na 164 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2013 inazitaka Taasisi zinazofanya Manunuzi kuzingatia upatikanaji wa nukuu za bei zisizopungua tatu kutoka kwa Wazabuni tofauti. Katika ukaguzi wangu katika jumla ya Taasisi tisa (9) nilibaini kuwa Manunuzi yenye thamani ya Sh. 27,121,224,071 yalifanyika bila kuzingatia Kanuni tajwa hapo juu. Orodha ya Taasisi ambazo hazikufuata Kanuni hizi ni kama inavyoonekana kwenye jedwali na. 76 hapo chini.

**Jedwali 76: Manunuzi yaliyofanyika bila ushindani**

| Na | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Manunuzi yaliyofanyika bila ushindanishi | 4,287,219,708 |
| 2 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Manunuzi yasiyokuwa na nukuu za bei | 14,706,603,298 |
| 3 | 28 | Idara ya Jeshi la Polisi | Kukosekana kwa uhalali wa kutumia Mzabuni mmoja katika Manunuzi | 1,517,600,000 |
| 4 | 39 | Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) | Manunuzi ya huduma za chakula yasiyofuata taratibu katika kambi ya Rwamkoma | 150,630,000 |
| 5 | 86 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | Mapungufu yaliyojitokeza katika Manunuzi kwa kutumia nukuu za bei | 23,997,265 |
| 6 | 82 | Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma | Kukosekana kwa uhalali wa kutumia Mzabuni mmoja katika Manunuzi | 59,309,600 |
| 7 | 56 | TAMISEMI | Manunuzi yaliyofanyika bila kuitisha nukuu za bei | 372,960,000 |
| 8 | 76 | Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi | Manunuzi yaliyofanyika bila kuitisha nukuu za bei | 2,904,200 |

| Na | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 9 | 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | Uchapishaji Wa vitabu 2,000,000 vya Katiba pendekezwa bila kufuata mchakato wa Manunuzi. | 6,000,000,000 |
| | Jumla | | | 27,121,224,071 |

***Chanzo:*** *Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Manunuzi yaliyofanyika bila kufuata ushindanishi yameongezeka kutoka Sh. 144.48 million hadi kufikia Sh. 27.12 billion ikilinganishwa na mwaka wa fedha uliopita. Katika mwaka 2013/2014 jumla ya Taasisi tatu zilihusika.

Nazishauri Menejimenti ya Taasisi husika kuzingatia ushindanishi katika Manunuzi ili kuweza kupata thamani halisi ya fedha katika Manunuzi. Kutokana na kutozingatiwa kwa Sheria ya Manunuzi, ni wazi kuwa thamani halisi ya fedha haikupatikana.

### 9.1.4 Mapokezi ya vifaa visivyofanyiwa ukaguzi Sh. 15.36 bilion

Kwa mujibu wa Kanuni ya 244(1) ya Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013, Manunuzi ya bidhaa na huduma yanatakiwa kufanyiwa ukaguzi kabla ya kupokelewa ili kuweza kuthibitisha ubora wake kama unaendana na makubaliano ya mkataba. Kanuni ya 245 ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 inamtaka Afisa Masuuli kuteua Kamati ya Ukaguzi na mapokezi ya vifaa ambayo itawajibika kukagua, kuthibitisha ubora wa vifaa au huduma na kupokea pindi zinaponunuliwa kutoka kwa Wazabuni. Wakati wa ukaguzi, nilizibaini Taasisi kumi na sita (16) za Serikali Kuu zilizofanya Manunuzi ya huduma na vifaa vyenye thamani ya Sh. 15,361,328,135 bila kufanyiwa utaratibu wa mapokezi na ukaguzi. Katika sehemu nyingine, Maafisa Masuuli hawakuunda Kamati ya Ukaguzi na Mapokezi ya Vifaa ambavyo

ina wajibu wa kukagua, kuthibitisha ubora wa huduma na vifaa vilivyopokelewa kutoka kwa Watoa Huduma. Taarifa zaidi zinapatikana kwenye jedwali na.77 hapo chini.

**Jedwali 77: Mapokezi ya vifaa visivyofanyiwa Ukaguzi**

| S/N | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 6 | Taasisi ya kusimamia matokeo makubwa sasa | Kutopatikana kwa ripoti za ukaguzi na mapokezi ya vifaa vilivyonunuliwa | 48,804,800 |
| 2 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Vifaa vilivyonunuliwa bila kuambatanishwa na ripoti za Ukaguzi | 14,706,603,298 |
| 3 | 92 | Tume ya kudhibiti Ukimwi (TACAIDS) | Matengenezo ya Magari bila kufanyiwa ukaguzi | 5,660,007 |
| 4 | 14 | Idara ya Zimamoto na Uokoaji | Mapungufu katika Manunuzi ya vifaa vya kuzimia moto | 132, 600,000 |
| 5 | 39 | Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) | Mkataba wa ununuzi wa pampu ya maji haukufuata utaratibu | 18,889,940 |
| 6 | 36 | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | Mchakato wa ununuzi wa samani haukufuata utaratibu wa Manunuzi | 32,650,000 |

| S/N | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 7 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa Ukaguzi | 7,644,920 |
| 8 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | Mapungufu katika ununuzi wa fomu za TSM 9 | 130,000,000 |
| 9 | 87 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | Mapungufu katika ununuzi wa fomu za TSM 9 | 143,708,400 |
| 10 | 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa Ukaguzi | 8,402,153 |
| 11 | 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | Mapungufu yalijitokeza katika ununuzi wa mabati 1000 | 14,625,002 |
| 12 | 47 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu | Manunuzi yaliofanika kinyume na taratibu | 2,757,720 |
| 13 | 86 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | Matengenezo ya Magari bila kufanyiwa ukaguzi | 4,732,800 |
| 14 | 68 | Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia | Matengenezo ya Magari bila kufanyiwa ukaguzi | 146,210,174 |
| 15 | 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Kutopatikana kwa ripoti za Ukaguzi na Mapokezi ya Vifaa vilivyonunuliwa | 72,177,660 |

| S/N | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 16 | 79 | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro | Vifaa vilivyonunuliwa na kupokelewa bila kufanyiwa Ukaguzi | 18,461,260 |
| | | | **Jumla** | **15,361,328,135** |

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Nimebaini ongezeko kubwa la Manunuzi ya vifaa na huduma vinavyopokelewa bila kufanyiwa ukaguzi ikilinganishwa na mwaka 2013/2014. Katika mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya Taasisi sita (6) zilikuwa na mapungufu yenye thamani ya Sh. 534.9 million ikilinganishwa na mwaka huu ambapo Manunuzi yenye thamani ya Sh.15.36 bilioni yalifanyika bila kufanyiwa ukaguzi na Kamati ya Mapokezi na Ukaguzi.

Kupokea Vifaa bila kukaguliwa na kukubaliwa na Kamati ya Ukaguzi, Mapokezi ya Vifaa na Huduma, kunaweza kukatoa fursa kwa Taasisi za Umma kununua vifaa na huduma zisizokuwa na viwango vya ubora au zisizofuata mahitaji muhimu ya Manunuzi. Nawashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi za Serikali Kuu kuteua Kamati ya Mapokezi na Ukaguzi wa vifaa na huduma pale inapotokea Taasisi husika imefanya Manunuzi ya vifaa na huduma.

### 9.1.5 Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 baadhi ya Wizara, Idara na Sekretatieti za Mikoa zilishindwa kutunza kikamilifu kumbukumbu za Manunuzi. Hii ni dalili ya udhaifu wa udhibiti wa mfumo wa ndani na ni kinyume na Kifungu Na. 61 (1) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011.

Katika ukaguzi wangu nilibaini Taasisi tano (5) za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara na Idara mbili (2) na Balozi za Tanzania tatu (3) kati ya Taasisi 121 zilizokaguliwa hazikuzingatia matakwa ya Sheria tajwa hapo juu.Orodha ya Taasisi hizo inapatikana katika Jedwali Na. 78 chini.

**Jedwali 78: Mapungufu katika utunzaji wa kumbukumbu za Manunuzi**

| Na. S/N | Fungu | Taasisi | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka |
| 2 | 29 | Idara ya Jeshi la Magereza | Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka |
| 3 | 2005 | UBalozi wa Tanzania Abuja, Nigeria | Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka na taarifa yake ya utekelezaji |
| 4 | 2001 | Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia | Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka na taarifa yake ya utekelezaji |
| 5 | 2012 | UBalozi wa Tanzania - Ottawa | Kukosekana kwa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka |

*Chanzo: Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Kutokana na kukosekana kwa kumbukumbu za Manunuzi, nimeshindwa kupata mtiririko wa miamala ya Manunuzi kuanzia mwanzo hadi mwisho. Nazishauri Taasisi husika kutunza vizuri kumbukumbu za Manunuzi kwa ajili ya marejeo ya baadaye.

### 9.1.6 Manunuzi ya Vifaa na huduma bila mikataba Sh. 5.21 bilioni

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 nilibaini Taasisi tano (5) za Serikali Kuu kati ya 121 nilizokagua hazikuweza kuwasilisha mikataba ya Manunuzi yenye thamani ya Sh. 5.21bilioni.Kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, kinatoa tafsiri ya neno mkataba kama ni makubaliano baina ya Taasisi za Manunuzi na Wazabuni unaotokana na mchakato wa Manunuzi.

Vile vile, Kanuni ya 10(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013, inaeleza bayana kuwa Taasisi za Manunuzi zitafanya malipo kwa Wazabuni kwa mujibu wa makubaliano yaliyoainishwa kwenye mikataba. Taasisi zilizohusika na Manunuzi bila ya mikataba zimeoredheshwa kwenye jedwali Na. 79 hapo chini:

**Jedwali 79: Orodha ya Taasisi za Serikali Kuu zilizofanya Manunuzi bila ya mikataba**

| S/N | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Manunuzi ya Vifaa na huduma bila ya Mikataba | 1,088,026,112 |
| 2 | 89 | Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa | Ukarabati wa jengo la Sekretarieti ya Mkoa bila ya Mkataba | 131,841, 000 |

| S/N | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 23 | Mhasibu Mkuu wa Serikali | Kuajiriwa kwa Mkandarasi bila ya Mkataba | 1,074,410,001 |
| 4 | 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Manunuzi yaliyofanyika bila ya Mikataba | 2,438,170,050 |
| 5 | 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | Malipo yaliyolipwa kabla ya Mikataba kufanyika | 612,933,093 |
| | | | **Jumla** | **5,213,539,256** |

***Chanzo:*** *Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Nimebaini kuongezeka kwa udhaifu huu katika Taasisi za Serikali Kuu ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo Taasisi saba (7) zilifanya manunuzi yenye thamani ya Sh.134,071,510 bila ya mikataba.

Ni muhimu Manunuzi ya Umma yakaambatanishwa na nyaraka za kutosha za mikataba ili kama kutatokea mmoja kushindwa kutimiza makubaliano ziweze kukubalika mbele ya Sheria. Nashauri Taasisi zizingatie Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake kwa kuingia makubiliano ya mikataba inayokubalika mbele ya Sheria.

### 9.1.7 Manunuzi kwa kutumia Masurufu Sh. 150 milioni

Katika kupitia uzingatiwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za mwaka 2013, nilibaini kuwa Taasisi za Serikali Kuu zilifanya Manunuzi kwa kutumia masurufu na Mikataba midogo ya Manunuzi (LPO) zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na jedwali la saba la Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka, 2013. Katika Jedwali hilo imeelezwa kwamba Manunuzi kati ya Sh. 10 milioni na Sh. 20 million yatatumia

Mikataba midogo (LPO) na Manunuzi yasiyozidi Sh. milioni 5 yatatumia masurufu/fedha taslimu.

Katika kupitia mchakato wa Manunuzi nilibaini kuwa Taasisi mbili (2) za Serikali Kuu zilifanya Manunuzi yenye thamani ya Sh. milioni 150 kwa masurufu/fedha taslimu kinyume na jedwali Na. 7 la Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013.Taasisi zilizohusika zimeoredheshwa kwenye jedwali Na.80 hapo chini:

**Jedwali 80: Taasisi zilizofanya Manunuzi kwa fedha taslimu/masurufu**

| S/N | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Manunuzi yaliofanyika kwa kutumia Masurufu | 52,036,250 |
| 2 | 39 | Jeshi la kujenga Taifa (JKT) | Manunuzi yaliofanyika kwa kutumia Masurufu | 98,292,300 |
| | **Jumla** | | | **150,328,550** |

***Chanzo:*** *Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Ikilinganishwa na ukaguzi wa mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi za Serikali Kuu zisizozingatia Kanuni hii zilipungua kwa asilimia 50 kutoka nne (4) hadi kufikia mbili (2) katika ukaguzi wa mwaka huu; hata hivyo kiasi kilichohusika kiliongezeka kutoka Sh. milioni 65.81 hadi Sh. milioni 150.

Nashauri Manunuzi yanayozidi Sh. 5,000,000 yapitishwe katika Bodi ya Zabuni ya Taasisi husika pamoja na kuzingatia njia mbalimbali za Manunuzi zilizoainishwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011.

### 9.1.8 Manunuzi ya Vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa Sh. milioni 8,556.82

Kanuni Na.131 (5) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka, 2013 inaeleza bayana taratibu za kununua bidhaa na huduma kutoka kwa Wazabuni walioidhinishwa. Hata hivyo, katika ukaguzi nilibaini kutokuzingatiwa kwa taratibu hizi ambapo jumla ya Taasisi kumi na sita (16) za Serikali Kuu zilifanya Manunuzi yenye thamani ya Sh. milioni 8,556.82 bila kuzingatia Kanuni tajwa hapo juu. Taasisi zilizohusika zimeorodheshwa kwenye Jedwali 81 hapa chini

**Jedwali 81: Manunuzi ya Vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasiodhinishwa.**

| Na | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi (SH.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 33 | Ofisi ya Rais-Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi | Matengenezo ya Magari yasiyofuata taratibu | 12,180,502.50 |
| 2 | 92 | Tume ya Kudhibiti Ukimwi | Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 32,658,456 |
| 3 | 73 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD) | 47,469,200 |
| 4 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa | 8,071,808,256 |

| Na | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi (SH.) |
|---|---|---|---|---|
| 5 | 31 | Ofisi ya Makamu wa Rais | Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 3,528,200 |
| 6 | 39 | Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) | Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni 'binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD) | 18,199,830 |
| 7 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 17,298,729 |
| 8 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa | 10,464,700 |
| 9 | 72 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dodoma | Manunuzi ya vifaa na huduma kutoka kwa Wazabuni wasioidhinishwa | 14,208,894 |
| 10 | 54 | Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe | Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 32,421,578 |
| 11 | 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD) | 55,539,173 |

| Na | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi (SH.) |
|---|---|---|---|---|
| 12 | 86 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga | Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD) | 50,127,931 |
| 13 | 73 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD) | 47,469,200 |
| 14 | 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | Manunuzi ya Madawa kwa Wazabuni binafsi bila ya kupata kibali kutoka Bohari Kuu ya Madawa (MSD) | 76,616,060 |
| 15 | 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 7,903,824 |
| 16 | 82 | Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma | Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) | 58,928,184.90 |
| **Jumla** | | | | **8,556,822,718** |

***Chanzo:** Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa Manunuzi yaliyofanyika kwa Wazabuni wasioidhinishwa yameongezeka ikilinganishwa na ukaguzi wa mwaka jana .Katika ukaguzi wa mwaka jana jumla ya Taasisi tisa (9) zilifanya Manunuzi ya Vifaa na huduma yenye thamani ya Sh. milion 519.02 ikilinganishwa na mwaka huu ambapo Manunuzi ya Sh. 8,556.82 milioni yalifanyika ikiwa ni ongezeko la asilimia 78 ya Taasisi zilizohusika mwaka jana.

Ninashauri Menejimenti ya Taasisi husika kuzingatia kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 ili Taasisi ziweze kupata

thamani halisi ya fedha zilizotumika katika Manunuzi.

### 9.1.9 Vifaa na huduma zilizolipiwa hazikupokelewa Sh.milioni 3,253.65

Katika Taasisi za Serikali Kuu nilizokagua nilibaini Manunuzi ya Vifaa na huduma vyenye thamani ya Sh. 3,253.65 million yaliyoagizwa na kulipiwa lakini hayakupokelewa. Makubaliano ya Mkataba yalibainisha kuwa Manunuzi ya vifaa na huduma yalitakiwa kupokelewa kati ya Aprili, 2014 na Julai, 2015, lakini Wazabuni walishindwa kutekeleza makubaliano ya mikataba. Taasisi zilizohusika na Manunuzi yasiyopokelewa zimeorodheshwa kwenye jedwali na. 82 hapo chini:

**Jedwali 82: Manunuzi ya Vifaa na huduma yasiyopokelewa**

| S/N | Fungu | Taasisi | Maelezo | Kiasi(Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 57 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | Malipo yamefanyika lakini Magari hayakupokelewa | 2,856,770,876 |
| 2 | 87 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kagera | Malipo yamefanyika lakini Magari hayakupokelewa | 88,928,632 |
| 3 | 99 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | Malipo yamefanyika lakini Magari hayakupokelewa | 302,670,681 |
| 4 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | LAN imelipiwa lakini haijafungwa Mt Meru Hospitali | 5,280,000 |
| | **Jumla** | | | **3,253,650,189** |

***Chanzo:*** *Ripoti ya ukaguzi kwa Menejimenti 2014/15*

Ikilinganishwa na ukaguzi wa mwaka 2014/2015,

idadi ya Taasisi zilizobainika kufanya Manunuzi yasiyopokelewa imepungua kwa asilimia 33 kutoka Taasisi sita (6) hadi Taasisi nne (4) zilizobainika katika mwaka huu wa fedha. Hata hivyo, thamani ya Manunuzi yaliyofanyika bila kupokelewa imeongeza kutoka sh. milioni 857.88 mwaka 2013/2014 hadi kufika sh. milioni 3,253.65 mwaka huu .Hali hii inaashiria kuwa bado kuna upungufu katika kuzingatia makubaliano na masharti ya kutekeleza mikataba.

Nawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha Wazabuni wanazingatia vipengele vya mikataba walivyokubaliana kutekeleza na kukamilisha mikataba yao bila kuchelewa zaidi.

**9.1.10 Mapungufu katika utekelezaji wa mikataba na Miradi**

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali Kuu zilishindwa kusimamia kikamilifu utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyoingiwa kati yao na Wakandarasi mbalimbali. Udhaifu huu ulisababisha kutokamilika kwa mikataba/miradi kwa wakati na baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

Katika ukaguzi wa Mikataba ya miradi nilibaini kuwa jumla ya mikataba/miradi ishirini na saba (27) yenye thamani ya Sh. milioni 109,683.40 kutoka katika Taasisi ishirini (20) ilitekelezwa nje ya muda wa mkataba/mradi. Nilibaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa kukamilika mikataba/miradi hii kwa kipindi kati ya mwezi mmoja hadi miaka minne. Taarifa za mikataba/ miradi na Taasisi husika zimeainishwa kwenye kiambatisho na 9.1

**Mabadiliko ya Mikataba yasiyoidhinishwa**

Kanuni Na.61 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya

Umma ya mwaka 2013 inatamka bayana kuwa mabadiliko yeyote katika Mikataba yenye lengo la kubadili bei ya awali ya mkataba kwa zaidi ya asilimia 15 yanatakiwa kuidhinishwa kwanza na Mamlaka ya Bajeti husika. Hata hivyo, nili,baini kuwa Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa (Fungu 34) pamoja na Wizara ya Maji (Fungu 49) kwa pamoja, walifanya mabadiliko ya mikataba yenye thamani ya Sh. 1,675,187,919 yaliyozidi kiwango cha asilimia 15 bila kuzingatia Kanuni tajwa hapo juu.

Nazishauri Menejimenti ya Taasisi husika kufuata Kanuni tajwa hapo juu, kuomba kibali cha kuhalalisha mikataba iliyoingiwa bila kibali cha Mamlaka ya Bajeti na kusimamia ikamilifu mikataba ili iweze kukamilika kwa wakati.

Mabadiliko ya bei ya mkataba yalikuwa na thamani ya Sh. 234,978,660 ikiwa ni sawa na 77% ya thamani ya mkataba wa Sh.416,415,250. Mabadiliko yalifanyika kinyume na Kanuni 61(2)(c)&61(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya mwaka 2013 ambayo inazuia mabadiliko ya mkataba kwa zaidi ya asilimia 15 bila kupata kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Vile vile, Kanuni Na. 110(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 inaagiza Taasisi za Manunuzi hazitakuwa na Mamlaka ya kufanya mabadiliko ya kuongeza gharama za mikataba bila kupata kibali kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali au Mamlaka za kuidhinisha bajeti hata hivyo Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje iliingia mkataba Na.ME/013/2011/2012/M2Q/W/01 wa Dola za kimarekani 2,107,028.89 sawa na Sh. 3,442,695,573.65 na Mkandarasi Ms CM Constructora Do Mondego kwa ajili ya

ukarabati wa jengo la UBalozi wa Tanzania-Maputo. Mkataba ulitegemewa kukamilika mwezi Februari mwaka 2013. Ilibainika pia kuwa gharama za mkataba ziliongezeka kwa Dola za Kimarekani 679,971.11 sawa na Sh.1,258,772,669.69 bila ya kuidhinishwa.

**1.1.10.1 Kuchelewa kukamilika kwa kazi za Ujenzi**

Tarehe 27/6/2014 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (Fungu 46) iliingia makubaliano ya Mkataba Na. ME-024/CTR/HQ/2013-2014/29 na Kikosi cha Ujenzi cha Magereza kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi la Ghorofa tatu katika Manispaa ya Dodoma. Mapungufu yaliyobainika katika Mkataba huo ni haya yafuatayo;

a) Mkataba ulikuwa na thamani ya Sh. 2,100,700,776 na ujenzi ulitakiwa kuanza tarehe 4/7/2014 na ulitegemewa kukamilika kabla ya tarehe 17/7/2015. Kinyume na Kanuni Na.61(4) &110(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za mwaka 2013 mnamo tarehe 26/9/2015 Menejimenti ilifanya mabadiliko ya mkataba wa kujenga Jengo la Ghorofa nne kwa thamani ya Sh. 4,430,734,935 bila ya kupata idhini ya Mamlaka husika.
b) Nilibaini pia Wizara ililipa Malipo ya awali yenye thamani ya Sh. 780,662,138 tarehe 26/6/2014 ikiwa ni siku moja kabla ya kuingiwa kwa mkataba.
c) Vile vile, nilibaini kuwa Wizara ilifanya makubaliano na Mkandarasi mmoja (Single source) bila ya kufuata mchakato wa Manunuzi wa ushindani na kufanya Mkandarasi mmoja afanyiwe tathmini.
d) Hadi ukaguzi unakamilika Desemba 2015 ujenzi wa mradi ulikuwa haujaanza na Mkandarasi hakuwepo eneo la ujenzi.

Matokeo ya ukaguzi yalibaini kuwa usimamizi wa mkataba haukuwa wa kuridhisha kuendana

na Sheria ya Manunuzi ya Umma. Nashauri Menejimenti ya Wizara kuomba idhini ya kuhalalisha mabadiliko ya ongezeko hilo la kazi kwa Mamlaka Husika pamoja na kuongeza bidii katika usimamizi wa mradi.

Nazishauri Taasisi kuendelea kufanya juhudi za ufuatiliaji raslimali fedha kutoka Hazina ili kuweza kutekeleza miradi iliyopangwa katika bajeti. Nashauri pia miradi yenye fedha kidogo itekelezwe kwa hatua ili kurahisisha usimamizi wa miradi na ulipaji wake. Hii itawezesha Serikali kuepuka gharama zisizo za lazima zinazotokana na mfumuko wa bei pamoja na kuongezeka kwa gharama za vifaa. Aidha, nashuari Menejimenti ya Taasisi husika kuongeza bidii katika usimamizi wa Miradi iweze kukamilika kwa wakati.

### 9.1.11 Mapungufu yaliyobainika katika Uchapishaji wa Vitabu vya Katiba inayopendekezwa Sh. milioni 7,080.

Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwa Wizara ya Katiba na Sheria ilipokea fedha kiasi cha Sh. milioni 7,125 kwa ajili ya kulipia gharama za kuchapisha vitabu vya Katiba inayopendekezwa. Kutokana na ufinyu wa muda, Wizara iliomba na kupewa Kibali na Wakala wa huduma za Manunuzi Serikalini (GPSA) kufanya Manunuzi kwa njia ya dharura kupitia barua yenye Kumbukumbu Na CAD.124/318/01/25 ya tarehe 11/12/2014. Katika Ukaguzi wangu nilibaini mapungufu yafuatayo:

**i. Vitabu vya Katiba vilivyopokelewa kabla ya kuingia Mkataba**

Nilibaini kuwa mkataba ulisainiwa tarehe 2/2/2015 lakini Vitabu vya Katiba vilipokelewa tarehe 26/1/2015. Pia, vitabu

365,092 vilipokelewa na kuingizwa kwenye lejista ya vifaa kabla ya Mkataba kusainiwa.

ii. **Dhamana ya utendaji kazi(Perfomance security Bond) haikuwasilishwa**

Nilibaini kuwa dhamana ya utendaji kazi (Perfomance Security Bond) yenye thamani ya asilimia 10% ya bei ya mkataba haikuwasilishwa na Mzabuni ndani ya siku thelathini toka kuingiwa kwa mkataba kinyume na kipengele cha 9.1 cha mkataba.

iii. **Uvunjaji wa maadili, utawala bora na mgongano wa kimaslahi**

Ukaguzi wa ripoti ya Kamati ya Tathmini ulibaini kuwa Afisa mmoja mwandamizi kwa niaba ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali alipendekeza na kuteua Wazabuni watatu wa kampuni binafsi kufanya kazi ya kuchapisha Vitabu vya Katiba inayopendekezwa kwa niaba ya Wizara ya Sheria na Katiba kupitia barua yenye Kumb Na. CHAPA/ORD/23/331 ya 6/12/ 2014.

Wakati wa mchakato wa tathimini ya zabuni ilibainika kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Tathmini aliyeteuliwa alikuwa Afisa Mwandamizi kutoka Ofisi ya Mpiga Chapa ambaye ndiye aliyehusika kuwapendekeza na kuwateua wale Wazabuni watatu wa kampuni binafsi hapo awali. Hii ni kinyume na taratibu za utawala bora na inaashiriakuwapo kwa mgongano wa masilahi, kwani mwenyekiti hawezi kutolea maamuzi jambo alilopendekeza yeye mwenyewe.

**Nakala 158,003 za Katiba Pendekezwa hazikupelekwa kwa walengwa Sh..**

**559,330,620**

Katika ukaguzi wa nyaraka mbalimbali uliofanyika tarehe 1/10/2015, ilibainika kuwa nakala 158,003 za Katiba Pendekezwa hazikupelekwa kwa walengwa kwa madhumuni ya kuelimisha na kuhamasisha umma juu ya kura ya maoni kwa ajili ya Katiba inayopendekezwa ; badala yake, vitabu hivi vilibaki stoo. Kwa hiyo, haikuwa rahisi kujua kama thamani halisi ya fedha ilipatikana na lini vitabu hivi vitasambazwa kwa walengwa.Pia, ilibainika kuwa, vitabu hivyo havikujumuishwa kwenye Taarifa za Fedha za Mwaka husika.

Mapungufu yametokana na Menejimenti kutozingatia ipasavyo Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011. Inapotokea Menejimenti inakiuka mifumo ya udhibiti ya ndani yenye lengo lakuangalia taratibu na kulinda raslimali za umma, inatia shaka katika uchumi, ufanisi, pia uhakika kulinda na kutumia rasilimali za umma.

Nashauri Afisa Masuuli azingatie kikamilifu Sheria za Manunuzi pamoja na Kanuni zake kabla ya kuingia mikataba na Wazabuni mbalimbali. Pia Wizara ifanye ufuatiliaji wa fedha hazina ili kuweza kupeleka vitabu vya katiba pendekezwa vilivyosalia kwa walengwa.

**9.1.12 Manunuzi ya Vifaa yaliyozidi mahitaji Sh.827,046,942**

Uhakiki uliofanyika katika Stoo za Tume ya Taifa ya Uchaguzi ulibaini kuwepo kwa vifaa vya uandikishaji wa piga kura kama vile fomu za kujiandikisha na fulana ambavyo muda wake ulishakwisha. Kulikuwa na Manunuzi yaliyopita

kiasi yakihusisha ya fomu za kujiandikisha zenye thamani ya Sh.518,374,872.99 pamoja na fulana na kofia zenye thamani ya Sh.308,672,069.42.

Nashauri kwamba Tume izingatie mahitaji halisi ya matumizi ya vifaa na huduma kabla ya kufanya Manunuzi pamoja na kutafuta matumizi mbadala wa vifaa hivyo kabla havijaharibika au kuchakaa.

### 9.1.13 Taarifa ya PPRA-Uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni zake za 2013

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) ilifanya ukaguzi wa Mikataba ya Manunuzi elfu tano mia mbili na sita (5,206) yenye thamani ya Sh. bilioni 214.63 katika Taasisi za Manunuzi (PE) zipatazo themanini (80). Ukaguzi ulihusisha mikataba ya ujenzi mia tatu arobaini na tano (345) yenye thamani ya Sh. bilioni 119.62.

**Kielelezo: Mawanda ya ukaguzi wa PPRA**




Mikataba elfu moja mia moja kumi na mbili (1,112) ya vifaa yenye thamani ya Sh. bilioni 35.11; Mikataba ya huduma za ushauri yenye

thamani ya Sh. bilioni 5.63; Mikataba elfu moja na arobaini na moja ya huduma zisizo za ushauri yenye thamani ya Sh. bilioni18.04. Manununizi madogo madogo ya huduma na vifaa yenye thamani ya Sh. Bilioni 29.68; Pamoja na Manunuzi binafsi (force Account) yenye thamani ya Sh. bilioni 6.54.

Kutokana na vigezo saba vilivyowekwa na Mamlaka ya Udhibiti na Manunuzi ya Umma matokeo ya ukaguzi yanaonesha kuwa Wizara, Wakala na Idara za Serikali hazikufanya vizuri katika kufuata Sheria ya Manunuzi kwa wastani wa 69%, ambacho ni kiwango kikubwa kidogo ikilinganishwa na wastani wa 65% wa mwaka uliopita. Hata hivyo, matokeo ya mwaka huu yamekuwa chini ya lengo la asilimia 75 lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Mchanganuo wa matokeo ya Ukaguzi yanaonyesha kuwaTaasisi za Manunuzi 27 zilifanya vizuri juu ya lengo la asilimia 75 wakati Taasisi 53 hazikufanya vizuri chini ya lengo lilowekwa.

Tathimini iliyofanyika katika maeneo mbalimbali ya uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ilibaini yafuatayo. Kuanzishwa kwa Kitengo cha Manunuzi na utendaji kazi wake (77%); Zabuni kufuata utaratibu (77%). Pamoja na kuandaa na kutekeleza Mpango wa Manunuzi wa mwaka (75%). Hata hivyo, maeneo yafuatayo yalifanyika chini ya kiwango kilichowekwa: Usimamizi na utekelezaji wa mikataba (70%). Usimamizi wa kumbukumbu za Manunuzi (67%); na Utekelezaji wa mifumo ya Manunuzi iliyoandaliwa na PPRA (35%)

**Mapungufu yaliyojitokeza katika Wizara na Idara za Serikali**

**zilizokaguliwa**

Jedwali na.83 linaonyesha mapungufu yaliyoonekana na PPRA wakati wa ukaguzi wa Manunuzi katika Taasisi zilizokaguliwa:

**Jedwali 83 : Mapungufu yaliyojitokeza katika Wizara na Idara za Serikali zilizokaguliwa**

| SN | Taasisi | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|
| 1 | **Wizara ya Mambo ya Nchi za nje Na ushirikiano Wa Kimataifa** | Afisa Masuuli hakusaini Mikataba kwa niaba ya Wizara kinyume na Kifungu 36(h) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma mwaka 2011 pia hakuteua Kamati ya Tathmini na majadiliano kinyume na Kifungu cha 36(e) cha PPA yam waka 2011 |
| | | Kitengo cha Manunuzi ya Umma kilihusika kuidhinisha orodha ya Wazabuni |
| | | Nukuu za bei hazikufunguliwa kwa uwazi |
| | | Kitengo cha Manunuzi ya Umma hakikutekeleza wajibu wake ipasavyo kama vile kuandaa nyaraka na taarifa za mchakato wa Manunuzi kinyume na Kifungu cha 38(h &l) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011. |
| 2 | **Tume ya Utumishi wa Umma** | Mahitaji ya Manunuzi hayakujumuishwa ipasavyo kwenye Mpango wa Manunuzi wa mwaka kinyume na Kifungu cha 49(b&c) cha Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011 pamoja na Kanuni ya 72,73 ya PPR mwaka 2013 |

| SN | Taasisi | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|
| 3 | **Ofisi ya Makamu wa Rais** | Zabuni 12 kati ya 17 zilizokuwa kwenye Mpango wa Manunuzi wa mwaka hazikutekelezwa kinyume na Kifungu cha 49(3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka, 2011 |
| 4 | **Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira** | Afisa Masuuli hakutoa taarifa ya kusudio la kusaini Mkataba kwa Wazabuni wote walioshiriki katika mchakato wa Zabuni kinyume na Kifungu cha 60(1,2 &3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011 na Kanuni Na.231(2) ya PPR ya mwaka 2013 |
| 5 | **Tume ya Taifa ya Uchaguzi** | Katika Zabuni Na. IE/018/2012-13/HQ/G/19 kwa ajili ya kununua (BVR).Idara yenye mahitaji ilihusika kuanda vigezo na hadidu za rejea lakini hazikuainishwa ili kuweza kuondoa mazingira ya uwezekano wa upendeleo kwa Wazabuni |
| | | Katika Zabuni Na. IE/018/2013-14/HQ/W/01 ya ukarabati wa chumba cha kuhifadhia taarifa (saver room) ubunifu wake haukuzingatia uwekaji wa umeme na viyoyozi ambavyo ni vitu muhimu. |

| SN | Taasisi | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|
| 6 | **Wizara ya Uhusiano wa Afrika Mashariki** | Zabuni Na. ME/027/2014/15/ NC/09 kwa ajili ya kuunganisha mtandao wa barua pepe haukuzingatia taratibu za Manunuzi ambapo Mzabuni mmoja aliteuliwa badala ya kufuata mchakato wa ushindani. Vile vile, Mkataba husika uliandaliwa na mtoa huduma badala ya Wizara. |
| 7 | **Ofisi ya Makamu wa Rais** | Vikao katika maeneo ya kazi za ujenzi havikufanyika; pia, kumbukumbu hazikuandaliwa kwa mujibu wa matakwa ya Mkataba.<br><br>Vipimo vya kazi iliyokwishafanyika kabla ya malipo havikuandaliwa na taarifa ya maendeleo ya kazi haikuandaliwa kinyume na Kanuni. Na 248,243(2) na 242(1) za PPR,yam waka 2013 |
| 8 | **Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI** | Mkataba kwa ajili ya kutoa huduma ya kuunganisha mfumo wa Kompyuta kwa Halmashauri mpya 34 haukuandaliwa. |
| 9 | **Wizara Ya Fedha** | Baadhi ya Taarifa za Manunuzi ya huduma za ushauri katika Idara mbalimbali hazikuweza kupatikana wakati wa ukaguzi. |

| SN | Taasisi | Matokeo ya Ukaguzi |
|---|---|---|
| 10 | **Tume ya Utumishi wa Umma** | Rejista ya Mikataba haikuwa na taarifa zote za Zabuni vile vile haikujumuisha mikataba yote. Taarifa zote za mkataba hazikuhifadhiwa katika jalada moja kurahisisha |

**Chanzo**: Taarifa ya PPRA ya mwaka 2014/2015

**Uchunguzi wa tuhuma, malalamiko pamoja na taarifa zinazowasilishwa kwa Mamlaka ya Udhibiti na Manunuzi ya Umma kutokana na Manunuzi yenye mapungufu.**

Kifungu cha 10 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma Na.7 ya mwaka 2011 kinatoa Mamlaka kwa PPRA kufanya uchunguzi inapotokea tuhuma za Manunuzi yenye mapungufu. Kutokana na Kifungu cha 11 cha PPA mwaka 2011 uchunguzi unaweza kufanywa na PPRA kwa kutumia juhudi binafsi au kupitia tuhuma zilizowasilishwa kwa Mamlaka. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Mamlaka ya Manunuzi Na Udhibiti wa Umma ilifanya ***Uchunguzi wa Zabuni Na. IE/08/2012-13/HQ/G/199(Supply of Biometric Voters Registration Kits) iliyofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi*** Matokeo ya Uchunguzi yalibaini kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi haikuzingaita Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni zake za Mwaka 2013 . Matokeo ya Uchunguzi yameainishwa katika jedwali Na. 84 hapo chini

**Jedwali 84: Matokeo ya Uchunguzi wa Zabuni Na. IE/08/2012-13/HQ/G/199(Supply of Biometric Voters Registration Kits)**

| SN | Kigezo | Hoja |
|---|---|---|
| 1 | Maandalizi ya Awali | Udhaifu ulibainika katika kuandaa vigezo na mahitaji ya BVR Kits hatua iliyosababisha kutumika vigezo hafifu au visivyoeleweka |
| 2 | Mamlaka iliagiza kurudiwa kwa mchakato wa Zabuni | Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilikiuka maagizo ya Mamlaka ya kurudia mchakato wa Zabuni na kuamua kuwaalika Wazabuni sita kuja kuelezea namna BVR Kits zinavyofanya kazi. |
| 3 | Tathimini ya Uwezo na Uzoefu | Tathimini ya Uwezo na Uzoefu wa Wazabuni haikufanyika |
| 4 | Masharti ya kuleta BVR Kits. | Kamati ya Tathmini ilishindwa kubaini tofauti ya Masharti ya kuleta BVR Kits yaliyokuwemo kwenye fomu ya Zabuni na na jedwali la Mahitaji, ambapo fomu ya zabuni ilionyesha Dola za Kimarekani 119,882,407.05 (DDP) wakati jedwali la mahitaji lilionesha Dola za Kimarekani 119, 882,407.05 (CIF) Dar es Salaam. Hata hivyo, Kamati ya Tathmini ilipendekeza kutolewa kwa Zabuni bila ya kuzingatia tofauti hizo. |

| SN | Kigezo | Hoja |
|---|---|---|
| 5 | Kuidhinishwa | Taarifa ya Kamati ya Tathmini, Taarifa ya kwanza ya kikao cha Majadiliano pamoja Barua ya kukubalika kwa Zabuni zote kwa pamoja ziliidhinishwa tarehe 15/02/2014. |
| 6 | Barua ya Kupewa Kazi | Barua ya kupewa kazi kwa Mzabuni ilitolewa kabla ya Bodi ya Zabuni haijaidhinisha matokeo ya majadiliano. |
| 7 | Kifungu cha 41 cha PPA, 2011 | Baadhi ya Wafanyakazi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi walishiriki kwenye mchakato mzima wa Manunuzi kuanzia Vikao vya Tathimini, Vikao vya Bodi ya Zabuni pamoja na vikao vinane vya Kamati ya majadiliano hatua iliyosababisha mgongano wa kimaslahi. |
| 8 | Kanuni Na.220(1,2&3) Ya PPR,2013 | Kitengo cha Manunuzi kilishindwa kupitia taarifa ya Kamati ya Tathmini kabla ya kuipeleka Bodi ya Zabuni. |

***Chanzo****; Taarifa ya PPRA ya mwaka 2014/2015*

**Mapendekezo yaliyotolewa na PPRA**

Taasisi zote za Manunuzi ambazo zimepata chini ya wastani wa asilimia 75 iliyotarajiwa kufikiwa na Taasisi zote, zinatakiwa kuwapatia watumishi mafunzo ya jinsi ya kutumia Sheria, Kanuni, miongozo na mifumo iliyoandaliwa na Mamlaka. Mafunzo haya yatokane na mahitaji ya Taasisi inayohusika kutokana na mapungufu yaliyoonekana katika ukaguzi. Gharama za mafunzo hayo zitalipwa na Taasisi husika. Maafisa Masuuli wa Taasisi watakiwe kuandaa mpango kazi au mpango mkakati ndani ya miezi mitatu

ya kuwasilisha taarifa za ukaguzi inayokusudia kuhakikisha kufuata Sheria na Kanuni za Manunuzi.

Kama nilivyopendekeza katika Ukaguzi wangu uliopita, ili kuweza kushughulikia mapungufu yaliyobainika katika utekelezaji wa Mikataba ya Taasisi za Serikali Kuu, juhudi za kujenga uwezo zinatikiwa kuchukuliwa kwa pamoja kati ya Mamlaka ya Udhibiti na Manunuzi ya Umma (PPRA,), TAMISEMI, Bodi ya Usajili ya Wakandarasi pamoja na wadau wengine.Mikakati ya kujenga uwezo inatakiwa kujumuisha: kuboresha Ofisi za Wizara,Idara na Wakala wa Serikali, kuboresha Ofisi za Mkaguzi wa Ndani ili ziweze kufanya Ukaguzi wa manunuzi na mikataba, kuboresha Ofisi za Wahandisi kwa kuwapatia vifaa, wafanyakazi na magari/pikipiki; kuwajengea uwezo Wakandarasi kwa kuwapatia vifaa, ujuzi wa kiufundi na usimamazi; kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa matukio yote yenye viashiria vya ubadhirifu.

**9.1.14Mapungufu katika Manunuzi na utunzaji wa bohari/ stoo kama yalivyoanishwa kwenye taarifa ya Kurugenzi ya uhakiki Mali za Serikali**

Ikiwa ni sehemu ya majukumu yangu nimepokea taarifa ya Mhakiki Mali na kujumuisha katika taarifa yangu ya ukaguzi ya mwaka huu kama na Kanuni 239-249 ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka, 2001 ambayo inamtaka Mhakiki Mali anatakiwa kuwasilisha nakala moja ya taarifa ya uhakiki mali kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kumbukumbu zake. Mapungufu yaliyobainika katika taarifa ya Mhakiki Mali yameorodheshwa kwenye jedwali Na. 85 hapa chini.

**Jedwali 85: Mapungufu yaliyobainika katika taarifa ya Kurugenzi ya uhakiki mali za Serikali**

| S/N | Hoja | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Bakaa ya Vifaa isiyohamishwa | 62,410,665.10 |
| 2 | Manunuzi ya Vifaa vya Bohari bila kutolewa maelezo | 2,241,408,322.90 |
| 3 | Samani na Vifaa visivyoingizwa kwenye daftari la Mali. | 1,099,869,200.00 |
| 4 | Vifaa vyenye Mapungufu | 361,935,605.00 |
| 5 | Mapokezi ya Vifaa vya Bohari bila maelezo | 398,668,378.10 |
| 6 | Mafuta yasiyoingizwa kwenye daftari la kuratibu safari za gari (log books) | 545,700,889.00 |
| 7 | Mafuta yasiyoingizwa kwenye daftari la kuratibu safari za gari (log book) | 537,588,062.94 |
| 8 | Matengenezo ya Magari yasiyoidhinishwa na TEMESA | 104,699,409.64 |
| 9 | Manunuzi yaliyofanyika bila Ushindani | 276,437,567.12 |
| 10 | Vifaa vilivyopokelewa bila kuhakikiwa | 5,424,428.10 |
| 11 | Vifaa vilivyobakia kwa Mkopo | 109,731,285.00 |
| 12 | Vifaa vilivyoidhinishwa kwa ajili ya dhamana ya Mkopo | 21,713,600.00 |
| 13 | Vifaa visivyopokelewa | 192,363,001.50 |
| 14 | Ugawaji wa Vifaa bila kuingizwa katika leja ya Vifaa | 258,153,112.00 |
| 15 | Manunuzi yaliyofanyika bila idhini ya Bodi ya Zabuni | 41,946,600.00 |
| 16 | Ugawaji wa Vifaa usio na nyaraka za kutosha | 960,100,646.59 |
| 17 | Upokeaji wa Vifaa vya Bohari wenye mapungufu ya nyaraka | 919,398,718.53 |
| | **Jumla Kuu** | **8,137,549,491.52** |

**Chanzo**: Taarifa ya Kurugenzi ya uhakiki mali za Serikali ya 2014/15

Kwa maelezo zaidi kuhusu Wizara/Idara na Sektretarieti za Mikoa Zilizohusika, angalia **Kiambatisho 9.2**

Katika kupitia taarifa ya Mhakiki Mali wa Serikali nimebaini kuwa Mapungufu katika Manunuzi na utunzaji wa stoo yameongezeka kwa asilimia 8.12% ikilinganishwa na mwaka ukaguzi uliopita. Kwa ujumla Mapungufu ya stoo yenye thamani ya Sh. 7,526,447,299 yalibainika katika mwaka 2013/2014 ikilinganishwa na Sh 8,137,549,491.52 katika mwaka huu wa fedha.

Napenda kutambua mchango na juhudi kubwa zinazofanywa na Kurugenzi ya uhakiki Mali za Serikali zenye lengo la kuhakikisha Taasisi za Serikali zinazingatia matumizi bora ya Vifaa na Mali za Serikali ili kupunguza na kuepuka upotevu wa mali za Serikali.

Ninapendekeza kuwa, Maafisa Masuuli waimarishe mfumo wa udhibiti wa ndani katika Manunuzi ili vifaa na mafuta yanayonunuliwa yaweze kuingizwa kwenye vitabu vya stoo.

# Sura ya Kumi

## USIMAMIZI WA MATUMIZI

## 10.0 Utangulizi

Sura hii inafafanua masuala muhimu niliyobaini wakati wa ukaguzi wa matumizi ya Wizara, Idara, Balozi na Sekretarieti za Mkoa (RSs) katika mwaka wa fedha 2014-15. Masuala hayo ni kama ifuatavyo:

## 10.1 Mambo muhumu yaliyojitokeza kwenye Ukaguzi wa usimamuzu wa matumizi

### 1.1.1 Hati za malipo zenye nyaraka pungufu -SH. 11,314,507,724

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, nimebaini kwamba, Wizara 17, Balozi 2 na Sekretarieti za Mikoa 11 zilifanya malipo yenye jumla ya Shilingi 11,314,507,724 (**angalia Kiambatisho 10.1**) ambayo yalikuwa na nyaraka pungufu kinyume na Kanuni 86 (1) ya Kanuni za Fedha, 2001 pia Kanuni 95 (4) & 18 (f) ya Kanuni za Fedha, 2001. Nyaraka za viambatisho zikikosekana inakuwa vigumu kuthibitisha pasipo shaka uhalali wa malipo hayo hivyo kufanya mawanda ya ukaguzi kuwa finyu..

Muhtasari wa miaka mitano (5) wa mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu ni kama inavyoonekana katika **Kielelezo** hapa chini:

**Kielelezo 19: Mwenendo wa malipo yaliyo na nyaraka pungufu**




***Chanzo:Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali***

kutokana na kielezo hapo juu, inaonesha kuwa kwa mwaka huu wa fedha kiasi cha malipo yaliyo na nyaraka pungufu kimeongezeka kufikia Shilingi 11.26bil kutoka Shilingi 7.15bil kwa mwaka uliopita, wakati huo huo Taasisi zilizohusika na tatizo hili pia zimeongezeka kutoka 27 mwaka jana hadi 30 kwa mwaka huu. Hii inamaanisha kuwa mfumo wa udhibiti wa ndani kwa kiasi fulani umezorota.

Ninashauri kuwa Maafisa Masuuli wa Taasisi zinanazohusika kuendelea kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani hasa kitengo cha ukaguzi wa nyaraka kabla na baada ya malipo.

### 10.1.2 Kukosekana kwa hati za malipo Sh. 361,793,870

Katika mwaka huu, Taasisi takriban sita za Wizara, Idara, na Sekretarieti za Mikoa zilishindwa kuwasilisha hati za malipo na nyaraka zake za kiasi cha Sh. 361,793,870 kinyume na Kanuni. Na.86 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya Mwaka 2001.

Kutokana na kukosekana kwa hati za malipo na viambatisho vyake, ilipelekea kutoweza kubaini uhalali, uhalisia, aina na madhumuni ya matumizi hayo. Jedwali lifuatalo linaonesha hati za malipo zilizokosekana kwa kila fungu:

**Jedwali 86: Taasisi zenye malipo yasiyo na hati za malipo**

| Na. | Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 94 | Tume ya Utumishi | 34,019,152 |
| 2 | 52 | Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii | 49,720,390 |
| 3 | 48 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 56,190,000 |
| 4 | 61 | Tume ya Uchaguzi (NEC) | 194,072,150 |
| 5 | 76 | Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi | 7,200,000 |
| 6 | 71 | Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani | 20,592,178 |
| | | **Jumla** | **361,793,870** |

***Chanzo:Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali***

Mwenendo kwa kipindi cha miaka mitano (5) wa matokeo ya malipo yasiyokuwa na viambatisho vya kutosha yameainishwa hapa chini kwa ulinganisho:

**Kielelezo 20: Chati ikionesha mwenendo wa matumizi yaliyokosa hati za malipo kwa miaka mitano**




***Chanzo:Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali***

Kutokana na kielelezo hapo juu, mwenendo unaonesha kuwa tatizo la hati za malipo kukosekana limeongezeka kwa mwaka 2014/2015 (Sh. 361.8mil) ikilinganishwa na mwaka jana 2013/2014 (Sh. 125.163mil), pia idadi ya Taasisi zimeongezeka kufikia 6 mwaka huu kutoka Taasisi 4 mwaka jana.

Kwa mujibu wa Kanuni 18(f) ya Kanuni za Fedha, 2001 kukosekana kwa hati za malipo ni sawa na hasara ya upotevu wa fedha, hivyo nashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi husika kuchukua hatua stahiki kwa waliohusika.

### 10.1.3 Kukosekana kwa Stakabadhi za mashine za kielektronici (EFD)- Sh. 6,185,012,346

Katika mwaka huu mwa fedha 2014/2015, baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilifanya malipo ya kiasi cha Sh. Bilioni 6.185 bila Taasisi husika kuambatisha Stakabadhi za kieletroniki (EFD) kinyume na Kanuni 28(1) ya Kanuni za Sheria ya Kodi ya Mapato (Mashine za Stakabadhi za Kielektroniki) ya mwaka 2012.

Aidha, kwa kutokudai Stakabadhi hizo za kielektroniki kunamaanisha kuwa Taasisi hizo za Serikali zinawasaidia wafanyabiashara kukwepa kodi na hivyo kuisababishia Serikali hasara kwa kupoteza sehemu kubwa ya mapato ya kodi kila mwaka.

Katika kipindi cha mwaka 2014/15, nimebaini Sekretarieti 8 za Mikoa na Wizara 18 zilifanya malipo ya kiasi cha Sh. 6,185,012,346 bila kuambatisha Stakabadhi za kielekroniki kutoka kwa wauzaji mbalimbali kama **kielelezo** kifuatacho linavyoonesha kwa muhtasari hapa chini:

**Kielelezo 21: Kukosekana kwa EFD Stakabadhi kwa miaka mitatu**




Kwa mujibu wa kielelezo hapo juu, inaonyesha kwamba, malipo yaliyokosa Stakabadhi za kielektroniki kwa mwaka huu 2014/15 yameongezeka kutoka Sh. Bilioni 4.1 mpaka Sh. Bilioni 6.19 sawa na ongezeko la Sh. Bilioni 2.09 sawa na asilimia 51.

Nashauri Serikali iendelee kutoa elimu juu ya utekelezaji wa hiari kuzingatia Kanuni za Sheria ya Kodi ya Mapato (Electronic Fiscal Devices) za mwaka, 2012 kuhusu matumizi ya hiari ya mashine za EFD ambazo zitachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato ya Serikali kama kila Manunuzi ya Serikali yataambatana na Stakabadhi.

Pia, ninapendekeza kwamba, Serikali isiendelee kufanya biashara na Wazabuni ambao hawatumii mashine EFD na kutoa Stakabadhi za kielektroniki.

### 10.1.4 Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili-Sh. 887,012,294

Katika kipindi cha mwaka wa ukaguzi, nimebaini kuwa, baadhi ya Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa zilifanya malipo ya kiasi cha Sh. 887,012,294 yalilipiwa kwa kutumia

vifungu vya matumizi visivyostahili bila idhini ya Mamlaka stahiki, hii ni kinyume na Kanuni 51 (1-8) Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali 87** hapo chini:

**Jedwali 87: Orodha ya Taasisi zilizolipa katika vifungu vya bajeti visivyostahili**

| Na. | Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 12 | Tume ya Sheria | 39,890,000 |
| 2 | 38 | Ulinzi | 86,564,355 |
| 3 | 25 | Ofisi ya Waziri Mkuu-Ofisi binafsi | 2,784,800 |
| 4 | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 255,834,855 |
| 5 | 48 | Ministry of Land and Human Settlement | 33,406,000 |
| 6 | 72 | Sekretarieti ya Mkoa-Dodoma | 30,085,412 |
| 7 | 63 | Sekretarieti ya Mkoa-Geita | 6,388,757 |
| 8 | 74 | Sekretarieti ya Mkoa-Kigoma | 32,344,246 |
| 9 | 86 | Sekretarieti ya Mkoa-Tanga | 12,580,666 |
| 10 | 85 | Sekretarieti ya Mkoa-Tabora | 372,973,203 |
| 11 | 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 9,935,000 |
| 12 | 71 | Sekretarieti ya Mkoa-Pwani | 4,225,000 |
| | | **Jumla** | **887,012,294** |

***Chanzo:Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali***

Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili ni matumizi ambayo yanaweza kuathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa. Mwenendo wa matumizi hayo kwa miaka sita ni kama inavyoonekana hapa chini:

**Kielelezo 22: Malipo katika vifungu vya bajeti visivyostahili**




| | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiasi (Sh. Bilioni) | 436.398 | 806.437 | 154.175 | 291.532 | 232.695 |
| Idadi ya Taasisi | 8 | 4 | 9 | 11 | 3 |

Kwa ujumla kwa ya kipindi cha miaka minne iliyopita malipo ya matumizi nje ya vifungu vya bajeti iliyoidhinishwa yamekuwa yakipungua, hata hivyo ninashauri Maafisa Masuuli katika siku zijazo kujiepusha na kufanya matumizi nje ya vifungu vya bajeti iliyoidhinishwa. Endapo italazimu, basi nashauri uhamisho wa fedha kutoka fungu moja kwenda lingine upate idhini ya Mamlaka husika kwa mujibu wa Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001.

### 10.1.5 Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa-Sh. 1,298,373,921

Katika ukaguzi wa hesabu za mwaka huu, nimebaini kwamba, Balozi 9, Wizara 2 na Sekretarieti 2 za mikoa zimelipa kiasi cha Sh. 1,298,373,921 kwa matumizi mbalimbali ambayo yalikua nje ya bajeti iliyoidhinishwa bila kutafuta idhini au kibali kinyume na Kanuni 46 (3) ya Kanuni za Fedha za Umma ya Mwaka 2001 (Iliyorejewa 2004). Hii ina maana kwamba, baadhi ya shughuli zilizopangwa hazikuweza kutekelezwa kama zilivyoidhinishwa kwenye bajeti.

Aidha, katika Jumla ya matumizi hayo, kiasi cha Sh. 147,662,326 kilikuwa matumizi nje ya bajeti na Sh. 1,150,711,595 kilikuwa ni matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kama jedwali linavyoonesha hapa chini:

**Jedwali 88: Taasisi zilizofanya malipo nje ya bajeti iliyoidhinishwa**

| Na. | Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | Kasma 2025 | Ubalozi wa Tanzania-Pretoria, Afrika ya Kusini | 27,813,874 | Matumizi nje ya bajeti |
| | 48 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 5,000,000 | Matumizi nje ya bajeti |
| | Kasma 2001 | Ubalozi wa Tanzania-Addis Ababa, Ethiopia | 103,494,252 | Matumizi nje ya bajeti |
| | 83 | Sekretarieti ya Mkoa -Shinyanga | 11,354,200 | Matumizi nje ya bajeti |
| | | **Jumla Ndogo** | **147,662,326** | |
| | Kasma 2025 | Ubalozi wa Tanzania-Pretoria, Afrika ya Kusini | 200,726,900 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |
| | Kasma 2008 | Ubalozi wa Tanzania-Maputo, Msumbiji | 146,847,102 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |
| | Kasma 2034 | Ubalozi wa Tanzania-Moroni, Comoro | 374,890,135 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |
| | 37 | Ofisi ya Waziri Mkuu | 15,165,515 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |
| | Kasma 2030 | Ubalozi wa Tanzania-Lilongwe | 42,902,594 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |
| | Kasma 2014 | Ubalozi wa Tanzania-Beijing, China | 109,448,872 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |
| | Kasma 2009 | Ubalozi wa Tanzania-Moscow, Urusi | 97,557,289 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |

| Na. | Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | Kasma 2015 | Ubalozi wa Tanzania-Rome, Italia | 154,733,188 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |
| | 76 | Sekretarieti ya Mkoa -Lindi | 8,440,000 | Matumizi zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa |
| | | **Jumla Ndogo** | **1,150,711,595** | |
| | | **Jumla Kuu** | **1,298,373,921** | |

***Chanzo:*** *Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali*

Mwenendo wa malipo yaliyofanyika nje ya bajeti iliyoidhinishwa kwa miaka minne ni kama inavyoonesha katika Kielelezo hapa chini:

**Kielelezo 23: Mwenendo wa matumizi yaliyofanyika bila idhini**




Uchambuzi kutokana na kielelezo hapo juu, unaonesha kwamba, idadi ya Wizara/Idara na Sekretarieti za mikoa zilizofanya malipo nje ya bajeti kwa mwaka huu zimepungua kutoka 21 kwa mwaka 2013/14 hadi 13 kwa mwaka huu 2014/15.

Hii inaonyesha kwamba, kuna uboreshaji katika udhibiti wa kufanya matumizi kwa kuzingatia bajeti. Hata hivyo, bado ipo nafasi ya kuboresha zaidi ili kuhakikisha kwamba, bajeti inaandaliwa na inafuatwa ipasavyo.

### 10.1.6 Masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa-Sh. 232,695,369

Katika mwaka huu wa fedha Wizara mbili (2) na Sekretarieti ya Mkoa moja (1) zililipa masurufu kiasi cha Sh. 232,695,369 ambayo hayakurejeshwa kwa mda mrefu baada ya shughuli iliyokusudiwa kukamilika kinyume na Kanuni 103 ya Kanuni za Fedha za Umma ya Mwaka 2001.

Masurufu yasiyorejesha kwa wakati yanaweza kutumika kwa matumizi yasiyokusudiwa. Wizara na Sekretarieti za mikoa zilizohusika ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

**Jedwali 89: Taasisi zenye masurufu ya muda mrefu**

| Na. | Fungu na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 85 | Sekretarieti ya Mkoa-Tabora | 2,457,103 |
| 2 | 32 | Ofisi ya Rais-UTUMISHI | 118,251,957 |
| 3 | 43 | Wizara ya Kilimo, Chakula na Maendeleo ya Ushirika | 111,986,309 |
| | | **Jumla** | **232,695,369** |

*Chanzo: Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali*

Mwenendo wa miaka mitano wa masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa ni kama inavyoonekana katika **kielelezo** hapa chini:

**Kielelezo 24: Mwenendo wa Masurufu yasiyorejeshwa**




| Mwaka wa Fedha | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kiasi (Sh. mil) | 436.398 | 806.437 | 154.175 | 291.532 | 232.695 |
| Idadi ya Taasisi | 8 | 4 | 9 | 11 | 3 |

Mwenendo wa masurufu yaliyokaa muda mrefu bila kurejeshwa ikilinganishwa na mwaka jana, inaonyesha tatizo kupungua kutoka Sh. 291.532mil mpaka Sh. 232.695, ikiwa ni pungufu kwa 20%, wakati huo huo Idadi ya Wizara/Sekretarieti za mikoa zilizohusika zimepungua kutoka 11 hadi 3.

Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba, Wizara/ Sekretarieti za Mikoa ziendelee kuhakikisha kwamba, masurufu yanarejeshwa mara tu baada ya kukamilika kwa shughuli iliyokusudiwa kwa kipindi kisichozidi siku kumi na nne vinginevyo, marejesho ya masurufu yafanywe kupitia makato kwenye mshahara wa mdaiwa wa masurufu hayo kwa mujibu wa Kanuni 103(2) ya Kanuni za Fedha, za Umma za 2001.

### 10.1.7 Malipo yaliyolipwa zaidi ya kiwango stahiki-Sh. 373,842,446

Wakati wa ukaguzi wa mwaka huu, nilibaini malipo ya kiasi cha Sh. 373,842,446 yaliyolipwa zaidi ya kiwango stahiki yakihusisha Wizara moja (1), Balozi moja (1) na Sekretarieti nne (4) za Mikoa. Fedha zilizolipwa zaidi ya kiasi kinachostahili au kwa kazi ambazo hazijafanyika kunapelekea kutofanikisha kwa

shughuli zingine zenye manufaa kwa Umma.Malipo zaidi ya kiasi kilichostahili ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapa chini:

**Jedwali 90: Taasisi zilizolipa malipo zaidi ya stahiki**

| Na. | Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 57 | Wizara ya Ulinzi | 226,132,130 |
| 2 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa-Arusha | 20,858,977 |
| 3 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa-Arusha | 9,100,000 |
| 4 | 86 | Sekretarieti ya Mkoa-Tanga | 97,104,247 |
| 5 | Kasma 2014 | Ubalozi wa Tanzania-Beijing, China | 15,677,092 |
| 6 | 76 | Sekretarieti ya Mkoa-Lindi | 4,970,000 |
| | | **Jumla** | **373,842,446** |

***Chanzo: Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali***

Mwenendo wa miaka mitano (5) wa malipo zaidi ya kiwango stahiki ni kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo** hapa chini:

**Kielelezo 25: Mwenendo wa miaka mitano (5) wa malipo zaidi ya Stahiki**




Mwenendo wa malipo zaidi ya kiwango stahiki unaonesha kwa mwaka huu kiwango kimeshuka mpaka Sh. Milioni 373.842 ikilinganishwa na Sh. Milioni

440.721 za Mwaka jana. Nashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi zilizohusika kufuatilia urejeshwaji wa malipo hayo yaliyolipwa zaidi ya kiwango.

### 10.1.8 Matumizi yasiyokuwa na manufaa - Sh. 53,017,013,737

Mapitio ya matumizi na malipo mengine yanaonesha kuwa Wizara/Idara sita (6) na Sekretarieti za Mikoa mbili (2) zilifanya malipo kiasi cha Sh. 53,017,013,737 ambayo yalifujwa na hayakuwa na manufaa yeyote kwa Serikali ambapo hasara hiyo ingeepukwa laiti maamuzi yangefanywa kwa umakini kama inavyoanisha Kanuni 21 ya Kanuni za Fedha, 2001.

Orodha ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa zilizohusika na aina ya malipo yaliyofanyika kama inavyoonesha katika Jedwali hapa chini:

**Jedwali 91: Taasisi zilizohusika na matumizi yasiyo na manufaa kwa miaka miwili**

| Na. | Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Aina ya Matumizi |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 2,172,547 | Tozo kutokana na kucheleweshа kulipa kodi kwa zaidi ya wastani wa miezi 14 |
| 2 | 38 | Ulinzi | 5,666,975 | malipo ya adhabu ya kuhifadhi shehena bandarini kutokana na kuchelewesha taratibu za forodha |
| 3 | 52 | Ministry of Health and Social Welfare | 3,355,981 | Payment of electricity and water bills to the staff who are not entitled to |
| 4 | 98 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 44,651,190 | Riba iliyotozwa kwa kuchelewesha malipo ya kukodisha ofisi |
| 5 | 48 | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 109,722,539 | Hasara ya Sh. Milion 109.7 kutokana na Ununuzi wa gari aina ya Toyota Land Cruiser VX V8 iliyogharimu Sh. Milioni 297.5 kutoka Toyota (T) Ltd badala ya Sh. 187.8 |
| 6 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa-Arusha | 15,000,000 | Malipo ya huduma za kiufundi za mfumo wa komputa ilihali haufanyi kazi |
| 7 | 85 | Sekretarieti ya Mkoa-Tabora | 9,925,000 | Posho ya kujikimu iliyolipwa kwa idadi ya siku ambazo muhusika hakuzifanyia kazi |
| 8 | 22 | Deni la Taifa | 52,826,519,506 | Tozo ya kuchelewesha malipo ya deni |
| | | **Jumla** | **53,017,013,737** | |

***Chanzo:*** *Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali*

**Kielelezo 26: Mwenendo wa miaka mitatu (3) wa malipo yasiyokuwa na manufaa**




Ulinganisho hapo juu unaonesha ongezeko kubwa la malipo ya kiasi cha Sh. Bilioni 53.017 cha matumizi yasiyokuwa na manufaa kwa mwaka 2014/2015 ikilinganishwa na Sh. Bilioni 1.699 kwa mwaka uliopita licha ya idadi ya Taasisi zilizohusika kupungua kutoka 12 hadi 8. Ninapendekeza kuwa Manejimenti za Wizara husika & Sekretarieti za Mikoa waimarishe mifumo yao ya udhibiti wa ndani kukabili changamoto hii.

### 10.1.9 Fedha kutumika kwa shughuli zisizokusudiwa -Sh. 1,788,881,933

Katika ukaguzi nilioufanya, nimebaini baadhi ya Wizara/Idara na Sekretarieti za Mikoa ambazo zimefanya malipo kwa shughuli zisizokuwemo katika bajeti iliyoidhiniswa. Jumla ya kiasi cha Sh. 1,788,881,933 kama ilivyoanishwa kwenye **Kiambatisho 10.3** hakikulipwa kwa shughuli zilizokusudiwa kinyume na Kanuni Na. 115 ya Kanuni za Fedha, 2001 ambayo inahitaji fedha zilizo katika bajeti kutumika tu kwa malengo yaliyokusudiwa, vinginevyo inaweza kusababisha matumizi mabaya ya fedha hizo na

kufanya malengo yaliyokusudiwa yasifikiwe. Mchanganuo wa malipo yaliyolipwa kwa matumizi yasiyokusudiwa kwa mwaka huu ikilinganishwa na mwaka jana ni kama inavyoonesha kwenye Jedwali hapa chini:

**Kielelezo 27: Ulinganifu wa malipo yasiyokusudiwa kwa miaka mitatu:**




Kutoka kwenye kielelezo hapo juu, inaonesha kuwa malipo kwa kwa shughuli zisizokusudiwa yameongezeka kwa kiasi cha Sh. Milioni 225.935 sawa na asilimia 14 ikilinganishwa na mwaka jana 2013/14.
Hata hivyo, Ili kuhakikisha kwamba, fedha zote kama zilivyoidhinishwa na Bunge zinatumika kwa matumizi yaliyokusudiwa pekee na kwa mujibu wa Sheria, ninashauri Menejimenti ya Taasisi zilizokaguliwa kuimarisha mfumo wa udhibiti wa matumizi kwa mujibu wa bajeti kuanzia maandalizi yake mpaka utekelezaji wake, ukiukwaji wowote utambuliwe na ushughulikiwe ipasavyo.

Hata hivyo, ili shughuli zilizokuwa zimepangwa zifanyike, ninapendekeza kwamba, fedha zote zilizotumika kwa ajili ya shughuli zisizotarajiwa

zirejeshwe na kutumika kwa malengo yayokusudiwa na kuidhinishwa na bunge.

### 10.1.10 Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za mapokezi Sh. 220,053,699

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nimebaini malipo ya kiasi cha Sh. 220,053,699 yalifanya na Wizara/Idara tatu (3) za Serikali kwenda kwa walipwaji anuai bila kudai stakabadhi za kukiri mapokezi.

Aidha, kwa kukosekana Stakabadhi za mapokezi imeshindikana kuthibitisha kuwa malipo haya yalipokelewa na mlipwaji sahihi kinyume na Kanuni 95(4) ya Kanuni za Fedha za Umma ya Mwaka 2001. Taasisi zilizohusika katika malipo haya ni kama inavyoonesha kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali 92: Taasisi zilizofanya malipo yasiyokuwa na Stakabadhi za mapokezi**

| Na. | Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 38 | Ulinzi | 90,581,698 |
| 2 | 42 | Ofisi ya Bunge | 27,836,074 |
| 3 | 43 | Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika | 101,635,927 |
| | | **Jumla** | **220,053,699** |

***Chanzo***: *Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali*

**Ulinganishi baina ya mwaka jana**

| Mwaka wa Fedha | 2013/14 | 2014/15 |
|---|---|---|
| Kiasi (Sh. Bil.) | 27.74 | 0.22 |
| Idadi ya Taasisi | 5 | 3 |

Ulinganishi hapo juu unaonesha kwamba, idadi ya Taasisi zenye malipo yasiyoambatishwa na stakabadhi za kukiri mapokezi zimepungua

kutoka tano (5) hadi tatu (3) pia ikihusisha kiasi kikipungua kutoka Bilioni 27.7 hadi Sh. Milioni 220.054.

Kuendelea kuwapo kwa tatizo hili kunaonesha uwepo wa udhaifu katika udhibiti wa ndani. Nazikumbusha Menejimenti za Taasisi husika kuzingatia wajibu wao wa msingi wa kuhakikisha malipo yao yote yanaambatishwa na stakabadhi za kukiri mapokezi.

### 10.1.11 Watoa huduma kutokata Kodi ya Zuio-Sh. 692,539,424

Katika ukaguzi wangu nimebaini ukiukwaji wa matakwa ya Kifungu 83(1)(b) cha Sheria ya Kodi ya Mapato (Iliyorejewa 2008) kinachowataka walipaji wa huduma kuwakata watoa huduma wakaazi na wasio-wakaazi katika malipo yao kodi ya zuio ya 5% na 15% halkadhalika ikitokea wametoa huduma ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Hata hivyo, mapitio ya hati za malipo kwa mwaka wa fedha 2014/15 nilibaini Kodi ya Zuio kiasi cha Sh. 692,539,424 haikukatwa kama jedwali hapa chini linavyoonesha. Ukiukwaji huu unapelekea kuinyima Serikali mapato kwa ajili ya utoaji huduma na kuwaletea maendeleo Wananchi.

**Jedwali 93: Taasisi ambazo hazikuwakata watoa huduma kodi ya zuio**

| Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 6 | Ofisi ya Rais -Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi ya Kipaumbele | 14,526,217 | Kodi ya Zuio haikukatwa |
| 28 | Idara ya Polisi | 626,635,374 | Kodi ya Zuio haikukatwa |
| 9 | Bodi ya Mishahara | 16,658,175.06 | Kodi ya Zuio haikukatwa |

| Fungu Na. | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 56 | Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa | 25,598,065 | Kodi ya Zuio Sh. 19,497,404 Haikukatwa, Sh. 6,100,662 ya Kodi ya Zuio haikuwasiliwa TRA |
| 54 | Sekretarieti ya Mkoa-Njombe | 6,583,166 | Kodi ya Zuio haikukatwa |
| 75 | Sekretarieti ya Mkoa-Kilimanjaro | 2,538,427 | Kodi ya Zuio haikuwasilishwa TRA |
| | **Jumla** | **692,539,424** | |

***Chanzo:*** *Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali*

Ninazikumbusha Menejiment za Taasisi zinazohusika kuhakikisha zinatekeleza matakwa ya kiSheria (Kifungu 83(1)(b) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, 2004 (Iliyorejewa 2008)) yanayowataka kuwakata watoa huduma Kodi ya Zuio wanapolipia huduma walizonunua.

## Sura ya Kumi na Moja

## USIMAMIZI WA MALI NA MADENI

### 11.0 Utangulizi

Sehemu hii ya ripoti inatoa muhtasari wa matokeo muhimu ya ukaguzi na mapendekezo husika kutokana na ukaguzi wa usimamizi mali na madeni kwa mwaka 2014/15.

### 11.1 Mambo muhimu yaliyojitekeza kwenye ukaguzi wa mali na madeni

#### 11.1.1 Ukaguzi wa Usimamizi wa Mali

Serikali ina sera rasmi na taratibu zake ili kuhakikisha udhibiti na usimamizi kuhusiana na kurekodi, matumizi, kuthamini, kuripoti na kutunza mali za Umma. Ukaguzi wa usimamizi mali kwa mwaka 2014/15 ulijikita katika mapitio ya kuwapo kwa uwajibikaji katika matumizi ya mali za Umma. Pia, tumekagua na kuhakiki kwamba, Maafisa Masuuli wanaendelea kutumia Viwango vya Kimataifa Vya uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na wanatekeleza kwa ufanisi na kusimamia raslimali za Umma.

Ufuatao ni muhtasari wa mapungufu yaliyoonekana wakati wa ukaguzi wa usimamizi mali katika Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kwa mwaka huu:-

#### 11.1.2 Uzingatiaji wa viwango vya Kimataifa katika kuripoti Mali za Kudumu kwenye vitabu vya hesabu

Serikali Kuu ilianza kuandaa Taarifa za Fedha kuzingatia viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma kuanzia tarehe 1/7/2012 na kufanikiwa kuandaa Taarifa za Fedha zinazozingatia viwango kwanza

katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30/6/2013. Katika kuandaa Taarifa za Fedha kwa kuzingatia viwango vya kimataifa, viwango vinaruhusu Taasisi kuwa na kipindi cha mpito cha miaka mitano ili kutekeleza matakwa yote yaliyopo katika kuripoti Mali za Kudumu za Umma, ambapo Serikali imetumia ruhusa hiyo itakayoishia 30/6/2017.

Mapungufu yaliyoonekana katika kutekeleza mpango maalum wa kufikia kutoa taarifa za Mali za Kudumu za Umma kwa viwango vya kimataifa unaoishia tarehe 30/6/2017 ni kama ifuatavyo:-

a) **Kuwapo kwa Rejista ya Mali za Kudumu isiyo timilifu**
Uandaaji na ukamilishaji wa Rejista ya Mali za Kudumu za Umma katika Wizara, Taasisi pamoja na Sekretarieti za Mikoa unatofautiana. Pia, nilibaini baadhi ya Rejista hazina taarifa za umuhimu kama vile tarehe ya manunuzi, tarehe ilipoanza kutumika, na aina ya mali. Vile vile, nilibaini kuwapo kwaTaasisi zipatazo 53 ambazo hazijaanza kuainisha Mali za Kudumu walizonazo ili kutengeneza Rejista iliyotimilifu. (**Kiambatisho Na.11.1**)

b) **Kuchelewa kukamilisha kuthamini Mali za Kudumu**
Ukizingatia muda uliobaki wa miaka miwili kufikia mwisho wa kipindi cha mpito tarehe 30/7/2017, niliangalia mpango maalumu wa kutekeleza matakwa yote ya mfumo wa viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma na kubaini ucheleweshwaji katika kuzitambua na kuthaminisha Mali za Kudumu. Ucheleweshwaji huu utakuwa ni kikwazo

kikubwa katika kufikia malengo ambayo Serikali ilijiwekea ya kuandaa Taarifa za Fedha kwa kuzingatia viwango vyote vya kimataifa kwa kipindi kilichobaki.

c) **Ukosefu wa Sera ya kiuhasibu ya kusimamia Mali za Kudumu**
Nimebaini kuwa hakuna sera ya kiuhasibu ya kusimamia namna ya kutoa taarifa ya Mali za Kudumu, hivyo, kusababisha kuwapo kwa taratibu tofauti za kiuhasibu zinazotumiwa na Taasisi za Umma katika kuandaa Rejista ya Mali za Kudumu. Kutokuwapo kwa sera kutasababisha kutofanikiwa katika kuandaa Taarifa za Fedha za pamoja kuhusu Mali za Kudumu kwa kuzingatia viwango vyote vya kimataifa. Vile vile, nilishindwa kuthibitisha kuwa mfumo wa komputa (Epicor ) uliopo unaweza kuwezesha uandaaji wa taarifa za Mali za Kudumu kwa kuzingatia mfumo mpya wa uandaaji wa Taarifa za Fedha.

d) **Mfumo wa kompyuta wa Mali za Kudumu haujatumika**
Nilibaini kwamba, hakuna uthibitisho wa mfumo uliopo wa kompyuta katika kuandaa hesabu na Mali za Kudumu ukifanya kazi kwa Viwango vya Kimataifa wa uhasibu katika Sekta ya Umma kama vile aina ya Mali za Kudumu, kiasi cha uchakavu, na jinsi ya kukokotoa, na tarehe ya manunuzi. Aidha, hakuna mafunzo yaliyofanyika kwa watumishi ili kuwajengea uwezo katika matumizi ya mfumo wa kompyuta.

e) **Kutotenganisha thamani ya Ardhi na Majengo katika Taarifa za Fedha**
Aya ya 17(74) ya Viwango vya Kimataifa

vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) vinahitaji kutoa taarifa inayotenganisha thamani ya Jengo na Ardhi kwa sababu ardhi haina mwisho wa matumizi wakati jengo lina mwisho wa matumizi.

Kama nilivyoripoti kwenye taarifa zangu za miaka iliyopita kuwa bado Taasisi za Umma zinachanganya Ardhi na Majengo kinyume na aya ya 17(74) ya Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa hesabu katika Sekta za Umma kama inavyoelekeza. Jedwali **Na 94** hapo chini linaonyesha orodha ya Taasisi husika.

**Jedwali 94: Taasisi ambazo zinachanganya thamani ya Ardhi na Majengo.**

| Fungu | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 14 | Idara ya Zimamoto na Uokoaji |
| 20 | Ikulu |
| 26 | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| 30 | Ofisi ya Raisi-Sekretariet ya Baraza la Mawaziri |
| 31 | Ofisi ya Makamu wa Rais |
| 47 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu |
| 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani |
| 88 | Sekretarieti ya Mkoa wa Dar es salaam |
| 2019 | Ubalozi wa Tanzania Brussels |
| 2020 | Ubalozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa Geneva |
| 2033 | Ubalozi wa Tanzania Hague |
| 2014 | Ubalozi wa Tanzania China |

Katika kuzingatia mfumo mpya wa kuandaa Taarifa za Hesabu za kifedha katika Sekta ya Umma, Serikali Kuu inatakiwa kutathimini mwenendo wa utekelezaji wa matakwa ya vigezo vya kimataifa katika kutoa taarifa za Mali za Kudumu huku ikihakikisha kuwa Mali za Umma zinatumika na kutunzwa kikamilifu ili kuleta tija iliyokusudiwa. Katika kufanikisha haya, napendekeza Afisa

Masuuli pamoja na Wizara ya Fedha kufanya yafuatayo:

i. Wahakikishe kuwa taarifa za Mali za Kudumu zinakuwa sahihi na timilifu katika Taasisi zote Serikali

ii. Wahakikishe kuwa mali zote ambazo thamani zake hazijulikani zinafanyiwa uthamini na kuharakisha kufanya uhakiki wa mali zilizopo ili kuhakikisha Mali za Kudumu kwenye Taarifa za Fedha zinakuwa timilifu na sahihi

iii. Serikali waanzishe mfumo wa ufuatiliaji katika kuhakikisha kuwa maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Fedha yanatelekezwa na Taasisi zote ili kufikia malengo yaliyokusudiwa

iv. Watengeneze sera maalumu ya kihasibu kuhusu Mali za Kudumu itakayotumika katika Taasisi zote ili kuhakikisha kuwa kunakuwapo na uhalali katika kuripoti Mali za Kudumu kwenye Taarifa za Fedha.

v. Wahakikishe kuwa mfumo wa kompyuta Epicor unaotumika kuandaa Taarifa za Fedha na unakidhi mahitaji ya kuandaa taarifa za Mali za Kudumu kulingana na matakwa ya viwango vya kimataifa, pia watumishi wajengewe uwezo kwa njia ya mafunzo katika kutumia mfumo wa kompyuta.

### 11.1.3 Magari na Mali za Kudumu ambazo hazitumiki kwa muda mrefu

Ikiwa ni sehemu ya ukaguzi, nilifanya uhakiki wa Mali za Kudumu katika sampuli zilizochaguliwa za Sekretarieti za Mikoa, Wizara na Balozi. Nilibaini magari 675 na vifaa vingine 273 ambavyo vimefikia ukomo wake wa matumizi na Maafisa Masuuli bado hawajafanya taratibu za kuziondoa kwa mujibu wa Kanuni Na. 254 (1) ya Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2001. Mali hizi zinachukua nafasi katika Majengo ya Taasisi husika kwa muda mrefu **(Kiambatisho Na. 11.2)**

Kwa kuwa kuna uwezekano wa Serikali kupata hasara ya mali kutokana na wizi wa vifaa au kutelekezwa, ninapendekeza kwamba, Serikali kupitia Wizara ya Fedha, itoe mwongozo/ maelekezo mahsusi kwa Taasisi zote kuhusu taratibu za kuziondoa Mali za Umma zilizomaliza muda wake wa matumizi.

### 11.1.4 Ukarabati wa Majengo ya Serikali na uendelezwaji wa Viwanja vya Serikali katika Balozi za Tanzania nje ya Nchi.

Serikali inamiliki majengo na viwanja katika Balozi za Tanzania nje ya nchi. Ukaguzi wa mwaka 2014/15 katika Balozi za Tanzania nje ya nchi ulibaini Balozi nane (8) kuwa na majengo mabovu ambayo yanahitaji matengenezo makubwa. Pia, ukaguzi ulibaini kuwapo kwa viwanja vinne (4) ambayo havijaendelezwa kwa muda mrefu. Kwa mfano, kiwanja kilichopo Abuja Nigeria hakijaendelezwa kwa zaidi ya miaka 30 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na.11.3.**
Kwa kipindi kirefu Balozi zetu hazijatengewa fedha za maendeleo kwa ajili ya kujenga majengo mapya na kukarabati majengo yaliyopo.

Napendekeza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuweka kwenye bajeti ya maendeleo gharama za matengenezo na ujenzi wa nyumba za Serikali nchi za nje ili kuwa na heshima na taswira nzuri ya Taifa letu.

### 11.1.5 Balozi kutotumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha

Taasisi za Umma ikijumuisha Balozi za Tanzania nje ya nchi wanatakiwa kutumia mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha uitwao IFMS kwa kutumia mfumo wa kompyuta (Epicor). Katika sampuli ya Balozi nilizokagua na kufanya mapitio ya mfumo

wa malipo pamoja na uandaaji wa Taarifa za Fedha, nilibaini kuwa Balozi zote zilizokaguliwa hazitumii mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha. Jedwali Na.95 hapa chini linaonyesha orodha ya Balozi hizo

**Jedwali 95: Balozi ambazo zimeonekana kutotumia Mfumo Funganifu wa Usimamizi wa Fedha**

| Na | Fungu | Jina |
|---|---|---|
| 1 | 2003 | Ubalozi wa Tanzania Cairo |
| 2 | 2017 | Ubalozi wa Tanzania Tokyo |
| 3 | 2022 | Ubalozi wa Tanzania Harare |
| 4 | 2005 | Ubalozi wa Tanzania Abuja |
| 5 | 2019 | Ubalozi wa Tanzania Brussels |
| 6 | 2020 | Ubalozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa Geneva |
| 7 | 2028 | Ubalozi wa Tanzania Bujumbura, Burundi |
| 8 | 2026 | Ubalozi wa Tanzania Kigali |
| 9 | 2023 | Ubalozi wa Tanzania Nairobi |
| 10 | 2020 | Ubalozi wa Tanzania Hague |
| 11 | 2001 | Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa |
| 12 | 2014 | Ubalozi wa Tanzania Beijing - China |
| 13 | 2006 | Ubalozi wa Tanzania London |

Mhasibu Mkuu wa Serikali aziwezeshe Balozi zote ziwe zinatumia mfumo funganifu wa usimamizi wa fedha ili kuwezesha kuwapo na usimamizi wa fedha uliokusudiwa; pia kuwa na taratibu za kuandaa Taarifa za Fedha zinazofanana katika Taasisi za Umma.

### 11.1.6 Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuingizwa katika Leja ya Vifaa-Sh.4,380,960,319

Ukaguzi ulibaini Taasisi kumi na nne (14) zikijumuisha Wizara sita (6), Sekretarieti za Mikoa sita (6) na Balozi mbili (2) ambazo hazikuingiza mali na vifaa vilivyonunuliwa kwenye Leja ya Vifaa ikiwa ni kinyume na kanuni Na. 198 ya Kanuni za Fedha za Umma ya Mwaka 2001. Kuna ongezeko la kiasi cha Sh.4,051,553,716.74 ikilinganishwa na kiasi cha Sh.329,406,602 kilichoripotiwa mwaka uliopita.

Maelezo ya vifaa ambavyo havikuingizwa katika Leja ya Vifaa yameonyeshwa katika jedwali **96** hapo chini:

**Jedwali 96: Taasisi zenye vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye Leja ya Vifaa.**

| Na | Fungu | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 38 | Jeshi la Wananchi wa Tanzania | 4,016,222,850.44 |
| 2 | 94 | Ofisi ya Rais - Tume ya Utumishi wa Umma | 18,183,576.30 |
| 3 | 27 | Msajili wa Vyama vya Siasa | 43,945,400.00 |
| 4 | 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 14,882,992.00 |
| 5 | 47 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu | 24,140,972.00 |
| 6 | 63 | Sekretarieti ya Mkoa wa Geita | 30,631,580.00 |
| 7 | 89 | Sekretarieti ya Mkoa wa Rukwa | 24,200,000.00 |
| 8 | 2034 | Ubalozi wa Tanzania Moroni | 26,845,425.00 |
| 9 | 85 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora | 94,906,152.00 |
| 10 | 53 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto | 11,845,342.00 |
| 11 | 43 | Wizara ya Kilimo, Chakula na Maendeleo ya Ushirika | 15,972,517.00 |
| 12 | 61 | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 15,154,425.00 |
| 13 | 2005 | UBalozi wa Tanzania Abuja | 44,029,087.00 |
| 14 | 80 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mtwara | 89,795,009.00 |
| | | **Jumla** | **4,470,755,327.74** |

***Chanzo:*** *Taarifa za ukaguzi kwa menejimenti mwaka 2014/2015*

Kwa kuwa matumizi makubwa ya Fedha za Umma yanatumika kununua vifaa na mali, ninapendekeza ma zinatumika ipasavyo katika kutoa huduma kwa watumiaji wake kwa muda stahiki.

### 11.1.7 Ukosefu wa Nyaraka za Umiliki wa Ardhi na Majengo ya Umma

Wakati wa ukaguzi wa Taasisi zilizochaguliwa kama sampuli, nilibaini kuwapo kwa Ardhi na Majengo vinavyomilikiwa na Serikali bila ya kuwa na hati miliki ambazo zinathibitisha umiliki wa mali zilizoonyeshwa katika Taarifa za Hesabu. Ukosefu wa nyaraka zinazothibitisha umiliki halali wa mali, nimeshindwa kujiridhisha kama mali

hizo zinamilikiwa na Taasisi husika. Hii inaonyesha kwamba, Taasisi hizo hazina umiliki wa kisheria wa Ardhi na Majengo. Hivyo, endapo ikitokea kutoelewana katika umiliki Serikali inaweza kupoteza haki yake.

Pamoja na kuishauri Serikali kufuatilia upatikanaji wa hati hizo katika mapendekezo yangu kwenye taarifa za ukaguzi za miaka iliyopita, mpaka sasa Hati miliki za Ardhi na Majengo yanayomilikiwa na Serikali hazijapatikana. Jedwali Na. 97 hapo chini linaonyesha orodha ya Taasisi ambazo hazina nyaraka za umiliki wa Ardhi na Majengo.

**Jedwali 97: Taasisi ambazo hazina nyaraka za umiliki wa Ardhi na Majengo.**

| Na | Fungu | Taasisi |
|---|---|---|
| 1 | 5 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji |
| 2 | 14 | Idara ya Zimamoto na Uokoaji |
| 3 | 29 | Idara ya Magereza |
| 4 | 36 | Sekiretarieti ya Mkoa wa Tabora |
| 5 | 43 | Wizara ya Kilimo, Chakula na Maendeleo ya Ushirika |
| 6 | 47 | Sekiretariet ya Mkoa wa Simiyu |
| 7 | 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani |
| 8 | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii |
| 9 | 53 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto |
| 10 | 88 | Sekiretarieti ya Mkoa wa Dar es salaam |
| 11 | 93 | Idara ya Uhamiaji |
| 12 | 2021 | Ubalozi wa Tanzania  Kampala |
| | | |

***Chanzo:*** *Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2014/2015*

Kutokana na ukweli kuwa Taasisi nyingi za Serikali hazina hati miliki za kisheria za mali walizonazo, Serikali inashauriwa kuwa na mkakati wa makusudi kuhakikisha kwamba, Taasisi zote zinapata nyaraka za umiliki kutoka Mamlaka inayohusika ili kulinda Mali za Serikali.

### 11.1.8 Mali za Kudumu ambazo hazina alama za utambulisho

Kutokana na mfumo dhaifu katika usimamizi wa mali za Umma, wakati wa ukaguzi nilibaini Taasisi kumi na nne (14) zikijumuisha  Wizara saba (7),

Balozi mbili (2) na Sekretarieti za Mikoa ni tano (5) ambazo zimeonekana kuwa na mali za kudumu ambazo hazina alama za utambulisho kama zinavyoonekana katika jedwali 98 hapa chini:

**Jedwali 98: Taasisi ambazo zina Mali za Kudumu zisizo alama na utambulisho**

| Na. | Fungu | Jina la Taasisi |
|---|---|---|
| 1 | 35 | Mkurugenzi wa mashitaka wa Serikali |
| 2 | 39 | Jeshi la Kujenga Taifa |
| 3 | 44 | Wizara ya Viwanda na Biashara |
| 4 | 47 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu |
| 5 | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii |
| 6 | 59 | Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania |
| 7 | 68 | Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia |
| 8 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha |
| 9 | 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro |
| 10 | 76 | Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi |
| 11 | 79 | Sekretarieti ya Mkoa wa Morogoro |
| 12 | 96 | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo |
| 13 | 2026 | UBalozi wa Tanzania Kigali |
| 14 | 2028 | UBalozi wa Tanzania Bujumbura |

***Chanzo: Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2014/2015***

Ingawa zoezi la kuwekea alama maalumu Mali za Kudumu linahitaji rasilimali watu, muda na fedha, nashauri Serikali kulitekeleza kwa ukamilifu katika Taasisi zote ili kuweza kuwa na mfumo bora wa pamoja katika kufikia viwango vya kimataifa vilivyokusudiwa.

### 11.1.9 Utendaji usioridhisha wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lina wajibu wa kutoa huduma Tanzania bara, huduma hizo zinajumuisha: kuzuia matukio ya moto, kutoa kinga na kusimamia huduma zote zinazohusiana

na majanga ya moto na uokozi. Hata hivyo, kuna upungufu mkubwa wa magari ya zimamoto, nilibaini kwamba, kiasi cha magari ya zimamoto yanayohitajika ni 157 dhidi ya magari yaliyopo yapatayo 90. Vilevile, katika ukaguzi wa magari ya zimamoto, ilibainika kuwa magari 35 kati ya 90 yaliyopo hayafanyi kazi kwa kipindi kirefu. Inamaanisha kuwa Jeshi la Zimamoto na Ukoaji halina uwezo wa kupambana na majanga ya moto nchini kutokana na upungufu uliopo wa magari 102 ambayo ni sawa na asilimia 65 ya mahitaji. Hivyo, ninashauri Serikali kuwa na mpango maalumu wa muda wa kati na mrefu wa kuliwezesha Jeshi kuwa na vitendea kazi vya kutosha vya kudhibiti majanga ya moto yanapotokea nchini.

**Kutofanyia Ukaguzi vifaa vya kuzima Moto kwa muda uliopangwa**

Katika ukaguzi uliofanywa wa kuangalia kuwapo kwa uimara wa vifaa vya kuzima moto katika majengo ya Taasisi nane (8) za Serikali nilibaini mapungufu kama yaliyobainishwa kwenye jedwali Na 99 hapo chini:

**Jedwali 99: Taasisi ambazo vifaa vyake vya zima moto vina mapungufu**

| Na | Fungu | Jina la Taasisi | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| 1 | 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | Vifaa vya zimamoto havifanyiwi matengenezo wala majaribio |
| 2 | 35 | Ofisi ya Mwendesha Mashitaka wa Serikali | Vifaa vya zimamoto havifanyiwi matengenezo wala majaribio |
| 3 | 27 | Msajili wa Vyama vya Saisa | Vifaa vya zimamoto havifanyiwi matengenezo wala majaribio |
| 4 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | Hakuna vifaa vya zimamoto kwenye stoo kubwa ya madawa hospitali ya Mkoa. |

| Na | Fungu | Jina la Taasisi | Mapungufu |
|---|---|---|---|
| 5 | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | Vifaa vya zimamoto havifanyiwi matengenezo wala majaribio |
| 6 | 53 | Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto | Vifaa vya kuzimia moto vyenye thamani ya TZS.6,300,000 vimehifadhiwa stoo kwa zaidi ya miaka 7 bila kufungwa sehemu husika. |
| 7 | 68 | Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia | Vifaa vya zimamoto havifanyiwi matengenezo wala majaribio |

Serikali inashauriwa kuhakikisha kuwa vifaa vya kuzima moto vilivyoko kwenye majengo ya ofisi za Umma vinafanyiwa uchunguzi, matengenezo na majaribio kama taratibu za utunzaji wa vifaa vya kuzima moto zinavyoelekeza. Vilevile, kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuwa na uwezo wa kuendesha ukaguzi katika Taasisi za Umma na kuendesha mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi.

## 11.2. Ukaguzi wa madeni kwa mwaka 2014/2015

Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Sekta za Umma aya Na.1 (IPSAS 1) kinatafasiri kwamba, "*madeni ni wajibu uliopo wa kulipa kwa Taasisi utokanao na matukio ya zamani, ambapo malipo yake yanategemea kupunguza fedha kutoka kwenye Taasisi ambayo imefaidika kiuchumi au uwezo wa huduma*". Ufuatao ni muhtasari wa masuala niliyoyabaini katika ukaguzi wa madeni kwa mwaka 2014/2015.

### 11.2.1 Madeni tarajiwa

Madeni tarajiwa ni matarajio ya wajibu wa kulipa unaotegemea matokeo ya tukio ya siku za baadaye. Katika kupitia Taarifa za Fedha nilibaini Wizara na Idara tisa (9) na Sekretarieti za Mikoa mbili (2)

zina kesi 94 za kisheria mahakamani zenye jumla ya madai yanayofikia Sh. 870,866,104,235 dhidi ya makampuni mbalimbali na watu binafsi ambazo zilikuwa zinasubiria maamuzi. Matokeo ya kesi hizi zitakuwa na athari kubwa za kifedha katika uendeshaji wa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa kama Serikali itashindwa katika kesi hizo. Baadhi ya kesi zipo katika hatua ya kusikilizwa na nyingine katika hatua ya upatanishi mahakamani.

Wizara ya Nishati na Madini ina kiasi kikubwa cha kesi za madai ambacho ni Sh.614,918,311,003 sawa na asilimia 71 ya madai yote, ikifuatiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Sh.213,727,001,693 sawa na asilimia 24. Taasisi ambazo zina kesi mahakamani ni kama zinavyoonekana katika jedwali Na. 100 hapo chini:

**Jedwali 100: Taasisi zenye kesi zinazoendelea**

| Na | Fungu | Taasisi | Idadi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 5 | Tume ya Taifa ya Umwagiliaji | 2 | 4,546,074,597 |
| 2 | 43 | Wizara ya Kilimo, Chakula na Maendeleo ya Ushirika | 6 | 8,978,714,155 |
| 3 | 46 | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | 11 | 495,987,034 |
| 4 | 49 | Wizara ya Maji | 12 | 2,331,696,126 |
| 5 | 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 5 | 2,095,000,000 |
| 6 | 57 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 17 | 213,727,001,693 |
| 7 | 58 | Wizara ya Nishati na Madini | 9 | 614,918,311,003 |
| 8 | 69 | Wizara ya Maliasili na Utalii | 20 | 22,583,614,827 |

| Na | Fungu | Taasisi | Idadi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|---|
| 9 | 77 | Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa | 7 | 5,104,800 |
| 10 | 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | 1 | 500,000,000 |
| 11 | 99 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 4 | 684,600,000 |
| | | **Jumla** | **94** | **870,866,104,235** |

***Chanzo***: *Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2014/2015*

Kuna hatari ya kuingia katika matumizi yasiyo na faida kwa Wizara, Idara na Sekretarieti za Mikoa yatokanayo na fidia ambayo itatakiwa kulipwa Mahakamani kama Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa zitashindwa kesi; aidha, kuna gharama kubwa ambazo zinaingiwa katika kufuatilia hizi kesi.

Ukizingatia mapendekezo niliyokwisha kuyatoa miaka ya nyuma, Ninapendekeza Serikali kufanya mkazo kwenye kila Taasisi kuwa na sera ya usimamizi wa vihatarishi vya upotevu wa fedha ili kuhakikisha vinapunguzwa.

### 11.2.2 Malimbikizo ya madeni Sh. 1,443,859,273,539.30

Mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2015 Wizara/Idara 52, Sekretarieti za Mikoa 25 na Balozi 14 zilikuwa na madeni ya kiasi cha Sh. 1,443,859,273,539.30 ikilinganishwa na mwaka uliopita uliokuwa na madeni yaliyofikia Sh. 772,508,290,161; kumekuwapo na ongezeko kubwa la madeni kiasi cha Sh.671,350,983,378.30 sawa na ongezeko la asilimia 89.

Sehemu kubwa ya deni ni kutoka Jeshi la Polisi ambalo lina deni sawa na asilimia 27 ya jumla ya deni lote; ya pili ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ikiwa na asilimia 13 ya jumla ya deni

ikifuatiwa na Wizara ya Maji ikiwa na asilimia 10 ya jumla ya deni lote kama ilivyoonyeshwa kwenye kielelezo kifuatacho:




Deni lililoonyeshwa linajumuisha kiasi cha TZS.27,800,677,740 kikiwa ni deni linalotokana na gharama za matibabu ya wagonjwa wanaotibiwa katika hospitali za rufaa nchini India. Mwenendo wa deni kwa kipindi cha miaka miwili ni kama ifuatavyo:

**Jedwali 101: Madeni ya Hospital za Rufaa**

| Na. | Jina la Hospitali | 2013/14 Kiasi (Sh) | 2014/15 Kiasi (Sh) |
|---|---|---|---|
| 1. | Apollo Hyderabad | 2,702,517,748 | 4,831,685,872 |
| 2. | Apollo Chennai | 6,630,974,112 | 8,685,499,033 |
| 3. | Apollo Bangalore | 380,246,720 | 1,245,306,554 |
| 4. | Apollo Ahmedabad | 582,268,288 | 1,906,267,772 |
| 5. | Apollo New Delhi | 6,082,196,624 | 10,117,292,151 |
| 6. | Madras Medical Mission | 562,189,712 | 1,014,626,358 |
| **Jumla** | | **16,940,393,204** | **27,800,677,740** |

***Chanzo:*** *Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2014/2015*

Kulimbikiza madeni kutaathiri utekelezaji wa mipango ya Serikali, hii ni kwa sababu, badala ya kutekeleza mipango iliyopo itakuwa inalipa

madeni ya miaka ya nyuma. Orodha ya Taasisi zenye madeni ya muda mrefu imeonyeshwa kwenye kiambatisho Na.11.4

Ongezeko kubwa la deni bila ya kuonyesha juhudi za kulilipa linavuruga uhusiano mzuri uliokuwapo kati ya Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa pamoja na watoa huduma wake na watumishi; na huweza kusababisha utoaji wa huduma kwa Umma usioridhisha. Wizara, Wakala, Idara na Sekretarieti za Mikoa zinaweza kushitakiwa kwa kosa la kushindwa kulipa deni kwa wakati. Licha ya mapendekezo yangu ya miaka ya nyuma ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali:

a) Kuhakikisha fedha zinatolewa kama zilivyoidhinishwa na kupitishwa na Bunge ili kupunguza limbikizo kubwa la deni ambalo linaweza kusababisha hatari ya kudaiwa na kupunguza uaminifu, kuingiza katika bajeti ya mwaka ufuatao madeni yote ili kuepuka mgogoro na watoa huduma na wadau wengine.

b) Kupitia upya mchakato wa maandalizi ya bajeti ili kuhakikisha bajeti inayoandaliwa inaendana na shughuli zilizopangwa na mahitaji yote kwa ujumla.

### 11.2.3 Kushindwa kuonyesha madeni kwenye Taarifa za Fedha kwa mwaka uliopita

Kanuni Na. 91(2) ya Kanuni ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 kuwa inaelekeza mwisho wa mwaka wa fedha madeni yote yaorodheshwe kwenye Rejista kwa ajili ya mwaka unaofuata. Ukaguzi ulibaini Taasisi sita (6) zimefanya malipo yanayofikia Sh. 731,317,717 kwa wazabuni mbalimbali waliotoa huduma kipindi cha miaka ya nyuma. Hata hivyo, ukaguzi pia ulibaini matumizi yaliyotokana na malipo

haya hayakuonyeshwa katika Taarifa ya Fedha iliyoishia tarehe 30 Juni 2014 kama madeni badala yake yakahesabiwa kama matumizi ya mwaka 2014/15 kinyume na kanuni Na. 91 (2). Taasisi ambazo zimefanya malipo hayo zimeonyeshwa katika jedwali Na. 102 hapo chini:

**Jedwali 102: Taasisi zilizoshindwa kuonyesha madeni**

| S/N | Fungu | Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 66 | Ofisi ya Rais Tume ya Mipango | 12,003,750.00 |
| 2 | 75 | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 33,664,925.00 |
| 3 | 47 | Sekretarieti ya Mkoa wa Simiyu | 134,103,898.00 |
| 4 | 21 | Hazina | 376,641,079.60 |
| 5 | 48 | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi | 21,151,293.41 |
| 6 | 70 | Sekretarieti ya Mkoa wa Arusha | 153,752,771.00 |
| | | **Total** | **731,317,717.01** |

*Chanzo: Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2014/2015*

Napendekeza kuwa, Mlipaji Mkuu wa Serikali ahakikishe kunakuwapo na uwiano mzuri katika kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Sekta za Umma kwa kuendesha mafunzo ya mara kwa mara kwa watumishi.

### 11.2.4 Madeni ambayo hayana nyaraka Sh. 23,265,941,376

Ukaguzi uliofanywa katika Taasisi tatu ulibainisha kiasi cha madeni yanayofikia Sh. 23,265,941,376 yaliyoko katika Taarifa za Fedha kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2015 yanayotokana na huduma kutoka kwa wazabuni mbalimbali. Hata hivyo, Taasisi husika zilishindwa kuthibitisha uhalali wa madai hayo

baada ya kushindwa kuwasilisha viambatisho na nyaraka za uhalali wake kwa wakaguzi. Taasisi ambazo zimeripoti madai hayo zimeonyeshwa katika jedwali Na. 103 hapo chini:

**Jedwali 103: Taasisi zenye madeni yasiyo na viambatisho**

| Na | Fungu | Jina la Taasisi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 57 | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Uchumi | 3,152,778,856 |
| 2 | 51 | Wizara ya Mambo ya Ndani | 1,771,336,399 |
| 3 | 52 | Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 18,341,826,121 |
| | | **Jumla** | **23,265,941,376** |

*Chanzo: Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2014/2015*

Kutokana na kutokuwapo kwa nyaraka za kuthibitisha madai yaliyoko kwenye Taarifa za Fedha, kuna uwezekano wa kuwapo kwa madai ambayo si halisi. Hivyo, nilishindwa kuthibitisha uhalali wa madai hayo.

Napendekeza kuwa Maafisa Masuuli wanaohusika waweke mifumo ya udhibiti iliyo madhubuti ili kuhakikisha madai yote kwenye Taarifa ya Fedha yanakuwa na nyaraka zinazothibitisha huduma iliyotolewa na wazabuni husika kulingana na masharti ya manunuzi au huduma iliyotolewa.

## Sura ya kumi na mbili

## UKAGUZI MAALUMU NA MASUALA MENGINE

### 12.0 Utangulizi

Katika sura hii, ninaeleza matokeo ya ukaguzi na mapungufu yaliyobainika katika kaguzi maalum zilizofanyika katika mwaka wa fedha 2014/2015 pamoja na mambo mengine yaliyobainika wakati wa Ukaguzi.

### 12.1 Kaguzi maalumu zilizofanyika kwa mwaka wa fedha 2014/15

Kaguzi maalum zilifanyika kwa mujibu wa Kifungu cha 29 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 pamoja na Kanuni ya 79(1) ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

Katika mwaka wa fedha 2014/2015 kaguzi maalumu zilizofanyika katika Taasisi za Serikali Kuu zimepungua kutoka nane zilizofanyika mwaka 2013/2014 hadi kufika mbili mwaka huu.

#### 12.1.1 Kuhakiki na kuthibitisha fedha zilizotumwa kwenye Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi

Ukaguzi maalumu ulitokana na ombi la Katibu wa Bunge kupitia barua yake yenye kumbukumbu namba CBC.155/188/01/26 ya tarehe 19/12/2013. Ukaguzi maalum ulilenga kubaini kama fedha zilizokuwa zinatumwa kwenda Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu na Ufundi kama zilipokelewa na taarifa kutolewa kwa usahihi kwenye hesabu za Taasisi husika.

Mambo muhimu yaliyobainika katika ukaguzi maalum yameonyeshwa kwa muhtasari katika taarifa hii; hata hivyo, taarifa husika za kaguzi maalum zilishapelekwa kwa Mamlaka husika

kwa mujibu wa Kanuni ya 81 ya Kanuni za Ukaguzi wa Umma za mwaka 2009.

**(i) Miamala yenye viashiria vya ubadhirifu NECTA Sh 185,350,000**

Katika mwezi wa nne mwaka 2010, kiasi cha Sh.185,350,000 kilitumwa NECTA kama fedha za matumizi ya kawaida. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa kiasi hiki cha fedha hakikuandikwa kwenye vitabu vya uhasibu vya NECTA. Hata hivyo,, ilibainika kuwa stakabadhi ya mapokezi ya fedha hizo iliyotolewa na watumishi wasio waaminifu wa NECTA ilikuwa ya kugushi.

**(ii) Fedha zilizotumwa kwa Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola na Chuo Kikuu Huria hazikuthibitika kupokelewa Sh. 108,409,893**

a) Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilihamisha kiasi Sh. 90,000,000 kwenda Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa kiasi cha Sh. 40,734,000 kilipokelewa na kiasi cha Sh. 49,266,000 hakikuthibitika kupokelewa.

b) Katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilihamisha kiasi Sh. 10,486,252,913 kwenda Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa kiasi cha Sh. 10,427,109,020 kilipokelewa na kiasi cha Sh. 59,143,893 hakikuthibitika kupokelewa.

**(iii) FedhazilizotumwaADEMhazikupokelewa Sh. 188, 838,528**

Katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilihamisha kiasi Sh. 712,798,788 kwenda kwa Wakala wa Maendeleo ya Elimu na Usimamizi (ADEM) Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa kiasi cha Sh. 523,960,260 kilipokelewa na kiasi cha Sh. 188, 838,528 hakikuthibitika kupokelewa.

**(iv) Kukosekana kwa Utaratibu wa ufuatiliaji wa Fedha zinazotumwa kwenye Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu**

Katika ukaguzi maalum ilibainika kuwa Wizara ya Elimu na mafunzo ya Ufundi haikuwa na mfumo madhubuti wa ufuatiliaji wa fedha zilizokuwa zinatumwa kwenye Taasisi zilizo chini yake. Hatua hii ilisababisha baadhi ya fedha kuchelewa kukatiwa stakabadhi na wakati mwingine hazikukatiwa stakabadhi kabisa. Kutokana na udhaifu huu hesabu za wizara hazikuwa na uhalisia kwani ziliandaliwa kwa kumbukumbu za upande mmoja tu wa Wizara.

Nashauri Taasisi za Serikali za kiuchunguzi kufanya uchunguzi wa kina ili kuweza kubaini na kuchukua hatua stahiki na kuzuia ubadhirifu kama huu usiweze kutokea katika idara nyingine za Serikali.

### 12.1.2 Ukaguzi Maalum wa Hesabu za Mpango wa pili wa Maboresho ya Serikali za Mitaa (LGRP II D by D) kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30/6/2013

Ukaguzi Maalum ulifanyika baada ya PWC

kuingia mkataba na SIDA tarehe 16/9/2014 kwa ajili ya kutoa huduma ya kufanya ukaguzi wa Hesabu za Mpango wa pili wa Maboresho ya Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30/6/2013. Ulihusisha Mapato na matumizi ya fedha za Ruzuku ya Maendeleo chini ya Serikali za Mitaa. Ukaguzi Maalum ulibaini yafuatayo:

**(a) Ukosefu wa uthibitisho wa matumizi ya Sh. 903,270,394**

Ilibainika kuwa kiasi cha Sh.903,270,394 kilitumika kwa ajili ya vikao pamoja na shughuli nyingine za mradi bila kuwapo kwa uthibitisho wa taarifa za matumizi au fomu za marejesho. Zaidi ya hayo, hapakuwa na uthibitisho endapo matumizi haya yalipata idhini ya afisa wa bajeti au Menejimenti ya Mpango wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Hivyo, sikuweza kuthibitisha kama kazi hizo zilifanyika.

**(b) Matumuzi yasiyofuata masharti ya Mpango Sh. 84,863,510**

Ukaguzi Maalumu ulibaini kuwa matumizi ya Sh. 84,863,510 yalifanyika bila ya kufuata masharti ya Mpango wa Maboresho. Hali hiyo ilitishia kuathiri lengo la utekelezaji wa mpango. Matumizi hayo ni pamoja na:

**(i) Matumizi yasiyoendana na Mpango wa Maboresho Sh. 13,040,075**

Kati ya Matumizi yaliofanyika kiasi cha Sh 13,040,075 kilitumika kwa kazi mbalimbali zilizokuwa nje ya Mpango wa Maboresho. Uhalali wa matumizi hayo haukuweza kuthibitika wakati wa ukaguzi Maalumu.

**(ii) Mapungufu katika malipo ya posho za Warsha na Mafunzo Sh. 18,967,500.**

Katika ukaguzi maalum, nilibaini kuwa matumizi ya kiasi cha Sh 236,190,000 kama posho ya safari kwa washiriki wa warsha na mafunzo mbalimbali yalilipwa kiwango kimoja cha Sh. 80,000 bila kujali cheo cha mtumishi isipokuwa madereva waliokuwa wanalipwa Sh. 45,000. Kutokana na malipo haya, nilibaini kuwa kiasi cha Sh. 18,967,500 kililipwa zaidi kwa wafanyakazi. Malipo haya yalifanyika kinyume na Kanuni za Fedha za Mpango wa Maboresho ya Serikali za Mitaa.

**(iii) Malipo ya posho kwa ajili ya simu, masaa ya ziada,likizo na vikao Sh. 31,762,360**

Katika ukaguzi Maalum nilibaini malipo ya kiasi cha Sh. 31,762,360 kwaajili ya posho ya simu, masaa ya ziada, likizo na vikao yalifanyika kinyume na Kanuni za Fedha za Mradi. Nilishindwa kujiridhisha uhalali wa matumizi haya wakati wa ukaguzi maalumu.

**(iv) Malipo yaliyofanyika nje ya bajeti Sh. 21,093,575**

Katika ukaguzi Maalum nilibaini malipo ya kiasi cha Sh. 21,093,575 kwa ajili ya mafunzo, warsha, tiketi za ndege na posho ya safari hayakuwemo kwenye bajeti. Kutokana na hali hii nilishindwa kubaini uhalali wa malipo hayo kutumia fedha za Mpango wa Maboresho.

Kulingana na matokeo ya Ukaguzi Maalum, kuna hatari kubwa ya Mpango kushindwa kufikia malengo yake kutokana na matumizi mabaya ya fedha, kukosekana kwa uhakika wa taarifa za fedha, kukosa ufanisi na kutozingatia Sheria husika na Kanuni.

Nashauri wadau wa utekelezaji wa Mpango kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ya kuendesha uchunguzi wa kina wa mapungufu yote yaliyobainishwa ili kuchukua taratibu sahihi za kiSheria na hatua za kinidhamu kwa wote waliohusika.

Kama ilivyobainika kwenye Ukaguzi Maalum matumizi mabaya ya fedha pamoja na matumizi yasiyozingatia Sheria yanatokana Menejimenti ya Taasisi husika. Nashauri matumizi ya Sh 988,133,904 yasiyokuwa na viambatisho vya kutosha fedha hiyo irejeshwa kwa Mpango wa maboresho pamoja na kuchukuliwa hatua kwa maafisa wote waliohusika.

### 12.1.3 Utekelezaji wa Sera ya mambo ya Nchi za Nje ya Kiuchumi na Diplomasia

Sera ya Mambo ya Nchi za Nje ya mwaka 2001, inaeleza bayana umuhimu wa dhana ya Diplomasia ya Kiuchumi baina ya Tanzania na Nchi za Nje yenye lengo kuinufaisha nchi katika nyanja mbalimbali kama biashara, uwekezaji na aina nyingine ya kubadilishana manufaa kiuchumi, ambapo yana faida kwa nchi zote mbili. Balozi za Tanzania nje ya Nchi ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa sera ya kigeni ya mahusiano ya kiuchumi.

Balozi za Tanzania Nje ya Nchi zimeanzishwa kutekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja a) Kuiwakilisha Tanzania katika nchi za Kigeni b) Ufuatiliaji na kutoa taarifa zinazohusu maendeleo ya kiuchumi, biashara na utamaduni ya nchi mwenyeji c) Kuendeleza mahusiano ya Kiuchumi, biashara, utamaduni kati ya Tanzania na Nchi mwenyeji.

Katika mwaka huu wa ukaguzi nilifanya tathimini ya mifumo mbalimblai katika Balozi zetu nje ya nchi ikiwa ni pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani, mifumo ya uhasibu kwa lengo la kubaini uzingatiaji wa Sheria mbalimbali. Vile vile, nilifanya mapitio uwezo wa Balozi zetu kutekeleza agizo la Rais kuhusu Balozi zetu kuwasilisha nchi na Taasisi mbalimbali katika kazi zote zinazotakiwa kufanyika katika nchi ya Kigeni ili kupunguza matumizi ya Serikali yanayotokana na safari za Maafisa wa Serikali nje ya nchi.

Katika Balozi nilizotembelea nilibaini kuanza kutekelezwa kwa maelekezo ya Rais lakini yakikumbwa na changamoto mbalimbali hali inayopelekea kukosekana kwa ufanisi katika utekelezaji wa maagizo hayo. Katika tathmini yangu nimebaini idadi ya changamoto kama inavyonekana hapa chini ambazo Serikali haina budi ya kuzishughulikia ili kufikia ufanisi wa shughuli za UBalozi nje ya Nchi wa kama vile kufuata Sheria na Kanuni zote na maelekezo ya Rais.

**(a) Ujuzi na kuwajengea uwezo watumishi**

Licha ya Tanzania kuamua kufanya Diplomasia ya Siasa na Uchumi tangu mwaka 2001, huduma za Balozi nje ya nchi zinakumbwa na changamoto za ukosefu wa Wafanyakazi wa kutosha pamoja na wenye ujuzi unaotakiwa katika nyanja mbalimbali. Nimebaini Serikali haijachukua hatua za makusudi kuhakikisha kuwa Ofisi za Balozi nje ya nchi zinakuwa na idara mbalimbali zenye wataalum katika nyanja ya biashara, uchumi, utalii na uhusiano za kimataifa hali inayopelekea kutoweza kutumia fursa mbalimbali za maendeleo na za kiuchumi zinazopatikana katika nchi za nje.

Baadhi ya Balozi zina upungufu wa wafanyakazi ikilinganishwa na eneo la utendaji kazi hali inayopelekea changamoto mbalimbali za kiutendaji. Nilibaini UBalozi wa Tanzania Berlin, Ujerumani unatoa huduma za kiBalozi kwa nchi za Poland, Slovakia, Jamhuri ya Czech, Austria, Switzerland, Romania, Bulgaria na Vatican. Vile vile China inatoa huduma za kiBalozi kwa nchi za Vietnam, Korea pamoja na Mongolia.Mahitaji halisi ya wafanyakazi ni kumi na saba ikilinganishwa na nane waliopo.

**Ufinyu wa Bajeti.**

Kwa kipindi kirefu Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi zimekuwa zikipewa fedha za bajeti pungufu hatua inayopelekea kushindwa kutimiza majukumu yao ya kazi kama kuhudhuria matukio mbalimbali ya kiuchumi na kidiplomasia katika miji mikuu na miji mingine ya Kati na Ulaya Mashariki ambazo zina uhusiano wa kihistoria na nchi yetu. Mfano mwingine ni UBalozi wa Tanzania katika Shirikisho la Urusi ambayo inato huduma za kiBalozi kwa nchi zifuatazo: Russia, Belarus, Georgia, Ukraine, Uzbekistan, Azerbaijan, Turkmenistan, Kyrgyzstan, Moldova, Armenia, Kazakhstan na Tajikistan.

Katika kutekeleza majukumu, Serikali imekuuwa ikichelewesha fedha za uendeshaji wa shughuli za Balozi kama mishahara, posho na matumizi mengine hatua iliyopelekea Maafisa Balozi kushindwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Changamoto nyingine iliyobainika ni ukosefu wa vitendea kazi kama magari hali inayopelekea baadhi ya Balozi kukodisha magari kwa gharama kubwa, mfano ni UBalozi wa Tanzania, Moroni

**(b) Kukosekana kwa Kituo cha uratibu na mawasiliano kati ya Balozi na Sekta mbalimbali za Wizara**

Balozi za Tanzania nje ya Nchi zinahitaji kupewa taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu maendeleo mbalimbali yanayofanyika nchini kupitia kwa kituo cha pamoja ambacho kinaweza kuanzishwa ndani ya Wizara ya mambo ya nchi za nje. Kituo hiki kinaweza kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu uchumi, utalii pamoja na faida zinazopatikana kutokana na Balozi. Hii itasaidia Balozi kuongeza majukumu yao ya kazi pamoja na kuipatia nchi faida. Imebainika kuwa hakuna uratibu madhubuti kati ya Wizara ya Mambo ya Nje na Wizara nyingine za sekta mbalimblali kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika upatikanaji wa taarifa hii na kuchukua hatua muafaka ikiwa ni pamoja na mikakati mbalimbali.

**Mapendekezo**

(a) Napendekeza kupelekwa kwa watumishi wa kutosha katika Balozi wenye taalumu katika nyanja za biashara, utalii, uchumi na uwekezaji kuhakikisha wanatoa huduma zinazohitajika.Hii inaweza pia kufanyika kwa njia ya mafunzo ya kuwajengea uwezo. Vile vile, napendekeza kupelekwa watumishi wenye ujuzi na wa kutosha kwa wakati, katika Balozi zenye upungufu.

(b) Nasisitiza mapendekezo yangu niliyoyatoa katika taarifa yangu ya ukaguzi ya mwaka 2013/2014 kwamba, Serikali kutenga fedha za kutosha kupitia fungu maalumu kwa ajili ya kazi za UBalozi nje ya Nchi. Pia, Serikali

kuhakikisha bajeti ya Balozi za Tanzania inakuwa ya kutosheleza kuweza kulipia mahitaji yake. Vile vile Serikali kutoa kwa wakati fedha za UBalozi ili kuziwezesha Balozi kuweza kulipa mahitaji na madeni yake kwa wakati.

(c) Naishauri Serikali kuwa na kitengo madhubuti cha uratibu ili kuweza kupeleka taarifa mbalimbali zinazohusu Tanzania kwenye Balozi nje ya nchi vile vile kupokea taarifa kutoka Balozini zinasohusu nchi nyingine. Kitengo hiki kinatakiwa kufanya kazi kwa kushirikiana kwa karibu na jumuiya za kibiashara, kujenga uwezo wa kiTaasisi ili kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kidiplomasia na kufuatilia fursa za kiuchumi zinazopatikana katika maeneo mengine ya ulimwenguni.

## Sura ya Kumi na Tatu

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 13.0 Utangulizi

Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo ya jumla kwa masuala yaliyojitokeza kwenye taarifa hii, ambayo yanahitaji mpango kazi na kushughulikiwa na Serikali, Bunge pamoja na Menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu. Mapendekezo haya kwa sehemu kubwa yametokana na taarifa za Ukaguzi za taasisi husika zilizowasilishwa kwa kila Afisa Masuuli wakati wa ukaguzi pamoja na maswala mengine ya muhimu ambayo Umma unapaswa kuyafahamu.

Kwa ujumla, Wizara, Idara, Wakala na taasisi nyingine za Serikali zinashauriwa kuanzisha mfumo na utaratibu ambao unaweza kushughulikia masuala ya maslahi ya umma pamoja na usimamizi makini wa raslimali za umma kwa ufanisi bila kuathiri ubora wa huduma zinazotolewa na Serikali.

Napenda kutoa mapendekezo ya ujumla kuhusu matokeo ya Ukaguzi wa Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Wakala wa Serikali, Mifuko Maalum na Taasisi nyingine kama ifuatavyo:

### 13.1 Kufuatilia Utekelezai wa Mapendekezo

Serikali kupitia kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali pamoja na Maafisa Masuuli wanashauriwa kuongeza juhudi katika kuhakikisha kuwa mapendekezo ya Ukaguzi yaliyotolewa pamoja na maagizo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali Kuu yanafanyiwa kazi ipasavyo. Mlipaji

Mkuu wa Serikali anashauriwa kuendelea kutoa miongozo ya kuwaelekeza Maafisa Masuuli kuchukua hatua muhimu ili kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani, ambayo ni moja ya sababu kuu inayochangia kukwama kwa utekelezaji wa mapendekezo yangu kwa wakati. Mapungufu mengi yaliyobainika yanafanana na ya miaka iliyopita ya Ukaguzi; hali inayoonyesha kueleweka kuwa mapendekezo yangu hayapewi uzito na kipaumbele na Maafisa Masuuli na watendaji wakuu wa Serikali.

Maafisa Masuuli wanakosa mpango maalumu wa utekelezaji wa mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mpango wa utekelezaji unatakiwa kueleza bayana wakati, nani, na jinsi mapendekezo yanavyotakiwa kutekelezwa.

## 13.2 Usimamizi wa Fedha za Umma

Kasi ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali imezidi kuimarika; kiasi kwamba hatua inayopeleka changamoto mbalimbali zilizokuwa zinajitokeza zitaweza kuanza kushughulikiwa kuanzia mwaka ujao wa fedha, hususani ufinyu wa bajeti, kutolewa kwa fedha mwishoni mwa mwaka pamoja na kutofikiwa kwa malengo ya bajeti. Hatimaye, mikakati na malengo ya Taifa kwa ujumla yatafanikiwa. Ukopaji wa fedha za ndani pamoja na malimbikizo ya matumizi yatapungua kwa kiasi kikubwa kutokana na fedha kutolewa kama zilivyoidhinishwa katika bajeti.

Kwa misingi hiyo, utekelezaji wa kazi zilizo katika mpango utafanyika kwa wakati. Ili Serikali iweze kupunguza utegemezi wa misaada ya nje kwa ajili ya kutekeleza mipango ya maendeleo ya Taifa, haina budi kubaini vyanzo mbadala vya mapato. Hatua

hii itasaidia kuepuka ucheleweshaji wa utekelezaji wa bajeti na kuongezeka kwa gharama kutokana na kuongezeka kwa muda na mfumuko wa bei. Mamlaka ya Mapato haina budi kuwalazimisha walipa kodi kuzingatia Sheria ya Kodi kwa hiyari. Maelezo ya kina yanapatikana katika sura ya nne ya ripoti hii.

## 13.3 Usimamizi wa Rasilimali Watu na Mishahara

Kama nilivyoeleza kwenye taarifa yangu ya mwaka uliyopita, Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Taasisi nyingine zimeendelea kuwa na udhaifu katika usimamizi wa Rasilimali watu na Mishahara, baadhi ya mapungufu yanayojirudia kujitokeza ni pamoja na: Upungufu wa Wafanyakazi, Mishahara iliyolipwa kwa Watumishi wasiokuwepo au wamestaafu kwenye utumishi wa Umma, Makato ya watumishi wasiokuwepo tena katika utumishi wa Umma kuendelea kuwasilishwa kwenye Taasisi mbalimbali, kutofanyika kwa tathmini ya utendaji Kazi kwa Wafanyakazi Serikalini, kuchelewesha kupelekwa kwa Makato ya Wafanyakazi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, pamoja na posho za kukaimu Ofisi kutolipiwa kodi kinyume na Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2004 (Kama ilivyorekebishwa mwaka, 2008).

Hivyo, napendekeza Serikali ihakikishe na kuzingatia matumizi bora ya rasilimali watu pamoja na kuipatia miongozo ili kupunguza mapungufu yaliyobainika katika taarifa yangu kwa ajili ya kulinda maslahi ya waajiri na waajiriwa ili kuweza kufikia lengo lilokusudiwa.

## 13.4 Wakala wa Serikali, Taasisi nyingine na Mifuko Maalum

Matokeo ya Ukaguzi ya Wakala wa Serikali,

Taasisi nyingine pamoja Mifuko Maalum yamebaini kuendelea kutozingatiwa kwa Sheria ya Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba. Vile vile, nilibaini mapungufu katika mapato na matumizi ambapo mapato yaliyotokana na kuuzwa nyumba za Serikali hayakukusanywa na mapato kutopelekwa benki, malipo kutoambatanishwa na risiti za kielektroniki, malipo kulipwa bila kukatwa Kodi ya zuio pamoja na hasara iliyotokana na kutouzwa kwa Shajara na Kalenda. Mapungufu haya yana athari ya moja kwa moja katika mapato ya Serikali; kama yakisimamiwa vizuri yataiwezesha Serikali kupata mapato yasiyokusanywa na yale yasiyotumika vizuri.

Zaidi ya hayo, nilibaini kupelekwa kwa fedha pungufu za Miradi ya Maendeleo na matumizi mengineyo; hatua iliyoathiri utekelezaji wa mipango na utendaji wa taasisi. Utegemezi wa Serikali bado ni changamoto kwa Taasisi hizi, kwani asilimia 90% ya shughuli za Taasisi hizi hufadhiliwa na ruzuku kutoka Serikalini.

Nazishauri Wakala wa Serikali, Taasisi nyingine pamoja na Mifuko Maalum kuzingatia Sheria na Kanuni kama Sheria ya Fedha ya Umma na Kanuni zake, Kanuni Na 24 ya Kanuni za Mashine za kielekitroniki *"Electronic Fiscal Device"* (EFD) za Mwaka 2012, Sheria ya Kodi ya Mapato ya Mwaka 2006, Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011 na Kanuni zake pamoja na Masharti na matakwa ya Mkataba.

## 13.5 Ukaguzi wa Vyama vya Siasa

Kati ya vyama ishirini na mbili (22) vya Siasa vyenye usajili wa kudumu ni chama kimoja pekee kilichowasilisha hesabu zake kwa kipindi cha miezi sita iliyoishia Mwezi wa Sita 2015. Vyama vilivyobakia ishirini na moja (21) havikuwasilisha hesabu zao kwa mujibu wa

Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja na Sheria ya Fedha ya mwaka 2001. Navishauri vyama vya Siasa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Siasa pamoja Sheria ya Fedha ya mwaka 2001.

### 13.6 Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

Licha ya kuwepo kwa Sheria mpya ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, bado baadhi ya Taasisi za Serikali Kuu hazizingatii kikamilifu Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2011, pamoja na kanuni zake za mwaka 2013. Nilibaini kuwa kuna uelewa hafifu katika Wizara, Idara, Wakala Sekretarieti za Mikoa na Balozi katika kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake.

Kutokana na mapungufu yaliyoelezwa katika Sura ya Tisa, Taasisi za Manunuzi ya Umma zinashauriwa kuzingatia kikamilifu vifungu vya Sheria ya Manunuzi ya Umma katika kuandaa na kutekeleza mpango wa manunuzi wa mwaka, kuidhinishwa kwa manunuzi na bodi ya zabuni, ukaguzi wa vifaa na bidhaa na manunuzi kutoka kwa Wazabuni waliodhinishwa.

Katika utunzaji wa kumbukumbu za manunuzi, nazishauri Idara za Manunuzi za Taasisi za Serikali Kuu kuhakikisha utunzaji sahihi/makini wa kumbukumbu za manunuzi. Nashauri Menejimenti ya Taasisi za Serikali Kuu kuzingatia vipengele mbalimbali kwenye mikataba wanayoingia ili kuhakikisha miradi/mikataba inakamilika kwa wakati; vile vile, tozo ya kuchelewesha kumalizika kazi inakusanywa kutoka kwa wakandarasi wanaochelewesha miradi.

## 13.7 Mapungufu katika Usimamizi wa Matumizi

Katika usimamizi wa matumizi nimebaini kuwa baadhi ya Taasisi za Serikali Kuu zina mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani; hali hii ilisababisha baadhi hati za malipo kuwa na nyaraka pungufu, kukosekana kwa risiti za Kielektroniki katika malipo, malipo yaliyolipwa zaidi ya kiwango stahiki, matumizi yasiyokuwa na manufaa kwa Serikali, masurufu yasiyorejeshwa, matumizi nje ya bajeti pamoja na matumizi yasiyokuwa na risiti. Hii ni dalili ya udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani. Baadhi ya Taasisi za Serikali kuu zimeshindwa kudhibiti mapungufu haya hali inayosababisha kuendelea kujirudia; hivyo, inatia shaka ufanisi katika wa usimamizi wa matumizi katika Wizara, Idara na Taasisi za Serikali Kuu.

Nawashauri Afisa Masuuli wa Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Ofisi za Balozi waendelee kuboresha Mifumo ya ndani ya udhibiti, vile vile wawajengee uwezo Wafanyakazi. Mbali na hayo, utunzaji wa nyaraka unatakiwa kuboreshwa pamoja na uzingatiwaji wa Kanuni.

Kwa upande wa kutozingatiwa kwa Kanuni Na 24 ya Kanuni za Mashine za Kielekitroniki *"Electronic Fiscal Device"* (EFD) za Mwaka 2012, napendekeza Serikali kutoa Mwongozo kwa taasisi zake kusitisha kufanya biashara na wazabuni wasiotoa risiti za kielekitroniki. Aidha, kuendelea kutoa elimu ya uhamasishaji ili kuhamasisha uzingatiaji wa sheria kwa hiyari.

## 13.8 Mapungufu katika Usimamizi wa Mali za Kudumu

Usimamizi wa Mali za Kudumu katika Taasisi zilizokaguliwa ni muhimu katika utendaji ili

kuhakikisha uthabiti katika utoaji wa huduma bora kwa Umma. Udhaifu katika usimamizi wa Mali unaweza kusababisha kupotea kwa Mali, hatimaye kusababisha utoaji wa huduma duni. Baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza ni pamoja na: Magari 675 yaliyofikia ukomo wake wa matumizi na hayatengenezeki, kuchelewa kukamilika kwa kazi ya kutathimini ya mali za kudumu, kutotengenezwa kwa rejista timilifu ya Mali za kudumu, kukosekana kwa mpango mkakati wa kuendeleza viwanja vya Ubalozi nje ya nchi pamoja na ukarabati wa majengo; ukosefu wa nyaraka za umiliki wa ardhi na majengo ya umma.

Kutokana na kuchelewa kwa tathimini ya Mali za Kudumu pamoja na kuandaa rejista timilifu ya Mali za Serikali, nashauri Mlipaji Mkuu wa Serikali kuandaa mpango mkakati ili kuhakikisha Wizara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa zinazingatia viwango vya Kimataifa vya kuripoti Mali za Kudumu. Aidha, nashauri Serikali ihakikishe Taasisi zake zinapata nyaraka za umiliki mali ili kuweza kulinda mali za Serikali. Vile vile, nashuari Serikali ichukue hatua madhubuti kwa kuyauza Magari ambayo hatengenezeki kwa mujibu wa Sheria na Kanuni ili kuweza kupata kiasi kidogo cha fedha kulingana na thamani ya gari iliyobakia kwenye gari husuka.

Hatua madhubuti zinatakiwa kuchukuliwa ili kupunguza madai/madeni kwa kuandaa sera ya kuwabana wadeni/wadaiwa na kuzidisha juhudi katika taratibu za kukusanya na kulipa madeni/madai kwa wakati. Malipo ya kabla ya huduma/vifaa yanatakiwa kufanyika inapothibitika kuwa vifaa/huduma vitapatikana kwa wakati.

Nilibaini malimbikizo ya madeni katika Taasisi

89 za Serikali Kuu ambapo 52 ni Wizara, Sekretarieti za Mikoa 25 na Balozi 14 kwa pamoja zilikuwa na malimbikizo ya madeni yenye thamani ya Sh. 1,443,859,273,539 ikilinganishwa na madeni ya mwaka 2013-2014 ya Sh. 772,508,290,161ikiwa ni ongezeko kubwa la Sh. 671,350,983,378 sawa na asilimia 89.

Pia nilibaini matumizi ya miaka ya nyuma hayakutengewa bajeti; hali hiyo ilisababisha fedha za bajeti za mwaka huu kutumika kulipia madeni ya nyuma. Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa madeni, kwani fedha za mwaka huu zililipia madeni ya nyuma.

Katika madeni, nilibaini likimbikizo la deni lenye thamani ya Sh. 27,800,677,740 zikiwa ni gharama za matibabu ya wagonjwa wanaopelekwa nchini India kwa matibabu.

Katika maelezo ya Vitabu vya Hesabu, Wizara Tisa (9) na Sekretarieti za Mikoa mbili (2) ilibainika kesi 94 zenye thamani ya Sh. 870,866,104,235 zilizopo mahakamani zikisubiri maamuzi mbalimbali dhidi ya taasisi na watu binafsi.

Katika madeni ya Serikali, nashauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa miaka ijayo kwa ajili ya kulipia Madeni yake ili kuweza kuepuka migogoro na wazabuni na wadau wengine.

### 13.8.1 Madeni yanayotegemea Matukio (Contingent Liabilities)

Nashauri Serikali kuziagiza taasisi zake kuandaa mpango mkakati wa kuzuia vihatarishi ili kuhakikisha madeni yanayotegemea matukio yanadhibitiwa na kupunguzwa katika taasisi.

**13.9 Matokeo ya Kaguzi Maalumu na mambo Mengine**

Katika Ukaguzi Maalum wa Hesabu za Mpango wa Maboresho ya Serikali za Mitaa (LGRP II D by D) nilibaini matumizi yenye mapungufu mbalimbali kama vile kukosa viambatisho, kuwa nje bajeti na kutoidhinishwa yenye thamani ya Sh.988,133,904. Baadhi ya Matumizi hayakuzingatia matakwa ya Mpango wa Maboresho, hivyo kutishia kuathiri Malengo ya Mpango wa Maboresho.

Nazishauri Taasisi za Utekelezaji na wadau wa maendeleo kuchukua hatua kwa kufanya uchunguzi wa kina katika mapungufu yote yaliyobainika.

Na kutokana na Ukaguzi Maalumu wa fedha zinazotumwa na Wizara ya Elimu kwenda kwenye taasisi zilizopo chini yake, nilibaini kuwa, kutokana na mfumo dhaifu wa ufuatiliaji, kiasi cha Sh. 476,820,735 hakikuweza kuingizwa kwenye vitabu vya taasisi husika.

Licha ya mapungufu haya kubainika katika Ukaguzi Maalum, nashauri Serikali kupitia kwa Maafisa Masuuli kuboresha mifumo ya udhibiti ya ndani kwa fedha zinazohamishwa kutoka Wizara kwenda kwenye Taasisi zilizopo chini ya Wizara na kubuni mbinu za kufanya ufuatiliaji ili fedha ziweze kuingizwa kwa usahihi kwenye hesabu za Taasisi husika.

Katika utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nchi za nje ya Diplomasia ya Uchumi, katika Ukaguzi wangu wa Balozi nilibaini changamoto mbalimbali kama nilivyoeleza katika Sura ya Kumi na Mbili; ambapo Serikali inatakiwa kuzifanyia kazi ili kuweza kufanikisha kwa ufanisi shughuli za Balozi pamoja na kuzingatia sheria na kutekeleza

maagizo ya Rais. Ofisi za Balozi hazina wafanyakazi wa kutosha katika kutekeleza Maagizo ya Rais. Nashauri wapelekwe kwa wafanyakazi wa kutosha pamoja na kujengewa uwezo ili kuweza kutoa huduma nzuri. Aidha, nashauri Serikali ipeleke fedha za kutosha na kwa wakati ili Balozi ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa muda uliokusudiwa.

### 13.9.1 Mapitio ya Mifumo ya Udhibiti wa ndani

Katika mapitio ya mifumo ya udhibiti wa ndani, nililenga katika kuangalia utendaji kazi wa Kamati ya Ukaguzi, utendaji kazi wa Idara ya Ukaguzi wa Ndani, udhibiti wa jumla wa mfumo wa Teknolojia ya Habari, mchakato wa kutathmini vihatarishi, pamoja udhibiti na uzuiaji udanganyifu. Nilibaini mapungufu mtambuka katika Wizara, Idara na Wakala kama yalivyoanishwa katika Sura ya Sita.

| Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | 11 | 4 | 3 | 4 | 0 | 0 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Msajili wa Hazina | 10 | 5 | 4 | 1 | 0 | 0 |
| Ofisi ya Rais-Tume ya Maadili | 10 | 8 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Bunge | 10 | 4 | 3 | 2 | 1 | 0 |
| Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi | 10 | 4 | 5 | 0 | 0 | 1 |
| Wizara ya Africa Mashariki | 10 | 6 | 1 | 0 | 3 | 0 |
| Idara ya Polisi | 9 | 0 | 5 | 4 | 0 | 0 |
| Wizara ya Uchukuzi | 9 | 3 | 4 | 2 | 0 | 0 |
| Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira Utumishi Wa Umma | 9 | 3 | 3 | 3 | 0 | 0 |
| Sekretarieti ya Mkoa Dar Es Salaam | 9 | 6 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Sekretarieti ya Mkoa Mara | 9 | 5 | 3 | 1 | 0 | 0 |
| Tume ya Kuzuia UKIMWI | 9 | 6 | 1 | 1 | 1 | 0 |
| Ubalozi wa Tanzania, Kinshasa,Congo | 9 | 1 | 1 | 3 | 4 | 0 |
| Ubalozi wa Tanzania, Abuja | 9 | 8 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Ubalozi wa Tanzania, Bujumbura | 9 | 3 | 3 | 3 | 0 | 0 |
| Ofisi Binafsi ya Waziri Mkuu | 8 | 2 | 3 | 3 | 0 | 0 |
| Tume ya Kuzuia Madawa ya Kulevya | 8 | 6 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Ubalozi wa Tanzania, in Brussels,Ubelgiji | 8 | 1 | 3 | 4 | 0 | 0 |
| Tume ya Huduma za Mahakama | 7 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Ofisi ya Rais Ikulu | 7 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 7 | 3 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Wizara ya Ujenzi | 7 | 3 | 3 | 1 | 0 | 0 |
| Ubalozi wa Tanzania, Harare | 7 | 2 | 2 | 2 | 0 | 1 |
| Ubalozi wa Tanzania, Kigali | 7 | 0 | 6 | 1 | 0 | 0 |
| Ofisi ya Makamu wa Rais | 6 | 4 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Wizara ya Fedha | 6 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Ubalozi wa Tanzania, Adis Ababa-Ethiopia | 6 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Kitengo cha uchunguzi wa Fedha | 5 | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Sekretarieti ya Mkoa Geita | 5 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Ofisi ya Rais,Tume ya Mipango | 5 | 4 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Ubalozi wa Tanzania, Geneva | 5 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Tume ya Pamoja ya Fedha | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Idara ya Hazina | 4 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Technologia | 4 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Ubalozi wa Tanzania, Heague | 2 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **2094** | **803** | **666** | **444** | **119** | **62** |

**Kiambatisho Na.3.3 Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa Wakala**

| Jina la Mkaguliwa | Jumla | Yaliyotekelezwa | Yaliyo katika utekelejaji | Ambayo hayajatekelezwa | Yanayotegemea matukio mengine | Yanayojirudia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wakala wa Majengo Tanzania | 31 | 1 | 21 | 9 | 0 | 0 |
| Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini | 28 | 11 | 16 | 0 | 1 | 0 |
| Wakala wa huduma za ugavi na manunuzi (GPSA) | 26 | 11 | 15 | 0 | 0 | 0 |
| Taasisi ya Uhasibu Tanzania | 25 | 18 | 5 | 2 | 0 | 0 |
| Wakala wa Chakula cha Akiba Taifa | 24 | 8 | 12 | 2 | 0 | 2 |
| Wakala wa magari ya mwendo kasi DSar es salaam (DART) Dar Es Salaam | 22 | 8 | 14 | 0 | 0 | 0 |
| Wakala wa Mbegu za Kilimo | 21 | 5 | 7 | 9 | 0 | 0 |
| Wakala wa Vipimo Tanzania | 24 | 6 | 10 | 2 | 0 | 6 |
| Wakala wa Ufundi wa Mitambo, Magari na Umeme Tanzania | 17 | 8 | 9 | 0 | 0 | 0 |
| Wakala wa Huduma za Ajira Tanzania | 17 | 5 | 0 | 12 | 0 | 0 |
| Chuo cha Utumishi wa Umma | 14 | 9 | 3 | 1 | 1 | 0 |
| Wakala wa Nyumba na Utafiti wa Majengo Tanzania | 13 | 1 | 5 | 7 | 0 | 0 |
| Wakala wa Huduma za Misitu | 12 | 9 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Wakala Wa Uchimbaji wa Visima na Mabwawa | 11 | 1 | 5 | 5 | 0 | 0 |
| Wakala wa Utafiti wa Miamba | 11 | 6 | 2 | 3 | 0 | 0 |
| Wakala wa Maabara za Serikali | 11 | 5 | 4 | 2 | 0 | 0 |
| Wakala wa Utabiri wa Hali ya Hewa Tanzania | 9 | 5 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Wakala wa Maendeleo na Usimamizi wa Elimu | 9 | 0 | 9 | 0 | 0 | 0 |
| Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo | 9 | 0 | 6 | 3 | 0 | 0 |
| Wakala wa Mafunzo ya Kimataifa | 7 | 3 | 3 | 0 | 1 | 0 |
| Chuo cha Usimamizi na Maendeleo ya Maji | 6 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Wakala wa Usalama na Afya Kazini (OSHA) | 5 | 1 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Wakala wa Elimu ya Uvuvi na Mafunzo | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wakal wa ndege za Serikali Tanzania | 4 | 1 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Chuo cha Taifa cha Utalii | 4 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Wakala wa Umeme Vijijini | 3 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **367** | **132** | **162** | **62** | **3** | **8** |

**Kiambatisho Na 3.4: Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa taasis nyinginezo na Mifuko maalumu**

| Jina la Mkaguliwa | Jumla | Yaliyotekelezwa | Yaliyo katika mutekelezaji | Ambayo hayajatekelezwa | Yanayotegemea matukio mengine | Yanayojirudia |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za wanyonge Tanzania-MKURABITA | 21 | 16 | 4 | 1 | 0 | 0 |
| Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela | 18 | 7 | 7 | 2 | 2 | 0 |
| Taasisi ya Sheria kwa Vitendo | 17 | 12 | 4 | 0 | 1 | 0 |
| Chuo cha Utumishi wa Mahakama | 13 | 5 | 8 | 0 | 0 | 0 |
| Mfuko wa udhamini wa pembejeo za Kilimo | 9 | 5 | 3 | 1 | 0 | 0 |
| Bodi ya Bonde la Maji Wami/Ruvu | 9 | 4 | 2 | 3 | 0 | 0 |
| Bodi ya Bonde la Maji Pangani | 9 | 5 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Bodi ya bonde la Maji Rufiji | 8 | 3 | 3 | 1 | 1 | 0 |
| Mfuko wa Misitu Tanzania | 7 | 4 | 3 | 0 | 0 | 0 |
| Taasis ya Uongozi | 6 | 4 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mpango wa Kujitathimini katika nchi za Afrika | 6 | 0 | 4 | 2 | 0 | 0 |
| Ofisi ya Bunge la Katiba | 6 | 4 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake | 6 | 2 | 1 | 3 | 0 | 0 |
| Mfuko wa Maji | 6 | 2 | 2 | 2 | 0 | 0 |
| Mfuko wa Mikopo Hazina | 6 | 2 | 4 | 0 | 0 | 0 |
| Bodi ya Bonde la Maji ya Ziwa Victoria | 6 | 3 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Chuo cha maendeleo ya Jamii Tengeru | 5 | 1 | 3 | 0 | 0 | 1 |
| Mfuko wa maendeleo ya haki ya Utafiti wa mbegu za miti | 5 | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 |
| Mfuko wa Taifa wa mambo ya kale | 4 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chuo cha Wanyama Pori Pasiansi | 3 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Wakala wa Umeme Vijijini | 3 | 1 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mfuko wa Kukagua na Kusimamia Vyama vya Ushirika | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **183** | **93** | **57** | **28** | **4** | **1** |

## Kiambatisho Na 3.5: Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Ripoti ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa miaka ya nyuma

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| | **2006/2007** | | |
| 1 | **Udhaifu katika kusimamia dhamana za Serikali** Wizara inashauriwa kupitia Sheria na Kanuni na kufanya marekebisho katika kuhakikisha sheria na Kanuni zinaendana na hali ya sasa | Marekebisho yamefanyika kwenye sera za Madeni,Mikopo na Dhamana za serikali.Sheria Na.30 ya 1974 imefanyiwa marekebisho na itawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa hivi karibuni. Mkakati wa Madeni pia umerekebishwa | Marekebisho juu ya Sheria Na 30 ya 1974 pamoja na mapitio ya Mkakati wa Madeni ya Taifa (NDS) yanasubiliwa |
| 2 | **Fedha zilizotolewa kuagiza bidhaa nje ya nchi ambazo hazijarudishwa Serikalini.** Tunaendelea kusisitiza kwamba, Wizara ifanye juhudi ikishirikiana na mkusanyaji wa madeni ya Serikali kusisitiza makusanyo ya kiasi kilichobaki cha JPY 16,699,499,858 na kuwasilisha maendeleo yaliyofikiwa kwa ajiri ya ukaguzi. | Kamati ya Kudumu ya Bunge ilisitisha hii huduma.Bado tunasubilia maelekezo kutoka kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge | Serikali inashauriwa kufanya ufuatilianji ili kupata utaratibu kutoka kwenye Kamati ya Bunge |
| | **2008/2009** | | |
| 3 | **Kutoandika kwa usahihi mikopo iliyotolewa na serikali kama dhamana** Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwasilisha makubaliano hayo yaliofikiwa baina ya Serikali ya Tanzania na Makampuni hayo ya maua, ratiba ya ulipaji mikopo pamoja na vielelezo vingine vinavyoonesha kuanza kulipwa kwa mkopo. | Makubaliano hayo yaliofikiwa baina ya Serikali na Makampuni hayo ya maua pamoja na vielelezo vingine vya msingi viwasilishwe ofisi ya ukaguzi kwa ajili ya uhakiki. | Nyaraka za makubaliano zinasubiliwa |
| | **2010/2011** | | |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 4 | **Madeni na Mihadi**<br>Mamlaka ya mapato Tanzania inatakiwa kuongeza ukusanyaji wa mapato na Hazina ihakikishe fedha zinatolewa kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji washughuli zilizopangwa kwenye bajeti | Serikali itaongeza juhudi ili kuboresha mikakati ya ukusanyaji wa mapato kuwezesha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa,kupitia mwendelezo wakurasimisha sekta isiyo rasmi ili kuingiza katika wigo wa kodi.Taasisi za Umma, Wakala za Serikali na Mamlaka ambazo hukusanya mapato yasiyo ya kodi kupeleka mapato yote iliyokusanya kupitia mpango wa mabakizo (retention schemes) kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali.Wizara, Idara zinazojitegemea,Mikoa, Manispaa, Halmashauri ya Jiji,Wakala na Mamlaka ambazo zinakusanya ada na ushuru zimeamuliwa kuanzisha mashine za EFD ili kupunguza upotevu wa mapato.Wakala wa Serikali ulioanzishwa chini ya Sheria ya Wakala wa Serikali, Shirika la Umma lililoanzishwa chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma, au taasisi ya umma itawasilisha bajeti ya mapato na matumizi kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uchunguzi na kibali. | **U t e k e l e z a j i unaendelea** |
| 5 | **Mali zisizoingizwa katika daftari la kudumu la mali**<br>Mlipaji Mkuu wa Serikali anatakiwa kuonyesha hatua (ratiba) za utekelezaji wa ushauri huu.Daftari la mali za kudumu linatakiwa kuwa tayari kabla ya mwaka 2016/2017 ambapo serikali itakuwa inatumia viwango vya kufunga Hesabu vya kimataifa (IPSAS) | Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali inafanya maandalizi juu ya rejista ya Mali za Serikali itakayojumuisha mali zote | U t e k e l e z a j i unaendelea |
| | **2011/2012** | | |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 6 | **Deni la Shirika la ndege (ATCL)**<br>¤Ninapendekeza hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya waliohusika katika kuiingiza Serikali katika biashara isiyozaa matunda ambazo zimesababisha Serikali kudaiwa limbikizo la deni la dola za Marekani<br>41,466,177.16 kuanzia 26/10/2012; na<br>¤ Kuanzia tarehe 26/10/2012 deni limekuwa likiongezeka mpaka kufikia dola za<br>Marekani 41,466,177.16 kutoka dola<br>39,000,000 Serikali inapaswa kujadili hili deni na kampuni ya Wallis kama kuna uwezekano<br>wa kulifuta kwa vigezo kwamba, Serikali haikufaidika na biashara hiyo | Uchunguzi unafanywa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).Uongozi utawasiliana na Wakaguzi juu ya hatua zilizochukuliwa baada ya TAKUKURU kukamilisha uchunguzi.Taarifa ya gharama za uendeshaji wakati Ndege zinafanyakazi na wakati zilikuwa hazifanyikazi iko tayari na itawasilishwa kwa Wakaguzi kwa ajili ya uhakiki.Maandalizi ya kuandaa andiko kwa ajili ya kuidhinishwa na Baraza la Mawaziri yanaendelea.Kwa sasa kamati ndogo iko kwenye Mazungumzo na wadai wa ATCL juu ya kupunguza deni kabla ya kuomba kibali cha Baraza la Mawaziri. | Haijatekelezwa |
| 7 | **Malipo ya matibabu nje ya nchi yasio na nyaraka za viambatisho kiasi cha Sh. 448,144,343**<br>Afisa Masuuli katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii anatakiwa kuboresha udhibiti wa ndani katika matumizi ya wizara na kuhakikisha kwamba, nyaraka zote zilizotakiwa zinazohusiana na matibabu ya nje zinawasilishwa kwa ukaguzi. | Matumizi hayo yanahusiana na Malipo katika Balozi mbalimabli kwa ajili ya kutibu viongozi wa Rais na kulipa ankra.Orodha ya wagonjwa waliotibiwa nje na risiti za kukiri kupokea fedha kutoka kila Balozi zilipokelewa na Wizara ya mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kuziwasilisha kwa wakaguzi kwa ajili ya uhakiki.Pia Wakaguzi watatembelea Balozi husika kwa ajili ya kufanya uhakiki | Hoja ipo kwenye utekelezaji. |
| | **2012/2013** | | |
| 8 | **Usimamizi wa manunuzi**<br>Ukaguzi ulibaini mapungufu yanayojirudia katika shughuli za manunuzi.Hivyo napendekeza:<br>• Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA) kuendesha semina kadhaa kwa lengo la Kujenga uwezo kwenye kitengo cha manunuzi, Bodi ya Zabuni, Maafisa Masuuli na Idara mbalimbali juu ya umuhimu wa kutekeleza Sheria ya Manunuzi na kanuni zake<br>• Pia ni muhimu kuwa na mfumo wa usimamizi wa taarifa za manunuzi katika kufanikisha shughuli za manunuzi. Mfumo huu uwe unasimamiwa na Mamlaka ya udhibiti wa manunuzi ya umma. Mamlaka hii inatakiwa kuhakikisha kwamba, mfumo huu ni rafiki kwa watumiaji wa mwisho ili kwamba, Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za Mikoa watumie mfumo huu kwa urahisi katika kuboresha shughuli za manunuzi. | Sheria ya manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011 imeipa jukumu Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma kuzijengea uwezo idara za manunuzi,Bodi za wazabuni,Afisa Masuuli na idara za watumiaji juu ya kuzingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma. Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma imepitia mfumo wa usimamizi wa manunuzi ya umma ambao utaanza kutumika June, 2015 | Utekelezaji wake unaendelea |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 9 | **Kutofanyiwa kazi kwa changamoto ya upungufu wa Wafanyakazi katika Wizara ,Idara na Wakala wa Serikali**<br>Ukaguzi ulibaini upungufu mkubwa wa wafanyakazi ikilinganishwa na ikama ya<br>watumishi katika taasisi.Kwa hiyo.Ninapendekeza:<br>Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO- PSM) ipitie upya ikama za Wizara, Idara na Wakala wa Serikali kuja na mapendekezo halisi ya<br>• idadi ya watumishi wanaohitajika.<br>• Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali wanapaswa kuhakikisha kwamba, wana idadi ya kutosha ya watumishi wenye sifa stahiki. Uhaba wa watumishi unapaswa kutolewa taarifa kwa mamlaka husika ikiwa ni pamoja na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa umma | Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Management ya Utumishi wa Umma imetoa mwongozi kwa waajiri kwa Mwaka 2014/15 ili kuwa ina ajiri kulingana na mahitaji ya wafanyakazi.Lengo kuu ni kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2008/09 na 2013/15 Serikali kuu na Serikali za mitaa zilikuwa na uhaba wa watumishi 373,280.Mchanganuo wa mgawanyo uko kama ifuatavy o:Elimu(183,299),Afya(54,370),Kilimo (11,288), Mifugo 7,926) na wengineo (116,397).Hatahivyo sio rahisi kumaliza tatizo la uhaba wa wafanyakazi kwa sababu za kibajeti.Hivyo Serikali itaendelea kuajiri kadri bajeti itakavyoruhusu. | U t e k e l e z a j i unaendelea |
| 10 | **Malipo ya mishahara kwa watumishi hewa**<br>Baada ya kubaini uwepo wa mishahara iliyolipwa kwa watumishi hewa ,napendekeza kwa serikali kwamba,:<br>▫ Ili kuepuka upotevu kama huu katika siku zijazo, Maafisa Masuuli katika Wizara,Idara na Mikoa husika wanapaswa kuangalia taarifa za mishahara ya watumishi wao mara kwa mara na kuthibitisha uhalali wa watumishi wote kabla ya malipo. Mawasiliano pia lazima kuimarishwa ili kuhakikisha kwamba, majina ya wastaafu, watoro/walioacha kazi au walioachishwa kazi yanafutwa katika taarifa za wafanyakazi mara moja.<br>▫ Mbali na hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha mishahara isiyolipwa kwa watumishi ambao muda wao wa utumishi umekoma kwa sababu moja au nyingine inarudishwa Hazina kwa wakati kulingana na maagizo.<br>▫ Zaidi ya hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa Mfumo wa kutunza taarifa za watumishi (HCMIS-LAWSON) unafanya kazi na unatumika kikamilifu ili kupata thamani ya fedha tarajiwa. | Serikali ilianzisha Mfumo wa usimamizi wa Raslimali watu(LAWSON).Mfumo huu umesaidia kupunguza idadi ya watumishi 6i,i36 kufutwa kwenye orodha ya wafanyakazi | Utekelezaji wake unaendelea |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 11 | **Usimamizi wa Matumizi**<br>Baada yakubaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, ninapendekeza kwamba,: Maafisa Masuuli wa Wizara/Idara, Mikoa na Balozi wanapaswa kuhakiki malipo yote na kuyathibitisha kuwa halali na yana nyaraka sahihi kama matakwa ya Kanuni za Fedha za Umma ya 2001, Kanuni ya 95 (4) inavyosema. Uangalizi wa ndani unahitaji kuboreshwa ikiwa ni pamoja na ukaguzi wa awali wa ndani | Waraka Na. 4 wa mwaka 2014/15 ulitolewa ili kuweka msisitizo wa kuhakikisha miamala na mambo mengine juu ya ufungaji wa mahesabu yanazingatiwa | Utekelezaji unaendelea |
| 12 | **Utendaji katika Balozi**<br>Mapungufu mbalimbali yalionekana katika shughuli za Balozi nje ya nchi. Kwa hivyo ninapendekeza kwamba,:<br>• Balozi husika zikishirikiana na Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa(MFAIC) zinatakiwa kusitisha malipo ya posho kwa maafisa wastaafu na kufanya utaratibu wa kuwarudisha nyumbani haraka pindi utumishi wao unapokoma.<br>Napendekeza mamlaka husika kuangalia ni jinsi gani zitakavyoweza kurudisha fedha zilizolipwa maafisa wasiostahili katika Balozi. | Uongozi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje inafanya tathimini juu ya uwezekano wa kutenga fedha katika bajeti ili kuchochoea diplomasia ya uchumi na kuongeza utalii ambao unategemea sana na upatikanaaji wa rasilimali | Utekelezaji unaendelea |
| | • Menejimenti ya Balozi iwasiliane na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa ajili ya kuwarejesha nchini watumishi waliomaliza utumishi wao ambao bado wanaendelea kuishi uBalozini na wale ambao wamekaa kituo kimoja muda mrefu wabadilishwe.Hii itakuwa ni chachu katika utoaji wa huduma kwa Balozi zetu.<br>• Menejimenti ya Wizara ya Mambo ya nje na Ushirikiano wa Kimataifa ione uwezekano wa kuanzisha mfuko katika bajeti yake kwa ajili ya kufanya shughuli za diplomasia ya kiuchumi na kukuza vivutio vya utalii, kwa kuzingatia kwamba, hii ni kazi muhimu kwa uchumi wa nchi. | | Utekelezaji unaendelea |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 13 | **Uendeshaji wa Hospitali Teule na Hospitali za Rufaa**<br>Wakati wa ukaguzi maalum, nilibaini mapungufu kadhaa za kiutendaji katika hospitali teule na rufaa, kwa hivyo ninapendekeza kwamba,:<br>• Wizara ya Afya inapaswa kuhakikisha kuwa fedha zote zinapohamishwa kwenda hospitali mbalimbali zinaambatana na mchanganuo wa matumizi yake badala ya utaratibu wa sasa usioainisha malengo ya fedha hizo kama ilivyodhihirika wakati wa ukaguzi.<br>• Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na Hazina ni muhimu waboreshe mawasiliano na menejimenti za Hospitali husika kuhakikisha kuwa watumishi hewa wanafutwa kwa wakati katika mfumo wa ajira serikalini makubaliano ya mkataba kati yao na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | Wizara imewasiliana na hospitali zote teule nchini kwa barua yenye kumbukumbu Na. HC.209/320/01 ya tarehe 30 Octoba, 2013 na kuwataka kurejesha Wizara ya fedha mishahara yote amabyo haikustaili kulipwa. | Imetekelezwa |
| 14 | **Vocha za Pembejeo za Kilimo (NAIVS)**<br>Kufuatia changamoto nilizozibaini wakati wa ukaguzi, ninapendekeza uboreshaji wa mpango huu wa NAIVS katika maeneo yafuatayo;<br>• Kuwashirikisha Maafisa ugani wa kilimo,mawakala wa Mbegu na Taasisi za utafiti wa Kilimo kupitia upya na kutathmini aina za mbegu na mbolea zinazosambazwa nchini,<br>Pia kudhibiti mbegu na mbolea bandia<br>• Kuhakikisha kwamba, ununuzi na usambazaji wa vocha unafanyika kwa wakati muafaka.Utafiti wa kutosha wa aina za udongo unafanyika kwanza kabla ya utoaji wa hati za mbolea ili kuhakikisha pembejeo zinazotolewa zinaendana na aina ya udongo wa mahali husika.<br>Kubuni mwongozo kazi rahisi wa namna ya utekelezaji wa mpango huu(ukiwa katika lugha ya Kiswahili)ukianisha vizuri na kuelezea namna nzuri ya utunzaji wa nyaraka, na utoaji wa taarifa za mara kwa mara zilizo fanyiwa | Wadau mbalimbali wakiwemo Maafisa ugani,Mamlaka ya udhibiti wa mbolea Tanzania,Wakala wa Mbegu za Kilimo,Taasisi ya kuthibitisha mbegu na Taasisi za utafiti wa Kilimo wamekuwa wakishirikishwa kikamilifu katika ku pitia,kupanga,kutathimini,kupendekeza mbegu na Matumizi ya Mbolea na upatikanaji wa pembejeo bora ikijumuisha mbegu na mbolea kwa matumizi ya baadaye | Imetekelezwa |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 14 | usuluhishi(reconciliation)na taarifa nyingine mbalimbali. Wakulima wakumbushwe na wapewe taarifa za kutosha jinsi mfumo wa vocha unavyofanya kazi na faida zake katika kuhimiza matumizi ya mbegu bora na mbolea | | |
| 15 | **Ununuzi wa Kivuko cha Misungwi**<br>Mapungufu kadhaa yalibainika katika Ukaguzi maalum wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi;Napendekeza Hatua stahiki zichukuliwe dhidi ya maafisa wa umma walioshindwa kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi kivuko cha Misungwi na hatua za kisheria zichukuliwe dhidi ya mzabuni M/S Sinnautic international ambaye alishindwa kutekeleza kazi zote za kuleta vipuri vya thamani ya Euro 41,140 za kivuko cha Misungwi kwa mujibu wa mkataba. | Hatua zimeshachuliwa dhidi ya maafisa wa umma ambao walishindwa kusimamia utekelezaji wa mkataba wa ununuzi wa kivuko cha Misungwi. Wizara ya Ujenzi kupitia kumbukumbu namba AB 13/179/07/42 ikimwagiza Mzabuni ailipe Wizara, kiasi cha Euro 41,140 ikiwa ni thamani ya vipuri na vifaa ambavyo havikuletwa katika mkataba wa ununuzi wa kivuko. Wizara itashirikiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuangalia utaratibu wa kuchukua hatua zaidi za kisheria dhidi ya Mkandarasi | Mpaka sasa Vipuri havikupokelewa kwa ajili ya kivuko. hatua za kisheria zinapaswa kutekelezwa |
| 16 | **Kituo cha mafunzo ya uuguzi Mkomaindo**<br>Kutokana na Ukaguzi maalum uliofanywa katika kituo cha mafunzo ya uuguzi Mkomaindo, nashauri uongozi wa kituo<br>kuimarisha mfumo wa udhibiti wa ndani ikiwa ni pamoja na kuboresha utunzaji wa<br>kumbukumbu. | Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imeendelea kuimarisha udhibiti yake ya ndani kwa Taasisi za Afya wake wote kwa kuanzisha mwongozo kwa ajili ya usambazaji wa bidhaa na huduma, malipo na makusanyo ya ada. mwongozo unataka kwamba, vifaa vyote mara baada ya kununuliwa viingizwe kwenye vitabu..Pia, vitabu vyote vya kupokeleaa zitachukuliwa kutoka Hazina ndogo. Mwongozo utatolewa kwa Wakaguzi kwa ajili ya uhakiki | Imetekelezwa |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 17 | **Utayari wa Serikali katika utekelezaji wa IPSAS yaani Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu kwa Taasisi za Umma**<br>• Kutenga rasilimali fedha na watu wa kutosha katika kurahisisha utendaji usio na vikwazo kwa zoezi hili,<br>• Ninashauri Serikali kuzingatia kikamilifu IPSAS 25(Mafao ya Wafanyakazi yanayofadhiliwa yote na mwajiri)inayohitaji kufanyika tathmini ya uwezo wa Mfuko ili kubaini kiwango cha deni la wanaodai wastaafu litakaoingizwa katika taarifa za hesabu za mwaka,<br>• Kuanzisha kamati ya kitaifa ya kuratibu utekelezaji wa IPSAS ambayo itashirikisha wataalam na wadau mbalimbali ambao watakuwa wasimamizi wa jukumu hili kwa miaka mitano ili kuhakikisha kila hatua inatekelezwa kwa umakini na kwa wakati.Hadi sasa mwaka mmoja umepita na imebaki miaka minne,<br>• Mhakiki Mali wa Serikali anapaswa kufanya kazi kwa karibu na wadau ili kuhakikisha utekelezaji wa mpango wa kuhamia IPSAS isiyo taslimu unazingatia IPSAS17,pia kufanya mabadiliko muhimu katika Taarifa za Fedha yanayo husu kutenganisha ardhi na majengo katika makundi mawili tofauti,<br>• Serikali inashauriwa kuanzisha mchakato wa kutengeneza ripoti ya fedha ya mwaka iliyounganisha taarifa za fedha za taasisi zake zote zikiwemo Serikali za Mitaa na vyombo vingine vilivyo chini yake,<br>• Kuboresha mfumo wa EPICOR na wa bajeti ili uweze kumudu kutengeneza ripoti za mwaka zinazokidhi matakwa ya viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu, | Tathimini ya mali katika Serikali za Mitaa inasubiri mapitio Sheria ya Fedha ya Umma ambayo itatoa mamlaka kisheria kwa Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali juu ya Usimamizi wa Mali katika Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na hesabu,<br>• Wizara ya Fedha iko katika mchakato wa kuandaa Juhudi za pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba & Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Ujenzi (kupitia Wakala wa Majengo) ili kuhakikisha maandalizi ya hati miliki kwa Wizara na Sekretariat za mikoa zinapatikana,<br>• Nia ya serikali ni kuhakikisha kuwa vipengele vyote vya mfumo jumuifu wa Usimamizi wa fedha(IFMS) unaamushwa(Activated) na kutumika ipasavyo.<br>• Hivi sasa Serikali inakamilisha uboreshaji wa mfumo jumuifu wa usimamizi wa fedha (IFMS / Epicor) kwa ajili ya maandalizi ya IPSAS Uhasibuusiotumiataslimu(Accrualaccounting).Pianimpangowaserikali ya kuanza kutumia moduli/vipengele ambazo hazijaanza kutumika.<br>• Mafunzo ya EPICOR toleo 9.05 yalifanyika kwa kwa Wahasibu wakuu, Wahasibu wa Mikoa, Wakuu wa Hazina ndogo, waingizaji wa taarifa na waandaaji wa taarifa za fedha za Wizara, na Sekretariat za Mikoa .Hatahivyo , mafunzo ni zoezi endelevu.<br>• Mafunzo juu ya matumizi ya EPICOR 9.05 yalifanywa na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali katika mwaka wa fedha 2014/2015 juu ya matumizi ya EPICOR (Asset Management Module), | U t e k e l e z a j i unaendelea |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| | • Mlipaji Mkuu wa Serikali ahakikishe Sheria ya Fedha ya Umma iliyorekebishwa na inaanza kutumika,<br>• Serikali ihakikishe Hati milki za Ardhi na Majengo yanayomilikiwa na Wizara, idara, wakara na sekretarieti za mikoa zinafuatiliwa mara moja ili kuwa na ushahidi wa umiliki wa mali hizo,<br>• Napendekeza kwamba, Menejimenti za Wizara, Idara, Wakala na Sekretarieti za mikoa kwa kushirikiana na Hazina ihakikishe kwamba, modules zote za IFMS zinarekebishwa na zinatumika kikamilifu. Na pia mafunzo yafanyike pale inapohitajika haswa wakati kuna waajiriwa wapya na kunapokuwa na maboresho mapya katika mfumo wa kihasibu,<br>• Serikali itoe mafunzo jinsi ya kutumia EPICOR 9.05 na viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu,<br>• Kuanza kutumika kwa viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu kabla ya marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Umma Na. 6 ya 2001 (iliyolekebishwa 2004), hivyo Sheria ya Fedha ya Umma inakinzana na falsafa ya viwango vya uhasibu vya kimataifa visivyo vya taslimu | • Serikali inaendelea na mageuzi mbalimbali ya fedha ambayo yamesababisha mapitio ya sheria ya Fedha za Umma ya 2001 (iliyorekebishwa 2004) ambayo itajumuisha changamoto zinazotokana na mageuzi hayo.<br>• Hivi sasa rasimu ya pili ya Sheria mpya imetolewa kwa mamlaka ya juu kwa ajili ya mapitio na mapendekezo. | |
| 18 | **Ufuatiliaji na tathmini ya miradi inayotekelezwa kwa fedha za mikopo**<br>Kuna ongezeka la mikopo ya miradi ya maendeleo ambayo ni kipaumbele cha Taifa hivyo Naishauri Serikali kuanzisha utaratibu maalum wa ufuatiliaji na kutathmini miradi ambayo imetekelezwa na inayotekelezwa kwa kutumia fedha za mikopo. Hali hii itasaidia kufanya<br>tathmini ya matokeo ya miradi kadiri<br>inavyoendelea.Hii itasaidia kupunguza hali ya sintofahamu kati ya Wadau na Serikali | Idara ya bajeit chini ya Wizara ya Fedha imeanzishwa kwa lengo la kufuatilia muenendo wa matumizi bora ya fedha za Serikali za miradi mbalimabli ili kuhakikisha yanazingatia thamani ya fedha | Imetekelezwa |
| 19 | **Kukosekana kwa Ofisi ya Usimamizi wa Madeni:**<br>Haja ya kuanzisha Ofisi ya Usimamizi wa Madeni ni moja ya suala muhimu ambalo nilizungumzia katika mwaka wa fedha 2010/2011. Nashauri Serikali kutilia mkazo uanzishwaji wa Ofisi ya Usimamizi wa Madeni (DMO) ili kuweza kukabiliana kimamilifu na kwa ufanisi kuratibu shughuli za usimamizi wa madeni. | Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitoa taarifa Na. 494 ya tarehe 17 Desemba 2010. Katika chombo hicho Rais aliunda Wizara ya Fedha ambayo miongoni mwa mambo mengine ilipewa mamlaka ya kusimamia mikopo na sera za mikopo na utekelezaji wake.Wizara ya fedha ilitumia chombo hicho kuanzisha Idara ya usimamizi wa madeni | Imetekelezwa |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 20 | **Kubadilisha Hati za Ukwasi(Liquidity Papers) kugharamia nakisi ya bajeti**<br>Nashauri Serikali kujiepusha na kubadili hati za ukwasi ili kuepuka uwezekano wa kuwa na deni kubwa siku za usoni lisilolipika. Iko haja ya Serikali kuchukua hatua za makusudi ikiwa ni pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kupunguza matumizi, na makadirio ya bajeti yenye ufanisi. | Serikali inakubaliana na mapendekezo ya Wakaguzi katika siku za usoni kusitisha kubadilisha hati za ukwasi kwenda kwenye hati za fedha mpaka pale patakapokuwapo sababu ya msingi ya kufanya hivyo.<br>Kwa lengo la udhibiti, Mabadiliko yatapaswa kupata kibali kutoka Mamlaka za juu za Serikali. | Haijatekelezwa |
| 21 | **Kutolewa migao ya fedha mwishoni mwaka wa fedha**<br>Ili kukabiliana na changamoto ya fedha zilizoidhinishwa kutotolewa kwa wakati,Nashauri Serikali kutengeneza makisio yake ya mwaka yakishabihiana na makusanyo ya mapato ili kuzuia kutolewa kwa kiasi kikubwa cha fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha. Kwa kufanya hivyo, inatarajiwa kwamba, shughuli zilizopangwa zitatekelezwa kama mpango kazi ulivyo na makusanyo ya mapato. | Kutolewa kwa fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha ni kutokana na changamoto katika utekelezaji wa bajeti | Utekelezaji unaendelea |
| 22 | **Usimamizi wa Forodha na Maghala ya Mali (customs bonded warehouses) ambazo hazijalipiwa kodi**<br>Nilibaini mapungufu mbalimbali katika usimamizi wa forodha na maghala ya mali.Hivyo, ninaishauri Serikali kuhakikisha udhibiti wa kutosha kwenye uendeshaji wa maghala ya ushuru wa Forodha ili kukusanya madeni yote yatokanayo na kutokusanywa kwa ushuru wa forodha. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania inapewa wito wa kuzingatia na kutekeleza sheria zilizopo. | Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato ya Tanzania imeimarisha udhibiti juu ya uendeshaji wa Forodha na maghala ya mali. | Imetekelezwa |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 23 | **Tathmini ya Wakala wa Serikali**<br>Ukaguzi ulibaini mapungufu mbalimbali katika shughuli za Wakala wa Serikali. Hivyo ninapendekeza kwamba,:<br>• Wakala zote za Serikali ambazo zimeanzishwa kwa lengo la kutoa huduma kwa umma na wanapata mapato kutokana na huduma wanazotoa, niwakati muafaka kwao kushindana katika ulimwengu wa kibiashara kwa kuwa wabunifu zaidi na kuongeza ubora na kiwango cha huduma. Hii itaboresha makusanyo yao na kupunguza utegemezi kutoka Serikali Kuu katika suala la fedha.<br>• ¤Wakala ambazo zimeanzishwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa idadi kubwa ya wateja inapaswa kuzingatia faida ya kuwa na wateja wengi kama msingi wa kuongeza makusanyo yao.<br>• Ili kutoa huduma bora ni muhimu kuwa na wafanyakazi wenye taaluma na vifaa vya kufanyia kazi. Wizara mama ikishirikiana na Tume ya Utumishi wa Umma zihakikishe wakala zao zinajitosheleza kwa wafanyakazi wenye uwezo na vifaa/nyenzo muhimu za kufanyia kazi ambazo zitasaidia kuongeza kiwango cha huduma nakuboresha utoaji wa huduma zao kwa umma | Serikali kupitia sheria ya Wakala wa Serikali Sura. 245 na Waraka Na. C / CAC.45 / 257/01 /Temp./ 13 ya Oktoba 6, 2009 Wakala walipewa fursa ya kutangaza nafasi zao ili kuvutia akili bora/vipaji na ushindani kutoka sokoni ili kusimamia Mashirika ya kibiashara. | Imetekelezwa |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 24 | **Ulipaji wa kodi ya kupanga ofisi Sh. 7,895,872,337**<br>Kuna umuhimu wa Serikali kuwekeza katika ujenzi wa majengo yake yenyewe. Ninaishauri Serikali kuwa na mpango endelevu wa kujenga majengo kwa ajili ya ofisi za Serikali. Serikali inaweza kufanya yafuatayo ili kufanikisha jambo hili.<br>• Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo ya Tanzania (TBA) watafute maeneo ambayo Serikali inaweza kujenga Ofisi za Wizara, Idara na Wakala zake.<br>• Serikali ifanye majadiliano na Mifuko ya hifadhi ya Jamii ili waweze kupata mkopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya ujenzi wa majengo ya Serikali.<br>• Serikali pia ifanye mazungumzo na washirika wa maendeleo kama vile Benki ya Maendeleo ya Africa (AfDB) na Benki ya Dunia ili waweze kupata mikopo/misaada kwa ajili ya miradi ya ujenzi wa Ofisi hizo.<br>Kwa zile wizara, idara na wakala za Serikali ambazo zinakusanya mapato kutokana na shughuli zao, nashauri watumie mapato ya ndani ya wizara kuanza kujenga ofisi zao binafsi. | • Serikali kupitia wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya makazi na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu(CDA) imeanza kugawa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya serikali mjini Dodoma,<br>• Serikali kupitia Wizara ya Fedha itaanzisha mazungumzo na Taasisi za Fedha na Mifuko ya Ustawi wa Jamii ili iweze kutoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Serikali,Serikali itaendelea kununua majengo na viwanja kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Balozi zetu nje ya nchi. Majengo ambayo yameshanunuliwa ni pamoja na jengo lililonunuliwa Amerika na viwanja vilivyonunuliwa Kenya, Saudi Arabia na Qatar. | Utekelezaji unaendelea |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 25 | **Changamoto zinazokabili huduma ya magereza Tanzania**<br>Kutokana na changamoto inayoikabili Idara ya huduma ya magereza ya Tanzania ninapendekeza yafuatayo kwa Serikali na kwa idara ya huduma ya Magereza yenyewe.<br>• Mahakama ya Tanzania iharakishe kutoa maamuzi juu ya kesi zilizopo. Kuna idadi kubwa ya mahabusu katika magereza ambao wanasubiri kesi zao kusikilizwa na haki kutolewa na Mahakama. Kwa kukamilisha kesi zinazowakabili mahabusu kutasaidia kupunguza idadi ya mahabusu katika magereza,<br>• Serikali inaweza kuchagua kutumia njia nyingine ya kuwaadhibu wafungwa baada ya kupatikana na hatia. Serikali inaweza kuchagua kutumia njia mbadala kama wafungwa kutumikia kifungo cha nje cha kuanzia mwaka mmoja mpaka miwili chini ya uangalizi wa Mkuu wa wilaya au Mkoa huku akijishughulisha na shughuli za jamii kama usafi maofisini bila malipo (extra Mural labour), kifungo cha nje chini ya uangalizi cha miaka minne na kuendelea kutokana na makosa madogo madogo kwa wafungwa ambao tayari wametumikia theluthi moja(1/3) ya kifungo chao gerezani huku wakishughulika na huduma za jamii bila malipo(Parole). Hii kwa kiasi kikubwa itapunguza idadi ya mahabusu na wafungwa katika magereza,<br>• Kwa ajili ya wahalifu wadogo na wanaokiuka sheria ni bora kulipa faini na kama wao wakishindwa kulipa faini, wanapaswa kupelekwa kwa uongozi wa miji yao, au wilaya na kupewa kazi za jamii (communal based labour),<br>• Kuwa hudumia mahabusu na wafungwa kunasababisha gharama kubwa kwa Serikali. Kuwalisha, kuwapa mavazi na matibabu ni ghali. Uongozi wa Idara ya huduma ya Magereza unashauriwa kuboresha shughuli zao za uzalishaji kama useremala, shughuli za kilimo, ushonaji, ujenzi wa nyumba na mafundi mitambo na magari. Baada ya hapo watafute soko la bidhaa zao na hii itawawezesha kuwa na uwezo wa kujilisha na kujinunulia mavazi wenyewe,<br>• Idara ya huduma ya Magereza inahamasishwa kuandika juu ya mapendekezo kadhaa ya maendeleo na kutafuta wahisani mbalimbali kama Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Misaada la Marekani (USAID), nk ambayo watatoa fedha kwa ajiri ya kupanua na kuboresha magereza,<br>Uongozi wa idara ya huduma ya magereza unashauriwa kutoa wito kwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Serikali Kuu (PAC) na Viongozi wengine wa Serikali kutembelea magereza na kuona hali halisi katika magereza. Hii itawasaidia kufanya maamuzi sahihi juu ya mgao wa rasilimali. | Serikali kupitia Sheria ya Huduma za Jamii, Sheria ya kifungo mbadala(Parole act) na Magereza (Kinga ya ziada ya kifungo cha nje) Kanuni na Sheria zote hizi zinafanya kazi lakini idadi ya wafungwa ambao wanastahili ni wachache sana kutokana na masharti husika . Jitihada zinafanyika ili sheria zilizotajwa kufanyiwa marekebisho ili wafungwa wengi waweze kustahili. Hadi Aprili, 2015 jumla ya wafungwa 4,402 waliandikishwa chini ya kifungo mbadala(Parole)<br>Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge(PAC) wataalikwa kutembelea Magereza na kuona hali halisi ili waweze kuendelea kutoa ushauri juu ya uboreshaji wa Idara ya Magereza. | Utekelezaji unaendelea |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 26 | **Miradi ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP)**<br>Pamoja na faida ambayo inaweza kupatikana kutokana na mipango ya ubia kati ya sekta ya umma na binafsi, kuna baadhi ya hatari zinazohusiana na ubia ambayo ni muhimu zaidi kwa Serikali kuingilia kati. Ubia unaweza kuongeza gharama za uendeshaji, kutoa huduma chini ya kiwango, madhara katika maslahi ya umma, na kuanzisha fursa mpya kwa udanganyifu, kula njama, na rushwa.Ili kukabiliana na hatari hizi, napendekeza;<br>• Serikali inapaswa kubuni kupitia mchakato wa manunuzi na tathmini ambao utapima utegemezi na uadilifu wa washirika wenye uwezo.Tathmini hiyo inapaswa kuzingatia uchaguzi wa mshirika mwenye rekodi zilizothibitishwa katika maendeleo ya mradi kwa njia ya mchakato wa ushindani wa zabuni,<br>• Kwa kutambua umuhimu wa upembuzi yakinifu ili maslahi kwa pande zote mbili yaweze kutumika na mafanikio kupatikana, Serikali inapaswa kuunda Mfuko wa fedha za uwezeshaji wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) ili kuwezesha upembuzi yakinifu juu ya miradi muhimu ya utekelezaji. Pamoja na hayo, Serikali inahimizwa kuzindua juhudi kamili za uhamasishaji ili kushirikisha kikamilifu sekta binafsi katika miradi ya taifa yenye vipaumbele vinavyotambulika. Kuendelea kukosekana kwa fedha katika kufanya utafiti wa upembuzi yakinifu kunaweza kusababisha jambo lenye gharama kubwa sana,<br>• Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa masuala ya kugawana faida (ikiwa ni pamoja na uwezekano wa faida kwa siku zijazo kutokana na mauzo ya mali au uwekezaji) yanawekwa wazi katika makubaliano ya ushirikiano. Ni lazima pia kuhakikisha kwamba, maslahi ya nchi yanalindwa wakati mali zilizochangiwa zinaondolewa katika ushirikiano (kwa mfano kuhakikisha Serikali inapata sehemu ya mapato). Serikali pia inapaswa kuwa na uwezo wa kuthibitisha jumla ya gharama zilizoingizwa katika mradi ambayo zinatarajiwa kurudi wakati wa uhai wa mradi huo,Naishauri Serikali kwamba, inapaswa kufikiria kama mali zenye umuhimu wa kitaifa zinaweza kukodishwa kwa sekta binafsi badala ya kuhamishwa kabisa. Makubaliano ya ushirikiano wa namna hii yanaweza kutoa fursa kwa sekta ya umma kuingilia kati katika tukio kubwa la kushindwa katika utoaji wa huduma au kufilisika kwa mbia, | Tunakubaliana na mapendekezo ya wakaguzi.Viatarishi katika ubia wa sekta binafsi na umma vinaweza kudhibitiwa kwa kutumia mbinu mbili ambazo ni.:<br>1) Mchakato wa kupima uchambuzi yakinifu huwa unachambuliwa, ili kuhakikisha masuala ya kiufundi,kisheria,kiuchumi,kimazingira ,Kibiashara na uwezo wa kifedha yanazingatiwa.<br>2) Mchakato wa kuidhinisha hatua zote za ubia wa sekta binafsi na umma unazingatia mzunguko mzima wa shughuli za ubia.Hatua hii inajumuisha kuidhinisha uchambuzi yakinifu unaofanywa na Waziri wa fedha,kuidhinisha pendekezo la maombi na kuidhinisha Muundo wa fedha za ubia na mikataba ya Ubia wa sekta binafsi na umma .<br>Mbinu hizi tayari zimeanza kufanya kazi katika utekelezaji wa Ubia wa sekta binafsi na umma<br>Suala la kugawana faida ni muhimu sana katika ubia hasa katika miradi ya pamoja.Kwa miradi iliyotekelezwa baada ya kutunga sheria ya Ubia wa sekta binafsi na umma ya mwaka 2010 inataka mikataba yote kuaininsha namna ya kugawana faida na hasara katika miradi ya pamoja | Imetekelezwa |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| | • Serikali inapaswa kutathmini kama gharama zote za kushiriki ni halali. Uchambuzi makini lazima ulenge kushughulikia mgao sahihi wa athari zinazoweza kutokea katika mradi huo kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kuhusiana na mradi huo.Katika mipangilio yote ya ubia (PPP), chombo cha umma kinapaswa kuangalia athari zinazoweza kutokea na kuhakikisha kwamba, zinaweza kudhibitiwa ipasavyo,<br>• Serikali inapaswa kuwa makini katika ubunifu wa mkataba na majadiliano ili kuhakikisha kwamba, athari yoyote kutokana na matukio yasiyoonekana inagawanywa kati ya pande zote mbili na kwa mujibu wa viwango vya athari hiyo<br>• Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa makubaliano yanaruhusu habari ya utendaji kuwa zinatolewa, kulingana na mahitaji, kwa mbia wa sekta ya umma. Wakati Serikali inakuwa kama taasisi ya kutoa mkopo au mdhamini ni lazima kuomba taarifa za ziada kutoka kwenye upande inayoshirikiana nayo ili kuhakikisha usalama wa mkopo wake,<br>• Katika uchambuzi wa vihatarishi kabla ya kuingia katika ushirikiano, Serikali inapaswa kufikiria kwa makini na kuweka vifungu kwenye masharti ya mkataba (mfano kifungu kinachohusu uwezo wa kujitoa inapotokea utendaji mbovu bila upotevu wa fedha kama fidia) au kifungu kinachoruhusu kuwapo kwa mipango ya dharura (mfano kuuza hisa),<br>• Serikali inapaswa kulinganisha malipo ya mikataba na mafanikio ambayo yalikubalika kufikiwa na kiwango cha huduma zinazotolewa. | | |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 27 | **Sheria ya Miradi ya ubia kati ya Sekta ya Umma na binafsi haimpi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali uwezo wa taarifa za miradi hiyo**<br>• Sheria inapaswa kuhakikisha kuwa mkataba wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) na makubalianao ya kushirikiana katika uzalishaji(PSAs) yanamwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata rekodi za fedha na taarifa nyingine za mbia binafsi au kampuni iliyo katika mpango wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP),<br>• Pamoja na hayo, Serikali inapaswa kusaidia na kumpatia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu taarifa zote muhimu za mkataba wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi (PPP) katika maisha yote ya mradi tokea mchakato wa zabuni, kupewa rasmi mkataba na awamu ya uendeshaji wa mradi. Mwongozo Na. 3 wa Viwango vya Shirika la Kimataifa la Asasi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs) 5220 inasema kwamba, kuchunguza mradi na Taasisi kuu ya Ukaguzi (SAI) katika hatua zote za mradi inafaida zake endapo udhaifu wowote ukigundulika unaweza kurekebishwa kabla ya mkataba haujasainiwa na matatizo mabaya zaidi kuepukwa katika hatua ya baadaye,<br>• Serikali pia inapaswa kutoa taarifa mara kwa mara juu ya utendaji wa mradi kuonyesha wazi wazi kama mbia binafsi anatekeleza majukumu yake kwa mbia wa sekta ya umma ili hatari yoyote ya hasara itambulike mapema iwezekanavyo, kuwezesha Serikali/mbia wa sekta ya umma kufikiria namna bora ya kulinda maslahi yake. | | Imetekelezwa |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 28 | **Ukaguzi wa hesabu za Vyama vya Siasa**<br>Kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa ukaguzi wa vyama vya siasa napendekeza;<br>• Ili kuboresha utoaji wa taarifa, uwasilishwaji na ulinganifu wa utendaji wa vyama vya siasa, vyama vinatakiwa kuandaa taarifa za hesabu kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vya kimataifa. Kuanza kutumika kwa mfumo mmoja wa taarifa za kihasibu utasababisha kufanana kwa taarifa za hesabu za vyama vya siasa. Hii inawezekana pale ambapo Msajili wa vyama vya siasa akishirikiana na Mhasibu Mkuu wakitoa mwongozo wa aina ya muundo wa taarifa za fedha utakaotumiwa na vyama vya siasa,<br>Napendekeza Serikali irekebishe sheria ya vyama vya siasa Na. 5 ya mwaka 1992 ili kutatua changamoto zilizopo. | Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Msajili wa Vyama vya Siasa inafanya kila jitihada juu ya suala hili kwa kuangalia namna ya kurekebisha Sheria ya Vyama vya Siasa No. 5 1992 (ilivyorekebishwa 2009) na kutoa mwongozo utakaojumuisha namna ya uandaaji wa taarifa za fesha za Vyama vya siasa | U t e k e l e z a j i unaendelea |
| | | Mwaka wa fedha 2013/2014 | |
| 29 | **Mapungufu katika mifumo ya misamaha ya kodi**<br>Napendekeza kuwa Serikali:<br>• Kuanzisha kitengo cha ufuatiliaji wa misamaha ambacho kitakuwa na wajibu wa udhibiti na kuhakikisha kuwa utoaji wa misamaha ya kodi unanakidhi matakwa ya kisheria na kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya misamaha hiyo ya kodi pamoja na kushirikiana na mamlaka zinazohusika na utoaji wa misamaha hiyo.<br>• Kufanya mapitio ya sheria za misamaha ya kodi kwa lengo la kupunguza mianya katika misamaha ya kodi. Aidha, serikali ihakikisha kwamba, misamaha ya kodi haizidi 1% ya Pato la Taifa au 5% ya mapato ya kodi yaliyokusanywa. | Serikali itaendelea kufanya mapitio ya sheria mbalimbali juu ya misamaha ya kodi.Katika utekelezaji huo, mwaka 2014 Serikali ilifanya mapitio ya ushuru wa mafuta,ushuru wa bidhaa kwa kusitisha misamaha iliyokuwa imetolea na Wizara ya fedha kwa Wawekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji.Hatua hii imechukuliwa ili kupunguza mianya ya ukwepaji wa kodi kupitia misamaha ya kodi.. | U t e k e l e z a j i unaendelea |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 30 | **Kuchelewa katika kushughulikia rufaa za kodi**<br>Naishauri Serikali kuongeza kasi ya kushughulika hizo rufaa kwa kuzingatia umuhimu wake katika uchumi | Kikwazo cha bajeti kwa Bodi na Baraza la rufaa za kodi ni moja ya sababu za ucheleweshaji wa kusikiliza na kutoa hukumu juu ya hizo rufaa.Serikali itatenga fedha za kutosha ili kurahisisha usikilizwaji wa hizo kesi kwa muda wa muafaka ikiwa ni pamoja na kutoa hukumu | Matokeo ya kesi zilizo katika hatua ya kusikilizwa hayawezi kutabiliwa kwa sasa. Hivyo ufuatiliaji utafanyika katika kaguzi zijazo |
| 31 | **Udhaifu katika usimamizi wa mapato**<br>Naishauri Mamlaka ya Mapato (TRA) kuyafanyia uchunguzi wa kina makampuni yote ya mafuta na gesi ikiwa ni pamoja na makampuni ya kuchimba madini kutathmini kiwango cha ushuru wa forodha ambacho hakijalipwa na kuchukua hatua ili kilipwe, pia, katika siku zijazo, mamlaka ihakikishe ushuru huo unalipwa na makampuni yote yanayopaswa kulipa. | Serikali kupita Mamlaka ya mapato (TRA) imefanya uchunguzi kwa makampuni ya gesi kama ilivyoshauriwa na Wakaguzi | Utekelezaji unaendelea |
| 32 | **Kujumuishwa kwa Taasisi za Umma zenye Vipindi na Kanuni Tofauti za uhasinu katika Hesabu jumuifu**<br>Uhasibu katika Hesabu Jumuifu<br>**Framework**<br>Naishauri Serikali ifanye yafuatayo:<br>• Mifumo ya uhasibu ya taasisi zinazomilikiwa na serikali iwianishwe pamoja na kuendana sambamba na mfumo wa uandaaji hesabu wa kimataifa usio wa taslimu (IPSAS Accrual).<br>• Taasisi zote zinazomilikiwa na serikali zijumuishwe kwenye hesabu za taasisi miliki ili hesabu za taasisi hiyo zioneshe uhalisia na kuendana na viwango vya kimataifa vya uandaaji wa hesabu. | Wizara ya fedha kupitia kwa Mhasibu mkuu wa Serikali imefanya jitihada katika kutekeleza mapendekezo wa Wakaguzi | Yametekelezwa |

| Na | Mapendekezo ya Ukaguzi | Majibu ya Mlipaji Mkuu wa Serikali | Maoni ya Mkaguzi |
|---|---|---|---|
| 33 | **Ukosefu wa Uwiano Sawia wa Ukomo katika Dhamana za Serikali**<br>Napenda kuishauri serikali kuongeza ushindani katika soko la ndani la dhamana za serikali na hivyo kuongeza ushawishi wa ununuzi wa dhamana za muda mrefu. | Mara kwa mara Serikali imekuwa ikichukua hatua kuboresha taratibu za ushiriki wa masoko ya dhamana za Serikali kwa kuwashawishi wawekezaji katika dhamana za Serikali za muda mrefu pamoja na kutoa misamaha ya kodi kwenye riba kutoka miaka miwili ya kuiva kwa dhamana za Serikali | U t e k e l e z a j i unaendelea |
| 34 | **Usimamizi Usiotosheleza Kwenye Uwekezaji wa Serikali na Vipaumbele Vyake**<br>Naishauri serikali Kuandaa Mfuko wa Uwekezaji utakaowezeshwa kutoka kwenye gawio na mapato mbalimbali ili kunusuru hisa za serikali, na pia kuiwezesha serikali kuwekeza katika sekta zingine ambazo itaona zinahitaji ushiriki wake. Mwisho, naishauri serikali kupitia mara kwa mara ufanisi wa uwekezaji wake na malengo katika makampuni ambayo inamiliki hisa chache. | Serikali inafanya jitihada ili kutekeleza mapendekezo wa wakaguzi kama ifuatavyo:<br>Utungaji wa sheria mpya ya Msajili wa hazina uko katika hatua za mwisho.Kwa sasa andiko la Baraza la Mawaziri linalopendekeza kutunga sheria ya Msajili wa Hazina linasubili kujadiliwa katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri.Andiko hilo limejumuisha mapendekezo yote | U t e k e l e z a j i unaendelea |
